# TASWIRA ZA ULEMAVU KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

**TASNIFU**

**YA**

**BETH NJERI MUTUGU**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI, SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA KWA AJILI YA KUTIMIZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU (Ph.D)**

**NOVEMBA 2019**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya utahini wa aina yoyote.

--------------------------------- 18/11/2019

BETH NJERI MUTUGU TAREHE

C82/22714/2011

Tasnifu hii imetolewa kwa ajili ya utahini kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu:

--------------------------------- 18/11/2019

PROF. CATHERINE M. NDUNGO TAREHE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

--------------------------------- 18/11/2019

DR. MIRIAM K. OSORE TAREHE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

ii

# SHUKRANI

Natanguliza shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uwezo wa kuifanya kazi hii. Amenijalia uhai, akailinda familia yangu na kunipa amani; jambo ambalo liliniwezesha kuyashughulikia masomo yangu. Kwa kweli singeweza kufikisha masomo yangu katika kiwango hiki bila Mungu kunilinda, kuniwezesha na kunipa matumaini hata wakati hali ilipokuwa ngumu. Amekuwa msaada wangu wa karibu, kimbilio langu na nguvu yangu kila siku.

Kazi hii haingekamilika bila mchango wa watu mbalimbali. Nawashukuru watu wote waliochangia kwa njia moja au nyingine katika kila hatua. Maoni, ujuzi na mawazo ya watu mbalimbali yamenifaidi sana na kuniwezesha kuifanikisha kazi hii.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuyafadhili masomo yangu. Msaada wa chuo hiki kwa hali na mali umechangia pakubwa katika kufaulu kwangu. Kadhalika nawashukuru wasimamizi wangu: Prof. Catherine Ndungo na Dkt. Miriam Osore kwa kuniongoza na kunipa ushauri ulioniwezesha kufikia lengo langu. Wamekuwa manahodha wakakamavu tangu chombo kilipong'oa nanga. Bila ushauri na busara kutoka kwao, chombo kingezama kabla ya kutia nanga. Aidha, walinihimiza na kunitia moyo kila wakati nilipoonyesha dalili za kukata tamaa na kuyumba katika bahari hii ya kitaaluma iliyojaa changamoto. Mungu awabariki sana. Kadhalika, nawashukuru walimu wangu na wahadhiri wenzangu wote katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunihimiza na kunitia moyo. Kwa namna ya kipekee nawashukuru Dkt. Leonard Chacha, Dkt. Richard Wafula na Dkt. Pamela Ngugi kwa kuwa hawakuchelea kuniuliza kazi hii imefika hatua gani kila walipopata nafasi. Ingawa sijataja majina yao wote, maoni yao yaliniwezesha kuiboresha kazi yangu.

Siwezi kuwasahau watoto wangu wapendwa; Kevin Wanjohi, Michelle Wangari na Steve Gathiru kwa upendo, welewa na uvumilivu wao nilipokuwa nikiishughulikia kazi hii. Mungu awabariki sana wanangu. Nawashukuru pia wazazi wangu; Bi. Helen Mutugu na marehemu babangu Bw. Obadiah Mutugu kwa kuwa walimu wangu wa kwanza na kunipeleka shuleni. Namshukuru mama yangu Helen na dada yangu Nancy Mutugu kwa kuniombea. Nawarudishia shukrani wandani wangu Dkt. Anne Munuku, Elizabeth, Agatha, Gladys na Olive kwa kunitia moyo na kunikumbusha kila wakati kuwa nimetoka mbali na sipaswi kukata tamaa. Walikuwa marafiki wa karibu kila wakati nilipohitaji msaada wa aina yoyote hasa nilipokuwa ughaibuni. Mungu awabariki.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Helen na Obadiah Mutugu pamoja na watoto wangu Kevin Wanjohi, Michelle Wangari na Steve Gathiru. Kuwepo kwenu maishani mwangu kumekuwa msukumo mkubwa wa kuyaboresha maisha yangu.

# YALIYOMO


**IKIRARI** ..... ii

**SHUKRANI** ..... iii

**TABARUKU** ..... iv

**YALIYOMO** ..... v

**VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA** ..... viii

**MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU** ..... ix

**IKISIRI** ..... x

**ABSTRACT** ..... xi

**SURA YA KWANZA** ..... 1

**UTANGULIZI WA UTAFITI** ..... 1

**1.0 Utangulizi** ..... 1

**1.1 Usuli wa Mada** ..... 1

**1.2 Suala la Utafiti** ..... 5

**1.3 Maswali ya Utafiti** ..... 6

**1.4 Malengo ya Utafiti** ..... 6

**1.5 Upeo na Mipaka** ..... 7

**1.6 Sababu za Kuchagua Mada** ..... 8

**1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada** ..... 12

**1.7.1 Matumizi ya Ulemavu kama Motifu ya Kikale katika Fasihi** ..... 12

**1.7.2 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Fasihi Simulizi** ..... 15

**1.7.3 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Tamthilia** ..... 22

**1.7.4 Matumizi ya Ulemavu katika Riwaya** ..... 24

**1.7.2 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Vyombo vya Habari** ..... 27

**1.8 Msingi wa Nadharia.** ..... 29

**1.8.1 Nadharia ya Mtindo** ..... 30

**1.8.2 Nadharia ya Semiotiki** ..... 34

**1.9 Mbinu za Utafiti** ..... 40

**1.9.1 Muundo wa Utafiti** ..... 40

**1.9.2 Mahali pa Utafiti** ..... 41

**1.9.3 Ukusanyaji wa Data** ..... 42

**1.9.4 Uteuzi wa Sampuli** ..... 43

**1.9.5 Uchanganuzi wa Data** ..... 44

1.10 Hitimisho ........ 45
SURA YA PILI ........ 46
TASWIRA ZA ULEMAVU WA AKILI KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI ........ 46
2.0 Utangulizi ........ 46
2.1 Dhana ya Ulemavu wa Akili ........ 47
2.2 Ulemavu wa Akili kama Chombo cha Kutetea Haki na Usawa ........ 51
2.3 Ulemavu wa Akili kama Mtindo wa Kuwasilisha Maudhui ya Malezi ........ 78
2.4 Ulemavu wa Akili kama Mtindo wa Kuwasilisha Maudhui ya Maadili ........ 94
2.5 Hitimisho ........ 102
SURA YA TATU ........ 104
TASWIRA ZA ULEMAVU WA TABIA KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI ........ 104
3.0 Utangulizi ........ 104
3.1 Dhana ya Ulemavu wa Tabia ........ 104
3.2 Ulemavu wa Tabia wa Kujidhuru ........ 108
3.2.1 Ulemavu wa Tabia ya Unywaji Pombe Kupindukia kama Mtindo ........ 108
3.2.2 Ulemavu wa Tabia ya Matumizi ya Mihadarati kama Mtindo ........ 129
3.2.3 Matumizi ya Ulemavu wa Tabia ya Kujiua kama Mtindo ........ 137
3.3 Taswira ya Ulemavu wa Tabia Unaohusu Mahusiano ya Kingono ........ 150
3.3.1 Ulemavu wa Tabia ya Uzinifu na Matumizi yake Kimtindo ........ 152
3.3.2 Ulemavu wa Tabia ya Ubakaji na Matumizi yake Kimtindo ........ 158
3.4 Hitimisho ........ 164
SURA YA NNE ........ 166
TASWIRA YA ULEMAVU WA VIUNGO KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI ........ 166
4.0 Utangulizi ........ 166
4.1 Dhana ya Ulemavu wa Viungo ........ 166
4.2 Matumizi ya Ugumba na Utasa kama Mtindo ........ 168
4.3 Matumizi ya Ulemavu wa Miguu kama Mtindo ........ 180
4.4 Matumizi ya Ulemavu wa Ubongomaji kama Mtindo ........ 193
4.4 Hitimisho ........ 200
SURA YA TANO ........ 201
MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 201
5.0 Utangulizi ........ 201

**5.1 Muhtasari wa Tasnifu** ........................................................................................ **202**
**5.2 Matokeo ya Utafiti**............................................................................................ **205**
**5.3 Mapendekezo**..................................................................................................... **213**
**MAREJELEO** ........................................................................................................ **216**
**VIAMBATISHO**...................................................................................................... **230**

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

AUDs: Alcohol Use Disorders

Uk: Ukurasa

TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

NIDA: National Institute of Drug Abuse

NIH: National Institute on Alcohol Abuse and Alcoholism

UNDP: United Nations Development Fund

CDC: Centre for Disease Control

KJV: King James Version

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

**Taswira**: Dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo yanayounda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo au za kiishara. Taswira za kiishara ni zile zinazounda picha inayoashiria jambo fulani au kuwasilisha ujumbe fulani kwa njia fiche.

**Ulemavu:** Hali inayoashiria upungufu fulani wa mtu unaodhihirishwa na mwonekano wake, tabia yake au kupungukiwa kiuamilifu

**Ulemavu wa akili**: Hali ya mtu kutokuwa na akili yenye urazini wa binadamu wa kawaida. Hali hii inadhihirika kutokana na mwonekano wa mtu, maneno na tabia zake.

**Ulemavu wa viungo**: Hali ambapo mtu anadhihirisha hali ya kupungukiwa kimaumbile na kiuamilifu kwenye kiungo fulani mwilini mwake.

**Ulemavu wa tabia**: Ukosefu wa maadili unaodhihirika katika tabia za mtu kwa mujibu wa matarajio ya jamii.

**Mtindo:** Ni dhana inayorejelea upekee wa kazi ya fasihi au upekee wa mwandishi. Upekee huu unadhihirika katika mbinu ambazo mwandishi anatumia katika uwasilishaji wa kazi yake. Kwa hivyo, mtindo ni mbinu zinazotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha maana katika kazi ya fasihi.

**Ubongomaji**: Ugonjwa wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida kutokana na kuzibwa kwa njia za kusafirisha maji katika ubongo.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizi ni: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Tata zaAsumini* (1990);za Said Ahmed Mohamed na *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanjawa Fujo* (1975) na *Rosa Mistika* (1976) zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Kwa kuwa matumizi ya ulemavu kama mtindo hayajachanganuliwa katika utanzu wariwaya ya Kiswahili, utafiti huu ulinuia kuliziba pengo hili. Taswira za ulemavu zilizozingatiwa ni za ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mtindo na nadharia ya semiotiki. Nadharia ya mtindo ilimwezesha mtafiti kutambua taswira za ulemavu zilizotumika katika riwaya teule. Nadharia ya semiotiki inajikita kwenye mtazamo kuwa kiashiria kinaweza kuzua maana tofauti kulingana na muktadha wa matumizi yake. Kwa hivyo, nadharia hii iliuongoza utafiti huu katika kutambua maudhui yaliyowasilishwa kupitia kwa aina mbalimbali za ulemavu. Utafiti huu ulijikita kwenye misingi kwamba ulemavu unapotumiwa katika kazi ya fasihi, huwa ni kwa lengo mahsusi ambalo ni kuwasilisha maudhui fulani kwa njia ya kipekee. Data ilikusanywa kwa kusoma na kuzichambua riwaya teule kwa kuzingatia wahusika wenye ulemavu na jinsi walivyotumiwa kama mtindo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Utafiti huu umebainisha kuwa taswira za ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo zimetumika na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali kwa njia ya kipekee. Matumizi ya mtindo huu yameiathiri hadhira lengwa ili itafakari zaidi kuhusu maswala ambayo hayajitokezi waziwazi. Maudhui yanayojitokeza ni ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Ingawa jumbe zinazowasilishwa ni za kawaida zinabeba uzito zaidi na kuiathiri hadhira zaidi zinapopitishwa kwa kutumia taswira za ulemavu. Aidha, waandishi wanafanikiwa katika lengo lao la kupitisha ujumbe wao kwa namna ya kipekee. Kwa hivyo, utafiti huuunadhihirisha kuwa mwandishi anapotumia taswira za ulemavu katika kazi yake, anafanya hivyo kwa lengo la kuwasilisha ujumbe mahsusi. Utafiti huu unatoa mapendekezo kuwa tafiti zaidi zifanywe ili kuchunguza matumizi ya ulemavu kama mtindo katika tanzu zingine za fasihi na kazi zingine zilizoandikwa na waandishi wengine wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, inapendekezwa kuwa aina zingine za ulemavu ambazo hazijashughulikiwa katika utafiti huu zichunguzwe kwa kuzingatia matumizi yake kama mtindo. Utafiti huu utawafaidi waandishi, wahakiki, walimu na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili kwa kuwa unaangazia mtazamo mpya kuhusu matumizi ya ulemavu kama mtindo katika fasihi.

## ABSTRACT

The research set out to investigate how disability images have been used as an element of stylein selected novels written by Said Ahmed Mohamed and Euphrase Kezilahabi. These novels are: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Tata zaAsumini* (1990);by Said Ahmed Mohamed; *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) and *Rosa Mistika* (1976) by Euphrase Kezilahabi. Disability images that were investigated are mental, behavioral and physical.The use of disability images has not been investigated in Kiswahili novels; therefore this research aimed at filling this gap. This research was guided by two theories: stylistics and semiotics. Stylistics theory guided the researcher in identifying disability images used in the selected novels. Semiotics theory has its basis on the relationship between a sign, an object and its meaning and argues that a signifier can have several meanings depending on its contextual usage. Therefore, this theory guided this study in identifying the various messages that were conveyed through disability images.The study also sought to analyze disability from a literary perspective by looking at how disability images have been used as literary tools in delivering author's messages. The study was based on the assumption that when disability images are used, they foreground meaning. Consequently the message is delivered to the intended audience in a unique way and the effect is more profound. Data was collected by reading the selected novels and identifying characters who were depicted as having various diasabilities.This study is qualitative in nature. Therefore, data was presented and analyzed through descriptive method.This study analysed three disability images: mental, behavioral and physical. Through these images, various themes were identified. These themes were based on political, social and economic issues affecting the society. Although these are seeemingly common themes in many literary works, the use of disability images makes them affect the audience in a profound way. The study underscores the fact that the selected authors were able to deliver their intended messages successfully and in a more effective manner. This study recommends that more research be done to investigate how disability images have been used as style by other Kiswahili literary authors and also in other literary genres. The use of other types of disability images could also be investigated. This research is relevant to authors, critics, teachers and students of Kiswahili literature because it provides a new perspective on the use of disability as style.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI WA UTAFITI

### 1.0 Utangulizi

Sura hii inaweka msingi wa utafiti mzima. Sura hii imeshughulikia, usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti. Katika sehemu hii swala la utafiti limefafanuliwa kwa kina kwa kuzingatia mada na malengo ya utafiti huu. Kadhalika, upeo na mipaka ya utafiti huu pamoja na sababu za kuchagua mada zimeshughulikiwa. Sura hii pia imefafanua mbinu za utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ambazo zilikuwa msingi wa utafiti huu.

### 1.1 Usuli wa Mada

Ulemavu ni hali ya kimsingi ya tofauti zinazopatikana miongoni mwa binadamu. Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni (2019), inakisiwa kuwa watu bilioni moja kote ulimwenguni wana ulemavu. Hii ni asilimia kumi na tano ya watu wote ulimwenguni. Asilimia themanini ya watu hawa wanaishi katika mataifa yanayoendelea. Kwa hivyo ulemavu ni hali ya maisha na tajiriba ya kijamii ambayo haiwezi kuepukika wala kupuuzwa.

Kulingana na Coleridge (2000), ufafanuzi wa dhana ya ulemavu unakumbana na changamoto nyingi kutokana na kuwepo kwa mitazamo tofauti katika tamaduni na mazingira mbalimbali. Kwa mfano, mtu anatambuka kama mwenye ulemavu kutokana na mwonekano wake ama ana maradhi yanayomlemaza. Aidha dhana hii inarejelea hali ya ukiukaji wa hali ya kawaida au kupungukiwa kwa namna fulani. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (2016), ulemavu ni hali ya ukosefu wa uwezo wa kufanya mambo au kutekeleza majukumu ya kijamii. Hali hii inaweza kusababishwa na kuwepo kwa ulemavu wa viungo kimaumbile, kupungukiwa kiakili

na kitabia. Ulemavu wa viungo hudhihirika kwenye watu ambao hawana uwezo wa kusikia, kuona, kuongea na kutembea kama binadamu wengine.

Ulemavu wa akili ni hali ambapo mtu hukosa uwezo wa kufanya mambo mbalimbali yanayoambatana na umri na urazini wake kama binadamu. Ulemavu wa tabia hudhihirika wakati mtu anapokuwa na tabia zilizo kinyume na maadili na matarajio ya jamii. Hata hivyo, maana ya dhana ya ulemavu wa tabia kwa kiasi kikubwa hutegemea maadili ya kila jamii na yanaweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii.

Bennet na Royale (1999), wanasema kuwa mitazamo kuhusu ulemavu inaweza kujikita katika imani za kidini. Hivyo basi inakuwa vigumu sana kueleza dhana hii kwani maana yake hutofautiana kutoka itikadi moja ya kidini hadi nyingine au kutoka muktadha mmoja hadi mwingine.

Geertz (1973), anasema kuwa utamaduni huashiria ruwaza mbalimbali za maana za kihistoria ambazo hujikita katika ishara za mifumo iliyorithiwa kutoka kwa jamii. Mifumo hii ya ishara hutumiwa na wanajamii kuwasiliana na kuendeleza ufahamu wao na mielekeo yao kuhusu maisha. Mitazamo kuhusu ulemavu hujikita katika maisha ya kila siku, nyanja za kihistoria na tamaduni mbalimbali. Kwa hivyo, mifumo ya imani kuhusu ulemavu ni tata kwa sababu inaegemea kwenye mambo tofauti. Kwa mfano, kama anavyoeleza Coleridge (2000), katika jamii ya Tuareg kutoka nchi ya Mali, madoadoa kwenye ngozi na makalio madogo huchukuliwa kuwa ni kipingamizi kikubwa kwa wanawake wanaotarajia kuolewa na hivyo basi huonekana kama ulemavu.

Kulingana na Leslie (2016), ulemavu ni dhana ya kisanaa inayozua maana teule ambayo hulingana na será, muktadha au utumikizi wake. Aidha, vigezo

vinavyotumiwa kubainisha watu wenye ulemavu hubadilika kulingana na wakati, muktadha, jamii na utamaduni. Ijapokuwa kuna fasili tofauti zinazojitokeza kuhusu dhana ya ulemavu, utafiti huu ulizingatia ulemavu kwa misingi ya fasihi. Kwa kurejelea mtazamo wa kifasihi, ulemavu hutumiwa na mwandishi kwa lengo mahsusi.

Kama anavyosema Wales (2001), lengo la kutumia mitindo tofauti sio tu kufafanua vipengele rasmi vya matini bali ni kudhihirisha uamilifu na umuhimu wake katika ufasili wa matini husika. Kwa hivyo, taswira za ulemavu zinaweza kutumiwa na mwandishi kama mtindo ili kuibua maana tofauti katika kazi ya fasihi na hivyo basi kuwasilisha maudhui mbalimbali.

Kwa mujibu wa Hickey (1993), mtindo katika uandishi ni mbinu ya kueleza fikra kwa kutumia lugha. Aidha, katika kufafanua mtindo matumizi ya lugha yanayojikita katika muktadha fulani wa kijamii huzingatiwa. Kadhalika, sababu zinazomfanya mwandishi kutumia mtindo fulani huchunguzwa na vipengele husika kuainishwa kulingana na dhima yake katika muktadha wa kijamii. Jambo hili ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu mbali na ulemavu wa viungo na ulemavu wa akili ambao hudhihirika moja kwa moja kimaumbile na kisayansi; ulemavu wa tabia unaodhihirika katika jamii mahsusi zinazoshirikishwa kwenye vitabu teule ulishughulikiwa kwa mujibu wa dhima mbalimbali katika maisha ya wanajamii husika.

Kulingana na Strunk na White (2009), uamuzi wa mwandishi wa kutumia mtindo fulani katika kazi yake huongozwa na mambo mawili. Jambo la kwanza ni kuweza kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira kwa njia iliyo rahisi, wazi na shawishi. Jambo la pili ni kukuza umakinifu na mvuto miongoni mwa wasomaji wake. Ni katika misingi hii ambapo utafiti huu ulichunguza namna Said Ahmed Mohamed na

Euphrase Kezilahabi wanavyotumia ulemavu kama mtindo katika kufanikisha dhamira na maudhui ya kazi zao.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1989), uasili wa mtunzi na upekee wake hubainika katika mtindo. Mulokozi anasema kuwa mtindo ni tabia ya utungaji ambayo humpambanua mtunzi mmoja na mwingine na kwamba mtindo wa mtunzi huathiriwa na jamii ambapo ametungia kazi yake. Hivyo basi uasili wa mtunzi na upekee wake hubainika katika mtindo wake.

Mulokozi anaendelea kusema kuwa mtindo huathiri jinsi ujumbe unavyopokelewa. Wakati mwandishi anapojieleza anatoa hisia na maoni yake kulingana na falsafa yake kuhusu yale anayoyaandika. Kwa hivyo, waandishi mbalimbali wana mitindo tofauti ya kuwasilisha maudhui yao.

Kuna vipengele mbalimbali vinavyobainisha na kuathiri mtindo wa mwandishi. Kama wanavyosema Strunk na White (2009) baadhi ya vipengele hivi ni mada au ujumbe unaowasilishwa, tajriba ya mwandishi, hadhira lengwa, mazingira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi, umilisi na ujuzi wa lugha anayotumia na ubunifu wake. Ulimwengu wa kisanaa ni ulimwengu wa hisia za kijamii, ni ulimwengu wa maneno na picha. Hisia hizi huwasilishwa kupitia kwa maneno na picha zinazotokana na tajriba na maisha ya mwandishi na wanajamii wote. Maneno haya na picha hizi hujengwa kutokana na tajiriba, mielekeo na amali za maisha ya wanajamii wote. Strunk na White wanaendelea kusema kuwa mtindo unaotumika katika kazi yoyote ya fasihi huathiriwa na kile kinachotokea katika jamii ambamo mwandishi huchota fikra, maudhui, falsafa, itikadi, tamathali za lugha, maumbo na miundo lugha. Kwa hivyo, mtindo una nafasi muhimu katika kuelewa ujumbe unaopitishwa na mwandishi.

Kama anavyosema Burton (1982), uchambuzi wa mtindo hauhusishi tu mjadala wa athari za lugha na matini lakini ni nyenzo muhimu katika kuelewa uhalisia wowote unaozuka kutokana na lugha. Mtindo unaotumiwa na mwandishi katika kazi yake hutegemea utamaduni wa jamii yake kwa kiasi kikubwa. Mtindo huashiria namna ambavyo mwandishi amewasilisha kazi yake na hivyo basi huwakilisha sauti yake.

Kulingana na Berube (2005), tafiti nyingi kuhusu ulemavu zinazingatia ulemavu katika muktadha wa siasa, ujumi na maadili. Katika fasihi, wahakiki wengi huchunguza kazi za fasihi kwa lengo la kubaini namna ambavyo ulemavu umewasilishwa katika vipindi mbalimbali vya historia na kitamaduni.

Katika uchunguzi wao wanazingatia jinsi ambavyo watu wenye uzima hubadilika na kuwa walemavu, kutengwa kwa watu wenye ulemavu na nafasi ya ulemavu katika simulizi mbalimbali. Madai ya Berube yanathibitisha kuwa ulemavu huashiria mambo yaliyojitenga na hali ya kawaida na hivyo basi kuufanya kuwa suala nyeti linalopaswa kuchunguzwa kwa kina zaidi kwa kuwa unaweza kuwa ishara ya masuala nyeti yanayoathiri jamii. Kwa hivyo, ulemavu unaweza kutumiwa na mwandishi kama mtindo wa kipekee utakaomwezesha kuwasilisha ujumbe.

### 1.2 Suala la Utafiti

Matumizi ya ulemavu kama mtindo hayajachanganuliwa kwa undani na ulemavu unatumika tu kama usuli katika tafiti pana. Utafiti huu ulikuwa hatua muhimu katika kuliziba pengo hili kwa kuchunguza matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase kezilahabi. Riwaya hizi ni: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980) na *Tata za Asumini* (1990); za Said Ahmed Mohamed na *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Rosa Mistika* (1976), zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi.

Ulemavu mara nyingi hutumika kama jazanda ya matatizo yanayopatikana katika jamii. Hata hivyo jazanda hizi huwa na maana zinazoelekeza mitazamo, utambulisho na tajiriba za watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, taswira za ulemavu zilichunguzwa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Utafiti huu ulijikita kwenye hoja kwamba ingawa matumizi ya ulemavu kama mtindo yanapatikana katika nyanja kama vile: isimu, falsafa, ujumi na sanaa mbalimbali; unapotumiwa kama mtindo katika fasihi mwandishi huwa na lengo mahsusi. Utafiti huu ulichunguza riwaya zilizoteuliwa ili kubainisha namna taswira za ulemavu zimetumiwa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali kwa njia ya kipekee.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

i. Taswira za ulemavu wa akili zimetumika vipi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi?

ii. Taswira za ulemavu wa tabia zimetumika vipi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi?

iii. Taswira za ulemavu wa viungo zimetumika vipi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

i. Kutathmini matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

ii. Kupambanua namna ambavyo taswira za ulemavu wa tabia zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

iii. Kuchunguza ni kwa jinsi gani taswira za ulemavu wa viungo zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulijikita katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizi ni: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Tata za Asumini* (1990); za S. A. Mohamed na *Kichwamaji* (1974). *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Rosa Mistika* (1976); za E. Kezilahabi.

Ingawa kuna riwaya nyingi zilizoandikwa katika lugha ya Kiswahili, riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi ziliteuliwa kwa kuwa utafiti wa awali ulithibitisha kuwa matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo yamejitokeza zaidi katika kazi zao nyingi ikilinganishwa na riwaya zingine za Kiswahili. Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wanatumia mitindo mbalimbali ya uandishi katika riwaya zao ili kuwasilisha maudhui mbalimbali. Aidha, riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu zinadhihirisha ufundi wa hali ya juu kwa jinsi ambavyo mbinu mbalimbali za uandishi zimetumika. Ili kufanikisha utafiti huu, data iliyolengwa ni ile iliyohusiana moja kwa moja na taswira za ulemavu zilizotumika kimtindo. Taswira hizi zilibainishwa kwa misingi ya matukio yanayotokea katika riwaya teule, kauli za waandishi na wahusika mbalimbali na matendo yao. Aidha, maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa kupitia kwa taswira hizi yamechunguzwa na kuchanganuliwa. Kupitia taswira za ulemavu, utafiti huu ulizingatia mbinu za kimtindo kama vile jazanda na

sitiari zilizohusiana na ulemavu na kubainisha namna zinavyotumiwa katika uwasilishaji wa maudhui.

Kama wanavyosema Wafula (1989), Senkoro (1985) na Njogu (2001); Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wameandika riwaya nyingi za Kiswahili zinazojikita katika mazingira mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kwa hivyo, kazi zao zinatoa picha halisi ya jamii katika kipindi kirefu. Jambo hili linadhihirika katika uandishi wao hasa katika riwaya zilizoshirikishwa katika utafiti huu kwa kuwa zilichapishwa katika miktadha mbalimbali ya kihistoria. Utafiti huu haukuwa na lengo la kuchunguza tanzu zingine za fasihi zilizoandikwa na waandishi teule. Riwaya zilizoteuliwa zilitoa data ya kutosha katika kubainisha matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Mtindo katika kazi mbalimbali za fasihi andishi umechunguzwa na watu wengi. Baadhi yao ni: Oiko (2017), Rono (2016), Tsuma (2014), Onchangu (2016) na Kairu (2005). Kutokana na matokeo ya tafiti hizi, inadhihirika kuwa vipengele vya fasihi vya kimtindo vinavyotumiwa na mwandishi vinahusiana na jamii. Kwa mfano, taswira mbalimbali za wanawake katika tanzu mbalimbali za fasihi zinaoana moja kwa moja na hali halisi ya kijamii ambamo zinapatikana. Katika utafiti huu, matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo ni muhimu kwa kuwa msomaji wa kazi ya fasihi anapokumbana nazo analazimika kutafakari zaidi kuhusu ujumbe uliowasilishwa na mwandishi badala ya kuchukulia ulemavu kwa maana ya juu. Msomaji anapotafakari zaidi anaweza kuuelewa ujumbe ulioashiriwa na taswira hizi kwa njia yenye uzito zaidi. Matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo humwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya kipekee na yenye uzito zaidi; jambo ambalo halingewezekana iwapo angetumia lugha ya kawaida.

Utafiti huu unanuia kuweka wazi maudhui ambayo hayajitokezi moja kwa moja katika riwaya teule. Kadhalika uchanganuzi wa taswira za ulemavu na matumizi yake kimtindo yanafafanua umuhimu wa kuzingatia muktadha wa matumizi ya mtindo wa mwandishi katika kuelewa dhamira na maudhui yaliyolengwa.

Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed, ni waandishi kutoka Tanzania bara na Kisiwani Pemba mtawalia. Ingawa kuna waandishi wengi Tanzania bara na Kisiwani, sababu za kuchagua waandishi hawa zilitokana na upekee unaodhihirika katika kazi zao. Waandishi wa Kiswahili kutoka sehemu za bara na pwani ya Tanzania wanadhihirisha matumizi mapana ya vipengele vya kitamaduni, kiisimu na nyenzo zilizo karibu na mazingira yao katika kazi zao.

Said Ahmed Mohamed ambaye asili yake ni Kisiwa cha Pemba kilichopo pwani ya Tanzania anajibainisha kwa namna ya kipekee. Kama walivyo waandishi wengi wa riwaya kutoka Unguja kama vile Z. Burhani, Shafi Adam Shafi, na M S. Abdulla, S. A. Mohamed anatumia tamathali za lugha, jazanda na maelezo yaliyofumbwa kwa njia inayoibua upekee wake kimtindo. Matumizi ya mtindo wa kitamathali yanalenga kuwasilisha maana halisi na mwafaka zaidi kwa uzito uliolengwa. Kwa upande wake, Kezilahabi ameshughulikia masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kisaikolojia ambayo ni ya kawaida katika fasihi ya Kiafrika. Kwa mujibu wa Acquaviva (2004), Kezilahabi anajitokeza kama mtunzi wa kipekee kwa namna ambavyo anatumia sitiari na mafumbo. Kezilahabi anayatazama mazingira na mambo ya dunia kwa umakini sana. Kama anavyoendelea kusema Acquaviva, Kezilahabi anatumia taswira zake za malimwengu na ubinadamu ili kueleza mambo kama yalivyo katika ulimwengu halisi na ulimwengu dhanifu. Kila ishara anayotumia katika uandishi wake ina picha ya

fikra zinazojificha katika ukweli wa maisha na Kezilahabi ana nguvu na ujasiri wa kuzifunua fikra zake.

Mtafiti aliamua kuchunguza kazi za waandishi hawa wawili kwa kuwa wanatoka katika mazingira tofauti ya kijamii. Aidha, kama anavyosema Murithi (2017) wanatofautiana kiitikadi. Said Ahmed Mohamed amejikita kwenye itikadi ya mfumo wa kibepari. S. A. Mohamed anaongozwa na itikadi ya mapinduzi na marekebisho ya asasi za mfumo mzima wa umwinyi. Ana maoni kuwa asasi za itikadi ya kimwinyi zikibadilishwa na kurekebishwa, haki na usawa zitapatikana katika jamii. Itikadi ya Said Ahmed Mohamed inabainika katika kazi zake za fasihi ambapo anajenga wahusika wa kimapinduzi wanaodhamiria kuleta mabadiliko katika jamii zao. Euphrase Kezilahabi anaegemea kwenye itikadi ya dini na maswala ya kifalsafa hasa kuhusu maisha. Kwa mujibu wa Mezger (2002), itikadi hii inatokana na mwingiliano wake na dini ya Kikristo alipokuwa masomoni. Anajitokeza kama mwandishi ambaye ana tajriba na ufahamu mkubwa katika maswala ya Kikatoliki.

Tofauti za kimazingira na kiitikadi za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi zilichochea utafiti huu. Hii ni kwa sababu mtazamo wa dhana ya ulemavu unafungamana na imani na utamaduni wa jamii mahsusi. Aidha, kama wanavyosema Ingstad na Whyte (1995), ulemavu ni swala la kiitikadi na hujikita katika falsafa ya jamii na mwandishi. Kila jamii ina mtazamo wake kuhusu ulemavu. Mtazamo huu unahusiana moja kwa moja na utamaduni wa jamii. Aidha, kila mwandishi katika utunzi wake huathiriwa kwa namna moja au nyingine na jamii inayomzunguka. Hali hii husababisha kuzuka kwa mitazamo na taswira mbalimbali kuhusu ulemavu. Hivyo basi, ulemavu unaweza kutumiwa kama mbinu ya kuwasilisha maudhui ya mwandishi kwa kuwa taswira mbalimbali za ulemavu zinaweza kuashiria maana tofauti.

Kwa mujibu wa Mazrui (1984), Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wanatambulika kama waandishi wa fasihi wanaotumia lugha kwa namna ya kipekee. Ingawa kipengele cha maudhui katika kazi zao kimechunguzwa sana, mtindo waliotumia katika kazi zao haujazingatiwa kwa kina. Kama anavyosema Mazrui, riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (S. A. Mohamed) inawakilisha maendeleo ya utanzu wa riwaya ya Kiswahili katika uchanganuzi wa masuala ya kijamii, kisiasa na matukio yaliyoikumba Afrika katika kipindi cha ukoloni. Aidha riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* inadhihirisha upekee katika uwasilishaji wa maudhui. Ingawa riwaya zilizochunguzwa ziliandikwa katika miaka ya sabini, themanini na tisini maudhui yaliyowasilishwa yana nafasi muhimu katika jamii ya sasa. Kwa hivyo, inatarajiwa kuwa kwa kuzingatia taswira za ulemavu kama mtindo, utafiti huu utawawezesha wasomaji kuelewa zaidi maudhui yaliyowasilishwa katika riwaya husika.

Kwa mujibu wa Bogdan na wengine (2012), matumizi ya ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi huathiri maana, mfumo na jinsi kazi husika inavyoeleweka. Wanadai kuwa dhana ya ulemavu inaweza kubeba jumbe mbalimbali kutegemea namna mwandishi anavyoitumia katika kazi yake. Utafiti huu ulinuia kutoa mchango wa mawazo kuhusu matumizi ya ulemavu kama mtindo kwa kuchunguza riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi na jinsi walivyotumia mtindo huu kuwasilisha ujumbe kuhusu masuala mbalimbali yanayoikumba jamii.

Uchunguzi huu ulikuwa na lengo la kuangazia mwelekeo tofauti wa uhakiki kuhusiana na swala la ulemavu kwa kuchunguza iwapo ulemavu unaweza kutumiwa na mwandishi siyo kwa lengo la kuangazia upungufu wa watu wenye ulemavu pekee, ila kama njia ya kuwasililsha ujumbe wake kikamilifu. Hii ni kwa sababu uteuzi wa maneno, taswira na ujumbe unaweza kutoa mwongozo kuhusu mitazamo, mielekeo na

tabia za wanajamii. Aidha, kwa kuwa uteuzi wa mtindo huathiri namna ujumbe unavyowasilishwa na kupokelewa na hadhira inayolengwa na mwandishi, kuna haja ya mhakiki kuchunguza mtindo wa mwandishi ambao si wa moja kwa moja ili kubainisha namna ambavyo mtindo huo umetumika kuawasilisha maudhui kwa njia ya kipekee.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii imeshughulikia uchambuzi wa yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Aidha, mihimili ya nadharia zilizoongoza utafiti huu na namna ilivyotumiwa katika kukusanya na kuchanganua data katika utafiti huu imeshughulikiwa katika sehemu hii. Suala la ulemavu ni pana mno na kuna tafiti nyingi ambazo zimelishughulikia. Kuna tafiti ambazo zimeegemea kwenye masuala ya tiba na zingine kwenye masuala ya kijamii na haki za watu wenye ulemavu. Tafiti hizi zinaegemea kwenye mtazamo wa soshiolojia. Hata hivyo kwa kuwa utafiti huu ni wa kifasihi, tafiti zilizozingatiwa ni zile zinazoshughulikia ulemavu kama mtindo. Matokeo ya tafiti hizi, mchango wake katika utafiti huu na namna zinavyotofautiana na utafiti huu ni mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika sehemu hii. Kadhalika, pengo lililotokana na tafiti za awali limebainishwa na jinsi ambavyo utafiti huu umeliziba.

#### 1.7.1 Matumizi ya Ulemavu kama Motifu ya Kikale katika Fasihi

Neno kikale ina maana ya '*archetype*.' Neno hili linatokana na neno la Kigiriki '*arkhetupon*' linalomaanisha kitu asilia ambacho baadaye hutokea katika hali mbalimbali. Kwa hivyo, kikale katika fasihi hurejerea taswira au motifu inayojitokeza mara kwa mara. Neno hili liliasisiwa na Karl Jung aliyelitumia kama msingi wa nadharia ya kijumla isiyofahamika. Vikale ni ishara za mwanzo za binadamu ambazo zimekuwa zikijitokeza katika hadithi za tamaduni nyingi kihistoria. Katika fasihi, kikale kinaweza kuwa mhusika, utamaduni, tukio, hadithi au taswira inayojitokeza

katika kazi mbalimbali za tamaduni na nyakati tofauti za kihistoria. Ishara hizi huibua hisia nzito kwa msomaji kulingana na wahusika, taswira na maudhui yanayoashiria maana za kijumla na tajriba za kimsingi za binadamu pasi na kuzingatia wakati walipoishi au mahali walipo. Kikale kinaweza kuwa mhusika, hali, kauli, tabia au vifaa ambavyo hurudiwa katika tanzu nyingi za fasihi. Aidha, ni kipengele kinachotambulika kote kuwa kinajitokeza katika fasihi zote na kinahusishwa na watu wengi wenye tajriba mahsusi. Kwa mfano, katika kazi ya fasihi, wahusika mashujaa huwa na sifa mahsusi zinazofanana. Kikale hudhihirika katika masuala yanayohusu tabia, nadharia ya saikolojia historia au uchambuzi wa fasihi. Kwa hivyo, kikale katika fasihi hurejerea taswira au motifu inayojitokeza mara kwa mara.

Motifu ni kipengele cha usimulizi chenye maana inayoashiria maana na kukaririwa kote katika kazi mahsusi ya fasihi. Motifu inaweza kujitokeza kama ishara, lugha au muundo katika kazi ya fasihi. Motifu inaweza kuwa wazo, kifaa, dhana, mhusika, hali ya hewa, rangi au kauli. Motifu ya kikale ni ishara inayojitokeza kote katika kazi ya fasihi na ambayo huwakilisha ruwaza bia za uhalisi wa binadamu. Kwa mfano, mhusika shujaa ni kikale kwa kuwa wahusika wote mashujaa katika kazi ya fasihi huwa na sifa kuu zinazofanana. Kwa mujibu wa Jung (1981), vikale ni ruwaza na taswira za kijumla za zamani zilizorithiwa na kufasiriwa kama taswira zinazodhihirika kwenye tabia na maingiliano katika ulimwengu halisi. Kadhalika, vikale hujikita kwenye tabia za watu na nafsi zao. Kulingana na Jung, kuna aina ya vikale kumi na viwili. Kila kikale kina maana na sifa zake. Matumizi ya motifu katika kazi ya fasihi huchangia katika uelekezaji wa toni na maudhui katika kazi husika.

Kwa mujibu wa Garry na Hasan (2005)) wahusika walemavu wamekuwa wakitumiwa katika fasihi tangu chimbuko lake. Kwa hivyo, wanaweza kuchukuliwa kama motifu ya kikale. Katika riwaya za kubuni, wahusika hawa wamekuwa wakihusishwa na

uovu na hatari. Jambo hili linasababisha kudhulumiwa kwao na kunyimwa haki na usawa katika maisha yao. Kadhalika, wahusika wenye ulemavu wanatengwa na kusawiriwa kama watu wenye njama za kuwadhuru watu wasio na hatia. Kwa hivyo, wahusika hawa kwa kawaida hawasawiriwi kama binadamu halisi ila wanatumiwa kama vipengele vya kimtindo kinachoashiria hila na matendo maovu. Ulemavu umetumiwa kama motifu ya kikale kuangazia mgogoro kati ya uovu na uzuri ambapo wahusika wenye ulemavu husawiriwa kama wenye nia ya kuwadhuru wahusika wazuri lakini hatimaye wanaangamia. Kwa mfano, katika tamthilia ya Shakespeare, ingawa mhusika Richard III hakuwa na ulemavu wa viungo katika hali halisi, alilemazwa kimakusudi na mwandishi ili kusisitiza uovu wake. Usawiri wa wahusika wenye ulemavu katika fasihi hulenga kuendeleza mwelekeo hasi kuhusu watu wenye ulemavu. Kwa hivyo, maangamizi yanayowapata wahusika hawa huchukuliwa kuwa ni majaaliwa yao.

Inabainika kuwa wahusika wenye ulemavu mara nyingi hawachukuliwi kuwa wanadamu wenye uwezo na hisia kama watu wengine. Familia na jamii kwa jumla huchukulia ulemavu kama adhabu na hali inayoleta aibu na hivyo basi hawapendi kutangamana na watu wenye ulemavu. Jambo hili hukuza mwelekeo wa kuogofya na shaka unaotumiwa katika fasihi ili kuwasawiri wahusika wenye ulemavu kama watu waovu na katili. Kwa mfano, katika tamthilia ya Edipode, mwandishi Sofokile anamlemaza mhusika Edipode na kuashiria kuwa matatizo yayoikumba nchi ya Thebes yalitokana na uongozi wake. Kwa hivyo, ulemavu wake unaonekana kuwa ni adhabu ya makosa aliyoyafanya. Edipode alijipofusha mwenyewe ili kujiadhibu kutokana na dhambi zake. Hata hivyo, Sofokile anaonekana akilihalalisha jambo hili, na kuashiria kuwa upofu si ulemavu ila ni mbinu ya kuadhibu mtu kwa kosa lake.

Jung (1981) anasema kuwa usawa wa kijamii hauwezi kufikiwa iwapo walimu wa fasihi hawatashughulikia masuala yanayohusu ulemavu kwa kuendeleza habari na maarifa yenye ukweli yanayowasawiri wahusika wenye ulemavu kwa njia ifaayo. Fasihi huashiria na kuunda jumbe za kitamaduni kuhusu uwezo na kutokuwa na uwezo, ulemavu na uzima. Aidha, inawawezesha watu kufahamu masuala yanayohusu ulemavu na mitazamo kuhusu ulemavu. Katika tamaduni mbalimbali ili watambue kuwa watu wenye ulemavu wana uwezo ambao wanaweza kutumia ili kuendeleza maisha yao. Katika sehemu inayofuata matumizi ya ulemavu katika tanzu mbalimbali za fasihi yatashughulikiwa kwa lengo la kutambua utumikizi katika fasihi na kutambua pengo lililozibwa na utafiti huu.

### 1.7.2 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Fasihi Simulizi

Tangu zamani, suala la ulemavu limekuwepo katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Kwa mfano, Kerenyi (1974) na Ebestein (2006), wanasema kwamba visasili na ngano zinazosimuliwa katika viasili vya Kigiriki kuhusu mhusika Hephaestus ni miongoni mwa maandishi ya zamani zaidi katika utamaduni wa ushairi wa kimagharibi kuhusu ulemavu. Hephaestus alikuwa mungu wa Kigiriki mwenye ulemavu wa mguu. Inasemekana kwamba aliupata ulemavu huu baada ya kurushwa kutoka juu ya mlima Olympus na mama yake. Ebestein anasema kuwa ulemavu wa Hephaestus una maana ya kiujumi. Hii ni kwa sababu licha ya kuwa na ulemavu wa mguu alikuwa na sura mbaya. Hephaestus alichukulia kuwa mama yake alikuwa anamdhulumu kwa sababu ya mwonekano wake, Aidha ulemavu ulisababisha mke wake kutokuwa mwaminifu kwake.

Kwa kurejelelea kisa cha Hephaestus wahakiki wa fasihi Hinz na Teunissen (1985) wameibuka na dhana wanayoiita tabia ya *‘Aphrodite / Hephaestus complex’* katika

muktadha wa kisasa. Wanasema kuwa wanaume walioathirika na tabia hii huwa wazuri sana katika kazi zao na hutumia muda mwingi wa maisha yao katika uendelezaji wa kazi zao. Hata hivyo, wanaume hawa hawana wakati wa kutosha kushughulikia maslahi ya familia zao. Kwa upande mwingine wanaume hawa hupendwa sana na vipusa kutokana na maisha yao ya kifahari na hali hii inasababisha kuvunjika kwa ndoa zao. Wanaume wenye tabia ya '*Hephaestus complex'* huishi maisha kama haya ili kufidia upungufu wao unaotokana na ulemavu. Ni njia wanayotumia kujikinga kutokana na mielekeo hasi ya jamii dhidi yao. Katika kisasili cha Hephaestus ulemavu umetumiwa kuangazia swala la maadili miongoni mwa wanajamii na kuweka wazi swala la uzinzi unaopatikana katika jamii husika.

Utafiti wa Ebeinstein, Hinz na Teunissen ulitoa msingi muhimu katika utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa ulemavu wa tabia unaojikita katika masuala ya maadili. Hata hivyo, tofauti na uchunguzi wao, utafiti huu ulizingatia riwaya za Kiswahili. Aidha uchunguzi wa Hinz na Teunissen unajikita katika mtazamo wa '*Hephaestus Complex'* ilhali utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mtindo na ya semiotiki.

Franks (2001) alichunguza nafasi ya ulemavu na maana yake katika hadithi za kichimbakazi zilizoandikwa na Grimm. Hadithi za kichimbakazi zina nafasi ya kipekee katika fasihi kwa kuwa ni hadithi zinazohusisha miujiza, mashetani, mambo ya kiuganga, kiuchawi au ya kimaajabu. Mhusika mkuu katika hadithi hizi hupambana na hali gumu ya maisha na huibuka kama mshindi. Lengo la utafiti wa Franks lilikuwa kubainisha nafasi ya ulemavu katika fasihi ya jadi. Katika utafiti wake, Franks aliongozwa na nadharia changamano ambapo aliutazama ulemavu kama swala la kiafya, tiba, maumbile na la kijamii. Misingi ya mtazamo wa ulemavu kama swala la kiafya lilimwongoza katika utambuzi wa wahusika waliokuwa na upungufu katika hadithi teule kwa mujibu wa maoni ya wataalamu wa tiba. Mtazamo wa kijamii

ulimwongoza katika utambuzi wa mielekeo ya jamii kuhusu watu wenye ulemavu na maudhui yanayoendelezwa kupitia wahusika hawa. Franks alihakiki hadithi za kwanza themanini na tano ambazo wahusika wake ni binadamu. Katika hadithi hizi aliainisha wahusika wenye ulemavu wa viungo na ulemavu wa akili. Kadhalika, aliwaainisha wahusika hawa katika misingi ya kijinsia. Alichunguza namna walivyochorwa kwa kuangalia sifa na nafasi zao katika uwasilishaji wa maudhui mbalimbali. Alitambua kuwa kulikuwa na idadi kubwa ya wahusika wenye ulemavu katika hadithi hizi wakiwemo wanaume, wanawake na watoto.

Kutokana na utafiti wake, Franks (2001) alibainisha kuwa ulemavu unatumiwa na mwandishi kuyaweka wazi masuala ya jamii ambayo hayaonekani waziwazi. Kadhalika, ulemavu umetumika katika hadithi hizi kama kipaza sauti cha watu wenye ulemavu kwa lengo la kuwazindua wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanayowakabili maishani. Utafiti wa Frank una mchango katika utafiti huu kwa kuwa alichanganua maudhui yanayoendelezwa katika hadithi teule kupitia kwa ulemavu. Aidha, alibainisha kuwa matumizi ya ulemavu yalikuwa kigezo muhimu katika kuyaweka masuala ya jamii ambayo hayakudhihirika wazi; jambo ambalo linaoana na malengo ya utafiti huu. Kadhalika, utafiti wa Franks ulimpa mtafiti mwongozo kuwa matumizi ya taswira za ulemavu katika kazi ya fasihi yanaweza kutumika kama sauti ya kuwahamasisha wanajamii kuhusu masuala yanayowakabili watu wenye ulemavu. Tofauti ya utafiti huu na ule wa Franks ni kuwa umeshughulikia riwaya za Kiswahili, na kuchunguza ni kwa namna gani masuala mbalimbali katika jamii yameangaziwa kupitia kwa matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa mwandishi. Kadhalika malengo ya utafiti wa Franks na misingi ya kinadharia aliyotumia ni tofauti na ya utafiti huu.

Devlieger (1999) ameandika makala kuhusu miktadha ya kimaisha na kimaana inayojitokeza katika methali hamsini na tano zinazohusu ulemavu. Amezingatia lugha kutoka nchi za Malawi, Senegal, Tanzania, Zambia, Zaire, na Zimbabwe. Devlieger ameshughulikia methali katika lugha hizi na kubainisha maana yake ya nje na ya ndani. Katika makala yake anatambua kuwa matumizi ya lugha ya kisasa kuhusu ulemavu katika Afrika huashiria mabadiliko katika mitazamo ya watu kuhusu ulemavu. Aidha, anatambua kuwa ulemavu kama tukio unahusisha taashira nzito. Devlieger anabainisha kuwa kwa upande mmoja, mtu mwenye ulemavu anadhihirisha taashira ya maisha yenye matumaini, ubunifu na maadili ilhali kwa upande mwingine ulemavu umewasilishwa kama uovu ambao chanzo chake lazima kichunguzwe. Tofauti na Devlieger aliyeshughulikia methali katika makala yake, utafiti huu umeshughulikia utanzu wa riwaya. Utafiti wa Devlieger ulichangia utafiti huu katika kubainisha kuwa wahusika wenye ulemavu wanaweza kutumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya kimaadili. Aidha, utafiti wake ulichochea mtafiti ili kudadisi kiini na mwingiliano wa ulemavu wa akili na ulemavu wa tabia na hivyo basi kuwahamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa kuchunguza kiini cha ulemavu huu badala ya kuwalaumu na kuwatenga watu walioathiriwa.

Ogechi na Ruto (2002) wameandika makala kuhusu ulemavu kama unavyosawiriwa katika majina na methali za jamii za Ekegusii na Nandi. Wamejadili mitazamo mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu kwa kuchanganua mfumo wa kupatiana majina na methali katika lugha za Ekegusii na Nandi zinazozungumzwa nchini Kenya. Katika makala yao, wanadai kuwa mitazamo mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu na nafasi wanazopewa katika jamii ni mambo yanayoongozwa na mifumo ya imani zao asilia. Wanatambua kuwa katika jamii hizi mbili ulemavu wa aina mbalimbali unaelezwa kikamilifu ukiwemo ulemavu wa akili na ulemavu wa viungo.

Jamii hizi zinawaona watu wenye ulemavu wakiwa sawa na wengine ila wenye tofauti kimaumbile. Kadhalika, wanajamii wana imani kuwa kila hali, ikiwemo ulemavu ina chanzo maalum. Kwa mfano, ulemavu huenda ukamkumba mtu ikiwa wahenga au mababu wa zamani hawakufurahishwa na jambo fulani. Katika jamii za Ekegusii na Nandi, watu wenye ulemavu wakati mwingine hupewa majina yanayooana na ulemavu wao. Majina haya yanaweza kutumiwa na wanajamii kwa muda mrefu kuwatambua watu hawa hivi kwamba majina yao halisi yanatoweka na haya yakawa majina yao halisi yanayowatambulisha. Katika utafiti wao, Ogechi na Ruto walizingatia swala la ulemavu kwa kujikita kwenye utamaduni na imani ya jamii kuhusu watu wenye ulemavu na nafasi zao. Hata hivyo, mbali na hali ya ulemavu, hawajafafanua vigezo vinginevyo vilivyochangia katika kuibua majina husika. Utafiti huu umechunguza namna taswira mbalimbali za ulemavu zimetumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui kwa kuzingatia mazingira mbalimbali ya kijamii na kitamaduni yaliyotawala kazi husika. Ingawa utafiti wa Ogechi na Ruto ulijikita kwenye methali ulichangia katika usuli wa utafiti huu ambapo inabainika kuwa dhana ya ulemavu inaoana na tamaduni, mila na desturi za jamii. Kadhalika, kama walivyogundua Ogechi na Ruto kuwa jamii inaamini kwamba ulemavu ni adhabu ya uovu fulani, utafiti huu ulibainisha kuwa katika riwaya teule wanajamii walikuwa na mtazamo kuwa baadhi ya aina za ulemavu kama vile utasa, ugumba na ubongomaji ulikuwa adhabu.

Kisanji (1998) alichunguza elimu ya jumla kwa kuzingatia sanaa ya jadi ya Kiafrika, hasa usimulizi wa ngano. Alichunguza methali, nyimbo za kitamaduni, mashairi, ngano na vitendawili vinavyohusiana na ulemavu kutoka Tanzania, Liberia, Zaire na Zambia. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya ufasiri wa dhana kijazanda. Nadharia ya ufasiri wa dhana kijazanda inajikita katika msingi kwamba dhana

hutawala namna binadamu anavyofasiri mambo na kuhusiana na wengine. Aidha, dhana mbalimbali hutawala fikra za binadamu na utendaji wake. Kwa mujibu wa nadharia hii, jazanda si kipengele cha lugha bali ni kipengele cha fikra. Lengo la utafiti wa Kisanji lilikuwa ni kubainisha mitazamo kuhusu ulemavu katika jamii za Kiafrika na mielekeo yao kuhusu watu wenye ulemavu kama msingi wa kubainisha usawa wa makundi mbalimbali ya kijamii. Alifanya hivi kwa kuchunguza namna lugha inavyotumika kijazanda katika fasihi simulizi ya Kiafrika inapowarejelea watu wenye ulemavu.

Kisanji alijikita katika sanaa ya jadi katika utafiti wake na kuangalia nafasi ya wahusika walemavu katika jamii. Tofauti na utafiti wa Kisanji, lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza matumizi ya ulemavu kimtindo kwa kuchanganua utanzu wa riwaya. Hata hivyo, uchunguzi wake uliufaidi utafiti huu kwa kuwa jazanda zilitumika kama kipengele cha kufasiri mitazamo mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu. Jazanda ni mbinu iliyoshirikishwa pia katika utafiti huu hasa katika kubainisha lugha inayotumiwa na wahusika wanaodhihirisha ulemavu wa akili.

Muundo wa majina na methali za Kiswahili huwadhalilisha watu wenye ulemavu. Haya ni kwa mujibu wa makala yaliyoandikwa na Waliaula (2009). Makala hii ilizingatia matumizi ya kiambishi awali *'k*i-', katika muundo wa kiisimu wa lugha ya Kiswahili na jinsi unavyoingiliana na ulemavu pamoja na athari zake katika ufasili wa ulemavu. Waliaula alitathmini namna muundo huu unavyoathiri uwasilishaji, ufafanuzi na usawiri wa dhana ya ulemavu. Makala yake yalijikita zaidi kwenye nafasi ya mtu mwenye ulemavu katika muundo wa majina na methali za lugha ya Kiswahili na namna ambavyo majina na methali hizi zinavyowachora watu wenye ulemavu. Alitambua kuwa matumizi ya kiambishi *ki-* katika *ki-lema*, *ki-pofu*, *ki-wete*,

*ki-ziwi*, *ki-gugumizi*, *ki-chaa*, *ki-guru* na *ki-tembe* kabla ya mzizi wa neno ni dhalilishi na inashusha hadhi ya mrejelewa. Kwa upande wa methali za Kiswahili, Waliaula alipata kuwa methali hizi kijuujuu zinaonekana kuwapendelea watu wenye ulemavu. Zinawasawiri kama watu wenye ujuzi wa hali ya juu na watu wa kuigwa katika ujitoshelezaji wa mtu binafsi. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa baadhi ya wahusika wenye ulemavu waliorejelewa katika utafiti huu kama vile: Mzee Gae katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, Kabi katika riwaya ya *Utengano* wanasawiriwa kama wahusika wanaochangia katika kuleta mabadiliko ya kisiasa na kijamii. Ingawa amegusia kidogo namna ambavyo methali za Kiswahili zinawasawiri watu wenye ulemavu, hajaendeleza utafiti wake ili kuchunguza ujumbe mpana zaidi unaowasilishwa kupitia methali hizi. Utafiti huu ulinuia kuziba pengo hili kwa kuangalia namna ulemavu umetumiwa kama mtindo wa mwandishi wa kuwasilisha ujumbe kwa wanajamii. Kadhalika, utafiti wake umeegemea zaidi katika kutambua nafasi ya watu wenye ulemavu katika jamii, suala ambalo ni la kisosholojia zaidi ilhali utafiti huu ulizingatia mtazamo wa kifasihi kwa kushughulikia mtindo.

Uhusiano uliopo kati ya utamaduni na uhusika wa watu wenye ulemavu kama unavyojitokeza katika sanaa ya jadi ya Kenya na muziki maarufu umeangaziwa na Mungai (2009). Katika makala aliyoandika, Mungai anazingatia sanaa ya jadi ya Kikikuyu, Kiacholi, Kidinka, Kiteso na Kilingala. Anabainisha kuwa ingawa utamaduni wenye umaarufu hauzingatii utabaka, thamani yake ambayo ni sehemu muhimu katika fasihi simulizi ina nafasi kubwa katika uelewaji wa desturi na suala zima la ulemavu. Mungai anadhihirisha kwamba katika tamaduni nyingi ulemavu unajitokeza kama hali ambayo mwathiriwa anastahili kuwa nayo, kwa kuwa inaonekana kama adhabu mwafaka. Kauli hii inaathiri kwa kiasi kikubwa fikra kuhusu suala la ulemavu katika tamaduni nyingi za nchi ya Kenya. Kadhalika,

anasema kuwa Wakenya bado wanashangazwa na ulemavu na kwamba majina hasi yanatumiwa kuwatambua watu wenye ulemavu na hivyo basi kuwatenga na watu wengine. Kwa upande wa muziki maarufu, Mungai anatambua kuwa hali ya ulemavu inaashiriwa kuwa mbaya zaidi kuliko hata umaskini na kwamba suala la uana limeingizwa katika swala la ulemavu ambapo mwanamume mwenye ulemavu anaonekana kuwa mnyonge na kudhalilishwa namna ambavyo; mwanamke anadhalilishwa katika tamaduni mbalimbali za Kiafrika. Hoja hii inaoana na matokeo ya utafiti wetu hasa inapodhihirika kuwa watu wenye ulemavu walikuwa wanadhalilishwa na kudumishwa. Kwa mfano mhusika Kapinga katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* anaposhindwa kushiriki kitendo cha ngono na mkewe, jamii ilimdhalilisha na kudai kuwa hakuwa mwanamume kamili. Aidha ulemavu wa kutokuwa na uwezo wa kupata mtoto uliowakumba Bigeyo na mumewe Ndalo, uliwafanya wataabike kimawazo na kupoteza mali nyingi katika jitihada za kutafuta matibabu, ishara kuwa walionekana kama watu waliokuwa na upungufu.

Utafiti wetu ulishughulikia matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya mwandishi. Mungai (2009) amejihusisha na majina yanayowatambulisha watu wenye ulemavu kionomastiki na namna yanavyowabainisha katika jamii. Kadhalika, ameangalia usawiri wa watu wenye ulemavu katika muziki maarufu wa Kikikuyu. Kwa hivyo, utafiti huu ni tofauti na wake kwa kuwa ulikuwa wa kina zaidi na uliongozwa na nadharia mahsusi. Aidha utafiti huu ulishughulikia utanzu wa riwaya katika fasihi andishi.

### 1.7.3 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Tamthilia

*Mfalme Edipode* ni mojawapo ya tamthilia za zamani zaidi za Kigiriki. Mulready (2003) alichunguza jazanda zinazotumika katika tamthilia hii na uhusiano wake na

maudhui ya ujuzi na ujinga miongoni mwa jamii. Alitumia nadharia ya mtindo ambapo alihusisha jazanda mbalimbali na hali ya maisha ya binadamu kama vile mahusiano yake na wenzake, miungu na uharibifu wa mazingira. Jazanda mbalimbali zilizotumika katika tamthilia ya *Mfalme Edipode* zilichunguzwa kwa kuzingatia jinsi zinavyohusiana na mazingira na athari zake. Mulready alizingatia ulemavu wa kutoona kama jazanda ya ujuzi na ukweli na kutambua kuwa katika tamthilia hii ulemavu wa kutoona unachukua nafasi mbili. Kwanza, mwandishi anauwasilisha ulemavu huu kama ulemavu wa viungo unaowaathiri wahusika Edipode na Teresia. Pili, ulemavu huu umetumika kijazanda kupitisha ujumbe kuhusu mitafaruku, maovu na unyonge unaomkumba mwanadamu. Sofokile ametumia hali ya kutoona kwa Nabii Teresa kuashiria kuwa watu wanaweza kukosa kutambua uovu unaowazunguka katika jamii na hali hii inaweza kuwaletea madhara makubwa.

Katika tamthilia hii, matumizi ya kejeli yanajitokeza kupitia kwa mhusika Edipode ambapo licha ya kwamba ana uwezo wa kuona, hajitambui. Nabii Teresia ana ulemavu wa macho lakini ana uwezo wa kutambua uozo ambao umemzunguka Edipode na maisha yake. Hata hivyo, Edipode anapotambua ukweli wa mambo anajitia upofu ili asione tena. Kama anavyoendelea kusema Mulready, upofu wa Teresia unatumika kuashiria kuwa uwezo wa kuona hauna maana ikiwa binadamu hautumii vyema na kwamba sio lazima mtu awe hana ulemavu ili kuweza kuuelewa ulimwengu. Ameupa ulemavu wa kutoona maana zaidi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe mahsusi. Kadhalika, inabainika kuwa ulemavu si hali hasi wakati wote. Ingawa utafiti huu ulizingatia namna ulemavu umetumika kama njia ya kuwasilisha maudhui, unatofautiana na wa Mulready kwa kuwa utafiti huu ulichunguza riwaya teule za Kiswahili na jinsi ulemavu umetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Aidha, utafiti huu unajikita kwenye muktadha wa kijamii, kiuchumi na

kisiasa ambao ni tofauti na unaopatikana katika tamthilia ya *Mfalme Edipode.* Hata hivyo utafiti huu wa Mulready ulitufaa kwa sababu tulizingatia jinsi ambavyo aina mbalimbali za ulemavu zimetumiwa kama taswira zinazoendeleza maudhui tofauti yanayodhamiria kuielekeza jamii.

### 1.7.4 Matumizi ya Ulemavu katika Riwaya

Kwa mujibu wa Hinz na Teunissen (1985) tabia ya '*Hephaestus Complex'* inadhihirika katika riwaya ya '*Lady Chatterly's Lover*.' Katika riwaya hii, mama Constance ameolewa na Clifford Chatterly ambaye ana ulemavu wa viungo. Ulemavu huu aliupata wakati wa vita vya kwanza vya dunia. Mama Constance haridhishwi na mumewe kimapenzi kutokana na ulemavu wake na anajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na mfanyakazi wao mmoja kwa jina Oliver Mellows. Katika uhusiano huu anahisi kuwa anaridhika kama mwanamke ila anakiuka maadili ya jamii kwa kushiriki ngono nje ya ndoa. Kisa hiki kinadhihirisha kuwa ulemavu wa viungo unaweza kusababisha ulemavu wa tabia. Aidha, kwa kuzingatia mtazamo wa kisosholojia ulemavu wa mtu mmoja unaweza kuwaathiri watu wengine katika jamii. Kazi hii inahusiana na utafiti huu kwa kuwa inazingatia ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo na chanzo chake. Kazi hii imetufaa kwa kuwa imebainika ulemavu wa viungo una uhusiano fulani na ulemavu wa tabia, jambo ambalo limejitokeza katika utafiti wetu. Hata hivyo, tofauti na kazi hii, utafiti wetu umeshughulikia taswira za aina hizi za ulemavu kwa kuzingatia matumizi yake kimtindo katika riwaya za Kiswahili.

Kwa kuongozwa na nadharia ya soshiolojia, Wright (2006) anachunguza maadili ya wahusika wenye ulemavu katika kazi zilizoandikwa na Lawrence. Anadai kuwa katika kazi nyingi za fasihi zilizoandikwa na Lawrence ikiwemo riwaya ya '*Lady Chatterly's Lover'*, wahusika wengi wenye ulemavu wanapata taabu kupigania nafasi zao katika jamii. Aidha, wanapata changamoto wanapojaribu kujitambua na

kujithamini. Wright anatambua ulemavu wa wahusika kama taswira inayotumika katika kazi za fasihi kama mtindo mwafaka wa kuwasilisha maudhui katika kazi husika. Katika kuchunguza kisa cha '*Lady Chatterly's Lover'*, Wright amejishughulisha na ulemavu wa viungo ambao umesababisha ulemavu mwingine wa kijamii. Tofauti na uchunguzi huu, yeye ameshughulikia riwaya moja ya Kiingereza, ulemavu wa aina moja na namna unavyowaathiri wahusika kimaadili. Utafiti huu ulichunguza riwaya sita teule za Kiswahili. Aidha, utafiti huu ulijikita katika misingi ya nadharia ya semiotiki tofauti na nadharia ya kisoshiolojia iliyotumiwa na Wright. Uchunguzi wa Wright umeufaa utafiti wetu katika kubainisha namna ambavyo aina mbalimbali za ulemavu zinavyoweza kuingiliana, Kwa mfano, ulemavu wa akili unaweza kusababisha ulemavu wa tabia ambapo mtu hukiuka kaida za jamii kwa sababu amepungukiwa kiakili na hana uwezo wa kufanya maamuzi yenye urazini.

Usawiri wa watu wenye ulemavu katika fasihi ya Kimagharibi umejitokeza katika kazi za Beauchamp na Chung (2010) na Thompson (2017). Beuchamp na Chung wamechunguza nafasi ya wahusika katika fasihi ya Marekani ya kisasa kwa kuongozwa na nadharia ya ulemavu inayozingatia mtazamo wa kijamii. Nadharia hii inajikita kwenye msingi kwamba ulemavu si tatizo linalopatikana katika mtu binafsi ila linalotokana na mitazamo ya kijamii inayoongozwa na nguvu za kiuchumi na kisiasa. Beuchamp na Chung wanatambua kuwa kwa kiasi kikubwa fasihi ya kisasa ya Marekani imewachora wahusika walemavu wa kike na kiume kama wanaoogofya, wanaotengwa, wasioeleweka na wanaohitaji huruma. Kimsingi, wahusika hawa wametumiwa kuzua hali ya kusikitisha, woga au chuki. Beuchamp na Chung wamebainisha kuwa usawiri wa wahusika walemavu jinsi hii ni mtindo unaotumiwa na waandishi wa fasihi ya kisasa ya Marekani kuendeleza na kukuza maudhui ya ubaguzi. Kadhalika, sifa za wema, uzuri na ubaya zilizopewa wahusika hawa

zinatumiwa kuendeleza maudhui ya kimaadili katika jamii. Utafiti wao unajikita katika ubainishaji wa wahusika walemavu kwa kuzingatia misingi ya kisoshiolojia unaoegemea kwenye mielekeo na mitazamo ya kijamii kuhusu watu wenye ulemavu na nafasi yao katika jamii kwa jumla. Utafiti huu ni tofauti na huo kwa kuwa ulizingatia taswira mbalimbali za ulemavu na kubainisha namna zinavyotumika kimtindo katika riwaya teule za Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya mtindo na ya semiotiki. Kwa hivyo unaegemea kwenye misingi ya kifasihi badala ya msingi wa kisoshiolojia. Hata hivyo matokeo yao yanayodhihirisha kuwa wahusika wenye ulemavu wabnatumiwa kuendeleza maudhui  ya maadili ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa unazingatia maudhui ya maadili kama mojawapo ya maudhui yaliyokuzwa kupitia kwa taswira za ulemavu.

Katika kitabu alichoandika kuhusu ulemavu wa macho na namna unavyodhihirishwa katika fasihi ya kibunifu ya Kifaransa, Thompson (2017), amesema kuwa usawiri wa ulemavu wa macho katika fasihi hii inadadisi mitazamo iliyopo katika jamii kuhusu ulemavu. Mitazamo ya Kimagharibi kuhusu ulemavu wa macho ni hasi. Thompson anasema kuwa badala ya jamii kuuchukulia ulemavu kama hali inayokandamiza, tanzia au majaaliwa, waandishi wa fasihi bunifu ya Kifaransa wanausifu ulemavu. Kwa mfano, waandishi wa riwaya wanauchukulia ulemavu kama kifaa muhimu cha kisanaa na kibunifu kinacholeta upya na upekee katika kueleza masuala halisi yanayoikumba jamii. Kuwepo kwa wahusika wenye ulemavu wa macho katika kazi ya fasihi kunamwezesha msomaji kujihusisha na ulimwengu kwa njia ya kihisia na ya kipekee. Maoni ya Thompson yanaoana na utafiti huu kwa kuwa anaelezea kuhusu nafasi ya ulemavu wa macho katika kuwasilisha maudhui kwa namna ya kipekee. Hata hivyo utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umejikita katika muktadha tofauti wa Kiafrika. Aidha, utafiti huu unazingatia taswira zingine za ulemavu.

Irwin na Moeller (2010) wamechunguza usawiri wa ulemavu katika riwaya za michoro za vijana. Uchunguzi wao unajikita katika misingi ya imani chapwa za kiasili zinazoshikiliwa na jamii kuhusu watu wenye ulemavu. Walitafiti riwaya thelathini zilizoteuliwa kimaksudi kulingana na malengo ya utafiti wao. Katika riwaya hizi wanachunguza namna ambavyo wahusika mbalimbali walivyosawiriwa. Irwin na Moeller wanatambua kuwa katika riwaya hizi wahusika wenye ulemavu katika jinsia zote wamewakilishwa. Hata hivyo wengi wa wahusika hawa wamechorwa kwa njia hasi. Wahusika wa kiume pekee ndio waliochorwa kama wahusika waovu ilhali wa kike wamesawiriwa kama wanyonge na wanaohitaji huruma. Tofauti na uchunguzi wa Irwin na Moeller unaochunguza riwaya za michoro, uchunguzi huu ulishughulikia riwaya sita teule za Kiswahili. Aidha, uliongozwa na nadharia mbili; ya mtindo na ya semiotiki. Utafiti wa Irwin na Moeller ulichangia katika utafiti wetu kwa kuwa suala la imani chapwa kuhusu watu wenye ulemavu limejitokeza katika utafiti wetu na hivyo basi utafiti huu ulitoa mwelekeo mwafaka katika utambuzi wa imani hizi.

### 1.7.2 Matumizi ya Ulemavu kama Mtindo katika Vyombo vya Habari

Barnes (1992), alichunguza matumizi ya tamathali za usemi zinazolemaza katika vyombo vya habari. Alizingatia imani za kiasilia zisizo na msingi wowote kimantiki, kuhusu watu wenye ulemavu, zinazojitokeza katika vyombo vya habari. Ili kufanikisha malengo ya utafiti wake alichunguza vitabu, filamu, magazeti, majarida pamoja na vipindi mbalimbali vya runinga na redio. Anatambua kuwa mambo mengi yanayojitokeza katika vyombo vya habari kuhusu ulemavu ni hasi mno. Imani zinazolemaza zinadhihirika ambapo watu wenye ulemavu wanasawiriwa kama viumbe ambao si binadamu kamili, wanaohitaji matibabu kila wakati, wategemezi na wahalifu. Kadhalika wahusika wenye ulemavu wanajitokeza kama vifaa vya kejeli katika michoro ya vibonzo, filamu na vipindi vya vichekesho katika runinga.

Wanachorwa hivi ili kuashiria hali ya unyonge, umaskini na uovu. Aidha, wanatumiwa kama mbinu ya kukuza hali ya taharuki. Maisha yao yamezungukwa na mambo ya miujiza yasiyoeleweka na watu wengine. Utafiti wa Barnes ni tofauti na huu kwa kuwa yeye anachunguza usawiri wa watu wenye ulemavu katika vyombo vya habari na jinsi usawiri huo unavyowalemaza watu hawa; ilhali uchunguzi wa taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe ndilo suala kuu lililochunguzwa katika utafiti huu. Mitazamo hasi kuhusu watu wenye ulemavu ni jambo ambalo lilijitokeza katika utafiti wetu. Kwa hivyo, utafiti wa Barnes ulidhihirisha uwiano wa kimtazamo unaopatikana katika jamii nyingi kuhusu watu wenye ulemavu na ulikuwa mwongozo uliomfaa mtafiti katika kuainisha sifa za watu wenye ulemavu kwa mujibu wa maoni ya jamii katika riwaya zilizochunguzwa.

Mathooko na wengine (2012) wameandika makala kuhusu nafasi ya watu wenye ulemavu katika vyombo vya habari. Wamezingatia hadithi zinazohusu ulemavu na watu wenye ulemavu na picha zinazoambatana na hadithi hizo. Katika makala yao, wamesema kuwa picha na hadithi zinazopatikana katika vyombo vya habari huathiri fikra za watu na huibua mitazamo fulani ya jamii. Aidha, watu wenye ulemavu wanaporejelewa katika vyombo vya habari wanasawiriwa kwa njia inayoonyesha kutengwa na kwa njia isiyo na uhalisia. Wanachorwa kama viumbe wenye uwezo wa kupindukia au watu wanaofaa kuhurumiwa tu. Makala ya Mathooko na wenzake imejikita katika mtazamo wa jamii kuhusu ulemavu kama unavyodhihirika katika vyombo vya habari ilhali utafiti huu ulijikita katika uchunguzi wa taswira za ulemavu kama mtindo katika riwaya teule za Kiswahili. Maoni kuwa watu wenye ulemavu ni wanyonge na wanafaa kuhurumiwa ni hoja muhimu katika utafiti huu kwa kuwa sifa hii ilimwongoza mtafiti katika kutambua wahusika wenye ulemavu ambao walidhihirisha sifa kama hizi.

Tofauti na utafiti huu ambao ulizingatia ulemavu kama mtindo wa mwandishi, tafiti hizi zinazochunguza vyombo vya habari zilijikita zaidi katika maudhui ya unyonge na dhuluma dhidi ya watu wenye ulemavu na nafasi yao katika jamii.

**1.8 Msingi wa Nadharia.**

Kama anavyosema Burton (1992), uchambuzi wa mtindo ni nyenzo muhimu katika kuelewa uhalisia wowote unaozuka kutokana na lugha. Mtindo unahusika na uchambuzi wa lugha pamoja na mbinu mbalimbali zinazotumiwa na mtunzi katika kazi yake. Uchaguzi wa mtindo unaotumiwa na mwandishi katika kazi yake hutegemea utamaduni wa jamii na mazingira ambapo kazi husika imeibuka. Wales (2001) anasisitiza haya kwa kusema kuwa lengo la kutumia mitindo tofauti siyo tu kufafanua vipengele rasmi vya matini ila ni kudhihirisha uamilifu na umuhimu wake katika ufasili wa matini.

Kimsingi, uhakiki wa mtindo unajikita kwenye matumizi ya vipengele vya lugha katika kazi ya fasihi. Uchanganuzi huu mara nyingi hauzingatii masuala ya kijamii, kisiasa, kimtazamo, kihisia, kitamaduni na kisaikolojia. Utafiti huu unajikita kwenye mtazamo kuwa fasihi haiwezi kujitenga na jamii ambapo inapatikana na hivyo basi mhakiki anastahili kuzingatia jamii husika anapochambua mtindo na maudhui katika kazi yoyote ile. Utafiti huu unajihusisha na uchambuzi wa mtindo siyo tu kama kipengele kinachoongeza mvuto katika kazi ya fasihi bali kama kipengele kinachomfanya msomaji kutafakari zaidi kuhusu ujumbe uliokusudiwa na mwandishi kwa njia ya kipekee. Kwa hivyo uchunguzi huu unazingatia kipengele cha mtindo ambacho hakijitokezi moja kwa moja kati ya vipengele vya mtindo vinavyoshughulikiwa na wahakiki wengi.

Kwa kuwa kazi ya fasihi huwasilisha masuala yanayoiathiri na kuizunguka jamii, utafiti huu unachukulia kuwa hali mbalimbali zinazoizinguka jamii zinaweza kuashiria maudhui yanayowasilishwa na mwandishi. Ulemavu ni mojawapo ya hali hizi. Utafiti huu unajikita kwenye mtazamo kuwa taswira za ulemavu zinaweza kutumiwa kuashiria maana mbalimbali zinapotumika kama mtindo na hivyo basi kuwasilisha jumbe mbalimbali katika kazi ya fasihi.

Kwa kuzingatia haya, utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya mtindo na nadharia ya semiotiki.

### 1.8.1 Nadharia ya Mtindo

Nadharia ya mtindo inajikita zaidi kwenye uchunguzi wa lugha kwa lengo la kubainisha ubunifu uliopo katika lugha. Kulingana na Crystal na Davy (1969), uchunguzi wa lugha una mchango mkubwa katika kuelewa matini na kufahamu ujumbe unaowasilishwa katika kazi za fasihi. Kimsingi, nadharia ya mtindo ina mwelekeo wa kifani na inalenga kuchunguza mtindo wa matini za kifasihi. Nadharia ya mtindo na utendaji kazi wake inaweza kuibua mitazamo mbalimbali inayosisitiza mambo tofauti. Mitazamo hii imeibua maana mbalimbali ya dhana ya mtindo kutegemea dhima ya vipengele tofauti vya kimtindo. Kuna wataalamu wanaosisitiza kuwa mtindo ni kipengele cha kutathmini kazi ya mwandishi na wengine wanaodai kuwa mtindo ni kipengele kinachodhihirisha upekee wa mwandishi. Mtindo unapotumiwa kama kipengele cha kutathmini kazi ya mwandishi mhakiki hutalii mtindo wake na kuuweka wazi ili kubainisha ufanisi wa mwandishi katika matumizi ya mtindo husika. Mtindo kama upekee wa mwandishi huzingatia namna ambavyo mtindo wa mwandishi mmoja unavyomtofautisha na mwandishi mwingine. Kwa hivyo, matumizi ya taswira za ulemavu ni mtindo mojawapo wa kipekee unaoweza kutumiwa na mtunzi katika kuwasilisha maudhui.

Mtazamo wa kimtindo uliwekewa msingi na maandishi ya Aristotle katika ya *The Rhetorics* ambapo aina tatu za mbinu za ushawishi zimezungumziwa. Arstotle anadai kuwa ushawishi unaweza kutokea kwa kutumia wahusika, utekaji wa fikra na hisia. Nadharia hii inaweza kutumiwa kuchunguza mtindo wa kinachosemwa au kuwasilishwa na jinsi kinavyosemwa au kinavyowasilishwa, yaani fani na maudhui ya kazi ya fasihi. Wanamtindo hujihusisha na uchunguzi wa namna lugha inavyotumiwa katika fasihi.

Kwa kuzingatia maoni ya Leech na Short (1981), mihimili ya nadharia ya mtindo ni kama ifuatavyo. Mhimili wa kwanza ni kuwa mtindo una uhusiano na dhima yake kisanaa. Suala muhimu zaidi la mtindo linahusu ujumbe ambao mwandishi anataka kuwasilisha na namna anavyouwasilisha. Mhimili mwingine ni kwamba mtindo unahusu namna mwandishi anavyoyapamba mawazo yake na kuyawasilisha. Leech na Short wanadai kuwa mtindo una sifa ya uwili kwa kuwa ujumbe mmoja unaweza kuwasilishwa kwa njia tofauti. Wanasema kuwa mtindo unajikita katika jinsi lugha inavyotumika siyo umilisi wake. Ni namna mwandishi anavyoamua kutumia lugha katika utanzu na matini fulani. Mtindo unaweza kubainishwa kutokana na vipengele kama vile usimulizi, matumizi ya lugha na mbinu mbalimbali za uandishi. Ili kubainisha mtindo wa mwandishi, mhakiki hudadisi mambo yafuatayo: lugha iliyotumika ni ya namna gani (rahisi, ngumu, urefu/ufupi wa sentensi, matumizi ya lahaja, matumizi ya tamathali za usemi), kuwepo kwa matumizi ya mbinu mbalimbali za kiuandishi (barua, ndoto, dayolojia, uzungumzi nafsi), kuwepo kwa mchanganyiko wa tanzu na nafsi iliyotumika katika usimulizi. Mambo haya ndiyo yanayobainisha mtindo katika kazi ya fasihi simulizi. Kimsingi, mtindo hujihusisha na lugha ya fasihi na dhima yake katika kazi ya fasihi. Mihimili hii ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ilimwongoza mtafiti kubaini taswira mbalimbali za ulemavu zilizotumika katika

riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi na dhima yake katika riwaya husika.

Kulingana na Leech na Short (1981), matumizi ya viashiria mbalimbali yanategemea ubunifu wa mwandishi na ufasili wa msomaji. Dhana ya uashiriaji wa kitu kimoja kwa kutumia viashiria tofauti inadhihirika katika matumizi ya mitindo tofauti. Vipengele tofauti vya kiisimu vinaweza kutumika kuelezea ujumbe unaofanana. Mhimili huu uliuongoza utafiti katika kubainisha taswira mbalimbali za ulemavu zilizotumika na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi katika kuwasilisha maudhui mbalimbali yanayopatikana katika riwaya teule.

Welleck na Warren (1982) wanaeleza taswira kama chochote kile kinachofanana na kitu au jambo fulani, ni picha bayana ya kimawazo. Picha na ishara ni mbinu za kimtindo ambazo msanii hutumia kuifinyanga kazi yake. Kwa hivyo, lugha inaweza kutumika kwa namna fulani ili kutimiza lengo fulani la kisanaa. Aidha, mwandishi ana uhuru wa kuchagua taswira atakazotumia kuwasilisha ujumbe wake. Matumizi ya vipengele tofauti vya kiisimu huibua mitindo tofauti ya matumizi ya lugha. Vipengele hivi ni kama fonetiki, maumbo ya kisarufi, miundo ya sentensi na msamiati. Vigezo hivi ndivyo hudhihirisha kazi upekee wa mawasiliano.

Leech and Short (1981) wanasema kuwa taswira mbalimbali zinaweza kutambulika kupitia kwa vifaa, matendo, hisia, fikra, maoni, hali ya akili ya wahusika, na hali mbalimbali za kidhahania zinazojitokeza katika kazi ya fasihi. Msingi huu ulimwongoza mtafiti katika kubainisha taswira mbalimbali za ulemavu zinazojitokeza katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kwa kuzingatia matendo, fikra na maoni ya wahusika na hali za kidhahania zilizodhihirika katika riwaya teule.

Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), taswira zinapotumika katika kazi ya fasihi huwa na maana ya juu na maana ya ndani. Kwa hivyo, taswira zinatumika na mwandishi kimaksudi kama mbinu ya kuwasilisha maudhui mahsusi. Mhimili huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ulimwongoza mtafiti kubainisha maana ya ndani iliyowakilishwa na taswira mbalimbali za ulemavu na hivyo basi kutambua ujumbe uliowasilishwa kupitia kwa taswira hizi.

Mtindo una misingi yake katika dhana kwamba uamuzi wa mwandishi wa kutumia mtindo fulani huathiri msomaji kwa namna maalum. Aidha, mwandishi hudhihirisha uhusiano wa matumizi ya mtindo fulani na athari za mtindo huo kwa msomaji. Mhimili huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa kama wasemavyo Leech na Short taswira zinaweza kutambulika waziwazi hivi kwamba wasomaji wanaweza kupuuza dhima yake kuu katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo kwa mujibu wa utafiti huu, taswira za ulemavu zilitumika kama viashiria vya ujumbe fulani wala sio viwakilishi vya ulemavu kama kipengele cha maisha ya binadamu.

Kulingana na Leech na Short (1981), nadharia ya mtindo huzingatia mazingira ya mwandishi na tajriba yake. Aidha, mwandishi hutumia mtindo mahsusi kwa lengo la kutoa maarifa kuhusu maswala yanayopatikana katika ulimwengu halisi. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ilimwongoza mtafiti katika kutathmini mazingira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyoitawala jamii na nafasi yake katika uteuzi wa taswira za ulemavu kama mtindo.

Nadharia ya mtindo imechangia katika kutambua taswira mbalimbali za ulemavu zinazojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Hata hivyo, haingeweza kumwongoza mtafiti katika utambuzi wa jumbe mbalimbali zilizoashiriwa kupitia kwa taswira hizo. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza

namna ambavyo taswira za ulemavu zimetumika kama mtindo, kulikuwa na haja ya kubainisha maana iliyoashiriwa na taswira husika. Kwa kubainisha maana, mtafiti angeweza kutambua maudhui yaliyowasilishwa na waandishi wa riwaya teule. Ili kufanikisha jambo hili, kulikuwa na haja ya kutumia nadharia nyingine ambayo ingetumika kubainisha maana inayoashiriwa na taswira hizi. Maana hii ilimwezesha mtafiti kupata maudhui yaliyowasilishwa kupitia kwa taswira mbalimbali za ulemavu. Nadharia ya semiotiki ilimwezesha mtafiti kufikia lengo hili.

### 1.8.2 Nadharia ya Semiotiki

Uchanganuzi wa kisemiotiki unajikita katika makisio ya nadharia pana inayohusu ishara na viashiria zinazoundwa kutokana na maneno. Kwa mujibu wa Berger (2004), uchanganuzi huu unahusisha semantiki, sintaksia na pragmatiki. Uchanganuzi huu unaweza kuwa uchunguzi wa ishara na matumizi yake katika lugha na unaweza kutumiwa mahali popote ambapo kitu kimoja kinaonekana kuashiaria kingine.

Hippocrates, mwasisi wa sayansi ya tiba za Kimagharibi; ndiye aliyeibuka na istilahi ya semiotiki. Kwa mujibu wa Danesh (2002), Hippocrates alieleza semiotiki kama tawi la tiba linalochunguza ishara inayosimamia kitu kingine zaidi yake. Hata hivyo, uchunguzi wa namna ambavyo vitu huashiria vitu vingine ni suala lililofuatiliwa zaidi na wanafalsafa wakati wa kipindi cha Plato. Kama anavyoeleza Danesh, Plato alidai kuwa ishara ni vitu vinavyohadaa kwa sababu haviwakilishi uhalisia moja kwa moja. Alisema kuwa ishara huwa na vipengele vitatu: ishara yenyewe, kiashiriwa na maana inayoibuka. Danesh anakubaliana na maoni ya Plato kuwa kiashiria kisichokuwa na kiashiriwa hakina maana. Aidha, kiashiriwa hubadilika kulingana mtu anayekitumia na muktadha.

Danesh (2002) anasema kwamba John Locke, mwanafalsafa wa Uingereza ndiye mwasisi wa uchunguzi rasmi kuhusu ishara. Lengo lake lilikuwa kuhakikisha kuwa wanafalsafa wameelewa mwingiliano uliopo kati ya uwakilishaji wa maana na maarifa.

Danesh anaeleza kuwa katika karne ya ishirini, nadharia ya semiotiki iliendelezwa na wanasemiotiki, wanaisimu, wanasaikolojia na wananadharia wa kitamaduni. Miongoni mwao walikuwemo Roman Jakobson, Louis Hjelmslev, Jacques Lacan, Charles Morris, Claude Levi-Strauss na Jacques Derrida. Kama anavyosema Matthews (2017), misingi ya wataalamu hawa, semiotiki imekuwa kifaa muhimu katika uhakiki wa fasihi kwa kuwa inaunganisha matini ya kazi ya fasihi na ulimwengu wa ishara. Wanaisimu hawa wameibua maoni mbalimbali kuhusu dhana ya semiotiki. Hata hivyo, utafiti huu umejikita katika mtazamo wa nadharia ya semiotiki ya kisasa ambayo iliibuka kutokana na maoni ya mwanaisimu Mswizi, Ferdinard De Saussure. Saussure alieleza semiotiki kuwa ni sayansi inayochunguza dhima ya ishara kama sehemu ya maisha ya jamii na kwamba maana hutegemea miktadha inayorejelewa na mifumo mahsusi ya kodi.

Nadharia ya semiotiki inatambua kuwa usemi wowote wa binadamu huwa na uwezo wa kuibua maana mbalimbali na kwamba kiashiria chochote kinaweza kuwa na viashiriwa tofauti. Maana ya matini na maana yake halisi haiwezi kubainishwa moja kwa moja kwa sababu matini huweza kuibua maana nyingi. Mtazamo huu unaegemea kwa kiasi kikubwa kwenye mtazamo wa kiisimu wa Ferdinard De Saussure. Kwa mujibu wa Saussure, ishara ya kiisimu ina sehemu mbili: kiashiria na kiashiriwa. Katika mifumo tofauti ya lugha, ishara mbalimbali hudhihirisha utata uliopo katika ishara za kiisimu. Ishara huzua maana yake kutokana na tofauti yake na ishara

zingine. Ishara haimiliki maana kivyake ila hupata maana yake katika mfumo mzima wa lugha.

Mhimili mwingine wa nadharia ya semiotiki ni kuwa maana haiashiriwi kwa wasomaji ila msomaji mwenyewe ndiye huiunda maana kulingana na mwingiliano changamano wa misimbo ambayo kwa kawaida haitambuliki. Binadamu huishi katika ulimwengu wa ishara na hana njia ya kuelewa chochote bila ishara na misimbo ambayo kwayo maana hudhihirishwa. Ni muhimu kutambua kuwa hata ishara za kawaida hazidhihirishi maana yake moja kwa moja. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kufahamu maana ya ishara za ulemavu zinazotumika katika riwaya teule na ujumbe unaowasilishwa kupitia kwa ishara hizi.

Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki maana huundwa kupitia ubunifu na ufasiri wa ishara. Ishara huchukua umbo la: maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na vifaa mbalimbali. Vipengele hivi huwa na maana ya ndani na hutambulika kama ishara pale ambapo vinapatiwa maana. Chochote chaweza kuwa ishara mradi tu kitafasiriwa kuwa kinaashiria jambo fulani. Katika utafiti huu, ulemavu ulichukuliwa kama ishara inayosimamia maana zaidi ya hali ya kuwa na ulemavu.

Kama anavyodai Saussure (1916), ishara si kiunganishi kati ya kitu na jina, lakini ni kiunganishi kati ya dhana (kiashiriwa) na mpangilio wa sauti (ishara). Ishara lazima iwe na kiashiria na kiashiriwa. Kwa mfano; neno '*fungua*' linapoandikwa mlangoni mwa duka linaashiria kuwa duka limefunguliwa kwa minajili ya kufanya biashara, ikiwa lipo kwenye swichi ya mlango linaashiria kuwa pahali pale panahitaji kubonyezwa ili mlango ufunguke, ikiwa limeandikwa juu ya katoni linaweza kuashiria kuwa hiyo ndiyo sehemu ya kufungulia katoni. Hii ina maana kuwa maana hutokana na muktadha. Msingi huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa maana ya

taswira mbalimbali za ulemavu zilichunguzwa kulingana na muktadha wake katika riwaya husika.

Saussure (1916) anasema kuwa watu wanapozungumza kuhusu vitu, wana mitazamo yao kuvihusu na mitazamo hii ndiyo hutoa maana na kuleta sifa ya unasibu katika lugha. Unasibu wa ishara ni sifa inayoelekeza kwenye hali kuwa lugha haidhihirishi uhalisia kwa kuwa inaweza kutumika kusema mambo yakinifu na ya kidhahania.

Mtazamo wa Saussure wa unasibu wa ishara unawaongoza wanasemiotiki kusisitiza kuwa uhusiano kati ya kiashiria unategemea mifumo ya jamii ambayo watu hujifunza, na utamaduni wao. Neno huwa na maana kwa jamii ya watu kwa kuwa kuna makubaliano kuhusu maana hiyo na watu wamezoea maana hiyo. Namna jambo linavyowasilishwa na chombo kinachochaguliwa kuwasilisha jambo huathiri mwelekeo wa watu kukihusu. Ujumbe unaweza kuwa na zaidi ya maana moja na jumbe tofauti zinaweza kuwa na maana moja kutegemea muktadha ambapo ujumbe huo ulitolewa. Maana inayokusudiwa kuwasilishwa na ujumbe inaweza tu kubainishwa kwa kurejelea maana nyinginezo. Hoja hii ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu umechunguza utanzu wa riwaya ambao huwa na matini yenye mitindo mbalimbali na huhakikiwa kwa kuzingatia vipengele vyake vyote. Saussure anaendelea kusema kuwa maana ya matini huongozwa na muktadha wa kisaikolojia, kimazingira na kijamii ambapo matini imeibuka au inakorejelea. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kuchunguza muktadha wa kijamii, kiuchumi na kisiasa unaotawala riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi na nafasi yake katika uteuzi wa taswira za ulemavu kama mtindo.

Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, kiashiria halisi kinaweza kuzua maana ya moja kwa moja au maana fiche. Maana zinazozuka katika muktadha mahsusi huitwa

uashiriaji. Katika semiotiki basi, ulemavu katika hali halisi ni hali ya kibayolojia, kimatibabu na kijamii. Kutokana na hali hizi ulemavu ni kiashiria kwa kuwa ni hali inayorejelewa kulingana na jinsi inavyojitokeza. Hata hivyo kiashiria kinaweza kuwakilishwa kwa namna fulani kimakusudi. Katika utafiti huu, msingi huu ni muhimu kwa sababu taswira za ulemavu zilichunguzwa kwa mujibu wa maana mbalimbali zinazoibua.

Saussure (1916) anadai kuwa hatua za kuzua maana kutoka kwa uwakilishaji hufungwa na mifumo ya kijamii, tajiriba zinazofanana na hali zingine za kimuktadha zinazotawala maana mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika hali fulani. Mhimili huu ni muhimu kwa kuwa uliuongoza utafiti huu katika kutathmini mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yaliyokuwapo wakati riwaya zilizohakikiwa zilipochapishwa na nafasi yake katika uteuzi wa taswira za ulemavu kama mtindo wa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

Maoni ya Saussure yaliendelezwa na mwananadharia, mhakiki na mwanafalsafa wa Kifaransa kwa jina Roland Barthes. Barthes (1968) alichukulia kuwa semiotiki ni sehemu ya isimu na hivyo basi inaweza kutumika katika visasili, simulizi na uanahabari. Barthes alikuwa mhakiki wa kwanza kutumikiza semiotiki na kuiimarisha kutoka kwa isimu hadi kwa ishara zilizo dhahiri. Barthes anadai kuwa viashiria vina sifa zinazoibua maana mbili. Maana ya kwanza ni ile ya kimsingi au ya kawaida iliyo wazi. Maana ya pili ni maana fiche ambapo kiashiria huwa na uwezo wa kuibua maana ya ziada au maana zaidi kulingana na matumizi yake katika muktadha na jamii mahsusi. Ishara ni vitu vinavyopatikana katika hali halisi ya kawaida lakini zinapotumika kwa lengo la kutoa maana ya ziada vinachochea akili na hisia za msomaji wa kazi ya fasihi. Kwa kuzingatia maoni haya ya Barthes, utafiti huu ulijikita kwenye wazo kuwa matumizi ya taswira za ulemavu yalilenga kuzua maana

ya ziada kwa kuchochea fikra na hisia za wasomaji wa riwaya teule kwa namna ya kipekee.

Kwa mujibu wa Barthes, maana hupatikana katika mfumo mzima wa viashiria na haiwezi kudhihirika katika ishara moja pekee. Kigezo hiki kilikuwa mwongozo muhimu kwa mtafiti kwa kuwa utafiti huu ulichunguza ni kwa namna gani taswira mbalimbali za ulemavu zimetumiwa kuibua maana mbalimbali katika riwaya za Kiswahili teule zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti kutambua maana ya taswira mbalimbali za ulemavu zinazojitokeza katika riwaya teule na hivyo basi kutambua maudhui yaliyowasilishwa.

Kwa mujibu wa Barthes, lugha ni asasi ya kijamii inayotawaliwa na mfumo wa desturi, kaida na thamani za jamii. Kwa hivyo, ina vipengele vyake mahsusi vinavyojikita kwenye mfumo wa jamii. Hata hivyo, kauli zinazotolewa na mtu binafsi zinalenga kuwasilisha fikra zake; hivyo basi msemaji ana uhuru wa kujieleza kwa njia anayotaka. Msingi huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa waandishi wanaeleza kuhusu masuala ya kijamii kwa kutumia taswira mbalimbali za ulemavu kwa namna tofauti huku wakizingatia mifumo ya jamii husika. Hii ni kwa sababu taswira zinaweza kuwa na uhusiano fulani lakini zikawa na maana tofauti ya kiziada kulingana na matumizi yake kimuktadha na kufasiriwa kwa namna tofauti.

Barthes analisisitiza kuwa viashiria vyote hutegemea na huzua maana kutoka kwa mfumo mzima wa viashiria. Kadhalika, viashiria hufanya kazi katika muktadha wa kijamii, jambo linalowezesha viashiria visivyokuwa na sifa za kiisimu kupata maana. Ingawa taswira za ulemavu zinaweza kutambulika kupitia lugha, si taswira za kiisimu. Hata hivyo zinaweza kutumika kuwasilisha maudhui katika muktadha wa kijamii.

Katika utafiti huu maana zinazoibuliwa na taswira za ulemavu zinahusishwa na tamaduni ambapo zinapatikana.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu zimefafanuliwa. Mbinu zilizotumiwa katika kukusanya, kuainisha, kuchanganua data zimeelezwa. Kadhalika, katika sehemu hii, mbinu zilizotumiwa na mtafiti katika kuwasilisha matokeo ya utafiti huu zimeelezwa. Mbali na hayo, mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli, njia na vifaa vya kukusanya data vimeshughulikiwa.

#### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo kwa kuwa umejikita katika uchambuzi wa riwaya. Kama anavyodai Sukamolson (2007), utafiti wa kimaelezo unahusika na ufafanuzi kuhusu matukio ya kijamii. Utafiti huu huwasaidia watu kuuelewa ulimwengu wanakoishi na ni kwa nini mambo huwa jinsi yalivyo. Utafiti wa kimaelezo unahusu maoni, tajiriba na hisia za watu ambako data hukusanywa. Kadhalika utafiti wa kimaelezo hujikita kwenye vipengele vya kijamii. Kwa mujibu wa Crossman (2018), utafiti wa kimaelezo ni utafiti wa kijamii unaotumia data ambayo si ya kitakwimu. Utafiti wa kimaelezo unalenga kufasiri maana kutoka kwa data kwa nia ya kuelewa maisha ya kijamii kupitia uchunguzi wa makundi ya watu katika maingiliano yao ya kila siku. Utafiti huu ulilenga kufasili maudhui kwa kuzingatia ulemavu ambao ni kipengele cha jamii, na jinsi ambavyo umetumiwa kama mtindo. Kwa mujibu wa Crossman, mbinu mojawapo ya kufanikisha utafiti wa aina hii ni uchanganuzi wa maandishi. Kwa kuzingatia maoni haya utafiti huu ulijikita kwenye uchanganuzi wa riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

Utafiti huu ulifanywa kwa awamu mbili. Kwanza mtafiti alifanya utafiti wa awali, kisha akafanya utafiti halisi. Lengo la kufanya utafiti wa awali lilikuwa kubaini upatikanaji wa data ya kutosha ili kutosheleza mahitaji ya utafiti huu. Katika awamu hii ya kwanza mtafiti alisoma kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili zilizoandikwa na watunzi mbalimbali. Kazi zilizosomwa ni riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi. Lengo la kusoma kazi hizi lilikuwa kubainisha ni zipi kati ya kazi nyingi zilizoandikwa na watunzi hawa zinazodhihirisha matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa kuwa si kazi zote ambazo zimeshirikisha dhana ya ulemavu. Kadhalika, mtafiti alilenga kushirikisha kazi ambazo zimedhihirisha aina mbalimbali za ulemavu na ambazo zingekuwa na data ya kutosha kufanikisha utafiti huu. Utafiti wa awali ulimwezesha mtafiti kuteua utanzu ambao ulidhihirisha matumizi ya ulemavu. Utanzu ulioteuliwa ni wa riwaya. Aidha, mwandishi aliweza kubainisha ni watunzi gani kati ya watunzi wa riwaya za Kiswahili zilizosomwa waliokuwa wameshirikisha matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha jumbe zao. Kadhalika utafiti wa awali ulimwezesha mtafiti kuteua aina ya taswira za ulemavu ambazo zingeshirikishwa katika utafiti huu na hivyo basi kuboresha au kurekebisha mbinu za utafiti. Baada ya kufanya utafiti wa awali, mtafiti aliteua riwaya ambazo zilichambuliwa katika utafiti halisi kwa mujibu wa mada ya utafiti.

### 1.9.2 Mahali pa Utafiti

Kwa kuwa utafiti huu ni wa uhakiki wa riwaya, mahali pa utafiti palikuwa maktabani. Katika maktaba tasnifu, vitabu, makala, magazeti, majarida na maandishi mbalimbali yanayopatikana kuhusu mada ya utafiti yalisomwa. Kadhalika, mtafiti alidurusu mtandao na kusoma vitabu, makala, majarida na maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Lengo la kusoma maandishi haya lilikuwa

kubainisha ni mambo yapi yamewahi kuchunguzwa katika tafiti za hapo awali na matokeo yake yalikuwa yapi. Hii ilikuwa hatua muhimu kwa kuwa ilimpa mtafiti ufahamu zaidi kuhusu mada ya utafiti huu na mwanya anaonuia kuziba.

### 1.9.3 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulizingatia mbinu ya makusudi katika ukusanyaji data ambapo mtafiti alikusanya data iliyohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Ili kupata data, mtafiti alisoma riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi zilizoteuliwa baada ya utafiti wa awamu ya kwanza. Aidha aina mbalimbali za ulemavu zinazojitokeza katika riwaya teule zilitambuliwa ili kuweza kubainisha taswira mbalimbali za ulemavu zinazodhihirika.

Mtafiti alisoma riwaya hizi na kukusanya taswira zote za ulemavu ambazo zilidhihirika katika kila riwaya. Kwa kuongozwa na nadharia ya mtindo taswira mbalimbali za ulemavu zilibainishwa kutokana na vipengele kama vile usimulizi, matumizi ya lugha na mbinu mbalimbali za uandishi. Mtafiti alidadisi mambo kama vile: namna lugha ilivyotumika kitamathali, matumizi ya mbinu mbalimbali za kiuandishi (barua, ndoto, dayolojia, uzungumzi nafsi), kuwepo kwa mchanganyiko wa tanzu na nafsi iliyotumika katika usimulizi wa riwaya zilizochunguzwa. Baada ya kutambua taswira hizi, mtafiti aliziainisha katika makundi matatu makuu kutegemea namna zilivyodhihirika katika riwaya teule. Makundi haya ni: taswira za ulemavu wa akili, taswira za ulemavu wa viungo na taswira za ulemavu wa tabia.

Ili kutambua taswira za ulemavu, mtafiti alizingatia yale wanayoyasema wahusika wenye ulemavu, vitendo vyao, tabia na mienendo yao na mwonekano wao. Kadhalika, yale yanayosemwa na wahusika wengine wasio walemavuu na yanayosemwa na msimulizi kuhusu ulemavu, wahusika walemavu, vitendo, tabia na

mienendo yao yalichukuliwa kama data. Aidha, maudhui yanayowasilishwa kupitia kwa taswira mbalimbali za ulemavu yalichambuliwa na kuchukuliwa kama data. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulilenga kuchunguza namna ambavyo taswira hizi zimetumika katika uwasilishaji wa maudhui mbalimbali. Aidha, mtafiti alizingatia muktadha ambapo taswira za ulemavu zilijitokeza katika riwaya husika ili kubaini mazingira ya kisiasa na kijamii yaliyotawala nyakati mbalimbali ambazo riwaya hizi zinawakilisha.

### 1.9.4 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulichanganua riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Uteuzi wa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi ulitokana na namna ambavyo wanatumia mitindo mbalimbali ya uandishi katika riwaya zao ili kuwasilisha maudhui.

Kati ya riwaya nyingi ambazo wameandika ni riwaya sita pekee zilizoteuliwa kama sampuli katika utafiti huu: riwaya tatu za Said Ahmed Mohamed ambazo ni; *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano (1980)* na *Tata za Asumini* (1990) na tatu za Euphrase Kezilahabi**:** *Kichwamaji* (1974**),** *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Rosa Mistika* (1976). Uteuzi wa riwaya hizi ulifanywa kimaksudi baada ya utafiti wa awamu ya kwanza ambapo mtafiti alisoma riwaya mbalimbali za waandishi hawa kwa lengo la kubaini ni riwaya zipi ambazo zingetosheleza malengo ya utafiti na kumwezesha mtafiti kuwa na data ya kutosha. Kwa hivyo, riwaya hizi ziliteuliwa kama sampuli kwa kuzingatia kigezo kuwa taswira za ulemavu zimetumiwa kama mtindo katika riwaya husika. Katika uteuzi wa sampuli, mtafiti alizingatia taswira za ulemavu ambazo zilikuwa zimetumika kama mtindo peke yake. Taswira za ulemavu ambazo hazikuwa zinaegemea kwenye matumizi kimtindo hazikuzingatiwa.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu umeshirikisha mbinu ya maelezo kwa kiasi kikubwa katika uchanganuzi wa data. Kwa mujibu wa Hsieh na Shannon (2005), uchanganuzi wa kimaelezo unatumiwa ili kuchanganua na kuwasilisha data iliyokusanywa kupitia uchambuzi wa maandishi kwa lengo la kufupisha mambo yaliyomo katika data kwa kuzingatia maswali ya utafiti. Ujumbe unaopatikana huwasilishwa kwa njia elezi ambayo ni ya moja kwa moja kulingana na mahitaji ya utafiti. Mbinu hii ya uchanganuzi inalenga kufasiri maana kutoka kwa data iliyodondolewa moja kwa moja kutoka kwa matini. Kwa kuzingatia maelezo ya Hsieh na Shannon, data iliyokusanywa katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa kuzingatia namna waandishi husika wametumia taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali. Ili kuchanganua data kimaelezo, matini huwekwa katika sehemu au kategoria ndogo ndogo ili kumwezesha mtafiti kuiwasilisha kwa kifupi. Katika utafiti, huu data iliyokusanywa iliwekwa katika kategoria tatu ambazo ni taswira za ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo ili kumwezesha mtafti kuichanganua hatua kwa hatua.

Kwanza taswira mbalimbali za ulemavu zilizojitokeza katika riwaya teule zimefafanuliwa kwa undani ili kuelewa maana zinazosimamia au kudhihirisha kulingana na muktadha wa matukio katika riwaya husika. Ufafanuzi wa taswira hizi ulikuwa muhimu kwa kuwa kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki iliyouongoza utafiti huu, kiashiria kinaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Aidha, kulikuwa na haja ya kuthibitisha kuwepo kwa taswira mbalimbali za ulemavu kwa kueleza sifa za wahusika mbalimbali zinazoashiria kuwa walikuwa wameathirika na ulemavu.

Baada ya kutambua na kufafanua maana ya taswira za ulemavu zilizojitokeza katika riwaya teule, maudhui mbalimbali yaliyokuzwa na kuendelezwa na taswira za

ulemavu yamebainishwa. Kadhalika, mtafiti alieleza kwa kina maudhui haya na kufafanua jinsi ambavyo taswira za ulemavu zimetumiwa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui haya. Katika ufafanuzi wa maudhui, mtafiti alizingatia na kufafanua kwa tathmini mazingira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyotawala katika miktadha ya riwaya teule. Aidha, nafasi ya mazingira haya katika matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi ulitathminiwa.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na sababu za kuchagua mada. Kadhalika, malengo ya utafiti huu yameshughulikiwa pamoja na mbinu za utafiti zilizotumiwa. Mbinu hizi zimefafanuliwa kwa kuzingatia mahali ambapo utafiti ulifanyiwa, namna data ilivyokusanywa, jinsi sampuli ilivyoteuliwa na namna uchanganuzi wa data ulivyofanywa. Mbali na hayo tafiti na maandishi mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti yameshughulikiwa katika sura hii kwa kuzingatia mapengo yaliyoachwa na tafiti hizi na tofauti yake na utafiti huu. Kutokana na maandishi yaliyoangaziwa, imebainika kuwa hakuna utafiti uliofanywa hapo awali kwa kuzingatia nadharia na mbinu za utafiti zilizotumika katika kazi hii. Nadharia ya mtindo na semiotiki imeshughulikiwa katika sura hii. Kwa kuwa nadharia hizi zinahusu utambuzi wa mbinu za uandishi na uashiriaji wa maana, mihimili yake ilitumiwa kama mwongozo wa utafiti huu. Katika sura inayofuata matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui yatashughulikiwa kwa kuzingatia ulemavu wa akili.

# SURA YA PILI

# TASWIRA ZA ULEMAVU WA AKILI KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kubainisha namna ambavyo taswira za ulemavu wa akili zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Kulingana na Bogdan na wenzake (2012) ulemavu unaweza kutumiwa na mwandishi wa fasihi kwa namna mbalimbali ili kuwasilisha jumbe tofauti. Kwa kutumia taswira ya ulemavu wa akili mwandishi anawaathiri wasomaji wake kwa njia ya kipekee kuliko jinsi ambavyo angewaathiri iwapo angetumia lugha ya kawaida. Kama anavyosema Sanchez (2010), matumizi ya taswira ya ulemavu kama mtindo yanaweza kuathiri pakubwa namna ujumbe unavyowasilishwa na kupokelewa na hadhira inayolengwa na mwandishi. Kwa hivyo, matumizi ya taswira za ulemavu wa akili zimetumika na S. A. Mohamed na E. Kezilahabi kwa lengo la kuwasilisha maudhui yao kwa namna ya kufana zaidi.

Kulingana na Elran (2011), wahakiki wanapaswa kufahamu umuhimu wa taswira kama nyenzo ya kuwasilisha matatizo yanayowakabili wanadamu. Kwa hivyo, badala ya kuchukulia taswira za ulemavu wa akili kwa njia iliyo hasi, wahakiki wanapaswa kuzichunguza taswira hizi kwa kuzingatia muktadha wake. Elran anaendelea kusema kuwa waandishi wengi hutumia taswira za ulemavu wa akili kama njia ya kuwasilisha ujumbe na tajriba zao kwa njia ya kipekee. Katika uhakiki wa fasihi, taswira za ulemavu zina umuhimu mkubwa kwa mhakiki na kwa mwanahistoria kwa sababu zinaashiria mabadiliko ya kitamaduni na kihistoria. Hii ni kwa sababu mwandishi hutumia mtindo mahsusi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe kuhusu maswala yanayopatikana katika ulimwengu halisi wenye utamaduni na historia yake. Kama

wanavyosema Leech na Short (1981), matumizi ya mtindo mahsusi katika riwaya za kubuni huashiria mazingira ya mwandishi na tajriba yake. Leech na Short wanaendelea kusema kwamba fasihi ni njia ya kujieleza na hivyo basi mtindo wa mwandishi wa kujieleza huathiriwa na hali mbalimbali zinazomzunguka. Aidha, wanadai kuwa fasihi inaweza kutumiwa kama chombo cha kueleza maswala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni ambayo huenda hayawezi kuelezwa waziwazi kwa kutumia njia nyingine. Kwa hivyo, ili kuelewa malengo ya mwandishi na sababu zake za kutumia mtindo fulani mahsusi, mhakiki anahitaji kuzingatia hali halisi ya muktadha wa kijamii, kitamaduni na kisiasa iliyomzunguka mwandishi.

Kulingana na Mazrui (1978), fasihi ya Kiafrika ni chombo kinachokutanisha siasa na ubunifu wa Waafrika. Waandishi hutumia fasihi kama kifaa cha kupinga au kuunga mkono maamuzi fulani ya kisiasa ama kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii na kisiasa. Madai ya Mazrui, Leech na Short yanadhihirika katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Waandishi hawa wametumia taswira ya ulemavu wa akili katika kazi zao kwa lengo mahsusi. Ulemavu wa akili umetumiwa kama kiashiria cha ujumbe au maana fulani katika kazi teule.

Ingawa utafiti huu kwa jumla unashirikisha riwaya sita teule, ni riwaya tatu pekee zilizoshirikishwa katika sura hii kwa kuwa ndizo zinazodhihirisha matumizi ya taswira ya ulemavu wa akili kama mtindo. Riwaya hizi ni: *Dunia Mti Mkavu* na *Tata za Asumini* zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed na riwaya ya *Rosa Mistika* iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi.

### 2.1 Dhana ya Ulemavu wa Akili

Ili kuchanganua matumizi ya ulemavu wa akili katika riwaya teule, dhana ya ulemavu wa akili inahitaji kueleweka kwa mujibu wa matumizi yake katika sura hii. Hii ni kwa

sababu dhana hii inaweza kufasiliwa kwa namna mbalimbali. Kimsingi, dhana ya ulemavu wa akili huduwaza kwa kuwa inahusu maarifa. Maarifa ni jambo la kidhahania ambalo kimsingi huwa na vipengele muhimu vinavyohusu uhalisia wa binadamu. Kama anavyosema Freud (1920), tabia ya binadamu hutawaliwa na hali ya ubongo wake. Kwa hivyo, ni vigumu kueleza dhana ya tabia kwa kuwa ni swala la kisaikolojia. Freud anadai kuwa binadamu anapokumbwa na wasiwasi mkubwa, nafsi yake hutafuta mbinu za kukabiliana na hali hii bila mwenyewe kufahamu. Ingawa mbinu hizi zinamsadia mtu kupunguza wasiwasi alio nao, zinamlazimu kutafuta mbinu za kimantiki za kukabiliana na mambo yanayomvunja moyo. Jambo hili linaweza kumfanya mtu kuathirika na ulemavu wa akili ambapo anaanza kuwa na tabia ambazo zinaenda kinyume na za binadamu mwenye akili razini.

Kwa mujibu wa Prendergast (2001), Felman (2003) na Mackenzie (2014) ulemavu wa akili ni hali inayoashiriwa na tabia inayojirudiarudia. Tabia hii kwa kawaida huwa inaenda kinyume na matarajio ya wanajamii. Watu wenye ulemavu wa akili aghalabu hukinzana na wanajamii wengine kitabia na kimawazo. Mackenzie anaeleza kuwa baadhi ya dalili za ulemavu wa akili ni: kufanya mambo yasiyo na urazini, kutowajibika, chuki, ukataji tamaa na kukosa uwezo wa kufanya maamuzi mwafaka. Mackenzie anaendelea kusema kuwa watu wenye ulemavu wa akili hudhihirisha mielekeo na tabia ambazo hazizingatii mila, matarajio na mitazamo ya wanajamii. Aidha, tabia za watu wenye ulemavu wa akili hukiuka kaida na maadili ya wanajamii.

Prendergast (2001) anadai kuwa ulemavu wa akili ni suala linalozua mjadala miongoni mwa jamii, wataalamu na asasi mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu wa akili. Anatoa maoni kuwa ulemavu wa akili ni suala la

mjadala linaloweza kuelezwa, kusisitizwa na wakati mwingine kupotoshwa na wanajamii, wataalamu wa matini na miundo ya asasi mbalimbali za wanadamu wenyewe. Kwa hivyo, ulemavu wa akili unahitaji kufasiriwa katika muktadha wa jamii husika.

Kwa mujibu wa Foucault (1977) wanadamu kwa kawaida huwa ni wendawazimu na kwamba kutokuwa na kiwango fulani cha ulemavu wa akili kunaweza kuchukuliwa kama ishara mojawapo ya kuwa na wazimu. Foucault anaendelea kusema kuwa ulemavu wa akili huhusishwa na binadamu, upungufu wake, ndoto zake na matarajio yake. Aidha, anasema kuwa ulemavu wa akili umefafanuliwa kutoka zama za '*Hippocrates*' hadi wakati wa imani na desturi za Wamisri na Wamaya. Foucault anadai kuwa ulemavu wa akili si tukio la kawaida lisilobadilika ila ni hali inayojikita kwenye jamii ambapo inapatikana. Aidha, mifumo ya kitamaduni, kiuchumi na kimaarifa hubainisha jinsi ambavyo ulemavu wa akili hutambulika na kushuhudiwa katika jamii yoyote ile. Suala la utamaduni ni muhimu katika ufafanuzi wa dhana ya ulemavu wa akili na matumizi yake kama mtindo, kwa kuwa kama anavyosema Saussure (1983), maana ya ishara hutegemea mifumo ya jamii ambayo kwayo watu hujifunza pamoja na utamaduni wao. Kwa hivyo, taswira ya ulemavu wa akili inaeleweka kwa kuzingatia muktadha ambapo imeibuka.

Roberts (1980) anasema kuwa wanasaikolojia wanakisia kuwa chanzo cha ulemavu wa akili hupatikana ndani ya mwathiriwa. Ingawa Roberts anasema kuwa wanasaikolojia hawazichunguzi sababu za kijamii ambazo zinasababisha ulemavu wa akili bali wanachunguza sababu za kisaikolojia, inabainika kuwa kuna wanasaikolojia ambao wanashughulikia sababu hizi. Kwa mfano, Corrigan na wengine (2001) katika harakati za kujaribu kuelewa vizuri suala la ulemavu wa akili, wamechunguza uhusiano kati ya ulemavu wa akili na mielekeo ya jamii, tofauti za kikabila na

kutengwa kwa watu wenye ulemavu huu. Wanatambua kuwa kuna mtazamo kuwa watu wenye ulemavu wa akili hawawezi kujitunza na wanahitaji vituo maalum vya matibabu ambapo watashughulikiwa. Aidha, wanadhihirisha tabia za kitoto. Hata hivyo, fasihi huzingatia ufasiri mpana zaidi kuhusiana na chanzo cha ulemavu wa akili. Katika fasihi, ulemavu wa akili huchanganuliwa kimuktadha kwa kuzingatia hali mbalimbali zinazowazunguka wanajamii. Kama anavyosema Elran (2011), dhana ya ulemavu wa akili huchukuliwa kama hali inayoibua taswira ya mtu aliyechanganyikiwa kifikra na kimawazo. Aidha, mtu huyu huwa ni mwenye akili punguani na hana mpangilio mwafaka wa fikra na hisia. Katika mahusiano yake na wanajamii, mtu mwenye ulemavu hujitokeza kama aliyetengwa na jamii. Elran anaendelea kusema kuwa ili kuelewa umuhimu wa jazanda za ulemavu wa akili, mhakiki anapaswa kuzingatia matini, muktadha na hali ya kisaikolojia na simulizi mbalimbali kuhusiana na ulemavu wa akili kwa kuwa jazanda ni kipengele kinachobainisha mtindo katika kazi ya fasihi. Madai ya Elran ni muhimu kwa kuwa matini na muktadha wa matukio yalitumiwa kama data katika uhakiki wa matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

Kwa mujibu Saussure (1983) usemi wowote wa binadamu huwa na uwezo wa kuibua maana mbalimbali na kiashiria chochote kinaweza kuwa na viashiriwa tofauti. Hii ina maana kuwa ishara moja inaweza kuzua maana mbalimbali kutegemea matumizi yake kimuktadha. Maana inayoashiriwa inaweza kuwa ya moja kwa moja au maana fiche. Maana ya moja kwa moja ni ujumbe unaojitokeza waziwazi ilhali maana ya ndani huwa ni ya kijazanda na haiwezi kufasiliwa kijuujuu bila kuzingatia matumizi ya ishara husika kimuktadha. Saussure anaendelea kusema kuwa ujumbe unaowasilishwa

na taswira mbalimbali hujikita katika mifumo ya kijamii na miktadha inayoitawala kazi ya fasihi.

Kwa kuzingatia madai ya Saussure, taswira ya ulemavu wa akili inaweza kufasiriwa jinsi mbili. Kwanza ulemavu wa akili unaweza kuchukuliwa kama suala la tiba ambapo waaathiriwa huonekana kama wagonjwa wanaohitaji matibabu. Pili, ulemavu wa akili unaweza kufasiriwa kama jazanda ama ishara inayotumiwa na mwandishi ili kuwasilisha ujumbe mahsusi kwa njia fiche. Katika sura hii, ulemavu wa akili umefasiliwa kwa kuzingatia maana fiche kwa kuwa ulemavu huu umechukuliwa kama mbinu ya mwandishi ya kuwasilisha maudhui kwa njia ambayo si ya moja kwa moja. Ili kufanikisha lengo hili, wahusika wanaoashiria hali ya kulemaa kiakili kupitia kwa matendo, mawazo na tabia zao wameangaziwa kama data iliyotumiwa kuchanganua jinsi ulemavu wa akili unavyotumika kama mtindo wa mwandishi. Kadhalika, mambo wanayoyasema wahusika katika riwaya husika kuhusu wahusika wengine yanayoashiria kuwa wahusika hao wana ulemavu wa akili yamezingatiwa.

Kutokana na fasiri mbalimbali za dhana ya ulemavu zilizowasilishwa na wataalamu tofauti inabainika kuwa ulemavu wa akili unaweza kutumiwa kama ishara inayoibua maana mbalimbali. Kama anavyodai Saussure (1983), maana huundwa kupitia ubunifu wa maumbo mbalimbali yanayowakilisha ishara zinazoweza kufasiliwa kwa namna tofauti ili kupitisha ujumbe mahsusi. Katika sehemu inayofuata ulemavu wa akili utashughulikiwa kwa kuzingatia namna ambavyo umetumiwa na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kuwasilisha jumbe mbalimbali.

## 2.2 Ulemavu wa Akili kama Chombo cha Kutetea Haki na Usawa

Sehemu hii itashughulikia ulemavu wa akili na namna ambavyo umetumiwa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya kutetea haki na usawa katika jamii. Roberts

(1980), anaeleza kuwa matumizi ya taswira ya ulemavu wa akili katika fasihi unaweza kuwa nyenzo ya kupigana na unyanyasaji katika jamii. Ulemavu huu unaweza kuwa ufunuo unaohamasisha watu kuhusu uhalisia unaowazunguka.

Kulingana na Mlacha (1987), Said Ahmed Mohamed katika kazi zake nyingi anazungumzia kuhusu ukosefu wa usawa na migongano ya kitabaka katika jamii ya Kisiwa cha Unguja. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* Said Ahmed Mohamed amesawiri jamii ambayo imegawika katika misingi ya kitabaka ambapo kuna tabaka la matajiri na maskini wanaonyanyaswa. Kupitia kwa ulemavu wa akili uliomwathiri mhusika mkuu Mzee Gae, anawasilisha ujumbe mahsusi unaofungamana na uhalisi wa jamii. Katika sehemu hii ulemavu wa akili wa Mzee Gae umeangaziwa kama mtindo unaotumiwa na Said Ahmed Mohamed kuwasilisha maudhui yanayofungamana na harakati za kutetea haki na usawa katika jamii.

Kwa mujibu wa Ohly (1981) na Bertocini (1989), riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* inajikita katika muktadha wa Kisiwa cha Zanzibar. Zanzibar ilikuwa na makabila mbalimbali na ilikuwa na visiwa kadhaa katika eneo la mashariki mwa Tanganyika vilivyokuwa vimepata uhuru kutoka kwa Waingereza mwaka wa 1963. Baada ya uhuru, Waarabu waliokuwa wachache walipata nafasi nyingi za uongozi na Waafrika wakapata nafasi chache mno za uwakilishi bungeni licha ya kuwa walikuwa na asilimia hamsini na nne ya kura zote zilizopigwa katika uchaguzi wa mwaka wa 1963. Jambo hili halikuwaridhisha Waafrika. Kwa hivyo, chama cha Afro-Shirazi kilichokuwa na Waafrika wengi kiliungana na chama cha mrengo wa kushoto cha Umma na pamoja, chini ya uongozi wa John Okello wakawaunganisha wanamapinduzi wapatao mia sita hadi mia nane katika kisiwa cha Unguja. Wanamapinduzi waliungana na kumng’oa mamlakani Sultani wa Kiarabu na serikali yake. Msukosuko dhidi ya Waarabu huko kisiwani Zanzibar ulienea na maafa mengi

yalitokea. Hatimaye kiongozi wa Chama cha Afro-Shirazi, Abeid Karume alichukua uongozi na akawapa mamlaka wanachama wa chama cha Umma. Kabla ya mapinduzi haya wenyeji wa Zanzibar walikuwa wanadhulumiwa na kunyanyaswa na Waarabu waliokuwa na uwezo wa kisiasa na kifedha.

Katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, Mzee Gae anawakilisha watu wanaodhulumiwa. Maisha yake yanadhihirisha hali ya umaskini na unyonge iliyokithiri kabla ya mapinduzi yaliyotokea Kisiwani Zanzibar. Mzee Gae ni mhusika wa kiishara. Kama anavyosema Kilanga (2014), dhana ya uhusika wa kiishara na uashiriaji katika kazi ya kifasihi zinahusiana na sayansi ya ishara au semiotiki. Mzee Gae ni mhusika wa kiishara kwa kuwa anaashiria mabadiliko katika jamii ya Kisiwa cha Zanzibar. Mwandishi anatumia ulemavu wa akili wa Mzee Gae kama njia ya kuwahamasisha wanajamii kuhusu hali halisi ya kisiasa iliyowazunguka. Ni mhusika wa kimapinduzi anayewakilisha wahusika wa aina yake katika jamii yoyote ile ambao hujitwika jukumu la kuwazindua wanajamii na kuwapa ari ya kuleta mabadiliko katika jamii yao. Maneno ya Mzee Gae yanaashiria kuwa alikuwa amepitia maisha magumu ya dhuluma. Anasema:

> Wa`linivunja kichwa changu kwa nyundo,'angeanza kumaka,'nyundo… yah , nyundo; yah, walinivuruga, walikivuruga kichwa changu' Na hapo angekitomasa kichwa chake kama vile akibonyeza fenesi. 'Waliparaganya,' angeendelea, 'yah, waliparaganya ubongo wangu, na halafu waliniita mbwa, *dog*, yah, mimi mbwa. Na mara nyengine waliniita Mswahili mwendawazimu. Walinitesa kama… he, he, he,' angecheka kwa kitisho, 'walinitesa kama mnyama. Kwa sababu… kwa sababu nilithubutu kuwaambia ukweli,' angesita hapa na mtu angedhani kuwa yamekwisha, lakini baadaye kwa kejeli angaliendelea:'Lakini nyinyi vijana wa sasa, haha, woga,' alivuma kama simba mkali, 'nyinyi ni majimbi tu si majogoo. (Mohamed, 1980, uk. 3).

Kutokana na maneno yake, inabainika kuwa Mzee Gae alikuwa amefungwa jela wakati mmoja. Huko jela aliteswa sana. Ingawa hajasema wazi ni kina nani

waliomdhulumu inadhihirika kuwa hawa ni watu ambao hawakutaka kusikia ukweli na walimwadhibu Mzee Gae kwa kuthubutu kuwaambia ukweli. Kauli hii ya Mzee Gae inadokeza chanzo cha kuvurugika kwake kwa akili. Ulemavu wake unadhibitika kwa kuwa kauli zake hazikamiliki kama wanadamu wengine. Anadai kuwa ulemavu wake ulitokana na kugongwa kichwa kwa nyundo na kuteswa kwa kuthubutu kusema ukweli.

Kwa mujibu wa Fumu, aliyekuwa jirani yake Mzee Gae, Mzee Gae alikuwa anasimulia kila siku kuhusu dhuluma aliyotendewa. Kama anavyodai Mackenzie (2014), ulemavu wa akili huashiriwa na tabia ya kujirudiarudia na tabia ya Mzee Gae ya kurudia jambo moja ni sababu mojawapo iliyowafanya wanajamii kumwita mwendawazimu.

Kupitia kwa namna ambavyo Mzee Gae anasitasita na kurudia maneno yake, msomaji anapata taswira ya mtu ambaye ana majuto na uchungu mwingi. Aidha, kauli yake inabainisha kuwa dhuluma, mateso na kudharauliwa kulikithiri katika jamii husika. Mzee Gae anatumia sitiari ya '*mbwa'* na '*Mswahili*' ili kufafanua dhuluma aliyokumbana nayo huko jela. Kwa mujibu wa Prahlad (1996), neno 'mbwa' hutumiwa na watu weupe kama matusi wanapowarejelea watu weusi hasa Waafrika. Aidha neno hili lilikuwa linatumiwa sana na Wamarekani weusi kuwarejelea watu kutoka Bara la Afrika. Neno 'mbwa', katika muktadha huu mara nyingi huashiria watu ambao hawafuati taratibu zilizowekwa katika jamii. Ni neno linaloashiria mtu mwenye hadhi ya chini. Kwa hivyo, kumrejelea mtu kama mbwa ni ishara ya kumdunisha na kumdhalilisha. Kadhalika, kwa kumwita '*Mswahili,'* wanyanyasaji anaowarejelea Mzee Gae wanadhihirisha ubaguzi kwa misingi ya kikabila. Kwa hivyo kwa kurejelea istiari kama kipengele cha nadharia ya mtindo inabainika kuwa Said Ahmed Mohamed ametumia ulemavu wa akili wa Mzee Gae kama sauti ya mnyonge,

anayenyanyaswa na kudhulumiwa na anapojaribu kutafuta haki anaadhibiwa. Mzee Gae anathibitisha haya kwa kutumia tashbihi anaposema:

> Walinitesa kama mnyama. Kwa sababu… kwa sababu nilithubutu kuwaambia ukweli. (Mohamed, 1980, uk. 3).

Mzee Gae analinganisha mateso aliyoyapata na mateso ambayo kawaida huweza tu kuelekezwa kwa wanyama. Wanyama katika ulimwengu halisi hawapewi thamani sawa na binadamu na hivyo wanadhulumiwa bila kujali. Tashbihi hii inatoa picha halisi ya kiwango cha mateso aliyopatana nayo Mzee Gae alipokuwa jela ambapo alikuwa amefungiwa kwa kusema ukweli kuhusu namna watu wenye nguvu za kisiasa na kiuchumi walivyokuwa wakiwadhulumu na kuwanyanyasa wanyonge. Mateso haya yalikusudia kumnyamazisha.

Licha ya kuwa si kawaida mtu mwenye ulemavu wa akili kutambua hali yake, Mzee Gae anaonekana kuielewa hali yake. Jambo hili linadhihirika katika maneno anayoyasema mwenyewe. Anadai kuwa ulemavu wake ulitokana na kugongwa kichwa kwa nyundo na kuteswa kwa kuthubutu kusema ukweli. Kulingana na Prendergast (2001), ulemavu wa akili ni dhana inayotokana na mtazamo wa jamii kuhusu mtu. Mtazamo huu unatokana na tabia zisizo za kawaida anazodhihirisha mtu mwenye ulemavu wa akili. Kwa hivyo, mtu mwenye ulemavu wa akili kihalisia hatambui kuwa ana ulemavu kwa kuwa mambo anayoyafanya au kuyasema kwake yeye huwa ni ya kawaida. Hata hivyo mwandishi wa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* anaashiria kuwa Mzee Gae alifahamu kuwa watu walikuwa wakimwita mwendawazimu. Ufahamu wa Mzee Gae kuhusu hali yake unaashiria kuwa alitumia ulemavu wa akili kama njia ya kukinga nafsi yake na mawazo yake dhidi ya hali ngumu ya dhuluma na unyanyasaji iliyomzunguka katika ulimwengu halisi. Wanajamii walimwona Mzee Gae kama mwendawazimu kutokana na mambo

aliyoyasema. Hii ni kwa sababu alisema ukweli ambao watu wengine hawangethubutu kusema.

Kadhalika, ufahamu wa Mzee Gae kuhusu chanzo cha ulemavu wa akili uliomwathiri ni ishara kuwa mwandishi amejenga uhusika wake kimaksudi ili aweze kutimiza dhamira ya kuihamasisha jamii kuhusu hali ya dhuluma na unyanyasaji iliyowazunguka. Ni ishara kuwa ulemavu wake si wa kawaida bali unalenga kutimiza wajibu fulani kulingana na malengo ya mwandishi. Ulemavu wa akili wa Mzee Gae unazua hoja kuwa mtazamo wa wanajamii kuhusu ulemavu wa akili wa Mzee Gae ulikuwa wa kawaida tu. Hata hivyo, wanajamii walihitaji kutafakari zaidi aliyokuwa akiyasema Mzee Gae badala ya kumchukulia kama mwendawazimu. Kadhalika, maneno yake licha ya kuonekana kuwa ya mwendawazimu, yanajitokeza kama wasia kwa wanajamii. Kwa mfano, aliwapa vijana changamoto kuwa walihitaji kuwa mstari wa mbele katika kupigania haki na usawa ili waweze kurudisha utu wao. Anasema:

> 'Lakini nyinyi vijana wa sasa, haha, woga,' alivuma kama simba mkali, 'nyinyi ni majimbi tu si majogoo. Nyinyi si watu; watu; watu hudadisi nafsi zao. Na nyinyi mtakuwa watu mtakapoanza kudadisi nafsi zenu, mtakapoanza kupekua mazingira yenu; mtakapoangalia mambo kwa jicho kali; mtakapoanza kutafuta asili ya mambo. Lazima muulize*, kwa nini*, *kwa vipi* na *kwa sababu gani*? Hapo ndimo mlimo na utu. Sio domo kaya. (Mohamed, 1980, uk. 3).

Mzee Gae anasema maneno haya baada ya kueleza kuhusu mateso aliyoyapata akiwa jela. Anaongea huku akicheka kuashiria kuwa azma yake ya kusema ukweli haikuwa imefifishwa na dhuluma aliyoipata. Kicheko chake kinalenga kuwakejeli wale waliomdhulumu. Anawapa changamoto wanajamii kuwa wanahitaji kudadisi hali iliyowazunguka kwa kuuliza maswali bila woga. Mzee Gae anadai kuwa vijana wa sasa ni waoga. Anawaita majimbi na kusema kuwa wao si watu kwa kuwa watu hudadisi nafsi zao.

Maneno ya Mzee Gae yanatumiwa na mwandishi ili kuwakejeli vijana na wanajamii kwa jumla kutokana na kushindwa kwao kupigania haki. Anatumia sitiari ya 'majimbi' na 'majogoo' kuwarejelea vijana. Sitiari ni kipengele cha mtindo, ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu moja kwa moja. Kwa hivyo vijana wanafananishwa na majimbi na majogoo. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki neno au kauli inaweza kuwa kiashiria chenye maana ya kimsingi na maana pana isiyo dhahiri. Kimsingi maneno jogoo na jimbi yana maana sawa kwa kuwa yanarejerea kuku dume. Hata hivyo, maneno haya yanaibua maana ya ziada kwa mujibu wa matumizi yake katika muktadha huu. Neno 'jogoo' linaashiria ukubwa, ukali na ujasiri ilhali neno 'jimbi' linaashiria woga na unyonge. Jogoo hupigana na adui ili kuilinda jamii yake dhidi ya adui yeyote anayeivamia. Vivyo hivyo vijana wanapaswa kuwa katika mstari wa mbele kupigania jamii yao bila woga; wasiwe wanyonge na waoga kama majimbi ila wawe vijana wenye ujasiri (majogoo). Mzee Gae anatumia sitiari hii ili kuwazindua vijana waweze kutambua nafasi yao na jukumu lao katika kuleta mabadiliko katika jamii. Nadharia ya mtindo inatumikizwa zaidi mwandishi anapotumia tashbihi kumrejelea Mzee Gae anaposema kuwa '*alivuma kama simba mkali*' ili kusisitiza kuwa Mzee Gae hakuwa na woga wowote katika kuwahamasisha wanajamii. Kisemiotiki, tashbihi ya simba inatumika na mwandishi kama ishara ya ujasiri.

Mzee Gae anatumiwa na mwandishi kama sauti ya kuwahamasisha watu ili watambue haki zao na kujinasua kutoka kwa minyororo ya ukoloni mamboleo. Kupitia kwa Mzee Gae mwandishi analenga kuwazindua wanajamii ili watambue uhalisia unaowazunguka. Analenga kuwahimiza wanajamii wadadisi mazingira yao na kujiuliza ni kwa nini maisha yao yako jinsi yalivyo; maisha ya unyonge na umaskini. Mzee Gae anasema:

> Lazima muulize, *kwa nini*, *kwa vipi* na *kwa sababu gani*? Hapo ndimo mlimo na utu. Sio domo kaya. (Mohamed, 1980, uk. 3)

Mzee Gae alikuwa akiyaelekeza maneno haya kwa Fumu. Anamwambia Fumu kwamba kulikuwa na haja ya jamii kudadisi mazingira yao badala ya kuendelea kulalamika tu bila kuchukua hatua yoyote ya kurudisha hadhi na utu wao kwa kudai haki yao. Kama mwandishi anavyoeleza, athari ya maneno ya Mzee Gae ilikuwa wazi:

> Mzee Gae: wenda wazimu wake, usodawi wake, ujuba au ufidhuli pengine; lakini pia ujasiri, ukweli, uthabiti na ushujaa. Maneno yake si rahisi kuyapeperusha…Na tabia yake isiyotikatika ilimuathiri kila mtu hapo kijijini pao. Hakusita kuwahujumu waliomuhujumu na kuwasimanga aliowadhania ni waoga. Na huo ndio labda uliokuwa wazimu wake mkubwa. (Mohamed, 1980, uk. 2).

Mwandishi anaeleza namna maneno ya ujasiri, ukweli, uthabiti na ushujaa wa Mzee Gae yalivyowaathiri wanajamii. Aliwakashifu wanajamii aliodhania kuwa ni waoga bila kujali. Maneno yake hayakueleweka moja kwa moja na ndiyo maana wanajamii walimchukulia kuwa ni mtu mwenye ulemavu wa akili. Jitihada za Mzee Gae za kuwazindua wanajamii zinaonekana kufanikiwa kupitia kwa Fumu, aliyekuwa jirani yake. Mwandishi anaeleza kuwa Fumu alitafakari kuhusu maneno ya Mzee Gae. Anaeleza:

> Na hapa nadhari ya Fumu ilikuwa dhahibu, ilirejea katika hali yake, mbali na kumbukizi. Katika upeo huo alikamata. Mwanzo kiini cha maneno ya Mzee Gae hakukigundua. Kililikuwa kama fumbo gumu lililomzidi kimo. Lakini baadaye nuru hafifu ilianza kupenya katika kiza alichokiweka mzee huyo. Kidogo kidogo nuru hiyo ilifunua siri kubwa iliyofichama, na baadaye Fumu alianza kubaini mambo. Aligundua. (Mohamed, 1980, uk. 3).

Mwandishi anaeleza kuhusu ufumbuzi alioupata Fumu baada ya Mzee Gae kusema yale yaliyompata jela na kuwakejeli wanajamii, hasa vijana kwa kuwa waoga na kukataa kudadisi maisha ya dhuluma yaliyowazunguka. Kama anavyosema Fumu,

maneno ya Mzee Gae yalikuwa kama fumbo. Wanajamii hawakuelewa alichokuwa anasema ila waliyaona tu kama maneno ya mtu mwenye ulemavu wa akili. Lakini Fumu alipoyatafakari aligundua kuwa ndani ya maneno yale kulikuwa na ujumbe mzito. Inabainika kuwa Fumu alielewa ujumbe uliofichika katika maneno ya Mzee Gae kwamba wakati wa watu kuamka na kuanza kutetea haki zao ulikuwa umewadia. Katika riwaya hii Fumu anajitokeza kama mmoja kati ya vijana waliokuwa mstari wa mbele katika harakati za kuleta mabadiliko kutokana na uzinduzi aliopata kutoka kwa Mzee Gae.

Matumizi ya ulemavu wa akili wa Mzee Gae kama chombo cha kuwazindua wanajamii yanadhihirika pia wakati Fumu alipoenda kumjulia hali kibandani mwake:

> ‘Shikamoo Mzee Gae,’ Fumu aliamkia kwa sauti nzito yenye pupa. Mzee Gae hakujibu kitu. ‘Je, nini cha mno mzee?’aliendelea Fumu. Kimya chengine. ‘Je, homa? Kimya tena. Fumu aliemewa. Alikuwa na nini mzee huyu? Ni wazi kwamba Gae hakuziba kauli. Labda walimpanda wa kwao. ‘Je, msaada gani?’ aliuliza Fumu huku akijua hakuwa na la kumsaidia Mzee Gae. Hisia ya maneno ni sehemu ya wajibu kwa rafiki mkweli, pindi vitendo vikiwa haviyumkiniki. ‘Jali nafsi yako, fanya ulilolijia, unanitakia nini mimi?’ Sauti ya Mzee Gae ilikuwa imejaa kitetemeshi. (Mohamed, 1980, uk. 11).

Matembezi ya Fumu kwa Mzee Gae yalikuwa na lengo la kumuuliza maswali zaidi kuhusu mawazo yaliyokuwa yanaisumbua nafsi yake. Fumu alibaini kuwa mawazo haya yalitokana na maneno aliyokuwa akiambiwa na Mzee Gae kuhusu umuhimu wa kutafakari namna ambavyo wangechukua hatua za kuibadilisha jamii.

Mzee Gae alinyamaza tu bila kusema lolote alipojuliwa hali na Fumu. Tabia ya Mzee Gae inaibua taswira ya mtu ambaye ana ulemavu wa akili kwa kuwa inakiuka desturi za jamii. Katika mahusiano ya jamii ya kila siku, ni jambo la kawaida mtu kumjulia hali mwingine. Kama anavyoashiria Fumu, salamu hudhihirisha urafiki wa dhati. Hata hivyo, Mzee Gae alimnyamazia Fumu na hakuitikia salamu zake licha ya kuwa

Fumu alikuwa rafiki na jirani yake. Kadhalika, Mzee Gae anaonekana kukasirika wakati Fumu alipomuuliza maswali kuhusu hali yake. Hasira za Mzee Gae zinadhihirika katika maneno yake alipoamua kumjibu Fumu. Tabia ya Mzee Gae, ya kumpuuza Fumu inatumiwa na mwandishi kuashiria hali ya unyonge na kukata tamaa iliyoikumba jamii. Jambo hili linajitokeza wakati Fumu alipomuuliza Mzee Gae alihitaji msaada gani. Mzee Gae alimjibu:

> ‘Jali nafsi yako, fanya ulilolijia, unanitakia nini mimi?’ Sauti ya Mzee Gae ilikuwa imejaa kitetemeshi. (Mohamed, 1980, uk. 11).

Mzee Gae alimwambia Fumu ajali nafsi yake kuashiria kuwa Fumu alihitaji kujisaidia kwanza kabla ya kuwauliza wengine walikuwa wanahitaji msaada gani. Hii ni kwa sababu kama anavyoeleza mwandishi, Fumu hakuwa na chochote cha kumpa. Uhalisia huu unadhihirika katika maneno ya Mzee Gae anapomcheka na kumfanyia stihizai Fumu:

> Mwanamme mzima hapo ulipo, kijana shababi mwenye nguvu zako…Fumu, wewe simba? Nani simba katika kijiji hiki? Nani simba katika nchi hii? Mimi tu; mimi simba; naweza kunguruma ninavyopenda. Mnaniita mwendawazimu, nani asiyekuwa mwendawazimu? Kila mtu mwendawazimu katika ulimwengu tajiri lakini wenye ulitima; na wewe Fumu simba, lakini simba mwoga. Tazama, umeufyata mkia wako. Una mkia ivyo, huuoni? Haki ya Mungu unao. Ah, unanikumbusha Mungu, ndio lakini ana viumbe dhaifu; la, sio viumbe hivi, marembeo ya jamii. Vimechanwachanwa, vimeraruliwa, lakini bado viumbe vya Mungu, watasema? Yah, wewe ni simba, simba mwoga wewe uliyeshindwa kumiliki kijiti kimoja cha kibiriti; unasafiri masafa yote kutoka kwako kuja kwa Gae kupaa moto; aibu; fedheha. Nimekufunzeni, nimekwambieni, nimekufunulieni siri za dunia. (Mohamed, 1980, uk. 12).

Mzee Gae anaonekana kushangazwa na ukweli kuwa Fumu licha ya kuwa kijana mwenye nguvu hakuweza kujitegemea. Ni kinaya kuwa Fumu alikuwa ameenda kupaa makaa ya moto kwa Mzee Gae ilhali anamuuliza Gae alihitaji msaada gani. Fumu anajitokeza kama kwamba ndiye aliyekuwa mhitaji zaidi ya Mzee Gae kwa kuwa hakumiliki hata kiberiti. Mzee Gae anamkejeli Fumu kwa kukosa kiberiti

ambacho ni kifaa cha kimsingi na kwenda kupaa makaa ya moto kwake licha ya kuwa wanajamii walimwita mwendawazimu. Anatumia sitiari ya simba kumkejeli na kumfanyia stihizai Fumu. Kinaya na sitiari ni vipengele vya mtindo. Mwandishi kupitia kwa Mzee Gae, anamkejeli Fumu kwa kutokuwa na ujasiri wa kupigania haki yake, jambo linaloelea kushindwa kwake kujikimu kimaisha.

Maana ya kimsingi ya neno simba ni mnyama wa mwituni. Hata hivyo, mwandishi ametumia sitiari ya simba kimtindo ili kuashiria maana ya ziada. Simba anatambulika kama mnyama mwenye ujasiri kiasi kwamba anaashiriwa kama mfalme wa wanyama wengine wa pori. Kutokana na nguvu na uwezo wake, simba hawezi kutishwa na mnyama yeyote porini. Hata hivyo, Simba kutokana na kauli ya Mzee Gae, Simba anaimbuka kama mnyama mwenye sifa nyingine kisemiotiki. Kwa mujibu wa nadharia ya semiotiki, ishara moja inaweza kuibua maana tofauti. Kwa hivyo, neno simba katika muktadha huu linaibua maana mbalimbali. Kuna simba ambaye ni mwoga na simba ambaye ni jasiri na mkali. Ingawa simba wote wanaweza kuchukuliwa kuwa na sifa zinazofanana katika hali halisi, mwandishi anatumia mtindo wa kiistiari kubainisha tofauti ya Fumu na Mzee Gae ili kusisitiza ujumbe wake.

Mzee Gae anaashiria kuwa kuna simba mwoga kumaanisha kuwa, licha ya kuwa na sifa zote za mnyama aitwaye simba, simba mwoga anadhihirisha hali ya unyonge na woga na hawezi kuitetea haki yake. Mzee Gae anajiita simba mkali kwa kuwa yeye ana ujasiri wa kukosoa na kusema ukweli kuhusu dhuluma na unyanyasaji. Haogopi kuwakashifu wanaoendeleza dhuluma licha ya kutishwa, kupigwa na kufungwa gerezani. Kadhalika, anamwita Fumu simba mwoga kuashiria kuwa ingawa yeye alikuwa na nguvu na uwezo wa kubadilisha hali mbaya ya maisha iliyomkabili pamoja na jamii kwa jumla, aliogopa kufanya hivyo. Maneno ya Mzee Gae yana

ujumbe mzito licha ya kuonekana na Fumu kama ya mwendawazimu. Mwandishi anasema kuwa Fumu alisalimisha nafsi yake imeze maneno yale mazito yaliyotokana na mwendawazimu. Kauli ya Mzee Gae kuhusu woga wa Fumu inathibitishwa wakati ambapo Fumu alimkabili Fauz aliyekuja kibandani chake na kumtisha. Mwandishi anaeleza woga uliomkabili Fumu kwa maneno haya:

> Kwa dhahiri, Fumu aliogofya na hadhi ya Fauz na babaake, Bwana Hamoud. Na hili si ila-nani asiyetetemeshwa na Bwana Hamoud au Fauz, mwanawe? Kwa ndani na labda kabisa, Fumu alikuwa na dharau kubwa kwa Bwana Hamoud na aila yake, lakini dharau hiyo ilididimizwa na wiano wa Fumu na binadamu hawa. Hamoud alimiliki ardhi ambayo yeye Fumu aliihitaji kwa maisha yake. Lilikuwa tegemeo ambalo Fumu alichelea kulivunja. Hakuweza kuufisidi mzizi wa maisha yake. (Mohamed, 1980, uk. 6).

Fauz alikuwa mtoto wa Bwana Hamoud ambaye alikuwa mmiliki wa shamba ambako Fumu alikuwa anaishi. Fauz alikuwa ameenda nyumbani kwa Fumu kumwarifu kuwa hakuwa na ruhusa ya kulima shamba la Hamoud wala kupanda chochote.

Mwandishi anaeleza kuwa, Fumu alikuwa na dharau kubwa kwa Bwana Hamoud na aila yake. Aidha, alichukizwa na wanyanyasaji lakini aliogopa kukabiliana nao kwa kuhofia kupoteza makao na tegemeo lake; kijishamba alichokuwa anaishi, kilichomilikiwa na Bwana Hamoud. Woga wa kukabiliana na wanyanyasaji kama vile Hamoud na mwanawe Fauz, ndio uliomfanya Mzee Gae kumwita Fumu simba mwoga. Zaidi ya hayo, Mzee Gae anatumia jazanda anaposema kuwa Fumu ni simba ambaye ana mkia lakini ameufyata. Jazanda kama kipengele cha mtindo imetumika kuchora taswira ya woga aliokuwa nao Fumu. Kisemiotiki, ufyataji wa mkia unazua maana zaidi kuhusu mnyama simba. Hii ni kwa sababu simba aliyefyata mkia anaashiria woga na kutojiamini. Katika hali ya kawaida simba haufyati mkia wake lakini anapopatana na hali inayoogofya anaufyata. Sitiari ya simba imetumiwa na Mzee Gae kuashiria kuwa wanajamii walikuwa na nguvu na uwezo wa kubadilisha

hali ya dhuluma na unyanyasaji iliyowakabili ila waliogopa kukabiliana na watu waliokuwa wakiwanyanyasa. Mzee Gae anasema kuwa uwezo huu ungetambulika iwapo wanajamii wangeanza kuuliza maswali ili wajue ni kwa nini maisha yao yalikuwa jinsi yalivyo na waanze kudai mabadiliko bila woga wowote.

Katika jitihada zake za kuwahamasisha wanajamii kuhusu hali ya dhuluma na unyanyasaji iliyowazunguka Mzee Gae anatumia sitiari ya marembeo.

> Ah, unanikumbusha Mungu, ndio lakini ana viumbe dhaifu; la, sio viumbe hivi, marembeo ya jamii. Vimechanwachanwa, vimeraruliwa, lakini bado viumbe vya Mungu, watasema? Nimekufunzeni, nimekwambieni, nimekufunulieni siri za dunia. (Mohamed, 1980, uk. 12).

Mzee Gae anayaelekeza maneno haya kwa Fumu alipoenda nyumbani kwake kupaa makaa ya moto. Mzee Gae anadai kwamba licha ya kuwa Mungu ana viumbe, viumbe hawa, kwa maoni yake hawakuwa viumbe ila ni marembeo ya jamii.

Neno marembeo linatokana na kitenzi remba. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) neno remba lina maana ya kupamba au kutia mapambo katika kitu ili kipendeze na kuvutia machoni. Katika muktadha huu tamathali sitiari imetumika kama mtindo wa kuwarejelea wanajamii wanaodhulumiwa. Kisemiotiki, neno marembeo lina maana ya kimsingi, Marembeo ni vitu au vifaa vya kurembesha na vinaweza kutumiwa kwa jinsi yoyote ile ili kukidhi maslahi ya anayevitumia. Marembeo yanaweza kuwekwa mahali popote pale na kwa namna yoyote ile kulingana na mapendeleo ya anayerembesha. Sifa hii ya marembeo inaibua maana ya ziada kisemiotiki. Mzee Gae anawaita wanajamii marembeo ili kuashiria kuwa wao ni wanyonge na wanatumiwa na wenye nguvu ili kutimiza maslahi yao; ni kama vifaa vya kurembesha tu, hawana thamani na wanaweza kufanyiwa chochote. Kadhalika, kimtindo, anatumia jazanda ya kuchanwachanwa na kuraruliwa ili kuchora taswira ya dhuluma wanayoipitia wanajamii. Mzee Gae anapobainisha kuwa wanajamii

wanapitia dhuluma licha ya kuwa wote ni watu wa Mungu, anaashiria kuwa jamii imegawika katika matabaka, tabaka la watawala wenye utajiri na tabaka la watu maskini wanaotawaliwa. Wainwright (2006) anasema kuwa kulingana na imani ya dini ya Kiislamu na Kikristo kuna kiumbe mwenye nguvu kuliko viumbe wote. Kiumbe huyu anaitwa Mungu mwenye nguvu na uwezo kuliko viumbe wote duniani na mbinguni. Mafundisho ya dini hizi yanaelekeza kwamba Mungu hana mapendeleo na watu wote wana hadhi sawa mbele yake. Kwa hivyo, Mzee Gae anapotoa kauli kuwa watu hawa ni wa Mungu, anadhamiria kuonyesha kuwa watu wote duniani wana thamani sawa mbele ya Mungu na wanastahili kupewa haki.

Matumizi ya mafumbo katika maongezi ya Mzee Gae yanajitokeza wakati alipoenda kibandani kwa Fumu usiku. Wakati huu Fumu alikuwa akiwasubiri wenzake ambao walikuwa wanakuja kuzungumza juu ya hali ya dhuluma na unyanyasaji iliyokuwa ikiwakabili na kupanga mikakati ya kutafuta haki. Mzee Gae aliingia nyumbani mwa Fumu kumwambia kuwa ngawa walishafika kutoka mjini. Alisema:

> Wameshafika ngawa, wameshafika, wamekuja toka mjini kwa miguu…
> Sio mimi n'nowaita ngawa! Sio mimi-hujapata kusikia, au hujapata kuitwa ngawa; fanya jambo lolote lisilowafurahisha, watakwambia, we ngawa! Mimi mwenyewe najiona ngawa, wewe Fumu pia ngawa, na wao vilevile… na wala silichukii jina la ngawa- siku moja ngawa atakata vichwa vyote vya kuku. (Mohamed, 1980, uk. 98).

Gae anatumia sitiari ya ngawa kuwarejelea watu waliokuja kwa Fumu. Fumu aliposhangaa ni kwa nini wageni wake wakaitwa ngawa, Mzee Gae alimjibu kuwa vijana waliofika kwake walipewa jina ngawa na wanyanyasaji. Aidha, anasema kuwa yeye na Fumu ni ngawa pia.

Kimsingi neno ngawa lina maana ya mnyama wa pori anayependa kula kuku. Kuku ni ndege ambaye hufugwa nyumbani. Kwa hivyo, ili kumpata kuku na kumshambulia,

ngawa huenda wanakofugwa kuku kuwashambulia na kuwakamata. Akishawakamata kuku, anawanyonya damu na kuwaacha. Kuku akishanyonywa damu hawezi kuishi tena ila huanguka na kufa. Kimtindo sitiari ya ngawa inatumika ili kuchora taswira ya vijana waliotoka mjini kuja kijijini kwa kina Fumu. Kisemiotiki, safari yao inafananishwa na jinsi ambavyo ngawa wanatoka porini na kwenda nyumbani wanakofugwa kuku na kuwashambulia. Kitendo cha ngawa kuwanyonya damu kuku hadi kufa ni ishara ya kisemiotiki kwa kuwa kinaashiria unyonyaji na unyanyasaji ambao watu wenye nguvu na mamlaka wanatekeleza dhidi ya wanyonge. Ni kinaya kuwa watu wanaodhulumu wanawaita wadhulumiwa ngawa ilhali wao ndio wanaostahili kuitwa ngawa kutokana na tabia yao ya unyanyasaji. Mzee Gae anaposema kuwa yeye ni ngawa anaashiria kuwa kuna uwezekano kwamba hali ya dhuluma iliyokuwapo ingebadilika. Sitiara ya ngawa na kuku inatumiwa na Mzee Gae ili kuashiria mapinduzi ambayo yanatokea baadaye katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ambapo wanajamii waliodhulumiwa waliungana na kupigania haki zao kwa kukabiliana na watu waliowanyanyasa. Mzee Gae anawafananisha wanaonyanyaswa na ngawa ilhali wale ambao ni wanyanyasaji anawalinganisha na kuku. Hii ni kwa sababu waliokuwa wananyanyaswa walitumia nguvu kuwang'oa mamlakani wale waliokuwa wanawadhulumu.

Mzee Gae anaonekana mara kwa mara akicheka kicheko cha ghafla hata alipokuwa peke yake. Kicheko chake kilikuwa cha kutisha. Mwandishi anachora taswira hii anapoeleza tabia ya Mzee Gae wakati Fumu alipoamua kurejea kwake baada ya kupuuzwa na Mzee Gae wakati alipokuwa ameenda kupaa makaa ya moto. Mwandishi anasema:

> Fumu alikuwa akigeuka ashike njia ya kurejea kibandani kwake, ndipo aliposhtukia Mzee Gae kaangua kicheko cha ghafla, kicheko cha kutisha.

> Aliendelea kucheka kwa muda mpaka lile blanketi lilimwanguka na kufedhehi hali yake dhaifu. Nguo zake zilizoroa majasho zimeganda kwenye mafupa ya mwili; utadhani alimwaiwa madoo ya maji. Aliendelea kucheka mfululizo, bali mwishowe alikikata kicheko chake ghafla. (Mohamed, 1980, uk. 12).

Fumu hakuona chochote kilichosababisha kicheko cha Mzee Gae ila aliiona tabia hii kama ya mtu aliyekuwa na ulemavu wa akili. Tabia ya kucheka kwa ghafla bila sababu yoyote inayodhihirika si ya kawaida kwa mtu mwenye akili timamu.

Kisemiotiki, kicheko katika hali halisi huashiria furaha na kuridhika. Hata hivyo, kulingana na Glasgow (2015), kicheko kinapotumika katika muktadha wa fasihi kama kipengele cha mtindo, kinaweza kuashiria kejeli, kinaya, aibu, uasi au dharau. Kwa hivyo, ni kinaya kuwa Mzee Gae alikuwa anacheka licha ya hali mbaya ya maisha aliyoishi. Kwa kuzingata mtazamo wa kisemiotiki ambapo ishara huweza kuwa na maana zaidi ya moja, kicheko cha Mzee Gae kiliashiria hali ya mtu aliyekuwa na ulemavu wa akili. Inabainika kuwa nguo zake zilikuwa chafu na mwili wake ulikuwa umedhoofika. Kicheko chake hakikuwa cha furaha ila kilibeba maana iliyoibua ujumbe mahsusi. Kilikuwa kicheko kilichodhihirisha dharau na kejeli kwa wanajamii ambao walikuwa wanadhulumiwa bila kuchukua hatua yoyote. Kwa mfano, Mzee Gae anamcheka Fumu kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kama moto. Kicheko cha Gae kinatumiwa na mwandishi kuwakejeli wanajamii kwa kuwa hata ingawa hawakuwa na mahitaji ya kimsingi, hawakuchukua hatua yoyote kubadilisha hali yao ya umaskini. Kukatika ghafla kwa kicheko cha Mzee Gae kunalenga kumpatia msomaji au mlengwa nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu ujumbe ambao mwandishi alinuia kuwasilisha, kwamba kulikuwa na haja ya mabadiliko.

Said Ahmed Mohamed kupitia kwa ulemavu wa akili wa Mzee Gae anatumia tashihisi katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* kwa lengo la kusisitiza ujumbe wa haja ya wanajamii kujenga jamii mpya yenye haki na usawa. Kwa mfano, Mzee Gae na

wenzake walipotambua kuwa Makame, mmoja wa vijana waliokuwa wanatarajiwa kufanya mapinduzi alikuwa msaliti, aliwaeleza haya:

> 'Ndio desturi ya njaa hiyo,' alizuka tena Mzee Gae, 'hukudhili ikakuvunjavunja wewe na watoto wako; isitosheke, tena hukutia utumwani, na mwisho hukutenga na aliye wako. Ni udhaifu mkubwa unaotutumburujikia sisi maskini. (Mohamed, 1980, uk. 105).

Makame alikuwa kijana mmoja kati ya wale waliokuwa wanapanga njama za kuvamia kituo cha polisi wakiwa na Fumu na Mzee Gae. Mzee Gae alitambua kuwa Makame alikuwa akimpelekea Fauz habari kuhusu mipango yao ya kuwavamia wanyanyasaji. Jambo hili liliwakasirisha sana Fumu na wenzake kwa kuwa Fauz alikuwa adui yao. Fumu alijawa na chuki alipokumbuka namna Makame alivyokuwa amemtendea mambo mengi mabaya. Makame alikuwa ameifisidi ndoa kati ya Fumu na Kazija. Kadhalika, alikuwa ameshiriki katika kuchoma shamba lake. Mzee Gae anamtuliza Fumu kwa kumwambia kuwa usaliti ni sifa inayodhihirika kwa watu wenye njaa.

Mzee Gae anaihuisha dhana ya njaa kwa kuipa sifa ya utendaji mithili ya kiumbe aliye na uhai. Uhuishaji ni kipengele cha kimtindo kinachovipat vitu visivyo na uhai sifa za viumbe wenye uhai. Mzee Gae anasema kuwa njaa ina uwezo wa kumvunjavunja mtu na watoto wake, kumtia utumwani na kumtenganisha na marafiki zake. Maneno yake yanaonekana kuwa ya mtu asiye na akili razini. Hata hivyo kuna ujumbe mzito unaowasilishwa kupitia kwa maneno hayo. Tashihisi ya njaa inaashiria tamaa waliyo nayo wasaliti kama Makame. Makame anajitenga na marafiki zake na kuwasaliti kwa lengo la kujinufaisha mwenyewe. Kwa kutumia tashihisi ya njaa, Mzee Gae analenga kuwafahamisha wenzake kuwa katika harakati za mapinduzi hapakosi watu ambao wanawasaliti wenzao. Watu hawa huongozwa na tamaa na maslahi yao binafsi. Aidha, kwa kubainisha madhara yanayowapata wasaliti hawa,

Mzee Gae analenga kuwaonya dhidi ya tabia hii. Anadai kuwa usaliti husababisha kuvunjika kwa familia na kutenganishwa na watu wa karibu kwa kuwa msaliti hujali maslahi yake pekee. Mtu mwenye tamaa huishi kama mtumwa wa wanaompa kazi ya kuwasaliti wenzake na daima huishi kwa woga kwa kuwa asipolitekeleza jukumu hili huenda watu hao ambao ni wanyanyasaji wakamdhuru au hata akadhuriwa na watu anaowasaliti. Aidha, mtu huyo husema uongo ili kujipendekeza kwa watu hawa, ni haini, na hatekelezi majukumu yake kulingana na matarajio ya jamii. Mzee Gae anaeleza zaidi sifa za msaliti:

> Lahaula, shujaa hugeuzwa mwoga; mkweli, mwongo; mwaminifu, haini; mwanamme, mwanamke…njaa (Mohamed, 1980, uk. 105).

Mzee Gae anasema kuwa njaa humgeuza shujaa kuwa mtu mwoga na msema ukweli kuwa mwongo. Aidha, mtu mwaminifu hugeuka na kuwa haini na mwanamume kuwa mwanamke. Maneno haya ya Mzee Gae hayaonekani kama yaliyokuwa na maana yoyote, Yalichukuliwa kama maneno ya mtu mwenye ulemavu wa akili. Hata hivyo, maneno haya yaliwasilishwa kwa njia ya kifalsafa na yalibeba ujumbe muhimu. Hivyo basi inabainika kuwa ulemavu wa akili wa Mzee Gae unatumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya semiotiki kuwa neno linaweza kuwa na maana ya kimsingi na maana ya ziada dhana za mwanamke na mwanamume zinajitokeza kuwa na maana za ziada na hivyo basi kuwasilisha ujumbe mahsusi.

Katika kufafanua athari za usaliti, Mzee Gae anatumia tanakuzi anapoeleza sifa kinzani za mtu msaliti. Anaashiria kuwa usaliti humfanya mtu kusema mambo ambayo si ya kweli na mtu mwenye ushujaa kuwa mwoga. Kadhalika, anasema kuwa mtu mwaminifu hugeuka kuwa haini. Haini ni mtu anayetoa siri na kutenda matendo maovu kwa nchi yake kwa manufaa ya nchi nyingine au watu wengine. Kwa hivyo,

kuwasaliti watu ni kitendo kinachodhihirisha woga. Aidha, msaliti anaweza kusambaza habari za uongo ili ajinufaishe yeye mwenyewe. Mzee Gae anatumia sitiara na kinaya anaposema kuwa njaa humgeuza mwanamume kuwa mwanamke.

Kama anavyosema Singh (2012), kinaya ni matumizi ya maneno yanayowasilisha maana ambayo ni kinyume na maana ya kawaida kwa lengo la kukejeli tabia fulani. Katika utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika, mwanamke huchukuliwa kama kiumbe dhaifu, mnyonge, mwoga na aliye chini ya mwanamume. Kwa hivyo, sitiari hii ya mwanamume kuwa mwanamke inaashiria kuwa mwanamume mwenye njaa huwa na sifa kama za mwanamke kwa kuwa anatawaliwa na wale anaowapelekea habari za uongo na yuko chini ya mamlaka yao. Kwa hivyo, Mzee Gae anaashiria kuwa mwanamume mwenye tamaa hujizusha hadhi na kuwa na tabia kama za mwanamke kwa lengo la kutimiza maslahi yake binafsi.

Kupitia kwa Mzee Gae mwandishi anatumia kejeli kama mbinu ya kuwasilisha ujumbe wake. Kwa mujibu wa Singh (2012) na Mrikaria (2010), kejeli ni mzaha wenye uwezo wa kuwasema, kuwasengenya na kuwakebehi wanajamii kwa lengo la kuwarekebisha, kuwaonya, na kuwaelimisha. Aidha, kejeli hutumika kwa lengo la kuyaweka wazi mambo yaliyopo katika jamii, kulingana na matukio yaliyopo na yanayotokea. Kejeli hutumiwa na waandishi ili wasomaji wafikirie kwa undani kuhusu mada inayowasilishwa na waelewe ujumbe na dhana iliyokusudiwa. Katika kusisitiza matumizi ya kejeli kama njia ya kumgusa mtu kwa namna fulani, Mrikaria (2010) anasema kuwa matumizi ya kejeli hunuia kufichua ubaya au udhaifu fulani alionao mhusika fulani. Mrikaria anaendelea kusema kuwa mhusika anaweza kumcheka mhusika mwingine aliyepatwa na matatizo fulani au msiba fulani ilhali msiba kama huo ukampata yeye hata bila yeye mwenyewe kutambua. Uhalisi huu unajitokeza katika maneno ya Mzee Gae anaposema:

> ‘Mwanamme,’ alianza kuhuruju huku kaviringa ngumi mikono yake yote miwili na kusema kwa hamaki, ‘mwanamme mzima hapo ulipo, kijana shababi mwenye nguvu zako…’ alisita, na sasa alikaza mviringo wa ngumi zake na kuanza kutafuna meno.’ Simba, simba, yuko wapi simba? Hahaaa… Fumu, wewe simba? Nani simba katika kijiji hiki? Nani simba katika nchi hii? Mimi tu; mimi simba; naweza kunguruma ninavyopenda. Mnaniita mwendawazimu, nani asiyekuwa mwendawazimu? Kila mtu mweendawazimu katika ulimwengu tajiri lakini wenye ulitima’ (Mohamed, 1980,uk 12).

Mzee Gae anayaelekeza maneno haya kwa Fumu wakati Fumu alipokuwa anaondoka baada ya kupaa moto kibandani kwake. Machoni mwa wanajamii wenzake maneno ya Mzee Gae hayakuwa na maana yoyote ila yalionekana tu kama ya mtu aliyeathirika na ulemavu wa akili.

Mzee Gae anatumia maswali ya balagha kumkejeli Fumu anapomuuliza iwapo yeye ni simba. Anatumia sitiari anapojiita simba kwa maana kuwa kama anavyosema, yeye pekee ndiye alikuwa na ujasiri wa kuwashutumu watawala waliokuwa wanawadhulumu wanajamii wa kawaida kiasi kwamba aliwahi kufungwa jela ili kunyamazishwa.

Kadhalika, Mzee Gae anamsimanga Fumu kwa kushindwa kumiliki hata kiberiti na kwenda kumwomba yeye ambaye walimwita mwendawazimu. Anamwambia:

> Yah, wewe simba, simba mwoga wewe unayeshindwa kumiliki kijiti kimoja cha kibiriti; unasafiri masafa yote kutoka kwako kuja kwa Gae kupaa moto; aibu, fedheha. Nimekufunzeni, nimekwambieni, nimekufunulieni siri za dunia. Mimi nimeona mengi, lakini ninapokuonyesheni nyinyi hamtaki kufahamu, hamjali. Nambie Fumu, unajiuliza nafsi yako yale maswala muhimu-unajiuliza kwa nini na kwa sababu gani?’ Hapa alisita, lakini kwa namna alivyouliza swala lake, ni wazi hakutarajia jibu, kwa hivyo alilijibu mwenyewe,’la, hujiulizi. Hebu jiulize swala rahisi hili: kwa nini unashindwa kupata kijiti cha kibiriti kuwashia moto? Na wewe unalima, unafuga wanyama… ha, ha, ha, ha, ha… mamaangu mzazi’ (Mohamed, 1980, uk. 12).

Maneno haya yananuia kumfikirisha Fumu ili aone uhalisia uliomzunguka ambapo umaskini ulikithiri. Ni kinaya kuwa Mzee Gae anamwita Fumu simba mwoga kwa

kuwa simba ni mnyama anayetambulika kwa ujasiri wake. Mzee Gae anasema kuwa ni aibu na fedheha kwa Fumu kusafiri mwendo mrefu hadi kwa Gae kupaa moto licha ya kuwa yeye na wanajamii wengine wameelimishwa na kuzinduliwa kuhusu namna ya kujitoa katika shida zinazowakabili lakini hawajali. Ni kinaya kuwa Fumu hawezi kukimu maisha yake licha ya kuwa analima na kufuga wanyama. Inatarajiwa kuwa angepata mahitaji yake kutokana na mazao na ufugaji wake lakini anabaki kuwa maskini kwa kuwa wanaonufaika na jasho lake ni wanyanyasaji, lakini kama anavyosema Mzee Gae, Fumu haonekani kujalishwa na hali hii. Mzee Gae anamsimanga zaidi Fumu na kusisitiza kuwa yeye ni mwoga anapomwambia:

> ‘Anakwenda zake,’ alibweka Mzee Gae, ‘anakwenda zake masikini, anakwenda kama kusi anayefukuzwa na Kaskazi, mwoga,’ alipaza sauti kama vile alikuwa mgonjwa wa homa. ‘Mwoga, anayepita kuniuliza mimi, Nikushaidie niini? Nikushaidie niini? Kwa nini hujisaidii nafsi yako? Usiniambie unisaidie, utanisaidia nini mwoga we?’ Alicheka kicheko cha nguvu kilichopaa kwenye hewa. ‘Mwoga rejeaaa Mwogaaa!’ Lilipaa sauti lake juu zaidi na kuharibu ukimya uliokuwepo. (Mohamed, 1980, uk. 13).

Mzee Gae alitamka maneno haya alipokuwa anamkaripia Fumu baada ya Fumu kwenda kwake kutafuta moto. Fumu alikuwa amekatisha safari ya kurudi kwake ili kumsikiliza Mzee Gae. Hakujua ni nini kilichokuwa kimemkasirisha Mzee Gae lakini kama anavyosema mwandishi; ‘*wakati wa machafuko ya tabia yake, ndipo maneno ya Mzee Gae yalipomwathiri Fumu kuliko pale mizimu yake ilipogonywa.’* Hii inadhihirisha kuwa licha tabia ya Mzee Gae kuonekana kama ya mtu mwenye ulemavu wa akili, alikuwa na athari kubwa kwa jamii.

Kwa kuzingatia nadharia ya semiotiki, inadhihirika kuwa maneno ya Mzee Gae yametumika kama ishara inayoibua maana mahsusi. Mzee Gae yanalenga kumzindua Fumu, ambaye kimsingi anawakilisha wanajamii wengine, ili watambue kuwa wanahitaji usaidizi zaidi kuliko alivyohitaji yeye. Usaidizi wa nafsi anaoulenga Mzee Gae ni kuwa wanajamii walihitaji kujisaili na kuelewa kuwa ni wao wenyewe tu

waliokuwa na uwezo wa kujitoa katika hali ya ukandamizaji iliyowazunguka. Aidha, ni wao wenyewe tu waliokuwa na uwezo wa kuleta mapinduzi na kujenga jamii mpya yenye haki na usawa. Ni kinaya kuwa Fumu anamuuliza Mzee Gae alihitaji usaidizi gani ilhali yeye ndiye aliyehitaji kusaidiwa. Kadhalika, mtu mwenye woga hawezi kumsaidia mwingine aliye kwenye hatari na ndio maana Mzee Gae anashangaa ni kwa jinsi gani Fumu angeweza kumsaidia. Anavuta silabi huku akipaza sauti na kucheka kwa kejeli huku akimwita Fumu mwoga:

> Mwoga rejeaaa Mwogaaa!'lilipaa sauti lake juu zaidi na kuharibu ukimya uliokuwepo.: (Mohamed, 1980, uk13).

Mzee Gae anajitokeza kama aliyekasirishwa na kitendo cha Fumu cha kwenda kwake kupaa makaa ya moto. Haya yanadhihirika alipomwamuru Fumu arejee kwake.

Uvutaji silabi na upazaji wa sauti unadhamiria kusisitiza maoni ya Mzee Gae kumhusu Fumu kuwa ni mwoga na kumfanya atafakari kuhusu hali ya maisha ya umaskini na dhuluma iliyokuwa inamzunguka.

Kwa mujibu wa Mrikaria (2010), wakati wa ukoloni fasihi ya Kiswahili ilitumika katika kusawiri hali halisi ya maisha ya wakati huo. Mrikaria anasema kuwa waandishi wa fasihi ya Kiswahili waligeuza mbinu zao za uandishi na kutumia mtindo wa mbinu ya kejeli katika kuonyesha jinsi jamii ilivyokuwa ikinyanyasika, ikionewa na ikitawaliwa kinyama, hali ambayo iliwakosesha amani katika maisha yao ya kila siku. Kejeli ilikuwa inatumika kama ishara ya dhuluma na unyanyasaji na ilenga kuwazindua watu ili wapiganie haki zao.

Katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu,* Mzee Gae anaonekana akisimulia hadithi ambazo kwa wanajamii wengine zinadhihirisha hali ya kulemaa akili. Usimulizi ni mbinu ya kimtindo ambapo hadithi inaweza kujitokeza ndani ya hadithi kuu. Ingawa usimulizi

wa Mzee Gae umebeba ujumbe mahsusi, watu wanauchukulia kama hadithi tu za ‘Abunuwas’ zisizokuwa na maana na kwamba ni hadithi zilizotokana na ulemavu wa akili. Kupitia hadithi hizi Mzee Gae anachora taswira mwafaka zinazolenga kupitisha ujumbe mahsusi. Kama anavyosema Elran (2011), taswira zinapaswa kueleweka kama vifaa vya kuhamisha maana kuhusu uwanja mmoja wa kisemantiki kwa kutumia uwanja mwingine. Kwa kuzingatia madai ya Elran, inadhihirika kuwa taswira ya ulemavu wa akili wa Mzee Gae inaibua maana ya ziada iliyofichika ndani ya maneno yake na tabia zake zinazoonekana kuwa za mtu aliyepungukiwa kiakili. Kulingana na Saussure (1983) kiashiria halisi kinaweza kuzua maana ya moja kwa moja au maana fiche.

Ulemavu wa akili kihalisia ni hali ya kibayolojia, kimatibabu na kijamii. Hata hivyo, katika fasihi ulemavu wa akili ni kiashiria kinachowakilisha maana fulani. Kama anavyosema Saussure (1983), hatua za kuzua maana kutoka kwa uwakilishaji hufungwa na mifumo ya kijamii na hali zingine za kimuktadha zinazotawala maana mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika hali fulani. Kadhalika, mwandishi huwa na sababu maalum ya kuwachora wahusika wake kwa namna fulani kulingana na mazingira yanayokithiri katika jamii husika. Kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, mwandishi anatumia hadithi fupi zinazozua uhusika wake kutoka kwa mazingira yanayoeleweka na jamii ili kuwasilisha ujumbe wake. Hadithi hizi zinahusu matukio ya kawaida lakini zinaelezea mazingira ya kisiasa yanayoizunguka jamii husika.

Kwa mujibu wa Bertoncini (1989), riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* inaangazia uhalisia wa hali ilivyokuwa huko Zanzibar kabla ya mapinduzi ya mwaka wa 1964. Hali hii ya kisiasa inajitokeza katika hadithi zilizosimuliwa na Mzee Gae. Hadithi hizi zimefumbwa na hazieleweki moja kwa moja ingawa zimebeba ujumbe mzito. Kwa

mfano, Mzee Gae na wenzake walipokuwa katika kikao cha kupanga namna ambavyo wangetekeleza mapinduzi, kijana mmoja kwa jina Hasani alionekana kuwa na wasiwasi kuhusu hatima yao iwapo wangekamatwa. Mzee Gae anawatuliza kwa kusimulia hadithi ya nyuki. Mwandishi anaeleza kuwa tangu kikao kianze, Mzee Gae alikuwa amenyamaza tu ila ghafla aliposikia kuhusu wasiwasi wa Hasani alianza kucheka tu kama mwendawazimu. Jambo hili liliwatatanisha wenzake. Alipoacha kucheka alianza kuwasimulia kisa cha nyuki. Aliwachorea taswira ya nyuki na kusema kuwa ingawa nyuki ni kiumbe mdogo na dhaifu, anapochokozwa huwa ni hatari mno. Kadhalika, licha ya kuwa anafahamu fika kuwa akishamchoma mtu hatima yake ni kifo, hajali kwa kuwa kifo chake hutokea katika harakati za kuipigania jamii yake. Mzee Gae anaendelea kusema kuwa mtu anapochomwa na nyuki, hatimaye maumivu huisha lakini mtu hawezi kuyasahau na hivyo huchukua tahadhari kila anapomwona nyuki mwingine. Mzee Gae anamalizia usimulizi wake kwa kicheko kama kwamba hakusema lolote la maana, lakini kama anavyoeleza mwandishi:

> Waliokuwepo walitumbua macho kwenye hewa kama kwa kuipekua picha aliyoichora mzee huyo. Kila mmoja alivutwa na ufundi wa kuzungumza wa Mzee Gae. Mifano mizito, maneno yake mateuzi na tashbihi zake husadifu vyema na kufunua ukweli wote kwa maneno machache. (Mohamed, 1980, uk. 105).

Kisa hiki cha nyuki kilinuia kuwafunulia vijana kuhusu jukumu lao katika kuleta mabadiliko kwenye jamii yao. Lengo la Mzee Gae katika kuwasimulia kisa cha nyuki lilikuwa ni kuwapa moyo vijana hawa, kwamba wasiwe na woga, watimize wajibu wao hata kama wangepatana na maafa. Kwa kuwa kama anavyosema Mzee Gae, licha ya nyuki kuonekana kuwa ni kiumbe dhaifu na mnyonge, madhara yake ni makubwa hasa anapokuwa na hasira. Dhana ya nyuki inazua maana ya ziada kisemiotiki ambapo nyuki licha ya kuwa ni mdudu, anasawiriwa kama kiwakilishi cha watu

waliokuwa wanadhulumiwa, wanyonge, waliodharauliwa na kuonekana kuwa hawakuwa na uwezo wowote. Hata hivyo kudhulumiwa kwao kwa muda mrefu kungewapa nguvu na ari mpya ya kukabiliana na adui jinsi nyuki anavyokabiliana na adui wake anapopatwa na hasira. Nyuki ni mdudu ambaye anapomchoma mtu hatima yake huwa ni kifo ila kitendo chake hutokana na azimio lake la kuilinda jamii yake kutokana na adui. Vivyo hivyo vijana walihitaji kujitolea mhanga kuipigania haki yao bila kujali matokeo ya kitendo hiki. Vijana walipaswa kuwa tayari kwa matokeo yoyote yale na kujua kuwa kitendo chao kingeweza kuwaangamiza, jinsi ambavyo nyuki humshambulia adui licha ya kufahamu kuwa hatima yake ni kifo, Hata hivyo, kifo chao kitakuwa kimetuma ujumbe kwa wanyanyasaji kwamba watu wanazitambua haki zao na watazipigania na hivyo basi watachukua tahadhari kuhusu jinsi wanavyoendeleza mambo katika jamii.

Mfano mwingine wa matumizi ya hadithi fupi unajitokeza pale ambapo Mzee Gae alifikishwa mahakamani pamoja na wenzake. Mwandishi anaeleza kuwa washukiwa wote, isipokuwa Mzee Gae walikataa kujitetea. Hata hivyo, kujitetea kwa Mzee Gae hakukuwa kwa kawaida. Alijitetea kwa kutoa kisa cha nyoka na chura. Nyoka ni aina ya mnyama ambaye anaweza kumudhuru mtu au mnyama kutokana na sumu iliyopo mdomoni mwake. Sumu hii humwathiri mtu au mnyama anayeumwa na nyoka kiasi kwamba anaweza kuaga dunia. Kwa hivyo nyoka ni mnyama hatari. Nyoka hana uwezo wa kuona vizuri ila hutumia ulimi wake ili kuyafahamu mazingira yake. Tofauti na nyoka, chura huwa na uwezo mkubwa wa kuona hasa wanapokuwa katika sehemu ambayo hakuna mwangaza wa kutosha. Kadhalika, chura wanaweza kukimbia kwa kasi.

Katika kisa cha nyoka na chura, Mzee Gae alieleza namna ambavyo chura hukimbia na kujificha shimoni mwake anapofukuzwa na nyoka. Huko shimoni, chura hutulia

huku akiwa ameweka kinywa chake wazi akimsubiri nyoka. Nyoka naye bila tahadhari, huku akifikiria kuwa anaingia shimoni, hujichoma kinywani mwa chura. Hatimaye chura hufumba kinywa chake. Licha ya jitihada za nyoka kujinasua, chura huzidi kujitumua na kuvimba pale shimoni na mwishowe kumdhibiti nyoka. Nyoka anaishiwa na pumzi na kufa. Mzee Gae alihitimisha hadithi ya nyoka na chura kwa kusema hivi:

> Na hii huthibitisha kwamba ijapo kuwa kila siku nyoka humwinda chura, iko siku japo moja, chura humwinda nyoka kwa ajili ya kujihami…chura humwua nyoka bwana, sikatae…usikatae… (Mohamed, 1980, uk. 114).

Hadithi ya nyoka na chura inachora taswira ya namna nyoka anavyoangamizwa na chura ambaye mwanzoni huwa ndiye mdhulumiwa. Taswira ya namna nyoka anavyommeza chura inajitokeza katika kauli ya Mzee Gae alipopelekwa mahakamani pamoja na wenzake baada ya jaribio lao la kuvamia gereza kutibuka. Alipopewa fursa ya kujitetea, alimwambia hakimu maneno yafuatayo kama njia yake ya kujitetea:

> Nyoka tokea lini kumpa chura nafasi ajitetee? Ni undanganyifu tu; sisi tuko hapa, na nyinyi mko huko, tumezeni kama mlivyozowea kumeza, tumezeni, tumezeni, sisi tumo kinywani mwenu. Maneno yatasaida nini? Maneno hayatasaidia kitu; hayatasaidia kuzuia uchu wenu. Tumezeni; hamna haja kutuuliza mtumeze vipi. Tokea lini nyinyi kufundishwa kumeza? (Mohamed, 1980, uk. 113).

Kutokana na maneno ambayo Mzee Gae anamwambia hakimu, inabainika kuwa nyoka ndiye mwenye nguvu na uwezo wa kumdhulumu chura. Hata hivyo kupitia kwa kisa cha nyoka na chura alichosimulia kuna uwezekano wa hali hii kubadilika. Kupitia kwa hadithi hii ya Mzee Gae, Said Ahmed Mohamed anaangazia suala muhimu kuhusu mabadiliko.

Nyoka ni kiwakilishi cha watu wanaowadhulumu wengine ilhali chura ni kiwakilishi cha watu wanaodhulumiwa. Nyoka ndiye mdhulumu lakini anaishia kuwa

mdhulumiwa pale ambapo chura anatumia uwezo wake wa kukimbia na uwezo wake wa kuona vizuri mahali penye giza ili kukabiliana na hatari ya kuuawa na nyoka. Katika mazingira ya kawaida mdhulumu ndiye humdhibiti mdhulumiwa lakini, kutokana na hadithi ya Mzee Gae inabainika kuwa kuna wakati ambapo uhalisia huu utabadilika; wakati ambapo mdhulumiwa atakapoamua kutumia ujanja, busara na jitihada zake ili kumdhibiti mdhulumu na kumwangamiza jinsi ambavyo chura alimwangamiza nyoka.

Baada ya masimulizi yake hakimu alimwona Mzee Gae kama mwendawazimu na hivyo akamwamuru azungumzie mambo yaliyohusu kesi hiyo asitoe '*hadithi za Aesopo.'* Jibu alilolitoa Mzee Gae liliwachekesha watu wote pale mahakamani. Walionekana kutoelewa ujumbe uliokuwa katika hadithi ya Mzee Gae kwa kuwa kama hakimu anavyosema; walimchukulia kama mtu mwenye upungufu wa akili.

Matukio yanayotangulia kufikishwa mahakamani kwa Mzee Gae na wenzake yanashahibiana pakubwa na matukio halisi yaliyoshuhudiwa wakati wa mapinduzi ya mwaka wa 1964 huko kisiwani Zanzibar. Mapinduzi haya yalitokana na hali ya wakazi wa Zanzibar kutoridhika na uongozi wa kiimla uliokuwa kisiwani humo na kama anavyosema Ohly (1981), mapinduzi haya yalikuwa kilele cha tofauti za kitabaka na kikabila zilizokuwa zimekithiri huko kisiwani.

Kulingana na Wilson (2013), inakisiwa kuwa thuluthi moja ya Waarabu waliokuwa wakiishi katika kisiwa cha Unguja waliuawa wakati wa mapinduzi yaliyotokea kisiwani humo katika mwaka wa 1964. Wengine walilazimishwa kuhamia kwingine mapinduzi haya yalipotokea. Waarabu waliobaki walinyang'anywa mashamba yao na kunyimwa ajira serikalini. Huu ndio ulikuwa mwisho wa miaka mia moja na hamsini

ya utawala wa kiuchumi na kitamaduni wa Waarabu na Wahindi waliotoka maeneo ya Asia Kusini.

Katika sehemu hii imebainika kuwa ulemavu wa Mzee Gae unatumiwa na mwandishi kuashiria matukio yaliyotokea kisiwani Zanzibar. Matukio haya yalisababisha mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kisiwani humo. Ulemavu wa Mzee Gae umetumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui ya kimapinduzi ambapo ulemavu wake unajitokeza kama nyenzo ya kuwazindua na kuwahamasisha wanajamii ili waweze kuchukua hatua ya kubadilisha hali ya dhuluma na unyanyasaji iliyokuwa ikiwazunguka. Masuala yanayopatikana katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* yanatoa taswira ya hali ilivyokuwa Kisiwani Zanzibar kabla ya mapinduzi. Hatima ya Kisiwa hiki inaweza kulinganishwa na mapinduzi yaliyotokea katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Mzee Gae alitekeleza wajibu mkubwa katika kuanzisha mapinduzi hayo kwa kuwa alikuwa mstari wa mbele katika kuwazindua wanajamii na kushiriki katika harakati za kuleta mabadiliko licha ya wanajamii kumchukulia kama mtu mwenye ulemavu wa akili.

### 2.3 Ulemavu wa Akili kama Mtindo wa Kuwasilisha Maudhui ya Malezi

Sehemu hii itashughulikia ulemavu wa akili na namna ambavyo umetumiwa katika kuwasilisha maudhui ya malezi. Kwa mujibu wa Alayi (2013), kuna uhusiano mkubwa kati ya mbinu za malezi na ulemavu wa akili miongoni mwa wasichana waliobaleghe. Alayi anadai kwamba kuna mbinu za malezi zinazoweza kusababisha ulemavu wa akili, mfadhaiko, wasiwasi na utovu wa nidhamu miongoni mwa wasichana waliobaleghe. Mtindo wa malezi ni suala la mtazamo wa kisaikolojia unaowakilisha mbinu ambazo wazazi hutumia katika kuwalea watoto wao. Kwa mujibu wa Halpenny na wenzake (2010), familia ndiyo mazingira ya kimsingi ambapo maisha ya watoto wengi hupewa mwelekeo. Kigezo muhimu katika mfumo

wa kuwingiza mtoto katika jamii ni mbinu za malezi na namna ambavyo wazazi hukabiliana na nidhamu ya watoto wao. Mbinu za malezi hutawaliwa kwa kiwango kikubwa na kaida na matarajio ya jamii. Kaida hizi ni kama imani za kitamaduni, dini na sheria zinazotawala imani na desturi mbalimbali za jamii.

Watoto wanapokua, wanapitia hatua mbalimbali za maisha. Katika kila hatua, wazazi huibua mbinu mbalimbali wanazotumia kuwalea watoto wao. Mbinu hizi hutawaliwa na wakati na upekee wa kila mtoto. Utamaduni pia unaathiri pakubwa mbinu zinazotumiwa na mzazi katika malezi ya watoto.

Darling na Steinberg (1993) na Spera (2005) wanasema kuwa kuna tofauti kati ya mbinu za malezi na mtindo wa malezi. Mbinu za malezi ni tabia mahsusi ambazo wazazi hutumia katika kuwalea watoto wao ilhali mtindo wa malezi unahusu mazingira ya kihisia na kiakili ambayo wazazi huwalelea watoto wao.

Kwa mujibu wa Erikson (1959) na Carpentier (2010), wanasaikolojia wanaohusika na masuala ya kukua kwa mtoto, kuna hatua nane ambazo mtoto lazima apitie anapokua kutoka utotoni, anapobaleghe, hadi anapokuwa mtu mzima. Ili kuingia katika hatua inayofuata, mtoto lazima aweze kukabiliana na mkinzano fulani ambao anahitaji kutatua katika hatua husika. Katika kila hatua mtoto ni lazima aelewe na kutatua mkinzano wa mambo mawili yanayomkabili. Kwa hivyo mzazi hana budi kutumia mbinu zinazofaa kumwelekeza mtoto katika kila hatua.

Kulingana na Barber na wenzake (2005) malezi yanayolenga kubadilisha fikra au hisia za mtoto na kupuuza maoni yake kunaweza kusababisha tatizo la akili baadaye maishani. Kadhalika, kunaweza kusababisha utovu wa nidhamu wa mtoto husika baadaye katika maisha yake. Madai ya Barber na wenzake yanathibitishwa kupitia kwa mhusika Asumini katika riwaya ya *Tata za Asumini*. Asumini anadhihirisha tabia

ambazo zinaashiria kuwa ana tatizo la akili. Inabainika kuwa tatizo lake lilitokana na malezi. Asumini alilelewa katika mazingira ambapo maadili yalisisitizwa. Mwandishi anaeleza:

> Mradi ilikuwa daima, fanya hivi au usifanye vile au usifanye hivi fanya vile, Asumini alikulia tetesi, lawama na hujuma kwa mwili wake mwenyewe ambao alitaka aufanye apendavyo. Jumlisho la yote hayo ilikuwa machozi na kilio na tokea hapo kukukua, kupenyapenya, hicho kitoto kikakua, kama mgomba, mnazi unakawia. Lakini siku zote hizo msisitizo ulikuwa uleule. Alikua nao ukapenya kwenye bongo lake na kurishai ndani ya fahamu yake hata ukageuka ukawa nafsi yake-ukawa yeye Asumini na Asumini akawa mchocheo mtupu. Na malezi ya babaake na mamaake yakawa malezi na kulemaza wakati mmoja. (Mohamed, 1990, uk.19).

Mwandishi anaeleza namna malezi ya Asumini yalivyokuwa tangu utotoni. Anasema kuwa wazazi wa Asumini hawakubadilisha mbinu zao za malezi kulingana na umri wa Asumini ila waliendelea kusisitiza mambo yale waliyokuwa wakisisitiza hata baada ya Asumini kubaleghe. Athari za malezi ya wazazi wake Asumini kama anavyoeleza mwandishi ni kuwa yalimwingia katika nafsi na kumlemaza akili Asumini.

Kwa mujibu wa Kimble na wengine (1980), wazazi huonyesha kuwa wanawapenda na kuwajali watoto wao kupitia mbinu mbalimbali za malezi ambazo wanatumia kuwapa wasia na kuelekeza tabia zao. Baumrind (1975), anatambua aina tatu za wazazi kwa kuzingatia mbinu za malezi wanazotumia. Anasema kuwa kuna wazazi wanaotumia mbinu ya kimabavu. Wazazi hawa wanawalea watoto wao kimabavu na wanaamini kuwa mtoto lazima atii yale anayoambiwa na hana uhuru wa kuuliza maswali yoyote. Erikson (1959) anasema kuwa watoto wanaolelewa katika mazingira ambapo wazazi hutumia mtindo wa malezi wa kulazimisha wanadhihirisha tabia ya kujidharau na kujilaumu wao wenyewe. Katika kujaribu kukabiliana na mawazo yao,

watoto hawa hujiingiza katika matumizi ya mihadarati na kuna uwezekano mkubwa wa watoto hawa kuwa na mawazo ya kujitoa uhai.

Baumrind anaendelea kusema kuwa aina ya pili ya mzazi ni yule ambaye humpa mtoto uhuru ili aweze kukabiliana na mazingira tofauti anayokumbana nayo maishani. Aina ya tatu ya mzazi ni yule ambaye anatumia mbinu ya kuamrisha. Mzazi anayetumia mbinu ya kuamrisha humwelekeza mtoto kwa njia yenye mantiki huku akizingatia masuala ambayo mtoto anakumbana nayo maishani. Kwa mujibu wa Baumrind, malezi yanayoshirikisha mbinu za mzazi wa tatu ndiyo yanayofaa zaidi kwa kuwa watoto hukua wakiwa wanajamii wanaowajibika, walio huru, wenye bidii na ufanisi.

Kutokana na maelezo ya Baumrind inaelekea kuwa wazazi wa Asumini walitumia mbinu ya malezi ya kulazimisha au ya kimabavu katika kumlea Asumini kwa kuwa hakuwa na uhuru wa kutoa maoni yake ila alihitajika tu kutii yale aliyoambiwa na wazazi wake. Wazazi wake daima walikuwa wanamwelekeza kuhusu ni mambo yapi alipaswa kufanya na ni yapi hakustahili kufanya bila kumpatia uhuru wa kuchagua kile alichokuwa anataka kufanya na kama anavyosema mwandishi jambo hili lilimlemaza Asumini akili. Mwandishi anadhihirisha haya anapoeleza namna malezi ya Asumini yalivyokuwa:

> Anajikumbukia Asumini, alipokuwa mdogo, maisha yake yalikuwa kama sahani ya wali aliyokuwa akipewa: mchuzi juu na kichinyango cha nyama, naye ilimbidi apokee mambo kwa unyonge kama alivyoipokea sahani ya wali. Alipokea kila jambo bila ya kulalama; angependa asipende, angetaka asitake, kwani hicho kilikuwa chakula pekee alichopewa, kama angeringa, angebaki muflisi! Basi akajikuta anakula chakula cha mambo hayo kwa hayo hata yakamkaa moyoni yakamchosha. Kama si wali, muhogo, kama si muhogo, ndizi na kinofu cha nyama au kipande cha samaki, nguru au papa kavu. (Mohamed, 1990, uk. 101).

Mwandishi anaeleza namna maisha ya Asumini yalivyokuwa wakati alipokuwa mdogo. Anatumia tashbihi kama kipengele cha mtindo ambapo anafananisha maisha ya Asumini na chakula alichokuwa akila kila siku. Asumini alilazimika kula chakula hicho bila kulalamika. Chakula kilikuwa ni kile kile kila siku mpaka kikamchosha lakini hakuwa na la kufanya ila kuhiari. Mwandishi anaeleza kuwa Asumini alipokea kila kitu kutoka kwa wazazi wake bila kulalamika kwa kuwa hakuwa na budi kufanya hivyo. Hakuwa na njia mbadala au mtu mwingine ambaye alimtegemea. Chakula kimetumiwa kimtindo kama jazanda inayowakilisha mawaidha aliyokuwa anapewa Asumini kila siku na wazazi wake. Licha ya kuwa alichoshwa na kurudiwarudiwa kwa mawaidha hayo, kama anavyoeleza mwandishi, ilibidi ayazingatie bila kulalamika. Hii ni kwa sababu hakupata nafasi ya kupewa mawaidha na mtu mwingine yeyote yule. Alitegemea mawaidha ya wazazi wake pekee na hakupata mengine isipokuwa hayo. Vipengele vya kimtindo vinabainika kupitia matumizi ya tashbihi na jazanda. Matumizi ya vipengele hivi yalimfaa mtafiti katika kubainisha tabia za Asumini zinazoashiria kuwa alikuwa na ulemavu wa akili uliosababishwa na malezi ya kimabavu.

Kama wanavyodai Darling na Steinberg (1993), mtindo wa malezi unaofaa ni ule ambao humpatia mtoto nafasi na uwezo wa kukabiliana na mazingira tofauti kwa njia yenye uwazi kulingana na umri wake. Wazazi wa Asumini walimlea Asumini bila kuzingatia kuwa alikuwa akibadilika kiumri. Kama anavyosema mwandishi, siku zote walimchukulia kama mtoto tu:

> Wazee wake walimwona Asumini kimalaika cha Mungu tu. Na wala si kwa utoto uliojaa udanganyifu na hadaa, bali kwa utepetevu na ujanajike wake ambao wazee walitambua utakuwa ukipigiwa vita tokea mwanzo mpaka mwisho. Wakachukua juhudi kumlinda kama wazee wote wanavyofanya. Wakafuata miiko na wajibu wote uliowekwa kumlea mtoto wa kike. (Mohamed, 1990, uk. 101):

Mwandishi anaeleza kuwa malezi ya Asumini yalijikita zaidi kwenye jinsia yake ya kike. Wazazi wake walitumia mbinu ya malezi ambayo kwa maoni yao ingemlinda Asumini kutokana na changamoto ambazo angepatana nazo kama mtoto wa kike. Hata hivyo, inadhihirika kuwa malezi yao hayakumtayarisha Asumini kukabiliana na mabadiliko ya kimazingira ambayo alipatana nayo pindi tu alipotoka pale kijijini alikolelewa. Kwa hivyo, pakawa na mkinzano kati ya mambo aliyokuwa amefundishwa na yale aliyoyapata katika mazingira ya mjini alikoenda kusomea. Mwandishi anasema:

> (Asumini) alihisi machungu ya mkinzano wa malezi yake, akaona machungu ya mkinzano wa elimu yake, akaona machungu ya mkinzano wa nje uliomo katika jamii yake: mvutano wa nafsi yake na yaliyoko nje yake, mvutano wa malezi yake na madhehebu ya watu wengine wengi, mvutano wa elimu na ujinga ulioenea pasi na kuweza hata kuusemea…mvutano wake na mahubiri matupu ambayo sasa yamekuwa maisha yenyewe; mvutano wa mahubiri na ukweli wa mambo unaochonota na kubabua kama upupu na kutia wazimu. Asumini au "maisha" yake tuseme, yalikuwa sarafu moja yenye nyuso mbili tofauti: mmoja mwangavu na mwingine kiza! Na mgongo wa sarafu yenyewe si duara safi bali wenye mikatomikato na mikwaruzokwaruzo kama gwaru la shilingi tano. (Mohamed, 1990, uk. 101).

Mwandishi anaeleza mawazo yaliyokuwa mawazoni mwa Asumini baada ya kukutana na Mkenjel, mwanamume aliyekuwa akimtaka kimapenzi. Hata baada ya kukubali kukutana na Mkenjel, Asumini hakukubali kushiriki ngono na yeye ila alimtoroka alipokumbuka mafunzo aliyokuwa amepewa na wazazi wake. Kisa hiki kilimfanya Asumini kulemewa na mawazo kiasi kwamba alihisi uchungu wa mkinzano kati ya malezi yake na nafsi yake.

Mwandishi anaashiria kuwa akili ya Asumini iliathirika kutokana na mvutano kati ya hisia zake na mafundisho aliyokuwa amepewa na wazazi wake hasa kuhusu namna mwanamke anavyopaswa kuishi. Mvutano huu ulitokana na tofauti kati ya mafundisho aliyopewa na wazazi wake, mafundisho ya elimu, mafundisho ya dini na

mafundisho aliyoyapata kutokana na utangamano wake na ulimwengu kwa jumla. Tofauti hizi zilimfanya Asumini kuchanganyikiwa kwa kuwa hakujua ni yapi yaliyofaa zaidi. Katika kueleza kiwango cha kuathirika akili kwa Asumini mwandishi anasema:

> Upeo ulianza kujitokeza kwa ishara dhahiri. Mambo yamejilimbikiza kwa miaka, nayo yamechukua uzito juu ya nafsi ya Asumini na sasa yamefikia upeo… Mara nyingine yeye mwenyewe alijihisi jinsi uzito wa mambo ulivyomwelemea. (Mohamed, 1990, uk. 100).

Mwandishi anaeleza kuwa malezi aliyokuwa amepewa Asumini yalikuwa yamemwathiri kwa miaka mingi kiasi kwamba hangeweza tena kustahimili. Asumini alihisi uchungu kutokana na kushindwa kubainisha ni mambo gani aliyopaswa kuzingatia kati ya mawaidha aliyopewa utotoni na mambo aliyokutana nayo katika mazingira tofauti.

Kupitia mivutano hii Said Ahmed Mohamed anasisitiza nafasi ya asasi mbalimbali katika malezi ya watoto. Aidha, ulemavu wa akili uliomkumba Asumini ni ishara ya hatari inayoweza kutokea ikiwa hakutakuwa na maelewano kati ya asasi zote zinazochangia katika malezi ya mtoto.

Said Ahmed Mohamed ametumia tanakuzi, mbinu ya kimtindo inayoonyesha mkinzano ili kusisitiza mvutano uliomkumba Asumini na kusababisha kulemaa kwake akili. Anasema:

> Asumini alikuwa akiishi malimwengu mawili, nje na ndani. Nje anaongozwa na tashwishi na mazingira: ule ukweli uliopo, hali halisi na uchafu wake na uvundo wake na_ghasia zake za kutaka hiki na hiki na kubadilisha hiki na hiki na kwenda na tamaa na kuiga na kufanya na kufanyiza na jua na mvua, kipepo na kimbunga na ukame, na tone au bahari au mafuriko na macho yanayoona na masikio yanayosikia na ulimi unaoonja hisia ya mwili mzima-mwili mzima! (Mohamed, 1990, uk. 56).

Mwandishi anaeleza mawazo ya Asumini alipokuwa anataka kufanya maamuzi iwapo angeenda '*disco*' na Miriam rafiki yake pamoja na Sawe na Moody. Ingawa alikuwa amemhakikishia Miriam kuwa angeandamana naye mawazo yake yanadhihirisha kuwa hakuwa na uhakika na alipata ugumu kuamua iwapo angeenda au hangeenda.

Mwandishi anatumia tanakuzi mbalimbali ili kueleza hali ya mkinzano uliomkumba Asumini. Tanakuzi ni mbinu ya kimtindo inayotumiwa kusisitiza ujumbe kwa kuambatanisha maneno yenye maana kinzani. Kwa mfano ametumia 'nje na ndani' ambapo nje inaashiria mazingira halisi yaliyokuwa yanamzunguka Asumini na ndani inaashiria mazingira alimolelewa pale nyumbani kwao. Asumini aliuona ulimwengu wa nje kama uliojaa maovu ya kila aina tofauti na ulimwengu uliokuwa katika nafsi yake, ulimwengu usiokuwa na uhalisia, ulimwengu uliojikita katika mafunzo aliyopewa na wazazi wake tangu utotoni. Mwandishi anazidi kuonyesha tofauti za 'malimwengu' haya mawili kwa kutumia tanakuzi ya jua na mvua, kipepo na kimbunga na ukame, na tone na bahari au mafuriko. Anaashiria kuwa panapo na jua hapawezi kuwa na mvua. Mawaidha aliyopewa Asumini utotoni ni kama kipepo tu ambacho hakikumwandaa vizuri kukabiliana na changamoto katika ulimwengu halisi. Aidha, mafunzo aliyopata aliyaona kama tone tu la maji, hayakumtayarisha ipasavyo kukabiliana na ulimwengu halisi uliojaa maovu yani uchafu, uvundo, ghasia na tamaa. Kadhalika, Asumini alitatizika kimawazo zaidi kwa kuwaona wanafunzi wenzake pale chuoni wakiyafanya mambo aliyokuwa amekatazwa na anapigana na nafsi yake na mwili wake kwa kuwa alitamani kuwaiga.

Katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mwandishi anazungumzia kuhusu suala la malezi kupitia mhusika Rosa. Rosa alijiingiza katika tabia ya uzinzi alipojiunga na chuo cha walimu. Tabia yake ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi

iliwafanya wanafunzi wenzake kusema kuwa alikuwa na ulemavu wa akili. Mwandishi anatumia sitiari na ambapo wanafunzi walimwita Rosa mwehu ili kuelezea mtazamo wao kumhusu Rosa. Anaeleza:

> Siku hiyo yote wanafunzi walikuwa wakizungumza juu ya Rosa: wengine walisema kwamba alikuwa punguani; wengine walisema alikuwa mwehu; wengine walisema kwamba malezi yake yalikuwa mabaya; na kadhalika. Lakini wengi walimsifu kwa kusema kwamba hapakuwa na msichana mwingine aliyeweza kuendesha maisha kama yeye. (Kezilahabi, 1976, uk. 67).

Wanafunzi wanasema maneno haya wakati Rosa alipofukuzwa chuoni kutokana na tabia yake ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengi. Wanafunzi wenzake Rosa walimwona Rosa kama mtu aliyekuwa na ulemavu wa akili.

Mwandishi wa riwaya ya *Rosa Misitika* analenga kuwasilisha maudhui ya malezi kwa kutumia tabia ya Rosa ambayo kulingana na mtazamo wa wanafunzi wenzake inaashiria kuwa ya mtu aliyekuwa na ulemavu wa akili. Mtazamo wa wanafunzi kuhusu Rosa unadhihirisha kuwa tabia yake haikuwa ya kawaida. Katika kujaribu kubainisha sababu za Rosa kuwa na tabia ya kushiriki ngono kiholela, wanafunzi wanaibuka na maoni mbalimbali. Baadhi ya wanafunzi walionelea kuwa huenda tabia yake ilitokana na ulemavu wa akili na kwamba Rosa alikuwa mwendawazimu. Wengine walisema kuwa huenda tabia yake ilitokana na malezi mabaya.

Rosa alilelewa katika mazingira ambapo baba yake aliwadhibiti Rosa na dada zake sana. Hawakuruhusiwa kutangamana na yeyote hasa wavulana lakini Rosa alipojiunga na chuo alipata uhuru wa kufanya alivyotaka mbali na uangalizi mkali wa babake na hapo ndipo tabia yake ilivurugika. Mtindo wa malezi wa baba yake Rosa unajitokeza kutokana na jinsi alivyowalinda binti zake kutokana na utangamano wa aina yoyote na wanaume. Kwa mfano, Mkuu wa Wilaya aliyekuwa rafiki wa kiume wa Rosa

alipofika nyumbani kwa Zakaria kumchukua Rosa waende wakajivinjari ufukoni, Zakaria alimfukuza.

> Rudi na motokaa yako! Unafikiri hapa kuna wasichana wengi wa kuchukua na gari. Toka hapa! Masikio makubwa mithili ya punda! Na wewe Rosa usitoe pua yako nje! Nisikuone unatoka hapa! (Kezilahabi, 1976, uk. 58).

Zakaria alikuwa amelala lakini aliposikia mlio wa motokaa nyumbani kwake aliamka, akatoka nje na kuanza kumfokea Mkuu wa Wilaya. Zakaria alimfukuza Mkuu wa Wilaya huku akimtukana. Mwandishi anatumia nidaa na tashbihi kueleza kuchukizwa kwa Zakaria na Mkuu wa Wilaya alipokuja kumchukua Rosa. Anamwambia kuwa masikio yake yalikuwa kama ya punda kuashiria kuwa alikuwa mwenye sura mbaya na hakustahili kuwa mpenzi wake Rosa. Nidaa ni mbinu ya kimtindo inayoashiria hasira na msisitizo.. Alimuonya Rosa binti yake kuwa asithubutu kutoka pale nyumbani. Tabia ya Zakaria inaashiria kuwa alitumia mtindo wa kimabavu katika kuwalea watoto wake.

Kwa mujibu wa Kroger (1996) watoto wanaolelewa katika mazingira ambapo wazazi hutumia mtindo wa malezi wa kimabavu huwa na nidhamu ya hali ya juu, ni wanyamavu na hawana furaha. Hata hivyo, watoto hawa huathiriwa na mfadhaiko. Mara nyingi wanapobaleghe watoto hawa huwaasi wazazi. Madai ya Kroger yanathibitishwa katika makabiliano yaliyotokea siku moja kati ya Rosa na baba yake wakati ambapo baba yake alijaribu kumkataza kwenda matembezini na rafiki yake Mkuu wa Wilaya. Mwandishi anaeleza:

> Rosa alikuwa tayari amekwishakata shauri juu ya jambo hili. Alingoja kuchokozwa. Kweli Zakaria alichokoza mzinga wa nyuki. Rosa alitoka nje ghafla. Alikwenda mpaka karibu na baba yake. Alitapika maneno. Maneno haya alikuwa ameyatunza moyoni mwake kwa muda mrefu. “Kila wakati unatuchunga. Unafikiri utatuoa wewe!” Rosa mwishowe aliyasema yale maneno. Maneno aliyopaswa kusema siku ile aliyopigwa angali msichana. Zakaria aliyapata yote: maneno aliyopaswa kuambiwa siku ile. Maneno hayo

> yalimchoma moyo Zakaria. Alisimama pale kwa muda bila kusema neno. Rosa sasa alitembea huku na huko kwa maringo hali ameinua mabega yake juu. Rosa alishinda. Mbele yake pandikizi la mtu aliloshinda likiwa limesimama bila damu. Damu ilikuwa imeliganda. (Kezilahabi, 1976, uk. 58).

Rosa alighadhabishwa na tabia ya baba yake ya kumfukuza Mkuu wa Wilaya na kumkataza kuandamana na yeye. Mwandishi anatumia kipengele cha mtindo cha sitiari anapofananisha Rosa na mzinga wa nyuki. Mzinga wa nyuki unapovurugwa kuna hatari kubwa kwa kuwa nyuki waliomo ndani hutoka kwa hasira na kumshambulia yeyote aliyewachokoza. Vivyo hivyo maneno ya Zakaria yalimkera Rosa kiasi kwamba hangejizuia kuyasema yaliyokuwa moyoni mwake. Katika kusisitiza hasira yake Rosa, Mwandishi anatumia kauli '*kutapika maneno'* kuashiria kuwa Rosa alitokwa na maneno mengi kwa mfululizo jinsi ambavyo matapishi humtoka mtu. Alitumia nafasi hiyo kumwambia baba yake kutofurahishwa kwake na tabia yake ya kuwadhibiti na kuwanyima uhuru pamoja na dada zake tangu utotoni. Zakaria alionekana kushtushwa na maneno ya binti yake kiasi kwamba alisimama tu bila kusema lolote. Mwandishi anatumia tashihisi anaposema kuwa maneno hayo *yalimchoma moyo* Zakaria. Matumizi ya tamathali hii yanasisitiza kuwa Maneno ya Rosa yalikuwa na athari kubwa kwa Zakaria.

Kauli ya Rosa inabainisha kuwa ingawa hakuwa anafurahishwa na mbinu ya malezi ya babake tangu utotoni, hakuwahi kumwambia ila alijitahidi kuishi kulingana na jinsi baba yake alivyomwelekeza. Tabia ya Rosa ya kutembea huku na huko kwa maringo inaashiria hali ya ushindi na uasi wa Rosa dhidi ya baba yake. Alihisi kuwa amepata uhuru baada ya kumwambia baba yake jambo lililokuwa likimkera tangu akiwa msichana. Kupitia kwa Rosa mwandishi anaashiria kuwa watoto wanapobaleghe wanapaswa kupewa uhuru wa kujiamulia mambo. Zakaria alionekana kutotambua kuwa Rosa alikuwa amekua na kukomaa na alihitaji kutangamana na watu wengine.

Uasi unajitokeza pia katika riwaya ya *Tata za Asumini* ambapo Asumini anafanya kinyume na mambo aliyofundishwa akiwa mtoto. Asumini alipokuwa mdogo alisisitiziwa na mamake kuwa mwili wa mwanamke ni wa kusetiriwa wakati wote na haupaswi kuonekana na yeyote wala hapaswi kujiingiza katika mahusiano yoyote na wanaume. Mama yake alimwambia:

> Mwanangu Asumini—kifua cha mwanamke sharti kitupiwe khanga…Mwili ni sitara, si vyema mtu kumwonesha mwenzake. (Mohamed, 1990, uk. 20, 27).

Mama yake Asumini alikuwa anamwelekeza binti yake kuhusu namna mavazi ya mwanamke yanavyostahili kuwa, kwamba ajisetiri mwili mzima na asimwoneshe yeyote mwili wake. Lakini Asumini anaathiriwa na uhalisi anaoshuhudia anapoishi mjini na kuanza kuudadisi wasia wa mama yake kiasi kwamba alitaka kuvua nguo mbele ya watu. Mwandishi anaeleza:

> Kwa muda mrefu Asumini aliwana na Zaina ambaye alijaribu kumzuia asifanye alivyotaka Asumini (kuvua nguo). "Niachie," alipigana Asumini. "Niachie nivue nguo kila mtu anione… kwani naficha nini nacho?...Niache niuonyeshe ulimwengu faida ya kunyimwa na kukatazwa…niachie…" Sasa Asumini alikuwa akiraruararua nguo zake, na kwa kweli alikuwa keshafaulu kuzirarua mpaka kiunoni, ndipo wanawake walipomwongozea Zaina na kumshika pamoja Asumini. (Mohamed, 1990, uk. 105).

Tabia ya Asumini ya kutisha kuvua nguo mbele ya watu ni mojawapo ya matukio yaliyotokea nyumbani walikokuwa wakiishi Zaina na Asumini. Mwandishi anabainisha kuwa Zaina alikuwa anajua kwamba Asumini alikuwa na matatizo makubwa lakini hakujua ni matatizo yapi hivyo hangeweza kumsaidia. Kwa hivyo, Asumini alipotisha kuvua nguo Zaina alikisia kwamba tabia hii ilitokana na ulemavu wa akili aliokuwa nao.

Kitendo cha kuvua nguo kinaenda kinyume na mafundisho ambayo Asumini alikuwa amepewa na mama yake kuwa mwanamke hastahili kuonyesha yeyote mwili wake.

Kwa hivyo, Asumini alipofanya hivyo aliasi dhidi ya mawaidha aliyopewa na mama yake. Uasi wa Asumini unajitokeza pia wakati alipoamua kucheza beni akiwa amevaa shumizi pekee. Mwandishi anachora taswira hii kwa kueleza namna ambavyo msukumo fulani ulimfanya Asumini kucheza beni bila nguo, jambo ambalo hangelithubutu kulifanya hapo awali. Kitendo hiki chake kilionekana kama cha mtu aliyekuwa na ulemavu wa akili kwa kuwa mtu mwenye akili razini hangeweza kufanya hivyo mbele ya watu. Mwandishi anaeleza:

> Asumini akakatika, akademka, akapeta na kupeteka mbele ya mastaajabu ya kila aliyemjua: na ohoo, mji umepata nini? Dunia imeharibika, mwanamke kucheza beni na kishumizi tu, a-a, mambo yamezidi. Asumini hajapata kucheza beni hata siku moja, seuze kucheza beni na shumizi. Leo alicheza na kutia fora. Asumini hakujijua wala kujitambua. Aliongoza mbele huku vile vile kazungukwa na watoto wahuni waliomfanyia kila vitimbi. Asumini hakujitambua, hakuona, hakusikia kitu kingine ila beni. Madadi yalimpanda, akahisi anainuliwa hewani, anaelea katika hewa ya shangwe na hoihoi, katika hewa ya vifijo na nyimbo. (Mohamed, 1990, uk. 145).

Said Ahmed Mohamed anaeleza hatua kwa hatua namna ambavyo Asumini alivyokuwa anacheza beni. Kitendo hiki kiliwastaajabisha watu kwa kuwa halikuwa jambo la kawaida kwa mwanamke kucheza beni akiwa amevaa kishumizi pekee.

Maelezo ya mwandishi hapo juu yanabainisha kuwa mwandishi anasisitiza mshangao wa wanajamii kwa kutumia msemo ‘*dunia imeharibika.*’ Msemo huu unaashiria uozo wa kimaadili kwa kuwa ingawa wanawake walikuwa wakicheza beni, wanajamii hawakupata kumuona mwanamke akicheza beni na kishumizi pekee. Aidha, mwandishi anasema kuwa wanajamii waliyaona ‘*mambo yamezidi’* kumaanisha kuwa tabia ya Asumini waliyoshuhudia ilipita mipaka ya matarajio yao. Katika kuelezea ustadi wake wa kucheza beni, mwandishi anasema kuwa Asumini ‘*alitia fora’*. Aidha, kauli kuwa ‘*hakujijua wala kujitambua’* inaashiria kuwa Asumini alikuwa katika hali ambapo hakuelewa alichokuwa akifanya. Kwa kawaida watu wenye ulemavu ndio

huwa na tabia ya kukaa nusu uchi na kufanya mambo bila kujali watakayoyasema wanajamii wengine. Inaelekea kuwa Asumini alikuwa katika hali ya mfadhaiko kiasi kwamba hakujua wala kujali alichokuwa akifanya.

Mwandishi anaendelea kueleza tabia ya Asumini anaposema kuwa *madadi yalimpanda*. Madadi ni mori unaompanda mtu kutokana na kupenda sana kitu na kumfanya kutenda jambo bila kujitambua. Inabainika kuwa Asumini alikuwa anafurahia uchezaji wake kwa kuwa alijihisi kama *anaelea katika hewa ya shangwe na hoihoi, hewa ya vifijo na nyimbo*. Mwandishi anatumia nahau hii kudhihirisha raha na utulivu aliokuwa nao Asumini. Kwa kuzingatia maana ya ziada ya kisemiotiki, hali ya kuelea hewani, inaashiria uhuru aliojihisi kuwa nao kwa kuwa alikuwa anafanya mambo bila kujali maoni ya wanajamii kuhusu tabia yake. Tabia yake inaashiria hali ya mtu aliyekuwa amejinasua kutoka kwa mikatale ya kila aina aliyokuwa amewekewa tangu utotoni hasa kuhusu suala la uadilifu wa mwanamke.

Kama anavyosema Kroger (1996), wanaolelewa katika mazingira ya kimabavu wanadhihirisha tabia ya kujidharau na kujilaumu wao wenyewe kutokana na kushindwa kuyadhibiti maisha na vitendo vyao. Katika kujaribu kukabiliana na mawazo yao, watoto hawa hujiingiza katika matumizi ya mihadarati na kuna uwezekano mkubwa wa watoto hao kuamua kujitoa uhai kutokana na mifadhaiko wanayopatana nayo maishani na kuwafanya wavurugike akili. Madai ya Kroger yanadhihirika katika maisha ya Rosa ambapo anaishia kujitoa uhai kutokana na kusalitiwa na kuvunjwa moyo na Charles, mpenzi wake, aliyekuwa amemwahidi kwamba atamuoa. Mwandishi anatumia tukio la Rosa la kujitoa uhai kama ishara ya ulemavu wa akili ambao kiini chake ni malezi yaliyomnyima nafasi ya kufanya maamuzi mwafaka hasa kuhusu suala la mahusano kati ya wanawake na wananaume.

Athari ya malezi aliyoyapata Rosa, inajitokeza katika sehemu ya mwisho wa riwaya ambapo mwandishi ametumia mtindo wa tamthilia ndani ya riwaya kuonyesha Rosa na baba yake wakiwa mbele ya Mungu wakati wa kumhukumu Rosa baada ya kujiua.

> *(Mungu amekaa juu ya kuiti cha enzi. Amevaa miwani mikubwa. Malaika mmoja anapita amebeba karatasi ngumu iliyoandikwa juu yake "Kesi ya Rosa Mistika")*
> MUNGU: Rosa, Kwa nini umejiua?
> ROSA: Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu ya baba yangu
> MUNGU: Zakaria una usemi gani kujitetea?
> ZAKARIA: Ee Mungu wangu. Haya yote yametokea kwa sababu ya ubaya na udhaifu
> wake mwenyewe.
> *Vere, Tu Rosa Mistica es*! [Kweli, wewe ni ua la waridi lenye fumbo!] (anaonyesha chini kwa mkono). *Homines interogabo*! [Nitawauliza watu!] (Kezilahabi, 1980, uk. 98).

Rosa alipoulizwa na Mungu ni kwa nini alijiua, alisema ni kwa sababu ya baba yake. Zakaria alipopewa fursa ya kujitetea alisema kuwa yaliyompata Rosa yalitokana na ubaya na udhaifu wake mwenyewe ila hakupaswa kulaumiwa. Anazidi kueleza kuwa ulimwengu mzima ndio shahidi wake.

Mungu anamwita Rosa ua la waridi lenye fumbo. Ulimwenguni watu hawakuwa wakielewa ni kwa nini Rosa alikuwa anaishi maisha yasiyokuwa na maadili na ndiyo maana wanafunzi wenzake walisema kuwa alikuwa na ulemavu wa akili. Mungu anatumia sitiari ya ua la waridi kuashiria urembo na uzuri wa Rosa lakini licha ya uzuri wake alikuwa kama fumbo ambalo halikueleweka. Fumbo kumhusu Rosa linadhihirika zaidi ikizingatiwa kuwa mwaridi huwa na miba. Miba ni ishara ya dhiki anazopitia mtu anapotaka kulichuma ua la waridi. Licha ya kufahamu changamoto hii watu hustahamili na kujitolea kwa ili waweze kulifikia ua hili. Kadhalika, ua la waridi linapendeza sana. Hata hivyo licha ya uzuri wake, kama ua lolote lile hunyauka haraka na kupoteza uzuri wake. Mungu hakutolea Rosa hukumu moja kwa

moja kwa sababu ya kujiua ila alimdadisi ili kuutafuta ukweli. Aliamua kuwauliza watu wa ulimwengu ili ajue kiini cha maovu aliyoyatenda Rosa. Uamuzi wa Mungu wa kutafuta ukweli kabla ya kumhukumu Rosa unaashiria kuwa ukosefu wa uadilifu unaweza kusababishwa na mambo mengi: mtu binafsi, wazazi na jamii kwa jumla na mtu hawezi kulaumiwa bila kiini cha tabia yake kueleweka vizuri. Aidha ni jukumu la wanajamii wote kuhimiza maadili katika jamii.

Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wanatumia taswira za ulemavu wa akili kuwasilisha maudhui kuwa wanajamii wanapaswa kuzingatia kiini cha upotovu wa maadili miongoni mwa vijana kabla ya kuwalaumu na kuwahukumu kwa kushiriki vitendo vinavyokiuka maadili na matarajio ya jamii. Hii ni kwa sababu malezi ya mtu huwa na athari kuu katika maisha ya mtu, hasa mienendo na hulka yake. Badala ya kuwalaumu vijana hawa, jamii inapaswa kutafuta namna itakavyowaelekeza ili waweze kujinasua kwenye mfadhaiko wa mawazo unaowakabili. Aidha, wazazi wanapaswa kuwa waangalifu na kuwalea watoto wao kwa kuzingatia mbinu na mtindo wa malezi utakaowafaa watoto wao na kuwafanya wawe watu wenye maadili maishani.

Katika sehemu hii ulemavu wa akili umeshughulikiwa kwa kuzingatia namna ambavyo umetumika na waandishi Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya malezi katika riwaya za *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika*. Kupitia kwa wahusika Asumini (*Tata za Asumini*) na Rosa (*Rosa Mistika*), Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wanawasilisha maudhui kuhusu nafasi ya malezi katika maisha ya vijana na namna ambavyo yanatawala mienendo na tabia za mtu binafsi hasa mtoto wa kike. Wahusika hawa wawili wanalelewa katika mazingira ambapo wanadhibitiwa mno kiasi kwamba wanalemaa

akili kutokana na mkinzano wa uhalisi wa maisha na nafsi zao unaojikita kwenye malezi waliyopewa.

## 2.4 Ulemavu wa Akili kama Mtindo wa Kuwasilisha Maudhui ya Maadili

Sehemu hii itashughulikia ulemavu wa akili kwa kuzingatia namna ulemavu huu umetumiwa na waandishi wa riwaya teule kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya maadili. Kwa mujibu wa Elran (2011), masimulizi yanayohusu ulemavu wa akili wakati mwingine huelezea tajiriba na maisha ya waathiriwa, na mitazamo yao kuhusu mambo mbalimbali yanayowazunguka kama vile maadili. Katika riwaya ya *Tata za Asumini*, Said Ahmed Mohamed analenga kuangazia mazingira ya kijamii yaliyokuwepo baada ya wakoloni kuondoka barani Afrika hasa nchini Tanzania. Ukoloni mamboleo ulishamiri miongoni mwa Waafrika katika kipindi hiki. Wanajamii walianza kuthamini tamaduni za kigeni na kupuuza mila na desturi za Kiafrika. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Tata za Asumini* kupitia kwa mhusika mkuu Asumini.

Katika riwaya ya *Tata za Asumini*, mwandishi ametumia taswira ya ulemavu wa akili ili kuwasilisha maudhui ya maaadili na namna yanavyoingiliana na malezi. Asumini, ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Tata za Asumini* ni mfano wa mhusika aliyeathirika na ulemavu wa akili kutokana na udadisi wake kuhusu jamii iliyomzunguka. Anaiona jamii kama iliyojaa uozo wa kila aina kinyume na maadili aliyofunzwa utotoni mwake. Said Ahmed Mohamed anatumia taswira ya ulemavu wa akili kuendeleza maudhui kuhusu namna jamii ilivyozorota kimaadili.

Asumini anashuhudia uozo wa kimaadili anapoenda mjini kwa masomo ya juu ambapo anakutana na watu ambao kwa maoni yake walifanya mambo kinyume na yale aliyokuwa amefundishwa na wazazi wake. Anapojaribu kung’amua ukweli

kuhusu ni tabia zipi alizofaa kufuata kati ya alizoshuhudia na mawaidha aliyopewa na wazazi wake anapata mfadhaiko ambao unamfanya apate ulemavu wa akili. Asumini anashuhudia vijana ambao walikuwa wamejitosa katika raha na anasa, walivaa mavazi ambayo aliyaona hayafai na walikuwa wakishiriki katika mahusiano ya ngono kiholela. Tabia hizi kama anavyoeleza mwandishi ziliashiria watu wenye ulemavu wa akili.

Kwa mfano, mwandishi anachora taswira iliyokuwa kwenye klabu kimoja ambapo Asumini alikuwa amepelekwa na rafiki yake, Miriam. Mwandishi anaeleza:

> Ukumbi wa *disco* ulimkunjukia Asumini kwa zogo na sauti zenye kuziba masikio na harufu kali ya uchachu na tumbaku na ukungu wa moshi uliokuwa ukikorogana na miale ya taa za rangi zilizokuwa zikipwesapwesa na kukonyezana kwa mizani ya muziki, na wale watu uwanjani, kike kwa kiume, wakicheza *kama wendawazimu*. Kijana mmoja mwenye manywele yaliyosokotana na kumwanguka mabegani kwa mtindo wa Rastafari alikuwa akicheza kwa wazimu zaidi kwa kutupa mikono juu na kuchezesha kichwa na kututumua kifua na kujibenua huku na huku na kuzunguka na kurusha miguu na kukatika kiuno. Alikuwa akicheza peke yake. (Mohamed, 1990, uk. 57).

Mwandishi anaeleza hali ilivyokuwa ndani ya klabu. Harufu na moshi iliyokuwa pale inaashiria kuwa mle ndani kulikuwa na watu waliokuwa wanatumia vileo mbalimbali. Taswira ya kijana aliyekuwa akicheza densi inaashiria namna ambavyo vijana katika jamii wamejitosa katika raha na anasa. Aidha, mitindo yao ya mavazi, nywele na uchezaji densi kama wendawazimu, kama anavyodai mwandishi, hakuambatani na maadili na imani ya dini ya Kiislamu na Kikristo ambazo Waafrika walifundishwa na wakoloni. Mwandishi anasema kuwa kijana aliyecheza densi alikuwa na mtindo wa Rastafari. Kwa mujibu wa Barrett (1977), watu wanaofuata imani ya Rastafari hucheza ngoma zenye mdundo maaalum unaoitwa ‘*reggae*.’ Kadhalika wanajulikana kwa namna wanavyokuza na kuzisokota nywele zao kwa mtindo mahsusi. Uvutaji bangi kwao ni jambo la kawaida na lililokubalika kwa kuwa ni mojawapo ya imani na

desturi zao. Aidha, wanahimiza watu wote watumie bangi. Matumizi ya bangi huathiri urazini wao na hata kuwalemaza akili kiasi kwamba wanakosa uadilifu. Mwandishi anatumia taswira ya kijana wa kirastafari ili kuwasilisha maudhui ya jinsi vijana wa kisasa walivyoathiriwa na raha, anasa na tamaduni za kigeni kiasi kwamba wanakosa kujitambua. Wanafanya mambo kama watu wasio na akili razini.

Katika riwaya ya *Tata za Asumini* Said Ahmed Mohamed anaeleza tabia za Asumini zinazoashiria kuwa alikuwa amechanganyikiwa kiakili. Wakati walipokuwa wanaishi na Zaina pamoja na majirani wake ambao walikuwa wanaendeleza biashara ya umalaya, Asumini anadhihirisha tabia ambazo hazikuonekana kuwa za mtu mwenye akili razini. Kwa mfano, kuna wakati ambapo Asumini alizifua nguo zote pale nyumbani walikokuwa wanaishi na wenzake. Kadhalika, alijipiga mswaki mpaka akajichuna ufizi na kumaliza dawa yote ya meno kisha akajisugua miguu mpaka akachubuka ngozi. Aidha, alivivunjavunja vitu pale chumbani mwao na kuwafukuza wenzake kwa madai kuwa wote walikuwa wachafu na waliifanya nyumba chafu kwa laana. Mwandishi anaeleza mawazo ya Asumini:

> Zaina ananambia uwongo leo…anamsingizia baba'ngu bure! Baba'ngu alikuwa safi, safi kabisa, ati leo nd'o anamwita mchafu…nitavunja, nitachana, nitavurugavuruga kila kitu nyumba hii: kila kitu kichafu.'' Asumini alianza kuyaingilia mashuka ya kitanda na kuanza kuyachana, akaziingilia khanga akaanza kuzichana…lakini ghafla aliamua vingine. Aliwacha kuvunja vitu na kuchana nguo akatoka nje kutaka kupigana na watu. "Leo mtanitambua,'' aliwaambia Zaina, Mwatima na Masika waliokuwa nje sasa wamemkimbia Asumini. "Ningojeeni kama nyinyi wanawake kweli. Sitaki abakie mtu nyumba hii leo, nyote kaeni huko huko nje, humu wabakie wazee wangu tu Bi. Time na Bi. Mize." Sasa Asumini alikuwa shetani kamili. (Mohamed, 1990, uk. 143).

Mwandishi anaeleza matukio yaliyotokea pale nyumbani walikokuwa wanaishi Asumini, Zaina na wanawake wengine. Kutokana na maneno yaliyosemwa na Asumini, inabainika kuwa tabia ya Asumini ilitokana na kugundua kwake kuwa baba yake mzazi ndiye alikuwa amemzaa Zaina na kwa hivyo Zaina alikuwa ndugu yake.

Asumini alikerwa na jambo hili hasa kwa kuwa baba yake alikuwa ameuficha ukweli huu kutoka kwake. Kwake Asumini, baba yake hangeweza kutenda kitendo kama hiki huku ikizingatiwa kuwa alikuwa amemlea Asumini kwa njia iliyosisitiza uadilifu maishani. Ni kinaya kuwa baba yake Asumini alikuwa anampa mwanawe mafunzo kuhusu umuhimu wa kuwa mwadilifu ilhali alikuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa na mama yake Zaina. Ni kutokana na uhusiano huu ambapo Zaina alizaliwa. Mwandishi anatumia jazanda ya shetani kudhihirisha namna unafiki wa baba yake Asumini ulivyomwathiri Asumini kiasi kamba alianza kufanya mambo yanayoweza kufungamanishwa na mtu mwenye ulemavu wa akili. Dhana ya shetani ni tamathali ya lugha ambayo inadhihirsha maana ya ndani kisemiotiki kwa namna inavyotumika katika muktadha huu. Mwandishi anasema kuwa Asumini alikuwa '*shetani kamili*.'

Kulingana na Lewis (2001), shetani ni kiumbe dhahania anayefungamanishwa na imani za kidini. Lewis anaendelea kusema kuwa katika dini nyingi Shetani huchukuliwa kama kiwakilishi cha uovu. Aidha, anapewa sifa za kuwa kiumbe mwenye ujeuri, mjanja na anayewapotosha wanadamu kimaadili na kuwafanya wafanye matendo yanayoenda kinyume na matarajio ya jamii. Matendo ya Asumini ya kugombana na wenzake, kuharibu nguo, kuvunja vyombo na kuwafukuza wenzake yanajitokeza kama ya mtu ambaye hakuwa na akili timamu. Tabia yake ilikuwa kinyume na matarajio ya jamii na hivyo ilionekana kuwa ya kishetani.

Mwandishi anatumia sifa ya 'ushetani' kuwasilisha maudhui kuhusu namna jamii inavyomwathiri mtu kimaadili. Kwa mujibu wa Lewis (2001), vijana wanaobaleghe hudhihirisha tabia za 'kishetani' kama njia ya kuiasi jamii na wazazi wao. Uasi huu unatokana na athari za kisaikolojia zinazosababishwa na malezi ya kidini, tajiriba na utamaduni wao. Kwa mfano, tabia ya Asumini inatokana na kuathirika kiakili kwa

sababu ya mikinzano kati ya mafundisho aliyopewa na wazazi wake pamoja na tabia za wazazi wake; hasa baba yake, na uozo alioushuhudia katika mazingira aliyoishi. Asumini alihishi kuwa alikuwa anadanganywa alipoambiwa kuhusu uadilifu. Hisia zake zinadhihirika katika maneno haya yake:

> Kwa nini na mimi nisinywe maji ya kukata kiu…nina kiu mimi wenzangu. Nataka maji baridi yaniburudishe rohoni. Nipeni, niruhusini.' (Wenzake hawakumfahamu. Walimpa maji gilasini). 'Hamnifahamu…Nataka n'nokikosa--- upeo wa kwenda mbio pasi na mtu kuniuliza au kunikemea, pasi na mtu kunitisha, pasi na mtu kunifanya mtoto au kunilea daima. Nataka niingie kwenye fungamano ili nafsi yangu ichague nikitakacho na kinotaka nafsi yangu: nikitake kinitake, nikipende pekee, kinipende pekee. Lakini tatizo ni kwamba naona hadaa tupu—pande zote. Hadaa ya nafsi yangu inayonidanganya. Mimi mwenyewe ninajidanganya na watu wengine wananidanganya.' (Mohamed, 1990, uk. 106)

Asumini aliyanena maneno haya wakati wenzake walijaribu kumdhibiti na kumzuia asiendelee kuharibu vitu na kuwatisha pale nyumbani. Alipoulizwa alikuwa anataka nini ndipo alipowaeleza maneno hayo. Mwandishi anatumia jazanda ya kiu ya maji kama kiwakilishi cha hamu kubwa aliyokuwa nayo Asumini ya kutaka kuwa huru kutokana na imani na makatazo aliyolelewa nayo. Maji ni kinywaji kinachokata kiu. Asumini alikuwa na hamu ya kupata uhuru wake, uhuru huu unawakilishwa na maji ya kunywa kwa kuwa uhuru huu ungemwezesha kukata kiu ya uhuru aliokuwa anatamani maishani mwake. Anahuisha nafsi yake kwa kusema kuwa inamdanganya kama anavyojidanganya mwenyewe na namna anavyodanganywa na ulimwengu.

Kwa mujibu wa Mackenzie (2014), watu wenye ulemavu wa akili huufasiri ulimwengu kwa njia iliyo tofauti na watu wengine. Mawazo na hisia zao kuhusu mazingira yanayowazunguka huathirika sana na ufasiri wao. Kwa mfano, wanaweza kuwa na imani zisizokuwa na msingi wowote, wanaweza kuhisi kuwa wanadhulumiwa au wakaonekana kama kwamba wako ndotoni. Watu wenye ulemavu

wa akili pia huona, hunusa au kuonja vitu ambavyo kihalisia havipo. Zaidi ya hayo wakati mwingine, watu wenye ulemavu wa akili huwatisha watu walio karibu nao na kuanza kuwapiga na kuwafukuza. Madai ya Mackenzie yanadhihirika katika tabia ya Asumini. Mwandishi anaeleza kuwa Asumini alifua nguo zote mpaka zile ambazo hazikuwa chafu. Alijiona mchafu kiasi kwamba aliamua kutumia dawa yote ya meno na kujichuna ufizi. Aidha, alijisugua hadi akachubuka ngozi katika jitihada zake za kuondoa uchafu ambao kihalisia haukuwepo. Zaidi ya hayo, aliwafukuza wenzake kwa madai kuwa walikuwa wachafu.

Mwandishi anatumia ulemavu wa akili wa Asumini katika muktadha huu ili kuwasilisha maudhui kuhusu maadili yanayofungamana na mahusiano kati ya wanawake na wanaume. Uchafu aliokuwa anajaribu kuuondoa Asumini katika mwili wake ni jazanda inayowakilisha mtazamo wake kuhusu suala la ngono. Mtazamo wa Asumini ulitokana na mawaidha aliyopewa na wazazi yake. Kwa mujibu wa mafundisho hayo, uhusiano kati ya mwanamume na mwanamke ulikuwa haufai kwa kuwa wanaume kama Asumini alivyoambiwa na mama yake walikuwa mashetani. Kwa mfano, Sewa, rafiki wake wa kiume alipoenda pale kibandani alikokuwa akiishi Asumini kumtembelea na kuashiria kuwa alikuwa akimtaka kimapenzi, Asumini alimwambia:

> “Mimi sitaki basi, mimi sitaki, utanilazimisha…wanaume wabaya…wanaume mashetani…hata wakikuoa…haramu…hata wakikuoa...haramu…haramu …kabisa.” (Mohamed, 1990, uk. 166).

Asumini alimsisitizia Sewa kuwa hakutaka uhusiano wowote na wanaume kwa kuwa wanaume wote walikuwa mashetani wasioaminika hata katika muktadha wa ndoa. Imani ya Asumini kuwa wanaume wote ni mashetani ilitokana na mawaidha aliyokuwa amepewa na mama yake tangu utotoni. Kwa mfano alipokuwa mdogo,

mama yake alimuonya dhidi ya urafiki wake na Jazume, mvulana aliyekuwa jirani yao. Asumini alionywa na mamake dhidi ya kucheza na Jazume na akaelezwa kwamba atahadhari na ‘ushetani’ wa mwanamume. Mwandishi anaeleza:

> Na ilitokea siku Ki –Asumini kilipomwomba mamake amruhusu afuatane na Jazume mvulana mtoto wa Kiembe, jirani yao, kwenda kupiga ndege, na mama-mtu alijibu kwa ukali, ‘Umesikia wapi mtoto mwanamke kupiga ndege wewe?’ uo mchezo wa kiume’uo!’’ Asumini anapokasirika na kununa anaambiwa, ‘He, mtoto akichaga ‘uyu: nenda, lakini utahadhari na ushetani wa mwanamme mwanangu; kinyaa ‘apo ulipo; utakujajua maneno yangu utakapokuwa mkubwa. Asikwambie Jazume, wala asikushawishi yaso…yaso muruwa ‘uyo Jazume wako.’ (Mohamed, 1990, uk. 27).

Mama yake Asumini hakutaka Asumini aandamane na Jazume na alimjibu Asumini kwa ukali wakati alipoomba ruhusa ya kuandamana na Jazume kwenda kupiga ndege.

Mama yake Asumini hakufafanua alichokuwa akimaanisha kwa kusema kuwa wanaume walikuwa na ushetani ila alimwambia Asumini kuwa angelijua jambo hili atakapokuwa mkubwa. Aidha, alimtahadharisha Asumini asije akashawishiwa na Jazume kufanya mambo fulani yasiyostahili ila hakuelezwa wazi hayo mambo yalikuwa yapi. Mawaidha kama haya yalimfanya Asumini kuamini tangu akiwa mtoto kuwa mwanamume daima ni mbaya. Kutoelezwa kwa uwazi sababu za ubaya wa mwanamume ndiko kulikosababisha kuchanganyikiwa kwake utu uzimani. Kwa mujibu wa Woods (2012), katika fasihi imani mbalimbali kuhusu wanawake na maswala ya ngono zimehusishwa na dalili za matatizo ya akili. Traore (2008) anaendeleza maoni haya ya Woods anaposema kuwa Asumini alizungukwa na ulimwengu uliojaa utumwa wa akili. Kutokana na utumwa huu wa akili, Asumini anajitokeza kama mwanamke aliyetengwa na uhalisi wa ulimwengu alioishi. Imani alizosisitiziwa na mama yake akiwa angali mdogo zinamfanya kuwa mtumwa anayeshindwa kufanya maamuzi kuhusu vipi uhusiano kati yake na mwanamume

ulistahili kuwa huku ikizingatiwa kuwa alikuwa tayari amekomaa. Licha ya kuwa Asumini hakuwa mtoto, aliamini kuwa kujiingiza katika mahusiano ya namna yoyote na mwanamume ni jambo ambalo lingemchafua kimaadili.

Kulingana na Familusi (2011) na Kenyatta (1965), katika jamii nyingi za Kiafrika maadili yanayohusiana na ngono yanathaminiwa sana. Kitendo cha ngono kinapaswa kufanyika baina ya watu waliooana kulingana na mila na desturi za jamii husika. Waafrika walikuwa na miongozo mahsusi iliyotawala kitendo cha ngono. Kwa mfano, kwa mujibu wa Kenyatta, miongoni mwa jamii ya Wakikuyu masuala yote yanayohusiana na ngono huzingatia utaratibu mahsusi unaofungamana na maadili. Hata hivyo vijana walikuwa na uhuru wa kutangamana ili kukuza hisia za mshikamo kabla ya ndoa. Uadilifu na ubikira ni mambo yaliyothaminiwa sana miongoni mwa wanawake waliotarajia kuolewa na hivyo basi yalisisitizwa mno katika malezi ya wasichana. Hii ndiyo sababu Asumini anawaona wenzake wanaofanya kazi ya umalaya kama watu wachafu na wasiofaa kumkaribia. Msisitizo wa umuhimu wa kutoshiriki mapenzi nje ya ndoa wakati mwingine ulifanywa bila kuyaweka kwa uwazi masuala muhimu na wasichana waliachwa katika hali ya taharuki na mkengeuko. Inaelekea kuwa usiri huu kama anavyosema Familusi, ulitokana na imani kuwa masuala yanayohusu ngono yalikuwa takatifu na hayangezungumziwa waziwazi mbele ya watoto. Kayode (1989) anasisitiza maoni ya Familusi anaposema kuwa haikuwa rahisi kuongea kuhusu suala la ngono kwa sababu kimila haikuruhusiwa. Kwa hivyo wazazi wengi hawaongei kuhusu suala hili kwa watoto wao kwa kuwa ni mwiko kufanya hivyo.

Kwa kuzingatia madai ya Familusi na Kayode, ni dhahiri kuwa umuhimu wa kutoshiriki mapenzi nje ya ndoa katika jamii nyingi za Kiafrika ulisisitizwa. Hata

hivyo, msisitizo huu ulifanywa bila kuyaweka wazi masuala muhimu kuhusu kitendo cha ngono na athari zake. Kwa hivyo, wasichana kama vile Asumini na Rosa katika riwaya teule, waliachwa katika hali ya taharuki na mkengeuko kuhusiana na swala la mahusiano ya kimapenzi kati ya wanaume na wanawake.

Katika sehemu hii matumizi ya ulemavu wa akili kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya maadili yamezingatiwa hasa kwa kuangazia namna ambavyo ulemavu wa akili uliomwathiri mhusika Asumini katika riwaya ya Tata za Asumini ulivyotumiwa na Said Ahmed Mohamed kuwasilisha maudhui kuhusu uhusiano uliopo kati ya malezi na maadili miongoni mwa vijana.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Ingawa utafiti huu kwa jumla unazingatia takriban riwaya sita teule zilizoandikwa na waandishi hawa wawili, sura hii imejikita katika riwaya tatu kwa kuwa ndizo zinazodhihirisha matumizi ya taswira ya ulemavu wa akili kama mtindo. Riwaya hizi ni *Dunia Mti Mkavu*, *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika.*

Katika sura hii imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametumia taswira za ulemavu wa akili kwa lengo la kuwasilisha jumbe mahsusi. Kupitia kwa wahusika ambao wanadhihirisha hali ya kuathiriwa na ulemavu wa akili, maudhui ya dhuluma, unyanyasaji, ujenzi wa jamii mpya, malezi na maadili yamewasilishwa.

Imebainika kuwa waandishi waliorejelewa wametumia taswira za ulemavu wa akili ili kuwasilisha maudhui yao kwa njia ya kipekee. Tabia na maneno ya wahusika husika pamoja na mienendo yao inaashiria maana ya ndani ambayo inaibua ujumbe mahsusi kwa mujibu wa hali za kijamii, kisiasa na kitamaduni zinazowazunguka. Aidha,

wahusika hawa wanatumia jazanda, sitiari na mbinu zingine za kimtindo katika kuwasilisha jumbe zenye uzito kwa wanajamii. Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wamefanikiwa katika kunasa umakinifu wa wasomaji wa kazi zao. Kadhalika wamewafanya wasomaji wao watafakari na kudadisi zaidi jumbe zinazowasilishwa kwa namna ambayo ni ya kipekee. Kwa hivyo waandishi hawa wamefanikiwa katika matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kama mtindo wa kipekee wa kuwasilisha maudhui waliyokusudia.

Katika sura inayofuata matumizi ya taswira za ulemavu wa tabia kama mtindo wa kuwasilisha maudhui yatajadiliwa.

## SURA YA TATU

## TASWIRA ZA ULEMAVU WA TABIA KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

### 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilishughulikia matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kwa lengo la kubainisha matumizI yake kama mtindo. Lengo la sura hii ni kudhihirisha namna ambavyo taswira ya ulemavu wa tabia imetumika kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Wahusika wanaoashiria hali ya kulemaa kitabia kupitia kwa matendo, mawazo na tabia zao wametumiwa kama data ili kuchanganua jinsi ulemavu wa tabia unavyotumika kama mtindo wa mwandishi. Kadhalika, mambo wanayoyasema wahusika wengine katika riwaya husika kuhusu wahusika wengine yanayoashiria kuwa wahusika hao wana ulemavu wa tabia yamezingatiwa kama data ya uchanganuzi. Sura hii inalenga kudhihirisha kuwa mwandishi anapotumia taswira ya ulemavu wa tabia katika kazi yake, huwa na lengo mahsusi. Riwaya zilizozingatiwa katika sura hii ni *Dunia Mti Mkavu*, *Utengano* na *Tata za Asumini* zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Aidha, riwaya za *Rosa Mistika*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji* zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi zimechanganuliwa. Kadhalika, mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanayoizunguka jamii na yanayoingiliana na matumizi ya taswira ya ulemavu wa tabia kama mtindo katika riwaya husika yamezingatiwa.

### 3.1 Dhana ya Ulemavu wa Tabia

Kwa mujibu wa Saussure (1983), uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa unategemea mifumo ya jamii ambayo watu hujifunza pamoja na utamaduni wao. Neno hupewa maana na jamii kwa kuwa kuna makubaliano kuhusu maana hiyo miongoni mwa jamii na watu wa jamii husika huizoea na kuitambua maana hiyo. Kwa kuzingatia

madai haya, maudhui yanayowasilishwa kupitia kwa taswira ya ulemavu wa tabia yamezingatiwa katika sura hii kwa kuwa yanatoa maana inayowakilishwa na taswira ya ulemavu wa tabia.

Jones na Learning (2010) wanadai kuwa katika hali halisi ulemavu huwa ni wa kibayolojia, kimatibabu na kijamii. Kwa mujibu wa wanasaikolojia wa kijamii, wanasoshiolojia na wanaanthropolojia, kaida zinazopatikana katika kila jamii zinajikita katika desturi zinazokubalika; imani yao, jinsi ya kuongea, mavazi na kazi mbalimbali. Ulemavu huwa ni kiashiria kwa kuwa ni hali inayorejelewa kulingana na jinsi inavyojitokeza na kufasiliwa na jamii. Danesh (2002) anadai kuwa kiashiria halisi kinaweza kuzua maana fiche au maana ya moja kwa moja. Katika sura hii, kigezo hiki ni muhimu katika kubainisha dhana ya ulemavu wa tabia na ujumbe unaowasilishwa kupitia kwa ulemavu husika.

Kwa mujibu wa Nixon na wengine (2003), fasiri ya watu kuhusu dhana ya ulemavu wa tabia hujikita katika mambo mbalimbali. Mambo haya ni kama vile: muktadha, mahali, maelewano miongoni mwa wanajamii na matarajio ya jamii. Bryant (2011) anakubaliana na Nixon kwa kusema kuwa watu tofauti hufasiri dhana ya ulemavu wa tabia kwa namna tofauti. Anadai kuwa fasiri ya ulemavu wa tabia hutegemea wakati, mazingira na hali ya jamii kwa jumla. Bryant anaendelea kusema kwamba fasiri ya dhana ya ulemavu wa tabia hutofautiana kutoka kizazi kimoja hadi kingine, utamaduni mmoja hadi mwingine na tabaka moja hadi lingine. Tofauti hizi zinatokana na kuwepo kwa mielekeo, mitazamo na tajriba zinazotofautiana miongoni mwa makundi mbalimbali ya wanajamii. Aidha, tofauti za kijamii, kisiasa na kimazingira zinadhihirika miongoni mwa makundi haya na kuathiri ufasiri wao kuhusu dhana ya ulemavu wa tabia. Kutokana na madai haya, inabainika kuwa tabia isiyokubalika miongoni mwa jamii moja huenda ikakubalika katika jamii nyingine. Hata hivyo,

inabainika kuwa kimsingi mtu aliyelemaa kitabia hufanya mambo yanayowakera, kuwadhulumu na kuwaudhi watu wengine.

Kwa mujibu wa Nixon na wengine (2003), ulemavu wa tabia ni hali ambapo mtu aliyeathiriwa huwa katika hali ya kutojali chochote kuhusu mambo yaliyo mazuri au mabaya; na mara nyingi hazingatii haki na hisia za watu wengine. Kadhalika, watu wenye ulemavu wa tabia huwagombanisha, kuwafanyia hila na kuwadhulumu watu wengine. Zaidi ya hayo, watu hawa huvunja sheria na hujipata kwenye matatizo kila wakati. Sifa nyingine inayowabainisha watu wenye ulemavu wa tabia ni kuwa hawaonyeshi majuto yoyote kutokana na matendo yao, ni wadanganyifu na wanapenda ghasia. Aidha, wengi wao hujiingiza kwenye tabia ya unywaji pombe na matumizi ya mihadarati.

Katika ufasiri wake kuhusu watu wenye ulemavu wa tabia, Mori (2007) anasema kuwa athari za ulemavu wa tabia huweza kukadiriwa katika misingi, mitazamo na mielekeo ya jamii kuhusu watu walioathiriwa na tabia hizi. Jensen (2011) anasema kuwa ulemavu wa tabia ni hali ya ukiukaji wa tabia na kaida zinazokubaliwa na wanajamii wenye mfumo fulani wa maisha. Kwa hivyo ulemavu wa tabia hubainika miongoni mwa watu wenye mielekeo inayofanana kuhusu mifumo na kaida mbalimbali za jamii. Kutokana na maoni ya waandishi hawa, inabainika kwamba kimsingi, watu wenye ulemavu wa tabia hutatizika katika utekelezaji wa majukumu yao ya familia, elimu, kazi na hata uongozi.

Kama anavyosisitiza Bryant (2011), ulemavu wa tabia ni jambo ambalo haliwezi kuepukika katika jamii. Kezilahabi (2007) anadhihirisha maoni ya Bryant anapotoa maelezo kuhusu riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Anasema:

> Riwaya hii inaeleza jinsi maisha yalivyo duniani-ni sawa na fujo kwa kuwa kila mtu huleta fujo zake na baadaye hutoweka. (Kezilahabi, 1975, uk.133).

Kezilahabi anatoa kauli hii katika ikisiri ya riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Riwaya hii ina wahusika wengi ambao wana ulemavu wa tabia.

Kauli ya Kezilahabi inaashiria kuwa duniani hapakosi watu wenye ulemavu wa tabia na kila mtu huwa na aina yake ya ulemavu wa tabia. Kwa hivyo, ulemavu wa tabia ni uhalisi wa namna maisha yalivyo duniani. Hata hivyo, ulemavu wa tabia unaweza kutumiwa kama mtindo katika kazi ya fasihi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa njia ya kipekee. Ingawa ulemavu ni tukio linalochukuliwa kuwa la kawaida, hali hii inaweza kutumiwa na mwandishi kuashiria maana zaidi ya hali husika kwa kuwa kama anavyosema Barthes (1968), kwa kuzingatia mtazamo wa kisemiotiki, kiashiria kinaweza kuwa na maana ya ndani.

Katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi na za Said Ahmed Mohamed taswira ya ulemavu wa tabia inajitokeza kupitia kwa visa na wahusika mbalimbali. Ulemavu huu unadhihirika kupitia kuweko kwa visa vya mauaji, uzinzi, ukahaba, ubakaji, wizi, matumizi ya mihadarati, ulevi wa kupindukia, ufisadi na kutoelewana miongoni mwa jamii. Taswira ya ulemavu wa tabia imetumika na Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed ili kuwasilisha jumbe mahsusi.

Kwa mujibu wa Bryant (2011) ulemavu wa tabia hudhihirika jinsi tatu. Kwanza kuna ulemavu wa tabia unaosababisha madhara kwa mtu binafsi. Pili, kuna ulemavu wa tabia unaojitokeza katika asasi mbalimbali za kijamii na mwisho kuna ulemavu wa tabia unaohusu mahusiano ya ngono. Aina hizi tatu za ulemavu wa tabia zinadhihirika katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Katika sehemu inayofuata aina hizi tatu za ulemavu wa tabia zimezingatiwa kwa mujibu wa jinsi zinavyojitokeza kama mtindo wa mwandishi katika riwaya husika.

### 3.2 Ulemavu wa Tabia wa Kujidhuru

Bryant (2011) anaeleza kuwa ulemavu wa tabia wa kujidhuru unajitokeza pale ambapo mtu hufanya mambo au huwa na mienendo inayomwathiri yeye kama mtu binafsi. Watu wenye ulemavu wa tabia wa aina hii huwa na tabia au mienendo inayowadhuru wao wenyewe. Aidha, watu hawa hujiingiza katika tabia hizi kimaksudi. Mifano ya tabia hizi ni; unywaji pombe kupindukia, matumizi ya mihadarati, kujitoa uhai miongoni mwa zingine.

Tabia zinazosababisha madhara kwa mtu binafsi zinazojitokeza katika riwaya za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi zitazingatiwa katika sehemu ifuatayo kwa kutilia maanani namna waandishi husika wamezitumia kama mbinu za kimtindo.

#### 3.2.1 Ulemavu wa Tabia ya Unywaji Pombe Kupindukia kama Mtindo

Kwa mujibu wa Kimble na wengine (1980), ulemavu wa tabia wa matumizi ya vileo huathiri kila kipengele cha jamii. Kimble na wenzake wanaendelea kusema kuwa matumizi ya vileo huathiri watu walioelimika, werevu, matajiri, wale ambao hawajasoma na maskini. Robin (1983) anasema kuwa pombe ni kinywaji ambacho kimekuwa kikimburudisha na kumtatiza binadamu kwa karne nyingi. Robin anaendelea kusema kuwa pombe ni maradhi yaliyofichika na hayatambuliki kwa urahisi. Kulingana na Torr (2000), kwa miongo kadha iliyopita kumekuwa na mwamko mpya ambapo taathira ya ulevi imetambulika kama suala la tiba badala ya suala la kimaadili ambapo wataalamu wa tiba wamefumbua kuwa taathira ya pombe inaweza kukabiliwa kwa kutumia njia za kimatibabu.

Katika mwaka wa 1951, Shirika la Afya Ulimwenguni lilitambua taathira ya ulevi kama mojawapo ya magonjwa yanayoathiri wanajamii. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Shirika hili (2018), zaidi ya watu milioni tatu walikufa kutokana na

matumizi hatari ya pombe. Kama anavyosema Robin (1983), taathira ya ulevi ni ugonjwa. Ugonjwa huu hudhihirika wakati ambapo unywaji pombe huwa ni mazoea hivi kwamba mtu hawezi kujizuia; kiasi kwamba afya yake na majukumu yake katika jamii yanaathirika. Aidha, Robin anasema kuwa matumizi mabaya ya pombe yanaweza kuhusishwa na visa vya mauaji, ugomvi wa nyumbani, kuzorota kwa afya, ajali za moto, ajali za barabarani na za majini. Hata hivyo, masuala ya kimaadili yamekuwa pingamizi kubwa katika kutafuta matibabu kwa wanaoathiriwa na ulevi kwa kuwa jamii nyingi hazitambui ulevi kama ukiukaji wa kaida za kijamii zilizokubalika.

Madai ya Robin yanathibitishwa katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* kupitia kwa mhusika Mashaka. Taswira ya ulemavu wa tabia wa Mashaka unadhihirika kutokana na jinsi ambavyo ameathiriwa na unywaji pombe kupindukia. Mwandishi anaeleza kuwa tabia yake inasababisha vita baina yake na mkewe, Bi Mtumwa, ambaye pia ni muuzaji pombe. Mwandishi anaeleza tukio mojawapo ya ugomvi huu:

> Bi. Mtumwa alikuja kwa dhamiri, akibeba uzito wa kiwiliwili chake, na mikono kainua kiti cha marimba; na pale alipokurubia Mashaka alimvurumisha nacho… 'Nitakuua mimi', sauti ya ghadhabu ya Bi Mtumwa ilihadharisha, 'ukisikia Mtumwa, mimi si mtumwa wako.' (Mohamed, 1980, uk. 27).

Tukio hili linatokea nyumbani kwa Mashaka wakati anapofika nyumbani akiwa mlevi. Jambo hili linamkera mno Bi Mtumwa, mkewe na ugomvi ukazuka baina yao.

Mwandishi anatumia majazi kwa kumwita mkewe Mashaka, '*mtumwa*'. Kama anavyosema mwenyewe, Bi Mtumwa alikuwa anaishi maisha kama ya mtumwa. Mtu anayeishi kama mtumwa hana uhuru wa kufanya atakavyo ila maisha yake hudhibitiwa na mtu aliye juu yake. Kwa mujibu wa TUKI (2004) neno 'mtumwa' linamaanisha mtu anayemilikiwa na mwingine na kufanyishwa kazi bila ujira. Bi

Mtumwa alikuwa anaishi kama mtumwa. Maisha yake yalikuwa hayana raha kutokana na tabia ya Mashaka ya ulevi. Aidha, alilazimika kuuza pombe ili kukidhi mahitaji yake kutokana na kushindwa kwa Mashaka kutekeleza majukumu yake pale nyumbani. Kupitia kwa ulemavu wa tabia wa Bi. Mtumwa wa kuuza pombe haramu, mwandishi anaangazia mojawapo ya sababu za kijamii zinazochangia kuwepo kwa biashara hii. Inabainika kuwa Bi Mtumwa alijiingiiza katika biashara ya uuzaji pombe haramu ili aweze kujimudu kimaisha kwa kuwa Mashaka, bwana yake alikuwa akimaliza pesa zake kwa kulewa na hakumsaidia kukidhi mahitaji yake pale nyumbani.

Kupitia kwa tabia ya Mashaka ya unywaji pombe kupindukia, mwandishi anaangazia suala la majukumu ya mwanamke na mwanamume katika ndoa kwa mujibu wa matarajio ya jamii. Kama anavyodai Wasserstrom (1997), majukumu kati ya mume na mke hutawaliwa na mielekeo ya jamii mbalimbali kuhusu kazi tofauti na maumbile yao. Wasserstrom anaendelea kusema kuwa kuwepo kwa desturi ya ugawaji majukumu baina ya wanawake na wanaume katika takriban jamii na tamaduni zote ulimwenguni ni ishara kuwa kuna umuhimu mahsusi unaoambatanishwa na ugawaji huu. Kwa hivyo mwanajamii anayekosa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa matarajio ya jamii huonekana kuwa na upungufu.

Kwa mujibu wa Martinez na wengineo (2011), wanawake katika Bara la Afrika hukabiliwa na matatizo mengi ya kijamii kutokana na unywaji pombe yakiwemo matatizo ya afya, ugomvi wa kinyumbani na kutengwa na jamii. Hali hii inadhihirika katika uhusiano baina ya Bi. Mtumwa na mumewe Mashaka. Mashaka alikuwa anaiba pesa za Bi Mtumwa ili anunue pombe. Jambo hili lilisababisha ugomvi baina yao. Maneno ya Bi Mtumwa; '*ukisikia Mtumwa, mimi si mtumwa wako*', yanadhihirisha namna alivyokerwa na tabia ya mumewe. Mumewe alikuwa kama mtumwa wa

pombe. Kupitia kwa ulemavu wa tabia ya unywaji pombe wa Mashaka na uuzaji pombe haramu wa Bi. Mtumwa, Said Ahmed Mohamed anawasilisha ujumbe kuhusu jinsi tabia hii inavyoathiri mahusiano ya familia na jamii kwa jumla.

Kama anavyosema Torr (2000), watu wanaokunywa pombe hutambulika kuwa na uraibu wa pombe iwapo wanaendeleza tabia hii licha ya kuathirika nayo kwa kuachishwa kazi, kuwadhuru jamaa na marafiki ama kuadhibiwa kwa kuvunja sheria za nchi. Kupitia kwa tabia ya ulevi wa Mashaka, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa unywaji pombe unaweza kumwathiri mtu kiasi kwamba anawadhuru jamaa na marafiki zake na kuzorotesha mahusiano mema miongoni mwa jamii. Inabainika kuwa ugomvi wa Mashaka na mkewe pale nyumbani uliwaathiri hata majirani. Kwa mfano, walipigana hadi wakauharibu mlango wa Bakari, jirani yao na kuingia ndani ya nyumba yake. Mwandishi anaeleza yaliyojiri:

> Kulikuwa na mwaliko mwengine kwenye mlango wa Bakari. Tena ulifuata mbingirisho uliochopoa kijiti kilichochomekewa kipeto cha mlango huo wa ndani. Ubao wa mlango ulioshindwa kuzuia uzito wa mwelemo, ulielemea ndani na kugonga ukuta. Na hapo viwiliwili viwili vilianguka ndani-Bi Mtumwa mwenye tani ya kifaru juu ya Mashaka mwenye mwili wa ng’onda. Bi Mtumwa, nywele zimemtimka, jicho limemwiva, kanga zinamporomoka, aliendelea kumzaba vibao mwenzake bila kujali kama wamo chumbani mwa watu. (Mohamed, 1980, uk. 27).

Maelezo haya ya mwandishi yanatoa taswira ya vurugu baina ya Bi Mtumwa na mumewe. Kutokana na unene wa Bi Mtumwa aliweza kumpiga Mashaka ambaye alikuwa amedhoofishwa na unywaji pombe. Kisa cha Mashaka kupigwa na mke wake kinatumiwa na mwandishi kuashiria jinsi ambavyo pombe humdhoofisha mwanadamu kiafya. Aidha, vita baina ya Mashaka na mkewe, Bi. Mtumwa, vinatumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui kuhusu athari za pombe katika muktadha wa mahusiano ya ndoa. Torr (2000), anadai kuwa taathira ya ulevi ni ugonjwa ambao humwathiri mtu na kustawi ndani ya mwili wake kwa kipindi kirefu

na hatimaye unaweza kusababisha kifo. Torr anaendelea kusema kuwa taathira ya ulevi ni ulemavu wa kimsingi unaoathiri kila sehemu ya mwili pamoja na ubongo wa mtu. Pombe inapoathiri ubongo, mwathiriwa hupata uraibu wa pombe hivi kwamba matendo, fikra, hisia na maamuzi yake hutawaliwa na pombe. Aidha, maisha yake na mahusiano yake na watu hujikita katika ulevi.

Kupitia kwa maneno ya Bi Mtumwa inadhihirika kuwa Mashaka alikuwa na uraibu wa pombe. Anasema:

> Ulevi kwake nd'o chai, nd'o chakula. Si anatafuta kufa. Ee, chakula mtu hana, na ulevi akaufanye ibada, si kutafuta kubabua machango na maini bure. Na jawabu yake 'bwana mkubwa' ni: 'sijui kinyokonyoko, kinyokonyoko; sijui mbona wewe unauza pombe; sijui wewe mbona unawapa watu.' maana anavyoona yeye, kuuza na kunywa pombe ni sawa. Eeee, maana mwenye kutoa sumu na mnywaji sumu ni sawa; na mimi labda nayataka haya. (Mohamed, 1980, uk. 29).

Bi Mtumwa katika maneno haya anaeleza namna ambavyo mumewe alikuwa anathamini unywaji pombe licha ya athari za kiafya zinazotokana na tabia hii.

Ulevi wa makame unalinganishwa na chai na chakula. Mwandishi anatumia sitiara hii kusisitiza kuwa kama ambavyo mtu hawezi kuishi bila chakula, Mashaka hangeweza kuishi bila kulewa na kwamba alithamini pombe sana. Maelezo ya Bi Mtumwa yanathibitisha kuwa mumewe alithamini pombe kuliko hata chakula. Hii ni ishara kuwa unywaji pombe wa Mashaka haukuwa wa kawaida ila ulikuwa ulemavu. Kwa mujibu Martin (2011) watu wenye tabia ya unywaji pombe hudhihirisha hali ya kutozingatia lishe bora. Shirika la Utafiti wa Taathira ya Pombe (AUDs) (2017), linaendeleza maoni ya Martin kwa kusema kuwa unywaji pombe kupindukia unaweza kusababisha ulemavu wa matumizi ya pombe, na hatimaye uraibu wa pombe ambapo mwathiriwa hutegemea pombe kurutubisha mwili wake.. Hivyo basi, suala hili linapaswa kushughulikiwa kwa misingi ya tiba  kwa kuwa mwathiriwa hutegemea

pombe bila kujali mahitaji yake ya msingi. Martin anaendelea kusema kuwa tabia ya unywaji pombe kupindukia inasababisha uraibu wa pombe kwa kuwa pombe huchukua nafasi ya madini muhimu yanayohitajika mwilini mwa binadamu na kumdhoofisha mwathiriwa. Bi Mtumwa anamkejeli mumewe kwa kumrejelea kama '*bwana mkubwa'* kwa kuwa kimsingi anapaswa kuwa kiongozi wa nyumba yake lakini alishindwa kutekeleza jukumu hilo kutokana na unywaji pombe na ilibidi mkewe ayatimize majukumu yote.

Mwandishi anatumia ulemavu wa Mashaka kuwasilisha maudhui kuwa tabia ya unywaji pombe huathiri familia kwa kuwa inasababisha kutokuwepo kwa maelewano kati ya mume na mke. Kwa mujibu wa Torr (2000), vita vya kinyumbani ni mojawapo ya athari za unywaji pombe kupindukia. Anaendelea kusema kuwa familia ambapo unywaji pombe hushamiri zinakosa umoja, zimejaa vurugu na zinakosa mahitaji ya kimsingi. Tukio la ugomvi kati ya Bi Mtumwa na mumewe linasawiri matatizo ya ndoa yanayosababishwa na ulemavu wa tabia wa unywaji pombe kupindukia. Kama anavyosema Robin (1983) ulevi husababisha ukosefu wa maelewano baina ya watu katika ndoa, ukosefu wa heshima na huwaletea wahusika aibu kubwa. Aidha, unywaji pombe huathiri wanajamii wengine wanaoishi pamoja na watu wenye ulemavu wa tabia. Hivyo basi tatizo la unywaji pombe kupindukia ni tatizo la kijamii linalopaswa kukabiliwa na wanajamii wote. Watu wenye taathira ya ulevi mara nyingi hawatambui kuwa wana ulemavu na vivyo basi ni muhimu kuwashirikisha wanajamii wengine kama vile marafiki na jamaa katika kuwafanya walioathiriwa waweze kutambua kuwa wana ugonjwa na wanahitaji kutafuta matibabu. Kupitia kwa ulemavu wa tabia wa unywaji pombe kupindukia wa Mashaka, mwandishi analenga kuwahamasisha wanajamii watambue kuwa hili ni tatizo la kiakili na linahitaji kushughulikiwa kama ugonjwa mwingine wowote ule.

Said Ahmed Mohamed anaonyesha nafasi ya wanajamii kwa jumla katika kutatua matatizo yanayosababishwa na taathira ya ulevi kupitia kwa Bakari ambaye ni jirani wa Bi Mtumwa na Mashaka. Bakari anamzuia Bi Mtumwa kumpiga Mashaka na kuwashauri Mashaka na mkewe watafute njia mwafaka ya kutatua matatizo yao. Bi Mtumwa hakuwa tayari kuuzingatia ushauri wa Bakari kwa sababu alihisi kuwa mumewe alikuwa akifaidi jasho lake na kwamba alikuwa kama mtumwa kwake. Hisia zake zinajitokeza kutokana na namna alivyomjibu Bakari:

> Salama na jibwa hili? Bi Mtumwa alimkata kauli Bakari, 'salama na guruwe hili linokula nguvu zangu..' Bi Mtumwa alitupa makono yake ovyo kwenye hewa, akasema kwa kichwa, macho, pua, midomo na mikono.'Hili…' alivuta hatua, lakini Bakari alijitia kati na kumzingia Bi. Mtumwa asimfikie Mashaka ambaye sasa alikuwa akisogea mlangoni.'Hili dude nd'o linalozidisha kunila na kuni..' alisita kwa kupima ukweli wa lile alilotaka kulisema,'kondesha,' alimaliza. (Mohamed, 1980, uk. 28).

Bi Mtumwa hakutaka kusitisha vita hata baada ya Bakari kuingilia kati. Analalamika kuwa mumewe alikuwa anamnyanyasa na kumdhulumu. Maneno ya Bi Mtumwa yanadhihirisha kuwa Mashaka hakutekeleza majukumu yake kama mume pale nyumbani kwake. Alimtegemea mkewe kwa kila hali. Kupitia kwa Bi Mtumwa mwandishi anadokeza kuhusu mojawapo ya sababu zinazoweza kuchangia katika tabia ya uuzaji na unywaji pombe kupindukia. Inabainika kuwa kutowajibika kwa Mashaka kulimfanya mkewe kuuza pombe haramu ili kuweza kukidhi mahitaji mbalimbali pale nyumbani. Biashara ya Mtumwa ilikumbwa na changamoto nyingi. Askari walimhangaisha pamoja na wateja wake na mara nyingi alilazimika kutoa hongo ili kuachiliwa. Mwandishi anatumia tabia ya askari ya kupokea hongo ili kuwasilisha ujumbe kuhusu namna ambavyo taathira ya pombe huzorotesha uwajibikaji katika jamii hasa miongoni mwa walinda usalama. Tamaa ya hela

inawafanya askari kutozingatia kazi yao. Jambo hili linachangia katika ongezeko la uuzaji na utumizi wa pombe haramu miongoni mwa wanajamii.

Jambo lililomkera Bi Mtumwa zaidi ni kuwa mumewe hakujali. Inaelekea kuwa mbali na kutowajibika kwake, Mashaka alikuwa akimhangaisha Bi Mtumwa kwa kuiba akiba yake na kwenda kununua pombe mahali kwingine. Changamoto hizi zilifanya biashara ya Bi Mtumwa kukosa faida. Anasema:

> Basi faida yangu nini? Hayasemeki, askari wananinyemelea kama nini sijui, na hili gombe-mtu halijui haya, linajitia wehu, limegeuka nyang'anyu manyung'unya hili, linaniibia viakiba vyangu na kwenda kulewea nje. Na likirudi hapa pangu, kucha silali. Kero, kero. Nipe nini sijui; mara matapishi, mara mate, mara madenda, mara mikojo, mara…' ah, hata hayasemeki. Uchafu, uchafu, uchafu moto mmoja; chumbani kwangu hakuingiliki, Pesa zangu achukue, ulevi alewe yeye, shida anikutishe miye, a-a bibiangu we! Balaa, shoti daka la moyo nililonalo, nyinyi nyote mnajua…kwa nini? A-a, Mashaka haya Mashaka kweli, lakini akamtwaze babaake na mamaake waliomleta duniani, sio mimi, aaaa-a!' Alisita, makono yake kayapachika kiunoni, macho yanampwesa, kupe, kupe. Pua inapwitapwita na midomo inamcheza. (Mohamed, 1980, uk. 29).

Bi Mtumwa anazungumza na nafsi yake anapowaza matatizo aliyokuwa akiyapitia kutokana na tabia ya ulevi ya mumewe. Maneno ya Bi Mtumwa yanaonyesha kero aliyokumbana nayo kila siku. Anasema kuwa Mashaka amegeuka na kuwa na tabia kama za mtu mwenye ulemavu wa akili na hakuaibika kutokana na vitendo vyake. Kadhalika, amekuwa mwizi kwa kuwa anamnyang'anya mkewe pesa zake na kununua pombe. Zaidi ya hayo, Mashaka alikuwa akileta uchafu pale nyumbani kwa kutapika, kukojoa na kutema mate ovyo ovyo chumbani. Aidha, alikuwa akimtisha mkewe.

Kupitia kwa maneno ya Bi Mtumwa mwandishi anasisitiza matatizo yaliyomkumba Bi Mtumwa kutokana na tabia ya mumewe ya unywaji pombe kupindukia. Bi Mtumwa anamwita mumewe '*gombe mtu'* kutokana na tabia yake ya kumgombeza.

Anasema kuwa ulevi umemgeuza mumewe kuwa '*nyang'anyu manyung'unya'* ili kusisitiza tabia ya mumewe ya kuchukua pesa zake bila idhini. Bi Mtumwa anaeleza shida nyingi alizopitia kutokana na ulevi wa mumewe. Anadai kuwa halali usiku kucha kutokana na kero ya mumewe ya kutaka kuhudumiwa kwa kila hali. Kadhalika, chumba hakiingiliki kutokana na uchafu wa kila aina unaosababishwa na Mashaka. Maneno ya Bi. Mtumwa yanadhihirisha kuchukizwa kwake na tabia hii ya mumewe. Ni kinaya kuwa Bi Mtumwa analalamikia tabia ya mumewe ya ulevi licha ya kuwa yeye ni muuzaji pombe. Bi Mtumwa anaelewa fika kuwa kijamii na kidini uuzaji wa pombe haramu ni jambo lisilofaa lakini hakuwa na njia nyingine ya kuyakimu maisha yake. Anasema:

> Wallahi kama angeeza kuukamilisha udume wake, akanifungia milango na kunikimu kwa vya nje na vya ndani, nishughulike nini na kuuza maji ya Firauni? Kwani kazi ya maana hii? Si basi tu. Kazi unayoambiwa wazi kuwa huonani na mtume. (Mohamed, 1980, uk. 29).

Haya ni maneno ya Bi Mtumwa alipokuwa anamweleza Bakari ni kwa nini matatizo yake na mumewe hayangeweza kusuluhishwa kwa njia mwafaka bila kupigana. Anamweleza Bakari dhiki aliyokuwa anapitia kutokana na tabia ya ulevi ya mumewe na ni kwa nini yeye aliamua kuwa muuza pombe haramu.

Kupitia kwa maneno haya ya Bi Mtumwa, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa watu wanaofanya kazi ya kuuza pombe haramu na wale ambao wana uraibu wa pombe hawafanyi hivyo kwa kupenda ila kuna sababu zinazowasukuma na kuwafanya wajiingize katika tabia hii. Kwa mfano, inabainika kuwa Bi. Mtumwa hakufurahia kazi ya kuuza pombe haramu ila ulemavu wa tabia wa mumewe ndio ulimsukuma kwenye biashara hii. Ingawa uuzaji pombe ni biashara inayoendelezwa na wanajamii kwa lengo la kujipatia riziki, inabainika kuwa biashara inayoendeshwa na Bi Mtumwa ni ya uuzaji wa pombe haramu kumaanisha kuwa ilikuwa marufuku na

haikuruhusiwa kisheria. Inaelekea kuwa Bi. Mtumwa alisukumwa kwenye biashara hii kutokana na kushindwa kwa mumewe kutelekeza majukumu yake. Jambo hili linajitokeza Bi. Mtumwa anapotumia msemo '*kukamilisha udume'* anapozungumza kuhusu mumewe kuashiria kuwa mwanamume kamili ni yule anayeweza kutekeleza majukumu yake nyumbani. Bi Mtumwa anaashiria kuwa Mashaka si mwanamume kamilifu kwa kuwa alikuwa ametelekeza majukumu yake. Ni dhahiri kuwa iwapo Mashaka angekuwa anamtimizia mahitaji yake yote Bi Mtumwa hangejiingiza kwenye kazi ya uuzaji pombe. Ngubane (2010) anasema kuwa katika utamaduni na maisha ya kitamaduni ya Kiafrika, jinsia hutambulika kwa kuzingatia majukumu na kazi za wanajamii. Kwa hivyo, mwanajamii anayeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa matarajio ya jamii huonekana kama mtu asiyekamilika. Hii ndiyo sababu inayomfanya Mashaka kuonekana kama kwamba si mwanamume kamili kwa kuwa kama anavyosema Blackstone (2003), kitamaduni, wanaume huchukuliwa kuwa ndio viongozi wa familia na wanastahili kuyakimu mahitaji ya kifedha ya familia zao.

Taswira ya taathira ya pombe inadhihirika pia kupitia kwa Bi Pili katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Inabainika kwamba licha ya kuwa Bi Pili alikuwa ajuza na mjane, alikuwa analewa kupindukia. Mwandishi anaeleza kuwa tabia hii yake ilimfanya kunywa pombe kwa deni. Tabia ya kutumia pesa zote kiasi cha kunywa kwa deni, ni ishara ya ulemavu wa akili na tabia kama inavyobainika katika maelezo yafuatayo:

> Bi Pili, kuni mkononi, alikuwa akirudi dukani kwa mshihiri, na kama kawaida alikuwa akiyumbayumba na kuporoja ovyo maneno ya kilevi. 'Anaaa, anaaaniidaaai, ananidai…potelea mbaaali. Nitamliiipa keeesho, kesho ka nitakuwa haaai…aaa nikijaliwa, ata, si lipi chochote.'(Mohamed, 1980, uk. 60-61).

Maelezo ya mwandishi kuhusu mwendo wa kuyumbayumba na mtindo wa maongezi wa kusitasita wa Bi Pili unaibua taswira ya mtu aliyekuwa mlevi. Kuyumbayumba na kuporoja maneno ovyo ni ishara ya kulewa. Unywaji pombe kwa deni ni ishara kuwa Bi Pili alikuwa na uraibu wa pombe kiasi kwamba hangeweza kuvumilia hata wakati hakuwa na hela za kuinunua. Sifa hii ni ishara ya mtu ambaye ana tatizo la akili. Bi Pili anaonekana kutojalishwa na hali hii kwa namna ambavyo anatumia msemo '*potelea mbali'*. Matumizi ya msemo ni mtindo unatumiwa kusisitiza hali ya kutojali kwa Bi Pili kuhusu tabia yake ya ulevi. Anajitokeza kama mtu aliyekata tamaa kwa kuwa anasema kwamba atalipa deni siku itakayofuata iwapo atakuwa hai. Bi Pili anajitokeza kama mwanamke ambaye hakuyajali maisha yake ishara kuwa alikuwa na tatizo la akili kutokana na unywaji pombe. Kupitia kwa Bi Pili, mwandishi anawasilisha ujumbe kuhusu mtazamo na mwelekeo wa watu walioathiriwa na pombe kuhusiana na maisha kwa jumla. Inabainika kwamba ulevi unamfukarisha mtu na kumkatisha tamaa maishani.Wengi hupoteza maisha yao ulevini na wengine hujitoa uhai.

Kwa mujibu wa Blackstone (2003), wanaume wanatarajiwa kuwa na jukumu la kimsingi la kukidhi mahitaji ya familia zao. Hivyo basi, mara nyingi wanawake wanapoondokewa na waume zao kutokana na talaka au kifo, wanaathiriwa na umaskini kwa kuwa hawana mtu wa kutegemea. Kadhalika, unywaji pombe husambaratisha ndoa. Inaelekea kuwa hata mumewe Bi. Pili alipokuwa hai maisha yao ya ndoa yalikuwa na mushkili kwa sababu kama anavyosimulia Bi. Pili, mumewe, Hasani, alikuwa mlevi. Ulevi ulimfanya Hasani kumpiga na kumtesa mkewe. Aidha, hakumshughulikia mke wake na kama anavyodai Bi. Pili, mume wake alimtwika mzigo wa maisha. Hali hii inadhihirika katika ndoa ya Zakaria na Regina katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Mwandishi anatumia taswira ya ndoa ya Bi Pili na

mumewe kuwasilisha ujumbe kuhusu matatizo ya ndoa yanayotokana na taathira ya ulevi kiasi kwamba wahusika hawatekelezi wajibu wao kwa mujibu wa matarajio ya jamii. Bi Pili anasema:

> Bwana Hasani mme waaa…Mungu amreheeemu amekufa sa…saaasa mwaka wa saba…na hata,'sasa alisema kama vile ulevi umemruka, ingawa alikuwa akiyumbayumba, 'hata angalikuwa hai, kwaangu ingalikuwa sawa; ni mateso yaaaleyaale…sijapaaata kuona furaaaha katika ndoa yaangu…alinipiga, alinitesa, hakunishughulikia; akanitwiisha mziiigo wa maisha…alikuwa mleeeevi kuliko ee miii.' (Mohamed, 1980, uk. 61).

Bi Pili alikuwa anamwambia Pandu, kijana aliyekuwa jirani yake, maneno haya alipokutana naye akitoka ulevini.

Maneno haya ya Bi Pili yanadhihirisha masikitiko aliyokuwa nayo tangu mumewe alipokufa licha ya kuwa hakuwa na furaha katika ndoa yake. Ni kinaya kuwa alisikitishwa na kifo cha mumewe kwa kuwa anadai kuwa hata kama angekuwa hai, hangekuwa na furaha. Hii ni kwa sababu mumewe alikuwa hawajibiki na alimtesa sana kwa kuwa yeye pia alikuwa na taathira ya ulevi.

Maneno ya Bi Pili yanaashiria hisia za uchungu alizokuwa nazo kwa sababu ya mateso aliyopata kutokana na tabia ya ulevi ya mumewe. Licha ya kuwa alikuwa mlevi, Bi Pili anatambua namna ulevi ulivyoathiri ndoa yao. Anatumia nahau '*kutwishwa mzigo wa maisha'* kumaanisha kuwa hakusaidiwa kwa namna yoyote na alikuwa ameachiwa majukumu yote na Hasani, mumewe. Hali hii ilitokana na ulevi wa kupindukia uliomwathiri Hasani. Ni kinaya kuwa Bi Pili anamlaumu mumewe kwa kutowajibika na kumtesa ilhali yeye mwenyewe anashiriki ulevi. Mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa wanajamii hujiingiza katika tabia ya unywaji pombe licha ya kufahamu athari zake. Kwa mfano, licha ya kuwa Bi. Pili alifahamu kuwa matatizo ya ndoa kati yake na mumewe yalitokana na ulevi, hakuacha tabia ya unywaji pombe.

Kama anavyodai Galbicsek (2016) unywaji pombe ni tatizo la kisaikolojia na kimaadili. Galbicsek anasema kuwa kuna watu wanaojiingiza katika tabia ya unywaji pombe kwa lengo la kupunguza mawazo yanayotokana na matatizo yanayowapata maishani. Anaendelea kusema kuwa watu wenye mawazo mengi na wasiwasi wanaweza kuathirika na uraibu wa pombe. Katika muktadha huu pombe inatumika kama njia ya kutuliza mawazo na kupunguza dalili za mhangaiko wa akili. Galbicsek anaendelea kusema kuwa kadri mtu anavyozidi kutumia pombe kama kiliwazo cha uchungu na matatizo, mwili wake huzoea hali hii kiasi kwamba hawezi kuishi bila kuitumia. Kwa kuzingatia maoni ya Galbicsek, inaelekea kwamba mwandishi wa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* anatumia unywaji pombe wa Bi Pili kuwasilisha ujumbe kuwa matatizo ya maisha yanaweza kuwa mojawapo ya sababu zinazowafanya baadhi ya watu kujiingiza katika tabia ya unywaji pombe kupindukia.

Kama anavyoeleza Bryant (2011), ulemavu wa tabia unaweza kuelezwa kutokana na jinsi wanajamii wanavyofasili tabia fulani na mtazamo wao kumhusu mtu mwenye ulemavu wa tabia. Kwa mfano, jamii ilikuwa na mtazamo mahsusi kumhusu Bi Pili. Kupitia kwa maneno ya Bi. Pili inabainika kuwa wanajamii walikuwa wanamtukana na kumpachika majina. Anasema:

> Siseeemi kwa uleeeevi, najua niko top, lakiiin naeeelewa n'nasema niiini… halafu wananitukaaana, wananiita afiriiiiti, mleeevi, hayawaaaan, ha, ndiyo miii mlevi, sitowacha uleeevi. Bila ya ulevi kwangu jitimai, ulevi hunichangamsha, hufifiza mawazo yaaaangu; husahau angalau…' Alifuta machozi. (Mohamed, 1980, uk. 62).

Katika mazungumzo haya, Bi Pili alikuwa anamweleza Pandu kuhusu Mwita, mwanawe wa kiume aliyekufa kutokana na ajali aliyopata akiwa kazini. Bi Pili anamweleza Pandu namna kifo cha mwanawe kilivyomhuzunisha na kwamba ingawa alikuwa mlevi alielewa kile alichokisema.

Kwa mujibu wa Kaye (2015), mtu mwenye tatizo la akili hudhihirisha tabia ambayo ni kinyume na ya wanajamii wengine. Aghalabu watu wenye tabia hii hukiuka mipaka ya kaida na desturi kwa mujibu wa matarajio ya wanajamii wenzao. Kwa mfano, kupitia kwa maneno ya Bi.Pili, mwandishi Said Ahmed Mohamed anaonyesha mtazamo wa jamii kuhusu ulevi. Bi. Pili anadai kuwa wanajamii walimwita afriti. Afriti ni mtu mwovu anayetumia ujanja kuwahadaa watu. Kadhalika, wanajamii walimwita Bi Pili hayawani kumaanisha mnyama au mtu asiye na ubinadamu; mtu asiye na haya wala adabu (TUKI, 2004). Kulingana na Kimble na wengine (1980), watu wenye ulemavu wa tabia ya kujidhuru hujitokeza kama wasiojali athari za tabia yao. Kwa mfano, Bi Pili hakujali wala kujuta licha ya mtazamo hasi waliokuwa nao wanajamii kumhusu. Yeye aliichukulia tabia ya ulevi kama inayofaa na kama anavyosema, hakuwa tayari kuiacha. Mtazamo wa wanajamii kwa Bi Pili ni ishara kuwa jamii haitambui kuwa ulevi ni tatizo la kisaikolojia na kiafya na kwamba mwathiriwa anapaswa kupata matibabu maalum. Aidha, kuwatenga, kuwadharau na kuwatusi wanajamii walioathiriwa na tatizo hili ni jambo lisilofaa. Mtazamo wa jamii kuwa mlevi ni mtu ambaye amepotoka kitabia, hadaa, mwovu asiye na ubinadamu ni kikwazo kikubwa katika kutafuta suluhisho au matibabu kwa walioathirika na unywaji pombe. Kama wanavyosema Prun na wengine (2010), kuna haja ya kuchunguza mwelekeo wa jamii kuhusu watu walio na taathira ya ulevi kama mojawapo ya hatua muhimu ya kutafuta suluhisho la tatizo hili.

Kupitia kwa tabia ya ulevi ya Bi Pili mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa ulemavu wa tabia husababishwa na tajriba ya maisha ya mwathiriwa na kwamba jamii inapaswa kutafuta kiini cha tabia hii badala ya kumhukumu na kumtenga mtu mwenye ulemavu huu. Kwa mfano kama anavyosema Bi. Pili, ulevi ulikuwa ni njia yake ya kujichangamsha na kujisahaulisha mawazo aliyokuwa nayo, ishara kuwa

kulikuwa na sababu fulani iliyomsukuma hadi akajiingiza katika ulevi. Unywaji pombe ulikuwa njia ya kujikinga kutokana na uchungu na mawazo ya ugumu wa maisha uliomkumba na kumfanya ajisikie huru. Jambo hili linajitokeza katika mazungumzo ya Bi Pili na Pandu. Anamwambia Pandu:

> Mtoto waaaangu, unamjua Mwiita,' sasa kilio kilikuwa wazi. Pandu kaemewa. Mlicheza pamoja, unajua namnaaaa alivyo…alivyokuuufa, aliporooomoooka kwenye mnara aliokuwa akiupaka rangi…' aligugumka, kwikwi, keefu, akakamata kitambaaa cha baibui lake akafuta machozi. 'Ulimwenguu ulimchukua, haaata mwananguuuu, hata yeye, umemchukua…haukumlipia fidia…amekwenda amesahauliwa.' (Mohamed, 1980, uk. 62).

Bi Pili anamweleza Pandu kuhusu kifo cha mwanawe Mwita. Huzuni aliyokuwa nayo Bi Pili inadhihirika kutokana na namna anavyolia anapoeleza kuhusu kifo cha Mwita. Maneno yake yanaashiria kuwa Mwita alikufa kutokana na ajali aliyopata akiwa kazini. Mwandishi anaeleza kilio na machungu yaliyomkumba Bi. Pili kutokana na kifo cha mwanawe. Kupitia kwa kauli ya Bi Pili, inabainika kuwa mawazo yaliyomsukuma kwenye tabia ya ulevi ni kuhusu mwanawe hasa ikizingatiwa kuwa hakuna fidia aliyopata licha ya kuwa Mwita alikufa kutokana na majeraha aliyopata akiwa kazini.

Said Ahmed Mohamed anatumia ulemavu wa tabia wa Bi Pili wa unywaji pombe kupindukia ili kuangazia kuhusu swala la dhuluma miongoni mwa jamii. Kupitia tabia ya ulevi wa Bi Pili maudhui ya haki kwa wafanyikazi yanaibuka. Mwandishi anatumia ulemavu wa tabia wa unywaji pombe wa Bi Pili kuendeleza maudhui ya dhuluma na unyanyasaji. Inaelekea kuwa wafanyakazi wanadhulumiwa na waajiri wao kwa kupewa kazi zinazohatarisha maisha yao lakini hawalipwi fidia wanapopata kudhuriwa na kazi hizi. Kisaikolojia imedhihirika kuwa walevi, wendawazimu na watoto hawasemi uongo. Kwa hivyo, inaelekea kuwa S.A. Mohamed anatumia walevi

kusema ukweli ambao hauwezi kusemwa na watu wengine wenye akili au hali timamu.

Licha ya jamii kumchukulia Bi Pili kama mtu afriti, muovu na mjanja asiyeaminika kutokana na tabia yake ya ulevi; anajitokeza kama mtu anayeelewa masuala yanayoizunguka jamii yake. Haya yanadhihirika katika mazungumzo yake na Pandu. Anasema:

> Kibanda changu kariibu kitavunjwa. Ati wanasema wanataka kupitisha barabara, miii najua, hakuna barabara waaala choochoote. Bi Kijakazi alivunjiwa kibaaanda chake hivyo hivyo, akaaaa… akaambiwa itapita barabara, siku chache tukaooona jumba la bwanamkubwa mmoja linaporomoshwa; jumba la kupangisha wauza duka…Hukurusha nje ya maskani yaaako kwa vijipesa viwili vitatu, ubaki kutamba na ulimweengu. (Mohamed, 1980, uk. 62).

Bi Pili anamweleza Pandu kuhusu arifa aliyokuwa ameipata kwamba kibanda chake kingevunjwa kwa kuwa barabara iliyokuwa inatarajiwa kujengwa ilifaa kupitia hapo. Anasema kuwa hakuna barabara itakayojengwa. Anarejelea yaliyompata Bi Kijakazi ambaye kibanda chake kilivunjwa ili barabara ijengwe lakini badala yake tajiri mmoja alijenga jumba la kupangisha mahali pale. Bi Pili anafahamu namna watu wenye nguvu wanavyowahadaa na kuwadhulumu watu wa tabaka la chini. Kadhalika, anafahamu kwamba watu hawa ni fisadi. Maneno ya Bi Pili yanadhihirisha tofauti za kitabaka katika jamii ambapo maskini anadhulumiwa ili kumfaidi mwenye uwezo. Mwandishi anachora taswira ya hali halisi kama ilivyo katika jamii husika ambapo mnyonge ananyimwa haki na mwenye nguvu. Kulingana na Prun na wengine (2010), umaskini na unyanyasaji unaweza kuwa chanzo cha taathira ya ulevi. Hii ni kwa sababu ulevi ni tabia ambayo mtu anaweza kuanza kama njia ya kukabiliana na tatizo fulani la kimaisha. Wanasaikolojia wanadai kuwa watu wenye taathira ya ulevi hutumia pombe kama njia ya kupunguza mawazo, lakini hatimaye mawazo haya

huongezeka badala ya kupungua. Kwa kuzingatia maoni ya Prun na wenzake inabainika kuwa kupitia kwa ulemavu wa tabia wa unywaji pombe kupindukia wa Bi Pili, mwandishi analenga kuwasilisha ujumbe kuwa wanajamii wanapaswa kutafuta kiini cha tabia hii badala ya kuwatenga na kuwahukumu waathiriwa ili waweze kuwasaidia.

Taswira ya ulemavu wa tabia ya ulevi inajitokeza pia katika riwaya ya *Rosa Mistika* kupitia kwa mhusika Zakaria. Zakaria anajitokeza kama mtu mwenye uraibu wa pombe. Mwandishi, Euphrase Kezilahabi, anadhihirisha haya anaposema:

> Tangu Ijumaa mpaka Jumapili Zakaria alikuwa anakwenda kunywa, na siku nyingine za juma alijifanya mgonjwa kitandani. Mke wake hakupata kufahamu mumewe alikuwa na shilingi ngapi benki kwani alimwona akinywa kila juma. (Kezilahabi, 1976, uk. 6).

Maelezo haya ya mwandishi yanaashiria kuwa Zakaria alikuwa anakunywa kila mwisho wa juma. Kwa mujibu wa Swegan (2011), pombe ni mojawapo ya vinywaji ambavyo vinatumiwa katika tamaduni nyingi. Kinywaji hiki hutumiwa na watu wengi kama njia ya kujistarehesha, lakini ikiwa kitatumiwa kwa muda mrefu bila tahadhari, kinamfanya mtu kupata uraibu hasa iwapo hawezi kukaa kwa muda mrefu bila kukitumia. Madai ya Swegan yanajitokeza katika maisha ya Zakaria. Swegan anaendelea kusema kwamba, mwathiriwa wa pombe huishi maisha yasiyo na mwelekeo. Madai haya yanadhihirika kupitia kwa Zakaria. Mwandishi anaeleza kuwa Zakaria hakuwa anafanya kazi yoyote kwa kuwa wakati hakuwa anakunywa alijifanya mgonjwa na kushinda kitandani. Taswira ya ulemavu wa tabia wa Zakaria inafanana na taswira ya wahusika Mashaka na Hasani katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ya Said Ahmed Mohamed kwa kuwa wahusika hawa kama alivyo Zakaria wanajitokeza kama wenye uraibu wa pombe kiasi kwamba walikuwa wanaenda ulevini kila siku. Aidha, kushindwa kwa wahusika hawa kutekeleza majukumu yao kunajitokeza kwa

kuwa kama Said Ahmed Mohamed alivyowasawiri wahusika hawa wawili, mwandishi Kezilahabi amemchora Zakaria kama mtu aliyeathiriwa na pombe kiasi kwamba alitelekeza jukumu lake la kuitunza familia yake.

Inabainika kuwa ulemavu wa tabia wa Zakaria wa unywaji pombe ulikuwa na athari nyingi. Mwandishi anaeleza kuwa Zakaria alikuwa mwalimu lakini alifutwa kazi kwa sababu ya ulevi. Hii ni ishara kuwa Zakaria alikuwa ameathiriwa na pombe kiasi kwamba urazini wake kama binadamu ulikuwa umeathirika. Kwa mujibu wa kitengo cha Shirika la Afya Ulimwenguni (1991), matumizi ya pombe kiasi cha kuathiri shughuli za mtu za kila siku ni ishara ya ugonjwa. Zakaria hakuwajibika pale nyumbani kwake; alimwachia Regina mkewe majukumu yote ya kuitunza familia yao. Mwandishi anaeleza kuwa Zakaria hakuwa anawalipia watoto wake karo ila mkewe alitumia kipato kutoka kwa kilimo cha pamba na kutengeneza pombe ya mihogo ili kukidhi mahitaji ya watoto wao. Regina analazimika kujitwika majukumu ya mumewe kutokana na kushindwa kwa mumewe kuyatekeleza majukumu yake. Hali kama hii inadhihirika pia katika riwaya ya Said Ahmed Mohamed, *Dunia Mti Mkavu* ambapo Bi Mtumwa na Bi Pili wanalazimika kukithi mahitaji ya familia zao kutokana na kutowajibika kwa waume wao waliokuwa na uraibu wa pombe.

Kama anavyosema Blackstone (2003), majukumu ya kijinsia yanajikita kwenye matarajio, amali na desturi za wanajamii kuhusu wanawake na wanaume. Majukumu ya wanawake na wanaume yanatokana na mahusiano miongoni mwa watu na mazingira yao. Aidha, mahusiano haya huashiria tabia zinazofaa na zisizofaa kwa mujibu wa jamii husika. Katika tamaduni nyingi ulimwenguni, wanawake wanatarajiwa kufanya kazi za nyumbani na kutunza familia ilhali wanaume wanatarajiwa kufanya kazi zitakazoiwezesha familia kukidhi mahitaji yao ya kifedha.

Wanaume wanaposhindwa kutekeleza wajibu huu, wanadharauliwa na kusutwa na wanajamii wengine. Kwa mfano, majirani wa Zakaria walifahamu namna ulemavu wa tabia ya unywaji pombe ulivyokuwa umemwathiri Zakaria. Mwandishi anadhihirisha madai ya Blackstone anapoeleza namna ulevi ulivyokuwa umemwathiri Zakaria kiasi kwamba hakuwajali watoto wake. Anaeleza:

> Jirani zake walisema (Zakaria) alijali pombe kuliko watoto: alikuwa hajatoa hata chapa kuwalipia watoto ada ya shule. Kama sasa watoto walikuwa shuleni, heko kwa mama yao. Regina alilima pamba kwa bidii, na pesa alizopata aliwavika watoto wake. (Kezilahabi, 1976, uk. 6).

Kutowajibika na kutowajali watoto wake kunadhihirika wakati inapoibuka kuwa Zakaria alichukua pesa ambazo Regina alikuwa ameweka ili kumlipia shule Rosa, binti yao. Regina alikuwa amezipata pesa hizo baada ya kumuuza ng'ombe mmoja kati ya ng'ombe wanne aliyokuwa amerithi kutoka kwa baba yake mzazi. Zakaria alichukua pesa hizo, akaenda kunywa pombe na kuwanunulia marafiki zake. Kitendo hili kinaashiria kuwa Zakaria alikuwa na ugonjwa wa akili. Kama anavyosema Beresford (2007), uchunguzi wa tiba wa unywaji pombe kupindukia unaonyesha kuwa mtu mwenye uraibu wa pombe hajali matokeo ya matendo yake ila hufanya chochote kile ili aweze kutimiza haja yake ya kulewa. Hivyo basi tabia yake huashiria hali ya kupungukiwa kifikra, kimwili na katika mahusiano yake na jamii. Hali ya kupungukiwa akili kwa Zakaria inadhihirika zaidi mwandishi anapoelezea zaidi kuhusu kutowajibika kwake kutokana na taathira ya pombe. Anasema:

> Zakaria alikuwa ameshindwa hata kujenga nyumba ya maana. Katika nyumba alimokuwa akilala sasa pamoja na watoto wake, nyota zilikuwa zikiwashangilia kila usiku. (Kezilahabi, 1976, uk. 6).

Mwandishi anaeleza namna nyumba ya Zakaria ilivyokuwa. Zakaria alikuwa ameshindwa hata kujenga nyumba ya maana.Yeye pamoja na familia yake walikuwa wakiishi katika nyumba mbovu. Mwandishi ametumia tashihisi kama mtindo wa

kueleza hali mbovu ya nyumba ya Zakaria. Anasema kuwa '*nyota zilikuwa zikiwashangilia kila siku'* kumaanisha kuwa wakiwa ndani ya nyumba usiku walikuwa wanaona mbingu, ili kuchora taswira ya hali mbovu ya nyumba ya Zakaria. Kupitia tashihisi hii inabainika kuwa paa la nyumba yake lilikuwa limeharibika. Uhafifu wa nyumba ya Zakaria unadhihirika zaidi mwandishi anaposema kuwa watu waliofika kwa Zakaria kunywa pombe walishangaa walipoona nyumba ya Zakaria ilikuwa '*imelala upande.'* Kulala upande ni ishara ya kisemiotiki inayowasilisha ujumbe kuwa nyumba ya Zakaria hakuwa thabiti. Nyumba iliyolala upande inaashiria hali ya kutokuwa imara ishara kuwa nyumba yenyewe imejengwa kwa vifaa hafifu au imezeeka mno kiasi kwamba msingi wake si imara. Kwa hivyo, kulala upande kwa nyumba ya Zakaria kuliashiria hali mbovu ya nyumba hii na kwamba ilikuwa karibu kuanguka. Makazi ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya binadamu, hivyo basi hali Zakaria ya kutojali usalama wa makazi ya familia ni ishara kuwa unywaji pombe ulikuwa umeathiri hata urazini wake kama binadamu. Kama wanavyosema wanasaikolojia Prun na wengine (2010), unywaji pombe unatokana na ulemavu wa akili ambapo mwathiriwa hukosa msukumo wa kihisia wa kutambua athari zinazotokana na tabia yake ya ulevi. Maoni ya hawa yanaweza kuwa kigezo cha kufahamu tabia ya kutojali kuhusu hali duni ya maisha ya familia ya Zakaria ikizingatiwa kwamba kufutwa kazi kwake kulitokana na ulevi na hatimaye kuchangia katika hali duni ya maisha ya familia yake.

Mwandishi anawasilisha ujumbe kuhusu athari zaidi za unywaji pombe kupindukia wakati inapobainika kuwa tabia hii ndiyo iliyosababisha kifo cha Zakaria. Zakaria alienda kwenye mazishi ya Ndalo, jirani yake, akiwa mlevi na kusema maneno yaliyowaudhi watu. Mwandishi anaeleza tukio hili:

> Watu wengi walikuwa wakizungumza kuwasalimu waliofiwa; mji wote ulikuwa na huzuni. Wakati huohuo mtu mmoja alisikika akiimba wimbo. Watu walishindwa kufahamu kama mtu huyo alikuwa akiimba au labda mlevi. Alipofika nyumbani kila mtu alimwangalia. Mji wote ulinyamaza kimya! Alikuwa Zakaria, alikuwa akiyumbayumba: alikuwa amekunywa. Alianza kupiga kelele. "Watu wote mliopo hapa, mnatafuta nini! Mnafikiri hapa kuna arusi! Ondokeni hapa! Ndalo amekwishakufa kesho ataoza! Sitaki kusikia mtu akilia bwe! bwe! hapa!" Watu wote walikuwa kimya. Zakaria alifanya jambo la ajabu. Kila mtu alishangaa: huu haukuwa wakati wa kusema maneno kama hayo. Zakaria alikuwa amelewa; lakini sio tu ulevi uliomfanya aseme hivi, lakini hasa kwa kuwa alikuwa amezoea mizaha. (Kezilahabi, 1976, uk. 89).

Ingawa ulikuwa mzaha tu, ulitumbuka karaha wakati mtu mmoja alipomchoma Zakaria mkuki na kumuua kwa madai kuwa alikuwa anaudharau mji wa Ndalo.

Kama anavyosema Byant (2011), mtu mwenye ulemavu wa tabia hukiuka kaida na sheria za jamii. Kadhalika, watu wenye tabia zinazowakera wanajamii hutengwa na kuadhibiwa na wanajamii. Tabia ya Zakaria ya kuleta mzaha mahali kwenye msiba huku akiwa mlevi iliwaudhi watu waliokuwa wamekuja kuomboleza na familia ya Ndalo kwa kuwa ni tabia iliyokiuka matarajio ya jamii. Ingawa kwake Zakaria ilikuwa ni utani, hali yake ya ulevi iliwafanya wanajamii kufasiri lengo lake kwa namna tofauti.

Kupitia kwa kisa cha kuuawa kwa Zakaria mazishini, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa pombe inaweza kumsukuma mtu hadi akafanya mambo ambayo yanawaudhi watu wengine. Swegan (2011) anasema kuwa watu wenye uraibu wa pombe hutumia pombe kama njia ya kupunguza mawazo wanapokumbwa na jambo linalowafadhaisha. Aidha ni njia ya kuwasahaulisha uhalisia unaowazunguka. Kitendo cha Zakaria kufika mazishini akiwa mlevi kinaweza kufasiliwa kwa msingi wa madai ya Swegan. Ndalo na Zakaria walikuwa marafiki na hivyo basi inaelekea kuwa kifo cha Ndalo kilimhuzunisha Zakaria. Zakaria alikuwa amefadhaishwa na kifo cha rafiki yake na kulewa kwake kulikuwa ni njia ya kujituliza. Hata hivyo wanajamii waliiona

tabia ya Zakaria kama ya mtu asiye na heshima; hawakufanya jitihada zozote kufahamu chanzo cha hali yake ila walimwadhibu kwa kumtoa uhai. Kupitia kisa hiki mwandishi anatoa ujumbe kwamba wanajamii wanapaswa kuwachukulia watu walioathiriwa na uraibu wa pombe kama watu walio na tatizo la akili wanaohitaji usaidizi wa kimatibabu badala ya kuwaadhibu, kuwashtumu, kuwatenga na hata kuwadhuru.

### 3.2.2 Ulemavu wa Tabia ya Matumizi ya Mihadarati kama Mtindo

Kwa mujibu wa Rexed na wengine (1984) matumizi ya dawa asili yamekuwepo tangu zamani. Kimsingi, dawa zilikuwa zinatumiwa kwa lengo la kutibu maumivu na magonjwa mbalimbali. Hata hivyo, kama wanavyosema Rexed na wenzake, binadamu amegeuza matumizi ya baadhi ya dawa hizi kwa kuzitumia kwa njia inayoleta madhara kwa mwili. Matumizi ya dawa hizi kwa kipindi kirefu kunasababisha hali ya mazoea na utegemezi kiasi kwamba mwathiriwa hupata uraibu wa dawa hizi. Kwa mujibu wa taasisi ya kitaifa inayohusika na matumizi ya dawa za kulevya nchini Marekani, NIDA (2011), uraibu wa dawa za kulevya ni ugonjwa sugu ambapo mwathiriwa hupatwa na msukumo mkuu ambao hawezi kujizuia licha ya madhara yake. Kwa miaka mingi binadamu amekuwa akitafuta mbinu mbalimbali za kukabiliana na hali ngumu zinazomkabili maishani. Mojawapo ya mbinu hizi ni matumizi ya mihadarati. Shirika la Afya Ulimwenguni (1990) linaeleza uraibu wa mihadarati kama matumizi mabaya ya dawa zozote zile zikiwemo zile zinazotumiwa katika tiba. Kadhalika, matumizi ya dawa za kulevya ni tabia ya kutumia dawa kwa kiasi kisichofaa au kwa mbinu zisizofaa na kusababisha madhara kwa mtu binafsi na kwa jamii. Matumizi ya mihadarati humwathiri mtu kiasi kwamba hawezi kuishi maisha ya kawaida bila kuzitumia na hivyo basi matumizi yake hudumu na hatimaye kuathiri kazi, majukumu na mahusiano yake na watu wengine kwa njia hasi.

Kulingana na taasisi ya kitaifa inayohusika na matumizi ya dawa za kulevya, NIDA (2011), matumizi ya dawa za kulevya ni ugonjwa tata ambao ni vigumu kutibu iwapo mhusika hana azma ya kuacha tabia hii. Mihadarati hubadili ubongo kiasi kwamba inakuwa vigumu kuacha kuitumia.

Matumizi ya dawa za kulevya ni ulemavu wa tabia ya kujidhuru. Dawa za kulevya ni kama vile: bangi, hashishi, kokeini, heroini, tumbaku, dawa za kupunguza uchungu na dawa za kutuliza mawazo. Baadhi ya dawa hizi hutumiwa katika matibabu lakini zinapotumiwa vibaya bila uelekezi wa daktari zinakuwa na madhara makubwa kwa wanaozitumia.

Dawa za kulevya zitakazoangaziwa katika sehemu hii ni bangi na hashishi kwa kuwa ndizo zinazojitokeza katika riwaya teule. Kwa mujibu wa Petersen (1980), marijuana hutokana na jani la mmea uitwao '*cannabis sativa'* ilhali hashishi hutengenezwa kutokana na ua la mmea huo. Petersen anaendelea kusema kuwa ingawa bangi haiathiri ubongo kwa kiasi kikubwa kama dawa zingine za kulevya, inaweza kuwa na madhara makubwa inapotumiwa kwa muda mrefu na kwa kiwango kikubwa. Mbali na athari za kiafya, bangi na hashishi hutatiza uwezo wa mtu wa kukumbuka mambo. Kama anavyosema Peterson, matumizi ya dawa hizi humfanya mtu kufanya mambo yanayodhihirisha hali ya kutokuwa na urazini wa binadamu wa kawaida.

Taswira ya ulemavu wa tabia ya matumizi ya dawa za kulevya inajitokeza kupitia kwa mhusika Haji katika riwaya ya *Dunia Mti mkavu*. Kijana huyu alikuwa mvuta bangi na hashishi. Tabia, mienendo, mwonekano wake na maneno yake yanadhihirisha athari za matumizi ya dawa hizi. Kwa mfano, Haji alipoenda kuchota maji mferejini mahali alipokuwa anaishi, hakuwajulia hali watu aliowakuta pale

wakisubiri kuchota maji. Mwandishi anatuchorea taswira ya mtu ambaye hakujielewa. Anasema:

> Wakati huu alitokea Haji, kijana mvuta bangi *aliyechongwa vibaya na mazingira yake* na kupuuzwa na walezi wake. Hakuna asiyemjua kwa *uchache wake wa adabu*. Alikuja na doo lake bila ya kujali waliokuwepo. *Hakuja na salamu wala shikamoo*. Uso wake unabashiri kisirani, umejaa makupekupe machoni. Dovuo limemganda kidevuni. Nywele zake zilizosongamana zimejaa usufi. Alikuja kifua wazi na mwili wake umerembwa ramani nyeupe iliyokuwa haikusaza nafasi. Ngozi yake *nyeusi tititi* haikuficha *damu ya ujana* inayochangia ukubwani. Suruali ya kijani iliyokunjwa hadi magotini imetonewa rangi za kila namna; siku nyengine Haji alipata bahati ya kuwasaidia waashi na wapaka rangi. (Mohamed, 1980, uk. 33).

Maelezo haya ya mwandishi yanatoa taswira ya hali ya Haji alipofika mferejini kuchota maji. Picha ya kijana mchafu ambaye hakuwa anajali yeyote wala chochote inajitokeza. Pale mferejini palikuwa na watu wengi waliokuwa wanasubiri kuchota maji lakini Haji hakuongea na yeyote ila aliwapita wote na kwenda kuchota maji bila kuzingatia kuwa watu wale walitangulia kufika pale.

Kuna sababu tofauti zinazosababisha matumizi ya dawa za kulevya. Kulingana na taasisi ya kitaifa inayohusika na mihadarati, NIDA (2011), hali ya maumbile pamoja na mazingira yanayomzunguka mtu yanaweza kuwa chanzo cha matumizi ya mihadarati. Mazingira ya mtu yanashirikisha familia, marafiki, hali ya kiuchumi na kiwango cha maisha kwa jumla. Kwa mujibu wa NIDA, marafiki, mfadhaiko, dhuluma ya kimwili na kimapenzi pamoja na malezi huchangia sana katika kumfanya mtu kujiingiza katika matumizi ya mihadarati. Madai ya NIDA yanadhihirika katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Mwandishi anaeleza sababu zilizomfanya Haji ajiingize katika matumizi ya mihadarati. Anaeleza kuwa (Haji) '*alichongwa vibaya na mazingira yake'*. Kuchonga ni kutengeneza au kuunda kitu. Kwa hivyo, msemo huu unamaanisha kuwa Haji hakuwa amelelewa katika mazingira mazuri ambayo

yangemuunda ipasavyo. Kadhalika, msemo huu unaashiria kuwa mazingira alikokulia Haji yalichangia katika kujiingiza kwake kwenye matumizi ya mihadarati. Kwa mujibu wa Kimble na wengine (1980), mihadarati hutumiwa na watu kama njia ya kukabiliana na matatizo na changamoto zinazowakumba maishani. Inabainika kuwa Haji alikulia katika mazingira ambapo walezi wake walimpuuza. Mwandishi anasema:

> Wakati huu alitokea Haji, kijana mvuta bangi aliyechongwa vibaya na mazingira yake na kupuuzwa na walezi wake. (Mohamed, 1980, uk. 33).

Kupitia kwa mhusika Haji mwandishi anaendeleza maudhui ya malezi na nafasi ya wazazi katika kuwalea watoto wenye maadili katika jamii. Anaashiria kuwa wazazi wasipojishughulisha na malezi ya watoto wao na kuwapuuza, watoto hawa wanaweza kuathirika katika maisha yao ya baadaye kwa kuwa hawakupata msingi bora na mawaidha kutoka kwa wazazi wao.

Mwandishi anaashiria kwamba wazazi wanapotelekeza majukumu yao athari zake hudhihirika katika maisha na tabia za watoto wao. Kwa mfano, inabainika kuwa Haji alikuwa haendi shuleni kama watoto wengine wa umri wake. Badala yake alikuwa anafanya kazi za sulubu kama vile kuwasaidia waashi, wapaka rangi na kuwachotea baniani maji ili aweze kupata pesa za kujikimu na kununua mihadarati. Kupitia kwa mawazo ya mhusika kwa jina Bakari, mchango wa malezi mabaya katika kukuza vijana wanaojiingiza katika matumizi ya mihadarati unajitokeza. Bakari anawaza haya kumhusu Haji:

> 'Masikini, si kosa lake,' aliwaza Bakari aliyekuwa kasita anamtazama (Haji), 'na hawa, watoto kama hawa, wako wengi.' (Mohamed, 1980, uk. 33).

Bakari alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wamefika pale mferejini kuchota maji. Anaonekana kusikitika kutokana na hali mbaya ya Haji hasa ikibainika kuwa

halikuwa kosa lake kwamba alikuwa katika hali ile. Kupitia kwa mawazo ya Bakari, mwandishi anaashiria kuwa kuna watoto wengi katika jamii ambao wameathiriwa na mihadarati kutokana na ukosefu wa malezi yanayofaa.

Mwandishi anasawiri upotovu wa tabia wa Haji anaposema kuwa Haji alikuwa '*mchache wa adabu*. Msemo huu una maana sawa na msemo '*mchache wa muhali*.' Kwa mujibu wa Mkota na Sakara (2011) msemo huu una maana ya mtu anayeweza kufanya lolote; mtu asiyejali; anayeweza kutenda maovu. Sifa hizi zinajitokeza katika mhusika Haji kwa kuwa anaonekana kutojali matendo yake, jambo linalodhihirika katika tabia yake alipoenda mferejini kuchota maji. Mwandishi anasema kuwa (Haji) '*hakuja na salamu wala shikamoo.'* Kauli hii inamaanisha kuwa Haji alikuwa mtovu wa nidhamu hivi kwamba hakuwaheshimu wengine. Kwa kawaida watu katika jamii hujuliana hali kama desturi inayokuza uhusiano mwema miongoni mwao. Kutowaamkua watu ni ulemavu wa tabia kwa kuwa ni kinyume na kaida na desturi za jamii. Kulingana na Spooner (1999), utovu wa nidhamu huibuka wakati vijana wanapokosa uhusiano ufaao na asasi za kijamii kama vile familia, shule na kanisa ambazo ni za msingi katika malezi. Utengano kati ya vijana, amali, mila na desturi za jamii unaweza kusababisha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Spooner anasema kuwa ukosefu wa uhusiano bora kati ya mtu na wanajamii wengine ni sifa mojawapo ya mtu anayetumia dawa za kulevya. Aidha, Spooner anadai kuwa mtu mwenye uraibu wa mihadarati hudhihirisha hali ya kuasi, ukiukaji wa kaida za jamii na ukosefu wa uwajibikaji unaojitokeza kupitia kwa kukataa masomo, mavazi mabovu, uchafu, upweke na ukosefu wa maadili. Said Ahmed Mohamed anathibitisha madai ya Spooner kupitia kwa mhusika Haji katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Haji alikuwa mvulana wa umri wa makamo lakini alikuwa mchafu kiasi kwamba ngozi yake ilikuwa imegeuka rangi. Taswira hii inaibua hali ya mtu ambaye hakujijali

kamwe. Kupitia kwa Haji mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa kuna vijana ambao wameathirika na matumizi ya dawa za kulevya katika jamii kiasi kwamba wanaishi maisha ambayo hayaambatani na maadili na kaida za jamii. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya huathiri afya na maisha ya mtu binafsi na jamii kwa jumla.

Ukosefu wa maadili wa Haji unajitokeza pia kutokana na jinsi alivyong'ang'ania kuchota maji kabla ya watu waliokuwa wamemtangulia. Hata hivyo, baadhi ya watu kama vile Mzee Fuko hawakukubali wapitwe. Mwandishi anaeleza hali ilivyokuwa:

> Mzee Fuko, mzegazega, ndiye aliyekataa kuchezewa na kitoto kidogo cha juzi kilichozaliwa akiona. Alikata kwamba katu hatokubali *kutapikia sandani*. … 'Shika adabu yako,' Mzee Fuko alimsukuma Haji, lakini Haji hakutikisa. *Alitia nanga* miguuni na kushikilia kuweka doo lake. 'Tutaona leo, mimi na wewe nani *aliyeanza kuliona jua*. Huteki maji hapa leo mpaka sisi sote tumalize, umetukuta eti. Wewe nani usiyekuwa na adabu?' (Mohamed, 1980, uk. 34).

Mwandishi anaeleza mvutano uliotokea kati ya Mzee Fuko na Haji. Mzee Fuko hakutaka kumruhusu Haji achote maji mbele ya watu wengine waliomtangulia kufika pale mferejini lakini Haji alitaka kuchota mwanzo bila kujali utaratibu uliokuwepo. Tabia ya Haji inadhihirisha ukosefu wa maadili kwa kuwa hana heshima na mahusiano mema na wanajamii wengine. Kama anavyosema Buckman (1971), vijana walioathiriwa na dawa za kulevya hukaidi kanuni zilizowekwa na wanajamii kuhusu mahusiano mema. Tabia hii inakusudia kuwaudhi, kukuza mkinzano, kuzua ubishi, kuharibu vitu, kuwakejeli watu na kuzua hali ya msukosuko na usumbufu miongoni mwa jamii.

Mwandishi anatumia ulemavu wa tabia wa Haji wa kutumia mihadarati kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya athari za ukosefu wa nafasi za ajira. Ukosefu wa ajira unawafanya vijana kujiingiza katika matumizi ya mihadarati kwa kuwa wamekata tamaa maishani. Kwa mujibu wa Jirapramukpitak na wengine (2008), uhamaji wa

watu kutoka vijijini kwenda mijini unasababisha hali ya ukosefu wa ajira. Vijana wanapohamia mijini wanakabiliana na hali ngumu ya maisha. Aidha, wanakosa misingi bora ya mawaidha kwa kuwa wako mbali na jamaa zao. Jambo hili linaweza kuwafanya wajiingize katika matumizi ya mihadarati. Kadhalika, ukosefu wa ajira unawalazimisha watu kujihusisha na kazi za sulubu. Wanawake wanajiingiza katika kazi ya umalaya na hatima yake ni uzazi wa watoto wanaokosa malezi bora kutoka kwa baba na mama. Kwa mujibu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa; UNDP (1990), kuongezeka kwa idadi ya watu katika miji mikuu ya mataifa yanayoendelea kumesababisha kuwepo kwa watoto wengi wa mitaani ambao wanaishi maisha ya umaskini, hali ambayo imezidisha matumizi ya dawa za kulevya. Kupitia kwa Mzee Fuko, mwandishi wa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* anaashiria hali hii anapomsuta Haji na kumkumbusha kuwa yeye hana baba. Anamwambia:

> (Mfereji) wa babaako, kama unaye; haya matoto yanayozaliwa njiani, nd'o yalivyo hivi. Yatamheshimu nani? Wallahi haya matoto yanayozaliwa vichochoroni ndivyo yalivyo. Yatamheshimu nani; mama mmoja, baba ishirini.' (Mohamed, 1980, uk. 34).

Mkinzano kati ya Mzee Fuko na Haji unajitokeza hapa. Fuko analalamika kuhusu watoto ambao hawana heshima. Anadai kuwa mazingira ambako walizaliwa yalichangia katika ulemavu wa tabia za watoto hawa.

Mwandishi anatumia uraibu wa dawa za kulevya wa Haji kuashiria matatizo mengi yanayowakabili watu wanaoishi mijini. Kwa mujibu wa Schifano (2011), mazingira ya mjini ni muhimu katika kubainisha tabia zinazoathiri afya ya jamii. Anaendelea kusema kuwa uhamaji wa watu kutoka vijijini kwenda kuishi mijini umeathiri miundo misingi katika maeneo ya mijini. Aidha, uhamaji huu unaweza kuwa chanzo cha mabadiliko ya tabia miongoni mwa jamii ambapo baadhi ya watu hujiingiza katika matumizi ya mihadarati kama njia ya kukabiliana na hali ngumu ya maisha

inayowakabili. Madai ya Schifano yanadhihirika katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ambapo watu wanang'ang'ania rasilimali. Mzozo wa maji unaashiria ukosefu wa mahitaji ya kimsingi miongoni mwa watu hawa kama inavyodhihirika katika majibizano kati ya Haji na Mzee Fuko:

> 'Pisha mzee wewe; sisi tunakwenda kazini,' alitoa ukali Haji. 'Kazi kazi, una kazi wewe? Una kazi gani? Kazi yenyewe ya kuosha vyombo kwa Baniani, mshahara dengu, si bora kazi yangu ya mzegazega? Ndiyo, wakeshashindwa kulima huko kwao shamba, hujipa: nataka mjini, nataka mjini. Ati kutafuta kazi. Kazi gani za mjini zitakazotafutwa na nyinyi! Nenda kafute hashishi huko, au kanywe kinibu kwa Mussa Kizibo.' 'Wewe nini mzee, unajidai tu, wewe ulizaliwa mjini wewe?' Haji aliuliza kwa ushupavu. Mzee Fuko alipwesapwesa macho kwa swala hilo. (Mohamed, 1980, uk. 34).

Wakazi wa mijini wanalazimika kung'ang'ania rasilimali chache zilizopo kama vile maji, choo, chakula na ajira. Aidha, wanaishi katika nyumba duni. Maisha haya yanasababishwa na watu wengi wanaohamia mijini kutoka vijijini. Mzee Fuko anamkejeli Haji anapotaka kupishwa pale mferejini kwa madai kuwa alikuwa anaenda kazini. Mzee Fuko anasema kuwa kazi yenyewe haikuwa kazi ya maana kwa kuwa ilikuwa ya kuosha vyombo na mshahara wake ulikuwa duni. Anadai kuwa kazi yake ya kuuza maji ilikuwa bora zaidi. Ni kinaya kuwa Mzee Fuko anawakashifu wanaohamia mjini kutafuta kazi na kushindwa kulima ilhali yeye mwenyewe alikuwa anaishi mjini na kufanya kazi ya kuuza maji.

Katika sehemu hii, swala la matumizi ya mihadarati kama ulemavu wa tabia na matumizi yake kama mtindo limeshughulikiwa. Kupitia kwa uraibu wa dawa za kulevya wa Haji mwandishi amewasilisha ujumbe kuhusu mazingira ya kijamii na kiuchumi yanayochangia katika matumizi ya mihadarati. Imebainika kuwa umaskini, malezi yasiyofaa, ukosefu wa kazi na mahitaji ya kimsingi ni baadhi ya mambo yanayowafanya watu kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, ulemavu

wa tabia wa matumizi ya dawa za kulevya kama mtindo wa kuangazia mahusiano ya jamii na mtu binafsi umeshughulikiwa.

Katika sehemu inayofuata ulemavu wa tabia ambapo mtu huamua kujidhuru kwa kujitoa uhai umeangaziwa kwa kuchanganua wahusika na matukio katika riwaya teule. Kadhalika, matumizi ya ulemavu huu kama mtindo wa mwandishi wa kuwasilisha ujumbe wake yamezingatiwa.

### 3.2.3 Matumizi ya Ulemavu wa Tabia ya Kujiua kama Mtindo

Shirika la Saikolojia la Uingereza (2015), limeeleza maana ya kujiua kuwa ni tabia ambapo watu hujidhuru kwa lengo la kujitoa uhai. Aidha, shirika hili linasema kuwa watu hawa hufa kutokana na matendo yao wenyewe. Watu ambao hunusurika kifo baada ya jaribio la kujiua wanaweza kupata majeraha mabaya. Geberth (1996) alifanya uchunguzi ili kubaini kuhusu saikolojia ya mtu anayeamua kujiua na kubaini kuwa mtu huyu huchukulia kuwa kitendo chake ni suluhu kwa mtanziko fulani wa kisaikolojia au wa kimwili unaomkabili. Kwa hivyo, mawazo ya kujiua yanajikita katika muktadha wa afya ya kiakili. Hii ni kwa sababu kama anavyodai Geberth, msukumo wa kitendo hiki ni mfadhaiko wa akili unaotokana na msongo wa mawazo au ugonjwa wa akili. Mbali na ugonjwa wa akili, ripoti ya Kituo cha Kukabiliana na Magonjwa cha Marekani, CDC (2015), inaeleza kuwa tabia ya kujiua inaweza kusababishwa na majaribio ya mtu ya awali ya kujiua, matumizi ya pombe, kuwepo kwa historia ya tabia hii katika familia, maradhi na upweke. Kutokana na maelezo haya inadhihirika kwamba watu wanaojiua huwa na ugonjwa wa akili na hali hii huwalemaza kifikra kiasi kwamba wanajiingiza katika tabia ambayo ni kinyume na matarajio ya jamii kwa kujiua. Kwa mujibu wa Kituo cha Kukabiliana na Magonjwa, watu wengi wanaojiua wanaamini kuwa kitendo hiki ndicho njia ya pekee ya

kukabiliana na hali gumu zinazowakabili. Watu wanaokuwa na fikra za kujiua mara nyingi hukumbwa na matatizo au uchungu mwingi kiasi kwamba wanashindwa kutafuta njia mbadala za kukabiliana na shida zinazowakabili.

Katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi, kuna wahusika ambao wanadhihirisha ulemavu wa akili unaosababisha ulemavu wa tabia kwa kukusudia, kupanga kujiua au hata kujiua. Waandishi hawa wametumia ulemavu huu kama mtindo wa kuwasilisha jumbe zao katika riwaya teule.

Katika riwaya ya *Tata za Asumini*, Asumini ni mhusika ambaye anaathiriwa na ulemavu wa akili. Ulemavu wa akili unamfanya aamue kujitoa uhai kwa kujirusha kwenye kidimbwi cha kuogelea. Kitendo cha kujiua au kukusudia kujiua ni ulemavu wa tabia kwa kuwa kinaenda kinyume na matarajio ya jamii inayothamini uhai. Kama ilivyojadiliwa katika sura ya pili, ulemavu wa Asumini ulitokana na mazingira aliyoishi ambayo yalikinzana na malezi aliyopewa na wazazi wake.

Kulingana na Joiner (2006), msukumo wa kujiua unajikita katika matukio mawili ya kisaikolojia. Kwanza, mtu anayeamua kujiua huhisi kuwa yeye ni mzigo kwa watu wengine kutokana na ugonjwa wake wa akili. Kwa hivyo uamuzi wake wa kujiua huwa ni njia ya kuwaondolea shida watu wengine. Pili, kutokuwapo na uwiano kati ya mtazamo wa jamii na wa mtu binafsi unaweza kumfanya mtu apate mawazo ya kujiua. Joiner anasema kuwa tofauti za kimtazamo zinaweza kusababisha mkinzano unaomfadhaisha mtu na kuathiri akili yake na hatimaye kumfanya ajitoe uhai. Watu wanaokabiliwa na mkinzano baina yao na jamaa wa karibu, wanaweza kuamua kujiua. Kwa mfano, katika jitihada za kuelewa uhalisi wa mazingira yake, Asumini katika riwaya ya *Tata za Asumini* anapata mfadhaiko unaoathiri akili yake na mtazamo wake kuhusu maisha. Kwa mujibu wa Robert (1980), tabia ya kujiua

inatokana na ugonjwa wa akili. Aidha, kama anavyodai Jensen (2011), tabia hii inaashiria hali ya ukataji tamaa inayosababishwa na hisia kali za ukosefu wa haki na usawa katika jamii. Kauli ya Jensen inadhihirika kwenye uzungumzi nafsi wa Asumini kabla ya kuelekea kwenye kidimbwi alikonuia kujitosa.

> "Maisha ni nini?" Alijiuliza moyoni mwake, "Siha ni nini?" aliendelea kujiuliza, "Tofauti gani iliyopo kati ya kuishi na kufa? Au siha na uzima?" Asumini aliishia kucheka tu. Alijicheka mwenyewe. Yule pepo aliyemwacha punde alimvaa tena Asumini. Alikuja tena ghafla akamtimua tena mbio hadi ukingoni mwa bwawa. Hapo alikita, akatuwama huku akiyaangalia maji ya bwawa yaliyopiga kioo kote. Yalikuwa maji matulivu yasiyo matibwi wala hatia, yameumana na kiza cha usiku isipokuwa ile miale ya taa moja iliyowashwa na kuchezesha danedane juu yake. Baada ya dakika chache atajichovya kwenye bwawa, jee hiyo itakuwa hatia? Hajui kuogelea, hilo analijua fika na kwamba kifo kilimwelekea si jambo alilolishuku sasa, kwani ameshaamua. (Mohamed, 1990, uk. 6-7).

Mawazo ya Asumini alipokuwa kando mwa bwawa yanajitokeza hapa. Inabainika kuwa Asumini hakujua kuogelea kwa hivyo alikuwa na uhakika kwamba kujitosa kwenye bwawa kungesababisha kifo chake. Kutokana na mawazo ya Asumini hali ya ukataji tamaa inadhihirika. Mwandishi anatuelekeza kwenye wazo kuwa ukataji tamaa maishani unaweza kuwa chanzo cha ulemavu wa akili ambao hatimaye unaweza kumfanya mtu kujitoa uhai kwa kuwa hayathamini maisha. Mawazo ya kukata tamaa na kutothamini maisha yanaegemea katika nadharia ya udhanaishi.

Kwa mujibu wa Mastin (2008), udhanaishi ni falsafa inayosisitiza kuhusu uhai, uhuru na uwezo wa binadamu wa kufanya maamuzi. Falsafa hii inaendeleza mtazamo kuwa wanadamu wana uwezo wa kufanya maamuzi yenye urazini maishani licha ya ulimwengu tata unaowazunguka. Baadhi ya wanawafalsafa wanaoendeleza falsafa ya udhanaishi ni kama vile Kierkegaad, Nietzsche na Sartre. Falsafa ya udhanaishi inajikita kwenye dhana ya maisha na wazo kuwa maisha hayana maana. Aidha, kama anavyoeleza Mastin, wanaudhanaishi wanashikilia kuwa hakuna Mungu ama kiumbe

yeyote mwenye nguvu za kiungu na kwa hivyo, binadamu yuko huru kuyaendesha maisha yake namna anavyotaka. Kuna wanaudhanaishi kama vile Nietsche ambao hawana imani ya kidini na wanaamini kuwa Mungu hayupo na kuwa dhana ya Mungu haipo. Wanafalsafa hawa wanajishughulisha zaidi na imani kuwa maisha hayana maana. Said Ahmed Mohamed anamtumia mhusika Asumini ili kuendeleza maudhui kuhusu namna malezi na mazingira yanavyoweza kumfanya mtu kuwa na mawazo ya kukata tamaa na kujiua wakati anapokosa suluhisho la matatizo ya maisha yanayomkabili.

Asumini anaonekana akidadisi umuhimu wa maisha. Kwa mfano anajiuliza; "*Maisha ni nini*? *Tofauti gani iliyopo kati ya kuishi na kufa*?" Maswali anayojiuliza yanaashiria hali ya kukata tamaa. Kadhalika, Asumini anadadisi tofauti ya kuishi na kufa na tofauti ya siha na uzima. Udadisi huu unaashiria hali ya mawazo mengi yaliyomkabili Asumini na kumkanganya hasa alipojaribu kufanya maamuzi kuhusu maisha. Mkinzano huu ulitokana na mtazamo wake kuhusu maisha na namna ambavyo mawaidha aliyopewa na wazazi wake yalivyokinzana na ulimwengu halisi alioishi. Mwandishi anaeleza:

> Asumini sasa alifikiri juu ya utulivu na hamkani za dunia. Alifikiri pia juu ya kuwa na kutokuwa na hatia. Baada ya nukta chache atajichovya kwenye bwawa, jee hiyo itakuwa hatia? Hajui kuogelea, hilo analijua fika, na kwamba kifo kilimwelekea si jambo alilolishuku sasa, kwani ameshaamua. Kubwa alilolitaka (Asumini) ni kuuchangamkia ureda wa kuwepo pale, miguu chini na chupi na sidiria. Aliona raha. Aliona *utamu*. Kwa muda wa maisha yake pale chuo kikuu amekuwa akiwatazama wenzake wakistaladhi na *utamu wa* kuwa hivyo mbele ya watu, *utamu wa* kutojali mtumbuo wa macho ya mabarubaru, *utamu wa* kujichovya majini na kuogelea, *utamu wa* kupiga mbizi na kuibuka, *utamu wa* mnyongeresho na msisimko wa maji yale baridi na *utamu wa* kujifunza na kufunzwa kuogelea na mwanamme. (Asumini) alitaka awe peke yake katika uchungu wa kupapatika na kutapia pumzi za uhai, asiwepo mtu wa kuja kumwokoa na kumrejesha katika dunia ya masimango yaleyale. Alitaka kesho wamwone kitumbo juu, anaelea huku keshashiba maji. Wamwone ili wajue jinsi walivyokuwa wakimnyima tamu

> zote zile—wao wote waliomnyima: wote pamoja na babaake na mamaake. Wote wajue hiana yao! Waone uchungu na pengine wajute. Watambue kwamba naye ameonja utamu ingawa ulijaa machungu. (Mohamed, 1990, uk. 7).

Maelezo haya ya mwandishi yanaashiria fikra za Asumini kuhusu maisha na maana yake. Mwandishi anatumia neno '*utamu*' kuweka wazi hisia za Asumini ambazo zilimlemaza akili na hatimaye kumfanya aaamue kujiua. Kwake Asumini, kifo kilikuwa jambo ambalo lingempa raha, licha ya kuwa alikuwa akidadisi uhalali wa kitendo alichodhamiria kutenda.

Neno '*utamu*' linamaanisha hali ya kunoga kwa kitu au mambo (TUKI, 2004). Mwandishi anatumia neno utamu kueleza hisia za Asumini na mawazo yake kuhusu hali yake ya kuwa na mavazi hafifu bila kujali watu waliomwona wangesema nini. Neno utamu limerudiwarudiwa ili kusisitiza uzito wa hisia alizokuwa nazo za kuwa huru. Asumini alitamani kuishi maisha yenye uhuru bila vikwazo vyovyote lakini hangeweza kwa kuwa kuishi maisha kama hayo kungeenda kinyume na mafunzo aliyopewa na wazazi wake kuhusu namna tabia ya mwanamke inavyopasa kuwa. Alionelea kuwa kifo kingempa uhuru alioutamani. Inaelekea kuwa azimio la Asumini la kujiua lilidhamiria kuwapasha ujumbe wazazi kuwa walifanya kosa kwa sababu ya kumnyima uhuru wa kuishi maisha ambayo hayakuwa na mikatale. Wazazi wake Asumini walimlea kwa kumwekea vikwazo na kumnyima haki ya kujiamulia mambo hasa kuhusiana na maadili yanayopaswa kufuatwa na mwanamke katika jamii.

Kama wanavyosema Halpenny na wenzake (2010), familia ndiyo mazingira ya kimsingi ambapo maisha ya watoto wengi hupewa mwelekeo. Kigezo muhimu katika mfumo wa kumjamiisha mtoto ni mbinu za malezi na namna ambavyo wazazi hukabiliana na nidhamu ya watoto wao. Mbinu za malezi hutawaliwa kwa kiwango kikubwa na kaida na matarajio ya jamii. Kaida hizi ni kama; imani za kitamaduni, dini

na sheria zinazotawala imani na desturi mbalimbali za jamii. Kwa hivyo Asumini alikuwa anaelekezwa kulingana na mafunzo ya dini (ya Kiislamu) na matarajio ya jamii iliyomzunguka. Ni katika jamii hii na imani za dini ya Kiislamu ambapo masuala ya maadili yalijikita. Hata hivyo, mafunzo haya yalimtatiza Asumini kwa kuwa hayakuoana na ulimwengu halisi aliokutana nao alipotoka kwao kijijini na kwenda kusomea mjini.

Jaribio la Asumini la kujitoa uhai ni ulemavu wa tabia unaotumiwa na mwandishi kuendeleza maudhui ya malezi. Kitendo chake kinaashiria kuwa malezi aliyopewa yalikuwa na kasoro kwa kuwa yalikuwa chanzo cha Asumini kulemaa akili kutokana na kutoelezwa wazi kuhusu baadhi ya maswala nyeti hasa yaliyofungamana na mahusiano ya kimapenzi. Wazazi wa Asumini walimnyima haki ya kufanya maamuzi kuhusu uhusiano wake na wanaume. Kadhalika, walimwekea vikwazo kuhusu mavazi na mwenendo wake kama mwanamke. Ingawa lengo la wazazi wake lilikuwa ni kumkuza kama mwanamke mwenye maadili hawakumweleza sababu za kumwekea mikatale ile. Kadhalika, hawakuzingatia kuwa Asumini angekua kiumri, kimawazo na kimtazamo na kwamba maishani mwake angetangamana na watu wenye mitazamo tofauti. Kwa hivyo wazazi wake Asumini walipaswa kumwelekeza kwa njia ambayo haingezua malumbano kati ya nafsi yake na ulimwengu halisi.

Ulemavu wa tabia umetumiwa na Kezilahabi kuendeleza maudhui ya malezi na athari zake kwa mtoto wa kike katika riwaya ya *Rosa Mistika.* Kwa mujibu wa Moges na Weber (2014), hali ya akili ya mtoto huchangia sana katika tabia yake. Kwa mfano, watoto wanaweza kuwa na mawazo hasi au majuto makuu iwapo walilelewa katika mazingira ambapo wazazi walikuwa wakali au walitelekeza majukumu yao ya ulezi. Madai ya Moges na Weber yanadhihirika katika mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika.* Rosa alijiua kwa kunywa vipande vya chupa vilivyokuwa vimesagasagwa.

Kutokana na kauli yake ya mwisho kabla ya kifo chake inabainika kuwa uamuzi wa Rosa wa kujiua ulitokana na malezi aliyopewa na baba yake. Baba yake alikuwa mkali mno na hakuitunza familia yake vyema kwa kuwa alikuwa mnywaji pombe kupindukia. Rosa aliamua kujitoa uhai baada ya kupokea barua kutoka kwa mchumba wake, Charles, aliyemfahamisha kuwa hangemuoa baada ya kugundua kuwa hakuwa bikira. Kwa mujibu wa Thomas (2006), tabia ya kujitoa uhai inaweza kusababishwa na ugomvi baina ya wapenzi, talaka na vurugu kati ya watu wawili wenye uhusiano wa karibu. Rosa hakupata maelekezo mazuri kuhusu mahusiano ya kimapenzi alipokuwa kijana. Jambo hili lilichangia kuzorota kwake kimaadili na matokeo yake yakawa ni kuachwa na mpenzi wake Charles. Rosa Anasema:

> Sasa ninakufa; ninakufa sasa. Maisha yangu yalikuwa magumu. Sasa nimeona wazi kwamba malezi yangu ndiyo yalikuwa chanzo cha taabu, malezi. Siyo malezi ya mama, lakini malezi ya baba yangu. Kweli baba alinichunga. Nilichungwa kama wasichana wa jela. Nilipopata uhuru nilishindwa kuutumia. Deogratias, Thomas, Charles; wote hao nimewapoteza. (Kezilahabi, 1976, uk. 91).

Rosa aliyasema maneno haya alipoanza kupoteza fahamu baada ya kunywa vipande vya chupa. Anamlaumu baba yake kwa kumchunga kama wasichana wa jela. Aidha, anaashiria kuwa aliwapoteza wanaume aliokuwa na uhusiano wa kimapenzi nao kutokana na athari za malezi aliyopewa na baba yake.

Rosa anadai kuwa maisha yake yalikuwa magumu na yenye taabu. Kauli hii ya Rosa inaashiria hali ya mtu ambaye aliridhishwa na ukweli kuwa alikabiliwa na kifo. Msomaji anapata wazo kuwa kifo ndicho kingemwondolea Rosa maisha magumu aliyoishi. Kama anavyosema Geberth (1996), watu wengi wanaojiua wanaamini kuwa kujitoa uhai ndiyo suluhu ya pekee ya hali ngumu ya maisha inayowakabili. Aidha, kujiua huwa ni mbinu inayotumiwa na watu wenye changamoto za kimaisha ili kujiepusha na uchungu wa moyo wanaohisi. Rosa anawaza kuhusu chanzo cha maisha

ya shida hasa kuhusu mahusiano yake na wanaume na kubaini kuwa yalisababishwa na malezi aliyopewa na baba yake. Kezilahabi anatumia ulemavu wa tabia wa Rosa kama njia ya kuwaonya wazazi dhidi ya malezi mabaya ambapo wanakosa kuwapa watoto mawaidha kwa namna ifaayo. Kadhalika anasisitiza umuhimu wa wazazi kuwa mifano bora kwa watoto wao ili wasije wakaathirika katika maisha yao ya baadaye kama ilivyokuwa kwa Rosa.

Rosa anatumia tashbihi anaposema kuwa '*alichungwa kama wasichana wa jela*'. Jela ni mahali ambapo wahalifu hufungwa kama adhabu ya makosa yao. Katika jela wafungwa hawana uhuru wa kufanya wanachotaka au kuishi maisha yao wanavyopenda kwa kuwa wanawekwa chini ya uangalifu mkali. Hivyo basi jela ni kiashiria cha ukosefu wa uhuru wa mtu kufanya maamuzi kuhusu maisha yake. Saussure (1983) anasema kuwa ishara ni sehemu ya maisha ya jamii na kwamba dhima na maana yake hutegemea miktadha inayorejelewa na mifumo mahsusi ya kodi. Kwa hivyo, Kezilahabi ametumia jela kuashiria kuwa baba yake Rosa alimlea binti yake katika hali ambayo alimwekea vikwazo vingi na kumfungia ili asitangamane na vijana wengine hasa wavulana kwa hofu kwamba wangemharibu kimaadili. Malezi ya Rosa yaliathiri maisha yake na kumchanganya katika maamuzi yake kuhusu mahusiano kati ya mwanamume na mwanamke. Alinyimwa uhuru na babake pale nyumbani na alipoenda chuoni, mbali na nyumbani, tabia yake ilibadilika kwa kuwa aliona kuwa amepata uhuru. Alijiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na wanaume tofauti. Maisha haya yalimfanya Rosa kutumiwa vibaya na wanaume na mwishowe kuachwa, hali ambayo ilimfanya akate tamaa. Kwa mfano, kabla ya kufa, Rosa alimwandikia Charles ujumbe ufuatao:

> Charles mimi nilikupenda. Ninakupenda hata sasa. Charles ninajiua kwa ajili yako. Lakini kwa kuwa ninakupenda, ninakwambia siri moja kubwa

> uizingatie. Charles kuoa bikira ni bahati tu wala si kitu cha kutafuta: ukimwonja mchumbako kabla ya ndoa si bikira tena, hata kama alikuwa. (Kezilahabi, 1976, uk. 93).

Rosa anaeleza sababu yake ya kujitoa uhai. Anasema kuwa alikuwa anampenda sana Charles na hangeendelea kuishi baada ya kuachwa naye. Ujumbe wa Rosa kwa Charles unaangazia upendo wa dhati aliokuwa nao kwake. Kwa mujibu wa Vitelli (2017) ingawa kuna mambo mengi yanayoweza kumfanya mtu aamue kujiua, suala la mahusiano limejitokeza kuwa sababu kuu ya ulemavu huu wa tabia. Vitelli anasema kuwa mtu anapokuwa katika uhusiano wa kimapenzi ulio thabiti hali yake kimawazo huwa tulivu, hivyo basi uhusiano huu unapovunjika, unaweza kuwa na madhara makubwa. Hii ni kwa sababu kama anavyodai Vitelli, uhusiano wa kimapenzi huhitaji kujitolea kiwakati na kihisia na unapovunjika, mwathiriwa huhisi kwamba amepoteza utambulisho wake na maisha yake. Hali hii husababisha mfadhaiko mkubwa kiasi kwamba mwathiriwa anaweza kuamua kujitoa uhai hasa iwapo sababu ya kusambaratika kwa uhusiano husika haikueleweka. Rosa anakumbwa na hali kama hii kwa kuwa hakuelewa ni kwa nini Charles aliamua kumuacha kwa sababu tu ya kutokuwa bikira. Katika ujumbe alioacha, Rosa anampa Charles wasia kuhusu suala la ubikira. Katika ujumbe huu inadhihirika kuwa Rosa alikuwa na uchungu kwa kuwa mwanamke ndiye alitiliwa maanani kwenye suala la ubikira na kwamba kulingana na maoni ya Rosa, kilichokuwa muhimu katika ndoa sio ubikira bali ni upendo wa dhati.

Kulingana na McKelle (2013), katika tamaduni nyingi ubikira wa mwanamke unathaminiwa zaidi kuliko wa mwanamume. Tangu wakiwa wadogo, wasichana husisitiziwa kuhusu umuhimu wa kuhifadhi ubikira wao hadi watakapoolewa rasmi na kwamba sifa ya ubikira inawapa thamani zaidi. McKelle anaendelea kusema kuwa mwanamke anapopoteza ubikira wake anaonekana kama mtu aliyeharibika na asiye na thamani. Katika baadhi ya tamaduni, wanawake ambao si bikira wakati

wanapoolewa hutimuliwa kutoka kwa makazi yao au kuuawa kwa madai kuwa wameaibisha familia zao. Kama anavyoendelea kusema McKeller, ubikira ni ishara ya usafi na mwanamke anapoolewa bila sifa hii huletea jamii yake aibu kubwa hata kama aliupoteza ubikira wake kwa kubakwa. Kwa upande mwingine, suala la ubikira wa mwanamume halitiliwi maanani na wanaume hawahukumiwi kwa kutohifadhi ubikira wao, badala yake wanasifika ikiwa wameshiriki ngono na wanawake wengi. Kama anavyosema Mbiti (1969), ndoa katika jamii za Kiafrika ni suala la kidini na ni wajibu wa kila mtu. Ni matarajio ya kila mtu ambaye hajaoa au kuolewa pamoja na jamaa yake kwamba atatimiza wajibu huu. Mtu anayekosa kuoa au kuolewa huonekana kama aliyeasi kaida za jamii. Kwa hivyo, kukatizwa kwa matumaini ya Rosa ya kuolewa kwa misingi kuwa hakuwa bikira kulimvunja moyo sana kwa kuwa alikuwa ameamua kutulia na kuolewa. Charles aliamua kutomuoa Rosa alipotambua kuwa Rosa hakuwa bikira kinyume na alivyokuwa amemwambia.

Kupitia ulemavu wa tabia wa Rosa wa kushiriki ngono kiholela na hatimaye kujiua, mwandishi anaashiria suala la mielekeo ya jamii nyingi kuhusu ubikira na nafasi yake katika kudumisha uhusiano mwema kati ya watu wawili wanaopendana. Rosa alihisi kwamba hakuwa na thamani na alikuwa ameleta aibu kwa familia yake na ndiyo maana aliamua kujiua. Jordan (2017) anasema kuwa dhana ya ubikira ni ya kimtazamo na chanzo chake ni jamii yenyewe. Anaendelea kusema kuwa mtu anapopoteza ubikira wake kitambulisho chake kama binadamu hakipotei na maisha yake hayabadiliki. Aidha, thamani yake haipotei. Hivyo basi ingawa ni muhimu kwa wanajamii kuzingatia maadili kuhusu mahusiano ya ngono, Jordan anasema kuwa kuwakashifu, kuwatenga na kuwaaibisha watu waliopoteza ubikira wao ni jambo lisilofaa.

Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kupitia kwa wahusika wa kike Asumini na Rosa wamedhihirisha namna malezi yanavyoweza kuwa chanzo cha ulemavu wa akili unaoweza kuwa sababu ya mtu kuamua kujiua. Waandishi hawa, kupitia kwa ulemavu wa akili unaosababisha ulemavu wa tabia ya kujidhuru kwa wahusika husika wanaendeleza maudhui kuhusu umuhimu wa wazazi kuwa waangalifu wanapowalea watoto wa kike. Inabainika kuwa ulemavu wa akili wa Asumini na wa Rosa ulitokana na mbinu ya malezi ya kimabavu iliyotumiwa na wazazi wao. Mbinu hii haikuwapatia wasichana hawa nafasi ya kutoa maoni yao na kueleza hisia zao. Walitarajiwa kufuata maagizo ya wazazi wao pasi na kudadisi amri na wasia wa wazazi wao. Matokeo ya mbinu hii ya malezi ni ulemavu wa tabia unaosabishwa na ulemavu wa akili.

Kisa kingine cha kujitoa uhai kinajitokeza katika riwaya ya *Kichwamaji.* Mhusika Kazimoto anajiua kwa kutumia bunduki. Kazimoto anajiua alipogundua kuwa alikuwa ameshiriki ngono na Pili ambaye alikuwa anaugua ugonjwa mbaya na alikuwa amemwambukiza mkewe Sabina aliyekuwa mja mzito. Ugonjwa alioambukizwa ulikuwa unavipata hata vizazi vya walioathiriwa. Kazimoto alipofahamishwa na Manase kuwa daktari aliyekuwa na uwezo wa kutibu ugonjwa huu alikuwa amekufa na vidonge vyote vya kutibu ugonjwa huu kuharibiwa, alikata tamaa na kuamua kujitoa uhai. Klonsky na wengine (2012) na Singh na wengine (1999) wanakubaliana kuwa kutokuwa na matumaini husababisha mawazo hasi kuhusu maisha ya siku zijazo ambapo mtu huamini kuwa hana uwezo wa kubadilisha hali gumu inayomkabili. Hali hii humfanya mwathiriwa kuwa na mfadhaiko na hatimaye hukata tamaa na kuamua kujitoa uhai. Kazimoto anaashiria hali ya kutokuwa na matumaini ya siku zijazo hasa alipogundua kuwa daktari aliyekuwa na uwezo wa kumtibu alikuwa ameaga dunia. Alimwachia mke wake ujumbe huu:

> Nimejiua. Siwezi kuendelea kuzaa kizazi kibaya. Pia sikuona tofauti kati yangu na mdudu au mnyama. Akili! Akili! Akili ni nini? Pia nikiwa duniani sikupata kukutana hata siku moja na mtu anayeamini kuna Mungu. Watu wanaogopa kufa na kwenda motoni hao nimewaona, tena wengi sana. Mtu yeyote asilaumiwe kwa kifo changu. Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimwua mdogo wangu ingawa sikumgusa. (Kezilahabi, 1974, uk.195).

Kazimoto anamweleza mke wake kuwa sababu ya kujiua ni kuepuka kuzaa kizazi kibaya. Aidha, alijiona kama mtu aliyepungukiwa na akili. Kujifananisha na mdudu au mnyama ni ishara ya kutojithamini kama binadamu. Sababu ya tatu aliyotoa ni kuwa alikuwa na shauku kuhusu imani ya watu kuhusu Mungu na kwamba kilichowaogofya watu wengi ni kufa na kwenda motoni. Hii ni ishara kuwa alikuwa na mawazo mengi yaliyomsumbua. Mawazo haya yalimfadhaisha Kazimoto. Sababu kuu ya msongo wa mawazo uliomwathiri Kazimoto ilikuwa kwamba alihofu kuwa yeye na mke wake walikuwa wameathiriwa na ugonjwa mbaya usiokuwa na tiba.

Mwandishi anatumia ulemavu wa tabia wa Kazimoto wa kujitoa uhai kwa lengo la kuwazindua wanajamii kuhusu chanzo cha tabia ya kujiua. Kupitia kwa Kazimoto, mwandishi anadhihirisha kuwa watu wanaojiua au kuwa na mawazo ya kujiua wana matatizo ya akili na wanahitaji kusaidiwa ili wasikate tamaa.

Kwa mujibu wa Mbiti (2012) jamii zote za Kiafrika huwa na dhana kuhusu kuwepo kwa Mungu kama kiumbe mwenye uwezo na nguvu zaidi ya viumbe wote. Mtazamo wa Waafrika kuhusu Mungu unajikita katika mazingira ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kitamaduni na kimuktadha. Hata hivyo, kama anavyodai Mbiti, mtazamo huu umeathiriwa na mtagusano wa utamaduni wa Waafrika na mataifa ya nje ya Afrika. Kwa mfano, dhana ya mbinguni na jehanamu inatokana na mafunzo ya dini ya Kikristo na Kiislamu. Kwa kuzingatia msingi huu maudhui ya ukoloni mamboleo yanadhihirika katika wazo la Kazimoto kuhusu adhabu inayowapata wale wanaotenda

dhambi. Kwa mujibu wa mafunzo ya kidini ya Kikristo, wanaotenda mema huenda mbinguni wanapokufa ilhali wanaotenda maovu wanaenda jehanamu. Haya ni kwa mujibu wa Bibilia Takatifu, KJV; (Ufunuo 22:12, Malaki 4:1, Akronia wa pili 28:3 na Muhubiri 37:20).

Kulingana na Saussure (1983), tukio moja au jambo moja linaweza kuashiria maana pana kulingana na muktadha wa matumizi yake. Kwa kuzingatia madai haya ya Saussure inabainika Kezilahabi katika riwaya ya *Kichwamaji* ametumia kifo cha Kazimoto kijazanda ili kuangazia matatizo mengi yanayozikumba nchi nyingi za Kiafrika. Jambo hili linadhihirika katika ripoti ya gazeti iliyoandikwa baada ya kifo cha Kazimoto:

> Siku chache baadaye, gazeti hili lilijaribu kumtazama Kazimoto kama mtu anayeweza kuwakilisha Afrika nzima. Gazeti hili lilinganisha Afrika na nchi zingine za ulimwengu. Liliandika habari hizi chini ya kichwa cha habari kilichosema '*Kutokuwa kwa Afrika katika Ujadiliano wa Kifalsafa.'* Liliendelea kueleza kwamba kujiua si jawabu la matatizo ya maisha. (Kezilahabi, 1974, uk. 196).

Hili ni mojawapo ya magazeti yaliyoripoti kuhusu kifo cha Kazimoto ambapo Kazimoto anachukuliwa kama kiwakilishi cha Afrika nzima. Kichwa cha habari hii, '*Kutokuwa kwa Afrika katika Ujadiliano wa Kifalsafa'* kiinaashiria kutengwa kwa nchi za Kiafrika na mataifa mengine ya ulimwengu katika majadiliano kuhusu masuala mbalimbali ya ulimwengu. Kauli kuwa kujiua si jawabu la matatizo ya maisha inaashiria kuwepo kwa matatizo mengi barani Afrika ambayo yanawafanya Waafrika kujiangamiza. Matatizo haya ni: umaskini, magonjwa, njaa, vita na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi ya kila siku. Katika juhudi za kukabiliana na matatizo haya watu wanapotoka kimaadili kwa kushiriki katika uzinzi, umalaya na ufisadi; mambo ambayo hatimaye yanaweza kusababisha magonjwa yasiyokuwa na tiba kama ugonjwa uliomwathiri mwanawe Kazimoto na kumfanya Kazimoto kuamua kujiua.

Hata hivyo, kama mwandishi anavyosisitiza, mataifa ya Kiafrika yanapaswa kutafuta suluhu ya matatizo yao badala ya kufanya maamuzi ambayo yatazidi kuwakandamiza wananchi wa mataifa haya. Kupitia kwa kisa cha Kazimoto kujitoa uhai mwandishi analenga kuwahamasisha Waafrika kuwa wao wenyewe ndio wanaweza kusuluhisha matatizo yao. Kadhalika, anawaonya dhidi ya mambo yanayorudisha nyuma ufanisi wa mataifa ya Kiafrika kama vile uongozi mbaya, utegemezi wa misaada kutoka kwa mataifa ya nje, vita vya wenyewe kwa wenyewe, ufisadi na ukosefu wa maadili kwa jumla.

Katika sehemu ifuatayo aina ya ulemavu wa tabia inayohusu mahusiano ya ngono itachanganuliwa. Sehemu hii inalenga kuchanganua namna ulemavu wa tabia unaohusiana moja kwa moja na mahusiano ya kingono unavyotumika na waandishi Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe.

### 3.3 Taswira ya Ulemavu wa Tabia Unaohusu Mahusiano ya Kingono

Kwa mujibu wa Bryant (2011), ulemavu wa tabia unaohusu ngono unajikita kwenye tabia zinazokiuka maadili yanayohusiana na kushiriki ngono kinyume na kaida na matarajio ya jamii. Ukiukaji wa kaida hizi unajitokeza kwa namna mbalimbali kama vile: umalaya, ubakaji, kushiriki ngono na watoto wadogo, utalii wa kingono na uhalifu mwingine wowote unaohusiana na ngono.

Kaye (1990) ana maoni kuwa tabia ya kingono inayokiuka kaida za jamii ni dhana pana isiyoweza kuelezeka moja kwa moja. Hata hivyo tabia hii inaashiria kuwa kuna kanuni zinazotambulika na kukubalika miongoni mwa wanajamii kuhusiana na tabia ya kingono. Tabia hizi zinatofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine na kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Hii ni kwa sababu kila jamii ina kaida zake mahsusi ambazo zinaweza kuwa tofauti na za jamii nyingine. Kwa mfano tabia fulani

inaweza kukubalika katika jamii moja na kukashifiwa katika jamii nyingine. Kadhalika, wataalamu na watafiti kutoka nyanja mbalimbali kama vile sheria, tiba, saikolojia, soshiolojia na elimu ya jinai huwa na mitazamo tofauti kuhusu suala la ulemavu wa tabia unaohusisha ngono. Hata hivyo, kuna tabia zinazohusu mahusiano ya ngono ambazo hutambulika na wanajamii wengi kote duniani kama zisizofaa. Tabia hizi ni kama vile ubakaji, umalaya, kutokuwa mwaminifu katika ndoa au katika uhusiano wa kimapenzi na kushiriki ngono na wanyama. Hata hivyo, mwelekeo wa jamii binafsi kuhusu ulemavu unaohusu ngono unategemea mila na desturi za jamii husika.

Mbiti (1969) anasema kwamba katika jamii za Kiafrika, ngono hutekeleza jukumu la kidini na kijamii. Kidini, ngono huchukuliwa kama njia ya kuunganisha wanandoa na kwa hivyo ni kitendo kitakatifu kinachokamilisha uhusiano wa ndoa. Kijamii, ngono ina nafasi muhimu sana katika ndoa kwa kuwa watu hushiriki ngono ili kujistarehesha na kupata vizazi vitakavyoendeleza jamii. Mbiti anaendelea kusema kuwa kutokana na umuhimu huu wa ngono, suala la ngono katika utamaduni wa Kiafrika huchukuliwa kuwa la heshima na takatifu kwa kuwa kitendo hiki huendeleza kizazi katika jamii. Kwa hivyo, ukiukaji wa kaida zinazohusiana na ngono huchukuliwa kwa uzito sana. Ulemavu wa tabia unaohusu ngono ni wa aina mbalimbali. Mbiti (1969) anatambua mifano ya ulemavu unaohusu mahusiano ya ngono kama ubakaji, kushiriki ngono baina ya maharimu, uzinifu, ushoga na kushiriki ngono na wanyama. Kutokana na utukufu unaoambatanishwa na ngono, Waafrika husisitiza kuwa kanuni na miiko inayohusiana na ngono inahitaji kuzingatiwa. Wanajamii wanaokiuka kanuni hizi wanakabiliwa na adhabu kali. Kimsingi, suala la ngono linajikita kwenye mtazamo wa kidini kwa kuwa ukiukaji wa sheria zinazotawala mahusiano ya ngono husambaratisha uhusiano mzuri miongoni mwa wanajamii.

Katika sehemu hii suala la ulemavu wa tabia wa ngono limeshughulikiwa kwa kuzingatia misingi ya jamii ya Kiafrika kwa kuwa riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi zimejikita katika mazingira ya Afrika. Katika riwaya hizi matumizi ya ngono kama mtindo wa kuwasilisha jumbe tofauti yatashughulikiwa. Tabia zinazokiuka matarajio ya wanajamii katika muktadha wa jamii zinazorejelewa kwenye riwaya husika ndizo zitakazozingatiwa. Kutokubalika kwa tabia hizi kunajitokeza kulingana na mwelekeo wa jamii kuhusiana nazo.

Taswira ya ulemavu wa tabia inayohusu ngono inajitokeza kupitia kwa wahusika mbalimbali katika riwaya teule. Wahusika hawa wanashiriki mapenzi kiholela na kuonekana kutojali. Tabia zao zinaashiria uozo uliokithiri katika jamii na athari zake. Tabia ya kutoaminiana katika ndoa, uzinzi, ukahaba na ubakaji ni baadhi ya mambo yanayojitokeza katika riwaya teule yanayoashiria ulemavu wa tabia. Tabia hizi ndizo zitakazoshughulikiwa katika sehemu hii.

### 3.3.1 Ulemavu wa Tabia ya Uzinifu na Matumizi yake Kimtindo

Katika sehemu hii, ulemavu wa tabia ya uzinifu na umalaya imeshughulikiwa kwa kuzingatia namna ulemavu huu ulivyotumika kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi**.** Kulingana na Clinard (1968), uzinzi na umalaya ni ulemavu wa tabia kwa sababu wanaoshiriki katika tabia hizi hukiuka matarajio na kaida za jamii.

Zare (2011) anaeleza uzinifu  kama kitendo cha kuvunja uaminifu katika uhusiano wa kingono katika muktadha ambapo kuna makubaliano ya kuweka uaminifu kati ya wanandoa au watu walio katika uhusiano wa kimapenzi. Brand na wengine (2007) wanakubaliana na Zare kwa kuwa wanadai kwamba uzinifu ni aina yoyote ya tabia ambapo mtu hujihusisha kimapenzi na mtu mwingine wakati ambapo ana uhusiano

wa kimapenzi na mwingine. Miljalkovic (2005) anadai kuwa ukahaba ni aina ya kitega uchumi hasa katika nchi zilizoendelea kiuchumi katika kipindi cha karne ya ishirini. Davies (1937), anaeleza kuwa ukahaba umejikita katika misingi ya kiuchumi ambapo kahaba hutarajia kupata hela na mteja wake kupata starehe. Kadhalika, Davies anasisitiza kuwa kuna uhusiano kati ya umalaya na hali ya akili ya mtu na kwamba umalaya ni suala linalopaswa kuzingatiwa kwa misingi ya tiba kwa kuwa wanaoshiriki tabia hii huwa na uraibu kiasi kwamba wanashindwa kuiacha. Madai ya Davies yanadhihirika kupitia kwa mhusika Tegemea katika riwaya ya *Kichwamaji* ambaye licha ya kutoka mjini na kwenda bara kwa lengo la kuacha umalaya anashindwa kuiacha tabia hii. Mwandishi anasema:

> Kweli chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba. Tegemea alikuwa bado Tegemea. (Kezilahabi, 1974, uk. 73).

Mwandishi anatumia maelezo haya kuashiria kuwa licha ya azma ya Tegemea ya kuiacha tabia ya ukahaba, hakuweza. Alikuwa ameizoea sana kule mjini na hivyo basi akawa ameathirika kiasi kwamba alishindwa kuiacha. Methali *chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba* imetumika na mwandishi kueleza tabia ya Tegemea. Methali hii ina maana kuwa chombo kilichotumiwa kupikia samaki huendelea kunuka samaki tu. Aidha, mtu aliyewahi kuwa na kitu fulani hakosi japo chembe cha kile alichokuwa nacho. Methali hii inaweza kutumiwa kwa maana ya kinyume kumweleza mtu mwenye sifa mbaya; kuwa huenda akawa na udhaifu fulani, hata baada ya kubadilika. Mwandishi anatumia methali hii kuashiria kuwa kama ambavyo chombo kilichotumiwa kupika samaki hakiachi kuwa na harufu ya samaki, mazoea ya mtu huwa vigumu kubadilika na hivyo basi ulemavu wa tabia wa Tegemea haukuisha licha ya kuhamia Ukerewe.

Katika kusisitiza ukahaba kama ulemavu wa tabia, Clinard (1968) anasema kuwa makahaba huwa na tabia zao za kipekee zinazotawaliwa na usiri na kutengwa. Anaendelea kusema kuwa makahaba huwa na mila na kaida ambazo zinakinzana na zile za jamii pana. Kezilahabi ametumia ulemavu wa tabia ya ukahaba wa Tegemea kuwasilisha ujumbe kuwa jamii inapaswa kuelewa kuwa walioathirika na tabia hii huhitaji usaidizi kwa kuwa sio kupenda kwao kuishi maisha ya ukahaba wanayoishi. Kama anavyoeleza Thomas (1990), wanawake hujiingiza katika ukahaba kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuvunjika kwa ndoa, kifo cha wazazi, kutelekezwa na wazazi na matatizo ya akili. Prakash (2013) anakubaliana na maoni ya Thomas anaposema kuwa umaskini na kuvunjika kwa ndoa kunaweza kuwa chanzo cha ukahaba. Aidha, anasema kuwa kisaikolojia mwanamke anaweza kushindwa kumnyenyekea mwanamume mmoja katika uhusiano wa ndoa na kuamua kushiriki ngono na wanaume wengi ili kudhihirisha kuwa ana uhuru. Hali hii inajitokeza katika maelezo ya mwandishi kuhusu Tegemea:

> Tegemea alipokuwa pwani alipata wazo kuwa aliweza kuwachezea mabwana wawili au watatu kama watoto wadogo. Kweli, Tegemea alikumbuka kwamba siku moja, bwana mmoja alilia machozi chini ya miguu yake. Alikumbuka jinsi alivyowafanya mabwana wapishane, mmoja anatoka mwingine anaingia, mmoja anapewa saa za usiku mwingine saa za mchana. (Kezilahabi, 1974, uk. 136).

Maelezo haya yanatoa taswira kuhusu maisha ya Tegemea kwamba hakuridhishwa kimapenzi na mwanamume mmoja na ilimbidi awapangie wanaume kadhaa ratiba ya kwenda kwake nyumbani.

Kwa mujibu wa Rossler na wengine (2010), kuna visa vingi sana vya ulemavu wa akili miongoni mwa wanawake wanaojihusisha na ukahaba. Wanaendelea kusema kuwa mara nyingi jamii huzingatia maslahi yao kiafya na namna ambavyo wanaweza kujizuia ili wasiambukizwe magonjwa ya zinaa bila kuzingatia athari za kazi hii

kwenye afya yao ya akili. Katika uchunguzi Rossler na wenzake walichunguza hali ya afya ya akili ya wanawake wanaofanya kazi ya ukahaba. Katika uchunguzi huu, ilibainika kuwa baadhi ya wanawake hawa hufanya kazi hii kama njia ya kuinua kiwango cha kujiamini kwao na kuwafanya wajitawale. Wengine wanajiingiza katika kazi hii ili wajisikie kwamba wana nguvu na mamlaka.

Kwa kuzingatia madai ya Thomas (1990), Prakash (2013) na Rossler na wengine (2010), inaelekea kuwa Kezilahabi, kupitia kwa mhusika Tegemea anawasilisha ujumbe kwamba makahaba hawapaswi kutengwa au kushutumiwa ila jamii inapaswa kutafuta kiini cha waathiriwa kujiingiza katika tabia hii. Inaelekea kuwa mbali na kuwa na ulemavu wa tabia wanaweza kuwa wameathiriwa na matatizo ya akili yanayohitaji usaidizi wa tiba.

Uzinifu unadhihirika kupitia kwa wahusika mbalimbali. Kazimoto ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Kichwamaji* anashiriki ngono kiholela na wasichana ambao anakutana nao kwa mara ya kwanza. Kwa mfano, anashiriki kitendo cha ngono na Vumilia shambani la mihogo licha ya kuwa Vumilia alikuwa anajiandaa kuolewa na Manase. Kadhalika, Kazimoto aliendeleza uhusiano wake na Pili licha ya kwamba alikuwa tayari amemchumbia Sabina. Kulingana na Zare (2011), mitazamo kuhusu uzinifu hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine; kutoka muktadha mmoja hadi mwingine na uhusiano uliopo kati ya watu wawili. Hata hivyo, kama anavyoendelea kusema Zare, katika tamaduni nyingi kuna kaida zinazomfunga mtu kuhusu mahusiano ya kingono kwa kuwa wanajamii wanahitajika kuwa waaminifu kwa wapenzi wao. Kwa hivyo, tabia ya Kazimoto na ya Vumilia kushiriki ngono huku wakiwa wamechumbiwa inadhihirisha ukiukaji wa kaida na matarajio ya jamii. Kwa mujibu wa Drigotas na wengine (1999), ulemavu wa akili unaweza kuwa chanzo cha tabia ya uzinzi kwa kuwa mtu anayejiingiza katika tabia hii huwa na wazo kuwa

haridhishwi kingono na yule ambaye ni mpenzi wake halali na ndiyo maana anakosa uaminifu wa kimapenzi.

Madai ya Drigotas na wengine yanadhihirika kupitia mhusika Tumaini katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Tumaini alishiriki ngono na wasichana wengi pale kijijini kwao. Alimdanganya kila msichana kuwa hakuwa na uhusiano na mwingine. Kwa mfano, alimpachika mimba Leonila kisha akavunja uhusiano naye na kumuoa msichana mwingine. Aidha, aliendeleza mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* Vera (Mama Resi) anajitokeza kama mhusika mwingine mwenye ulemavu wa tabia. Vera alimhadaa mumewe Dennis, kuwa alikuwa anatarajia kupata mtoto wake huku akijua kuwa alikuwa amepachikwa mimba na mwanamume mwingine. Lengo la Vera lilikuwa ni kumshurutisha Dennis amuoe. Hata baada ya kuolewa aliendelea kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Vera alishiriki mapenzi na John wakati mumewe alipokuwa safarini. Uhusiano huu ulikuja kujulikana na mumewe na hatimaye kusababisha ndoa yao kusambaratika.

Mwandishi anatumia ulemavu wa tabia wa uzinifu kama mtindo wa kuashiria kuwa uzinzi ni tabia ambayo inajikita katika masuala mbalimbali yanayofungamana na mtu binafsi na jamii kwa jumla. Kama anavyodai Zare (2011), kuna sababu nyingi zinazomfanya mtu kuwa na tabia ya uzinzi. Anasema kuwa uzinzi unaweza kusababishwa na kiwango cha elimu, unafsi, mtindo wa maisha, uchumi, ukosefu wa ajira, mkinzano wa tamaduni, mielekeo na kaida za jamii, muktadha na hali ya akili. Exner (1977) anasema kuwa kuna wanawake wanaojiingiza kwenye tabia ya uzinzi na usherati kwa lengo la kutaka kujitambua kiuana. Anaendelea kusema kuwa wengine wanasukumwa kwenye kazi hii kutokana na kutengwa na kubaguliwa na jamii kama wanawake. Wanapokuwa katika biashara hii wanahisi kuwa wanapendwa na kuthaminiwa na wale wateja wao. Aidha, wanahisi kuwa wana mamlaka juu ya miili

yao. Kupitia kwa wahusika walioathiriwa na ukahaba na uzinifu; Kezilahabi anatathmini mazingira ya kijamii na kiuchumi yanayosababisha ulemavu huu. Kwa mfano, inabainika kuwa Tegemea, Kazija, Jeni na Bi Sururu ni baadhi ya wahusika waliojiingiza katika tabia ya ukahaba ili kuweza kukimu mahitaji yao. Tegemea anabadilisha wanaume anavyotaka bila kujali kuwa jamii itamhukumu. Mama Resi alijiingiza katika uzinzi kutokana na tamaa ya mali na kutaka utambuzi miongoni mwa wanajamii. Haya yanadhihirika katika barua aliyomwandikia Dennis baada ya kutalikiwa. Alisema:

> *Bwana Dennis*
>
> *Mwaka mmoja umepita bila kukuandikia barua. Bila shaka unafikiri kwamba niko shamba nachimbua udongo; au labda unafikiri ninaishi ndani ya mapipa-bado ulikuwa na mawazo hayo, basi umedanganyika. Mimi sasa nimekwishaolewa na nimeolewa na mtu mkubwa. Ninakuomba sasa usiwe unatajataja jina langu mbele ya watu. Heshima niliyonayo sasa, ni kubwa. Uhusiano uliokuwapo zamani kati yako na mimi utatia kutu maisha yetu ya sasa na mume wangu. Vipi maisha? Je umekwisha-maliza kulilipia gari lako? Sisi tunayo mawili. Kila mtu lake, na hatuna madeni. Nitakuambia siri moja. Je bado unafikiri Restituta ni mtoto wako?*
>
> *Ni mimi*
>
> *Bibi Kimaloa*
>
> (Kezilahabi, 1975, uk. 123).

Katika barua hii unafiki wa Vera unajitokeza. Vera anamfanyia stihizai Dennis kwa kumjulisha kuwa maisha yake hayakusambaratika hata baada ya Dennis kumtaliki ila aliolewa na mtu mwenye mali zaidi na mwenye cheo kikubwa zaidi kuliko Dennis. Kama anavyosema Vera, kuolewa na mtu mwenye sifa hizi zilimfanya kuwa na heshima kubwa. Matumizi ya kejeli na balagha, yanadhamiria kumdhalilisha Dennis. Maneno ya Vera pia yanadhihirisha unafiki aliokuwa nao kwa kumdanganya Dennis kuwa ndiye alikuwa baba mzazi wa Resituta, binti yake. Kupitia kwa barua ya Vera

na ujumbe uliowasilishwa kwayo, mwandishi analenga kuwasilisha maudhui kuhusu uzinifu katika ndoa na kiini cha tabia hii.

Kwa mujibu wa Allen na wengine (2008), tabia ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa inatokana na ulemavu wa akili, kutokuwa na uwezo wa kukuza mahusiano na watu wengine, kutoridhika na mpenzi mmoja, ukosefu wa mawasiliano kati ya wanandoa na kuzorota kwa uhusiano kati ya wanandoa. Uhusiano kati ya Vera na Dennis unaonekana kuzorota kadri siku zilivyokuwa zinapita. Aidha, inabainika kuwa Vera hakuwa anaridhishwa na mapenzi kutoka kwa mumewe kwa kuwa alikuwa anamkaribisha mwanamume mwingine pale nyumbani bila kujali. Kwa hivyo inaelekea kuwa Vera alikuwa na tatizo la akili, hangeweza kudumisha uhusiano wa kingono na mwanamume mmoja. Inabainika kuwa Kezilahabi anaangazia kuhusu umuhimu wa wanajamii kuzingatia chanzo cha tabia ya uzinzi badala ya kuwakashifu na kuwahukumu watu wenye tabia hii. Hii ni kwa sababu watu hawa wana ugonjwa wa akili na wanahitaji usaidizi mahsusi ili waweze kuachana na tabia hii.

Ubakaji ni ulemavu mwingine wa tabia unaohusiana na ngono. Katika sehemu ifuatayo ulemavu huu utashughulikiwa kama mtindo wa mwandishi wa kuwasilisha maudhui.

### 3.3.2 Ulemavu wa Tabia ya Ubakaji na Matumizi yake Kimtindo

Kwa mujibu wa Kilpatrick (1992), tabia ya ubakaji ni tukio linaloshuhudiwa katika tamaduni nyingi kote duniani. Kilpatrick anasema kuwa kubaka ni kufanya ngono na mtu kwa nguvu bila hiari yake au kufanya ngono na mtu kwa lazima na kwa kutumia vitisho. Aidha, ubakaji unahusisha kufanya ngono na mtu asiye na uwezo wa kuhiari kwa mfano; mtoto, mzee, mlevi au mtu mwenye akili punguani. Ubakaji unadhihirisha dhuluma na unyanyasaji katika jamii. Mbakaji ni mtu mwenye ulemavu

wa tabia kwa kuwa tabia yake inaenda kinyume na utu na matarajio ya jamii kwa mtu mwenye urazini. Kulingana na Kontula na Mannila (2009), kitendo cha ngono miongoni mwa binadamu ni njia ambayo inatumiwa na wanadamu kushuhudia na kuonyesha hisia zao. Kitendo hiki kinahusisha vipengele vya kisoshiolojia, kihisia, kiakili na kibayolojia. Kaida na sheria zinazotawala uhusiano wa kingono hutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, katika tamaduni nyingi ni hatia kwa mtu kumlazimisha mwingine kushiriki kitendo hiki bila hiari yake (ubakaji). Lang (1999) amefafanua kuhusu mtazamo wa Bibilia kuhusu tendo la ngono. Anaeleza kuwa kwa mujibu wa Bibilia Takatifu, KJV; (1 Wakorintho:6-18), uhusiano wa ngono sio suala la kimwili pekee ila ni suala la kiroho na takatifu. Kwa mujibu wa Biblia, hakuna dhambi inayoathiri mwili kama uzinifu kwa kuwa ni dhambi dhidi ya mwili wa mtu binafsi. Aidha, Lang anasema kuwa kwa mujibu wa kitabu cha Waebrania (13:4), Bibilia inatoa onyo dhidi ya wale wanaoshiriki katika uzinzi na wale wasio waaminifu katika ndoa; kwamba Mungu atawahukumu. Ubakaji katika jamii nyingi huchukuliwa kuwa ni dhuluma dhidi ya mtu na ni tabia inayopaswa kukashifiwa. Katika Korani Takatifu uzinzi umekashifiwa pia. Kama anavyoeleza Ghafoor (2014), katika dini ya Kiislamu, uhusiano wa ngono unakubalika katika muktadha wa ndoa pekee. Kadhalika, ukahaba na ubakaji ni tabia zisizokubalika katika dini ya Kiislamu na huchukuliwa kuwa dhambi kubwa (Korani 17:32). Mtazamo wa dini za Kikristo na Kiislamu unaafikiana na mtazamo wa jamii nyingi kote ulimwenguni kuhusu swala la ngono. Inabainika kuwa katika jamii nyingi kuna sheria zilizowekwa kuhusiana na uhusiano wa ngono. Sheria hizi zinakataza uhusiano wa ngono kati ya mtu mzima na mtoto ambaye hawezi kujiamulia mambo, kushiriki ngono hadharani na ukahaba. Kwa hivyo, mtu anayekiuka sheria hizi

anaonekana kuwa na upungufu kimaadili. Aidha, mtu anayefanya mambo yanayomletea aibu huashiria upungufu wa akili.

McKibbin na wengine (2008), wana maoni kuwa wanaume wamekuza mbinu za kisaikolojia zinazowasukuma kushiriki katika kitendo cha ubakaji katika miktadha mahsusi. Kwa hivyo, tabia ya ubakaji ni ulemavu wa akili kwa kuwa mtu anayetekeleza kitendo hiki hajali matokeo ya kitendo chake na jinsi kitakavyomwathiri yule anayebakwa.

Katika maeneo mengi kote ulimwenguni kuna ripoti nyingi katika vyombo vya habari kuhusu visa vya ubakaji. Ripoti hizi zinadhihirisha kuwa visa vya ubakaji vinaongezeka kila siku. Baloyi (2010) anadai kuwa kulingana na ripoti zinazotolewa katika vyombo vya habari, visa vya ubakaji na dhuluma dhidi ya wanawake hujitokeza kila siku. Kwa hivyo, hili ni suala linalostahili kuzingatiwa kwa makini zaidi. Katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi, kama ilivyo katika jamii ya sasa, inabainika kuwa kuna visa vya ubakaji. Waandishi hawa wanatumia taswira ya ulemavu huu wa tabia kama mtindo wa kuashiria namna jamii ilivyooza kimaadili. Aidha, tabia ya ubakaji inabainisha nafasi ya mwanamke katika jamii ambapo mwanamke anasawiriwa kama kiumbe anayedhalilishwa, kudhulumiwa na kuonekana kama kifaa cha starehe. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (2017), mitazamo ya jamii kuhusu jinsia inaweza kuathiri tabia inayohusu uhusiano wa ngono. Shirika hili linadai kuwa asilimia kubwa ya visa vya ubakaji hutokea katika maeneo ambako inaaminika kuwa wanaume wana haki ya kushiriki ngono kuliko wanawake na kuwa wanawake hawana uwezo wa kuwakataza kushiriki nao kitendo hiki. Kwa kuzingatia maoni haya inaelekea kuwa wanaume wanawabaka wanawake kwa kuwa wanawadunisha na kuwadharau, jambo ambalo limejikita katika jamii zenye mtazamo unaomtukuza mwanamume na kumdharau mwanamke.

Katika riwaya ya *Kichwamaji,* Rukia anabakwa na Manase na kupachikwa mimba. Kupitia kwa barua, Rukia anamweleza kaka yake, Kazimoto tukio la kubakwa kwake. Manase anapoulizwa kuhusu jambo hili anasema hakuwajibika ila aliwaandikia wazazi wa Rukia barua ifuatayo:

> Ninawaarifuni kwamba kwa sababu fulani kubwa siwezi kumuoa Rukia. Nimekwisha pata mchumba mwingine, na mzuri kuliko Rukia. Kama nia yenu ni kutaka nioe, semeni tu, nami nitawaambia mahali anapoishi ili muanze kazi ya kuposa. Lakini Rukia siwezi. (Kezilahabi, 1974, uk. 26).

Barua hii ilikuwa jibu la Manase kwa familia ya Rukia alipotakiwa awajibike na kumuoa Rukia ambaye alikuwa na ujauzito. Kwa mujibu wa Stromwall na wengine (2012), katika jamii nyingi kulikuwa na sheria zilizowekwa kuhusu hatua zinazofaa kuchukuliwa ikiwa mwanamke atapata mimba baada ya kubakwa. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kiafrika mbakaji alilazimishwa kumuoa msichana aliyepata mimba na iwapo angekubali, basi aliweza kuepukana na adhabu nyingine yoyote. Hatua hii ilichukuliwa kama njia mwafaka ya kusuluhisha tatizo hilo na kudumisha uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii. Hata hivyo, sheria za kisasa zinasisitiza kuwa hatua mahsusi zinapaswa kuchukuliwa ili kumwadhibu yeyote anayepatikana na hatia ya ubakaji.

Madai ya McKibbin na wengine kwamba mbakaji hajali athari za kitendo chake yanajitokeza kupitia kwa maneno ya Manase. Manase anaonyesha hisia za kutojali. Anaifanyia stihizai familia ya Rukia kwa kusisitiza kuwa amempata msichana mwingine wa kuoa. Kumlinganisha Rukia na msichana huyo na kudai kuwa ni mzuri kuliko Rukia ni ishara ya dharau.

Kwa mujibu wa Polashek na wengine (1997), kuna ushahidi wa kutosha kuashiria kuwa wabakaji huwa na mawazo hasi kuhusu wanawake. Mawazo haya huwashawishi na kuwafanya kuwabaka wanawake kama njia ya kutilia nguvu

mtazamo wa wabakaji. Kwa kuzingatia mawazo ya Polashek inaelekea kuwa mwandishi ametumia ulemavu wa tabia wa Manase kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe kuwa tabia hii inaweza kusababishwa na mwelekeo hasi wa wanaume kuhusu wanawake kwamba ni wanyonge na dhaifu. Hali hii inajitokeza pia katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mhusika Tumaini alimbaka Leonila, akampachika mimba na kisha kumkana. Aidha, baada ya kumkana Leonila alihama kule kijijini na kumuoa Anastasia bila kujali hatima yake Leonila.

Kutokana na yaliyowapata Rukia na Leonila mwandishi anawasilisha maudhui kuhusu kudhulumiwa kimapenzi kwa wanawake. Wanaume wanaotekeleza kitendo cha ubakaji katika riwaya husika hawachukuliwi hatua yoyote licha ya kuwa wanajulikana. Badala yake wasichana wanaodhulumiwa wanalaumiwa na wanajamii. Inadhihirika kwamba suala la ubakaji linahusu mamlaka na nguvu katika mfumo wa ubabedume ambapo mwanamke ndiye anayelaumiwa hata wakati amedhulumiwa. Kadhalika, kupitia ulemavu wa tabia wa ubakaji nafasi ya mwanamke katika jamii inajitokeza ambapo wanaume wanasawiriwa kama viumbe wanaowachukulia wanawake kama vifaa vya starehe.

Katika riwaya ya *Kichwamaji* mhusika Kalia anajitokeza kama mwenye ulemavu wa tabia kwa kuwa ni mbakaji. Kalia alikuwa ndugu yake Kazimoto. Kijana huyu alikuwa mbakaji aliyekuwa akihangaisha kijiji kizima. Msimulizi anachora taswira ya ulemavu wa tabia wa Kalia anapoeleza:

> Ajabu nyingi duniani. Wakati sisi tukiendesha mapenzi, kitu fulani cha ajabu kilikuwa kikitendeka kijijini. Nunda mla watu alikuwa amezuka. Kila mtu alikuwa akijiuliza jinsi ya kumkomesha nunda huyu. Mwanzoni huyu nunda alikuwa mtu ambaye alikuwa hajulikani. Alikuwa mtu ambaye aliingilia nyumba za watu usiku, hasa zile nyumba ambamo walikuwa wakilala wanawake watupu. Huyu nunda aliwaingilia usiku, kisu mkononi, na

> kuwashurutisha wamtimizie haja yake bila kupiga kelele. Hata wazee walipitiwa. (Kezilahabi, 1974, uk. 110).

Kulingana na maelezo haya ya msimulizi, jambo lililokuwa likiendelea kijijini lilikuwa ni la kustaajabisha. Kule kijijini mtu asiyejulikana alikuwa akivamia nyumba za watu na kuwabaka wanawake. Msimulizi anasema kuwa hata wazee walikuwa wanabakwa kusisitiza kuwa aliyeshiriki kitendo hiki hakujali umri wa waathiriwa wake. Anamrejelea mbakaji huyu kama nunda ambaye hakuwa anatambulika. Hatimaye ilikuja kubainika kuwa Kalia, ndugu yake Kazimoto ndiye aliyekuwa akitekeleza kitendo hiki. Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne ya 21, nunda ni paka aliyetoroka nyumbani na kwenda kuishi porini; ni paka shume, gwagu au duzi. Aidha, ni mtu aliyetutumka mwili mzima akawa kama jitu. Sifa za mnyama huyu zinadhihirisha kuwa ni mnyama hatari anayewadhuru watu. Kalia anawavamia watu usiku na kuwabaka, Tabia ya Kalia ya kuwashambulia watu usiku inaoana na ya mnyama huyu kwa kuwa inamtenga na jamii. Jamii inamsaka mbakaji huyu kama ambavyo wanaweza kumsaka mnyama hatari anayetishia maisha yao. Mwandishi anamwita '*mla watu'* kuashiria unyama na ukatili wa kitendo chake. Tabia yake inasababisha kufukuzwa kwake mle kijijini na hatimaye kuuawa.

Kwa mujibu wa Mahamuth na wengine (1993), malezi ya awali ya mtoto na tajiriba yake yanaweza kumfanya mtu kujihusisha na tabia ya ubakaji. Malezi ya mtoto yanaweza kumfanya mtu kupata upungufu wa kisaikolojia au wa akili na kuathiri tabia yake kwa njia itakayomfanya ajiingize katika tabia ya kuwadhulumu watu kingono. Aidha, malezi mabaya yanaweza kumfanya mtu kutoweza kushiriki katika uhusiano wa kimapenzi wa kudumu. Jambo hili wakati mwingine linamfanya mtu kuridhisha hamu yake ya mapenzi kwa njia zisizo halali. Kwa kuzingatia madai haya ya Mahamuth na wengine, inadhihirika kuwa Kalia alijiingiza katika tabia ya ubakaji

kutokana na tabia ya ndugu yake mkubwa, Kazimoto, ambaye alikuwa ana tabia ya uzinzi. Kazimoto, licha ya kuwa ndugu yake mkubwa, alikuwa kama mlezi wake Kalia kwa kuwa walikuwa na uhusiano wa karibu na walifanya mambo pamoja. Kwa hivyo tabia zake Kazimoto ilimwathiri sana Kalia maishani mwake. Kazimoto anakiri kuwa alisababisha kifo cha Kalia kwa kutomwelekeza kwa njia ifaayo kama ndugu yake mkubwa. Anasema:

> Mimi, kabla ya kufa, ninaungama mbele ya ulimwengu kwamba nilimuua mdogo wangu ingawa sikumgusa. (Kezilahabi, 1974, uk. 195).

Kazimoto alisema maneno haya katika ujumbe aliouacha kabla ya kujiua. Anajilaumu kwa kutomwelekeza kimaadili ndugu yake Kalia. Kalia aliadhibiwa na wanajamii kwa kuuawa kutokana na tabia yake ya ubakaji.

Mwandishi anatumia ulemavu wa tabia wa Kalia kuwasilisha ujumbe kuwa tabia ya ubakaji ni tatizo la kisaikolojia na linastahili kutafutiwa tiba kwa misingi ya kijamii kwa kuwa linahusiana na malezi, mazingira na tajriba ya mwathiriwa. Kumuua Kalia bila kujaribu kutafuta kiini cha ulemavu wake wa tabia kunaashiria kuwa jamii haikujaribu kutafuta tiba ya kudumu ya uraibu wa Kalia wa ubakaji ila waliona kifo chake kuwa suluhu ya kudumu.

Kutokana na ulemavu wa tabia ya ubakaji mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa tabia hii inaashiria tatizo la kimalezi na la kimtazamo miongoni mwa jamii. Aidha, inadhihirika kwamba ulemavu huu unatokana na sababu mahsusi na hivyo basi katika kutafuta suluhisho la kudumu jamii inahitaji kuchunguza kiini cha tabia hii.

### 3.4 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kubainisha namna ambavyo ulemavu wa tabia ulivyotumika kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Taswira za ulemavu wa tabia zimedhihirika kwa jinsi tatu: ulemavu wa

tabia ya mtu kujidhuru, ulemavu wa tabia unaowaathiri wanajamii kwa jumla na ulemavu wa tabia ya mahusiano ya ngono. Ulemavu wa tabia ambao umechunguzwa katika sura hii ni unywaji pombe kupindukia, matumizi ya mihadarati, kujiua, ubakaji, uzinifu, umalaya na kutoaminiana katika ndoa.

Kupitia taswira hizi waandishi wamefanikiwa katika kuwasilisha maudhui mbalimbali katika kazi zao. Maudhui kuhusu chanzo na athari za tabia hizi yameshughulikiwa kwa pamoja. Aidha, maudhui ya dhuluma, utamaushi, maisha ya ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, umaskini na malezi yamedhihirika kutokana na matumizi ya taswira za ulemavu wa tabia kama mtindo. Katika sura hii imebainika kuwa ulemavu wa tabia ni suala ambalo linastahili kuzingatiwa kwa upevu zaidi kwa kuwa ulemavu huu unatokana na masuala mahsusi yanayoiathiri jamii kwa jumla. Hivyo basi watu walioathiriwa hawapaswi kulaumiwa bali jamii inapaswa kuelewa chanzo cha tabia hii ili iweze kuwasaidia waathiriwa. Katika sura inayofuata, taswira za ulemavu wa viungo na matumizi yake kama mtindo wa kuwasilisha maudhui zitashughulikiwa.

# SURA YA NNE

# TASWIRA YA ULEMAVU WA VIUNGO KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura iliyopita matumizi ya taswira za ulemavu wa tabia kama mtindo wa kuwasilisha maudhui yalishughulikiwa. Sura hii imeshughulikia taswira za ulemavu wa viungo kama inavyojitokeza katika riwaya zinazochunguzwa kwa lengo la kubainisha namna ambavyo taswira hizi zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Sura hii imezingatia wahusika ambao wanadhihirisha ulemavu wa viungo kama data na namna ambavyo wahusika hawa wametumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui mbalimbali.

Kulingana na takwimu za Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (2011), idadi ya watu wenye ulemavu wa viungo kote duniani imefikia bilioni moja. Katika Bara la Afrika, inakisiwa kuwa asilimia kumi ya Waafrika wana ulemavu wa viungo. Ripoti ya shirika hili inabaini kuwa ulemavu wa viungo husababishwa na uzee, magonjwa, ajali za barabarani, vita na majanga yanayopatikana katika maeneo mbalimbali kote ulimwenguni.

## 4.1 Dhana ya Ulemavu wa Viungo

Llewellyn na Hogan (2000) wanaeleza kuwa dhana ya ulemavu wa viungo inaweza kufasiriwa kwa kuzingatia mitazamo miwili; mtazamo wa tiba na mtazamo wa kijamii. Mtazamo wa tiba unautambua ulemavu kama tatizo la mtu binafsi ambapo mtu mwenye ulemavu wa macho, masikio, miguu, mdomo na kadhalika huashiriwa kuwa mmiliki wa ulemavu huo kama mtu binafsi. Wanaotetea mtazamo huu wanadai kuwa matatizo ya watu wenye ulemavu wa viungo yanatokana na ulemavu wao.

Mtazamo tiba ndio unaotambulika na Shirika la Afya Ulimwenguni. Kwa mujibu wa Oliver (1990), mtazamo wa jamii kuhusu dhana ya ulemavu wa viungo uliasisiwa na watu walioathirika na ulemavu wa viungo. Mtazamo huu ulitokana na mwelekeo hasi wa jamii kuhusu watu wenye ulemavu wa viungo uliowafanya watu hawa kuhisi kuwa wanatengwa na kudhulumiwa.

Kwa mujibu wa Mac-Donald na Buterre (2010), ni vigumu kufasiri dhana ya ulemavu wa viungo kwa kuwa ufasiri wa dhana hii hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine na kutoka jamii moja hadi nyingine. Hata hivyo, katika sura hii ulemavu wa viungo umechukuliwa kuwa na maana ya kulemaa kimaumbile ambapo athari za kulemaa zinadhihirika kupitia ukosefu wa uwezo wa mtu wa kuona, kusikia, kuongea, kuzaa au kutembea. Kadhalika, taswira ya ulemavu wa viungo imechukuliwa kuwa na maana ya kupungukiwa kwa mtu kimaumbile au kuwa na maumbile yanayotofautiana na ya binadamu wengine. Lutz na Bowers (2003), wana maoni kuwa ili kuelewa namna ya kufafanua ulemavu wa viungo na masuala yanayohusiana nao katika fasihi kuna haja ya kuelewa namna watu wenye ulemavu huu wanavyofasiri athari zake katika maisha yao. Fasiri tofauti za jamii kuhusu ulemavu zinaweza kuibua jumbe mahsusi ambazo hazijitokezi moja kwa moja. Kwa kuzingatia madai haya, inaelekea kuwa ulemavu wa viungo unaweza kutumiwa katika fasihi kwa lengo la kuwasilisha maudhui. Lengo la sura hii ni kubainisha namna ambavyo ulemavu wa viungo umetumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mahsusi kwa kuzingatia ulemavu wa viungo mbalimbali vya mwili na hali mbalimbali zinazotokana na kulemaa kwa viungo hivi.

Kulingana na Sherry (2007), ulemavu mara nyingi hutumika kama jazanda ya matatizo yanayopatikana katika jamii. Hata hivyo jazanda hizi huwa na maana

zinazoelekeza mitazamo, utambulisho na tajiriba za watu wenye ulemavu. Maoni ya Sherry yanaendelezwa na Bogdan na wengine (2012) wanaodai kuwa matumizi ya ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi huathiri maana, mfumo na jinsi kazi husika inavyoeleweka.Wanadai kuwa dhana ya ulemavu inaweza kubeba jumbe mbalimbali kutegemea namna mwandishi anavyoitumia katika kazi yake.

### 4.2 Matumizi ya Ugumba na Utasa kama Mtindo

Ugumba ni hali ya mwanamume au mwanamke kushindwa kutia mimba au kupata mimba ilhali amefikia umri mwafaka au amekomaa kimaumbile kiasi cha kuwa na uwezo wa kutia au kupata mimba. Neno utasa lina maana ya hali ya mwanamke kushindwa kushika mimba. Ulemavu wa kutokuwa na uwezo wa kutia au kupata mimba huathiri wanaume na wanawake. Kwa mujibu wa Nordqvist (2016), katika jamii nyingi ulemavu wa kutokuwa na uwezo wa kuzaa unarejelea ukosefu wa mwanamume au mwanamke kutunga mimba hata baada ya kushiriki ngono bila kinga kwa takriban mwaka mmoja. Kadhalika, utasa hutumiwa kumrejelea mwanamke ambaye hawezi kubeba mimba kwa miezi tisa na kwa hivyo huipoteza mimba kabla ya muda wa mtoto kuzaliwa kufika. Mwanamume ambaye hawezi kushiriki katika kitendo cha ngono ili kumtunga mwanamke mimba pia huchukuliwa kuwa ana ulemavu wa kiungo cha uzazi.

Devlieger (1995), anasema kuwa katika jamii nyingi za Afrika mtu hutambulika kuwa na ulemavu iwapo hana uwezo wa kushiriki katika shughuli ya uzazi, kwa kuwa uzazi ndio unaoendeleza jamii. Kwa mujibu wa Mbiti (1969), kuzaliwa kwa mtoto ni mfumo unaoanza mapema hata kabla ya mtoto kuzaliwa na huendelea hata baada ya mtoto kuzaliwa. Kwa hivyo, kuzaliwa kwa mtoto ni suala linalohusu jamii nzima wakiwemo watu walio hai na wale ambao wamekufa.

Tabong na Adongo (2013) walifanya utafiti kuhusu maana ya kijamii kuhusu ulemavu wa uzazi. Katika utafiti wao walitambua kwamba ugumba na utasa hutokana na sababu za kijamii na za kibayolojia. Tabong na Adongo wanadai kuwa kijamii, ulemavu wa viungo vya uzazi unaweza kusababishwa na ushirikina na ukiukaji wa miiko na kaida za jamii. Kwa kuzingatia misingi ya bayolojia, ulemavu huu unaweza kusababishwa na kuavya mimba, matumizi ya dawa za kupanga uzazi, kujipiga punyeto na usagaji. Kadhalika, Tabong na Adongo walibainisha kuwa wanandoa ambao wanashindwa kupata watoto hutafuta matibabu kutoka kwa mizimu, waganga wa kienyeji na hospitalini. Kwa hivyo, uwezo wa kuzaa ni jambo linalothaminiwa sana na huonekana kama sifa muhimu ya kumtambua mtu kama mwanamke au mwanamume aliye kamilifu. Mwanajamii ambaye anashindwa kupata watoto huchukuliwa na wanajamii kama mtu asiye kamilifu na mwenye upungufu mkubwa.

Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* inabainika kuwa mhusika Kapinga alishindwa kushiriki ngono na mke wake Muyango alipomleta nyumbani baada ya kumuoa. Inadhihirika kuwa Kapinga alipoingia chumbani na mke wake ili kukamilisha ndoa kama ilivyotarajiwa kimila na kidesturi katika jamii husika, alikaa ndani kwa muda wa saa mbili mpaka wazazi wake na vijana waliokuwa wakimsubiri wakaanza kulalamika. Mwandishi anaeleza:

> Watu walianza kujiuliza alikuwa bado akifanya nini. Nje; baba yake alikuwa amekwishaanza kufoka; 'Ng'ombe wangu utawalipa! Utawarudisha ! Sijazaa mtoto kama huyu!' Mama yake alikuwa akilia, 'Mtoto wangu! Ni aibu!' Vijana waliokuwa nje walikuwa sasa wakipiga kelele kwa nguvu. 'Kipofu! Kipofu! Washa taa uone vizuri!' (Kezilahabi, 1975, uk. 10).

Katika maelezo haya, taswira ya hali iliyotawala nje ya chumba alichokuwa Kapinga na mke wake inajitokeza. Wazazi wa Kapinga pamoja na vijana wenzake walionekana kughadhabishwa na Kapinga kwa sababu ya kukaa ndani ya chumba kwa muda mrefu

bila kuwepo kwa dalili yoyote kuwa alikuwa amekamilisha ndoa yake kwa kitendo cha ngono.

Baba yake Kapinga alihofia kuwa kushindwa kwa Kapinga kushiriki ngono na mke wake kungemlazimisha Kapinga kumtaliki mkewe hata ingawa tayari alikuwa amelipa mahari. Jambo hili lingekuwa ni hasara kwa baba yake aliyekuwa amempa ng'ombe wa kulipa mahari na ndiyo maana anamwambia Kapinga kuwa angemlipa ng'ombe wake. Hasira za baba yake zinadhihirika kutokana na namna anavyomkana Kapinga kama mtoto wake. Mama yake Kapinga anakiri kuwa ilikuwa ni aibu kwamba mtoto wake alishindwa kushiriki kitendo cha ngono. Vijana wenzake Kapinga walimdharau na kumfanyia stihizai huku wakimwita kipofu (mtu asiyeona) na kumshauri awashe taa ili aone vizuri.

Kwa mujibu wa Tabong na Adongo (2013) katika jamii za Kiafrika mtoto si wa mtu binafsi bali ni wa jamii nzima. Kwa hivyo, uzazi ni jambo linalothaminiwa sana katika jamii. Watu ambao hawana uwezo wa kupata watoto hudharauliwa na kutengwa na wanajamii wengine. Kauli ya baba yake Kapinga inadhihirisha madai ya Tabong na Adongo kwa kuwa anamkana mtoto wake kwa kushindwa kushiriki ngono na mkewe. Aidha, mama yake anasema kuwa ilikuwa aibu kubwa kwa Kapinga kushindwa kushiriki kitendo cha ngono. Umuhimu wa mwanamume kuwa na uwezo wa kushiriki ngono unajitokeza zaidi kutokana na jinsi Kapinga alivyoathiriwa na kushindwa kutekeleza tendo la ngono na mkewe. Mwandishi anaeleza:

> Mwili wake (Kapinga) ulikufa ganzi kwa hofu. Alianza kutetemeka. Kufuatana na desturi bibi arusi hana ruhusa kumsaidia bwana arusi. Kapinga alikata tamaa. Alitoka nje kwenda kumwambia kaka yake kwamba ameshindwa. "Rudi tena!" Kaka yake alimsukuma ndani ya nyumba kwa ghadhabu. Kapinga alirudi ndani. Alijaribu tena lakini hakuweza. Usiku huo ngoma hazikuchezwa, kwani arusi ilikuwa bado kuthibitishwa kwa kitendo.

> Kesho yake watu walikuwa wakiwazomea wazazi wake. Mama yake nusura ajiue kama asingalishikwa. (Kezilahabi, 1975, uk. 10)

Maelezo ya mwandishi yanathibitisha kuwa Kapinga alishindwa kushiriki kitendo cha ngono na mke wake licha ya kujaribu mara kadhaa. Upungufu huu ulimwathiri sana Kapinga kiasi kwamba alijawa na hofu na kuanza kutetemeka. Inabainika kuwa mwishowe alikata tamaa na kwenda kumwambia kaka yake kuwa alishindwa kutimiza kitendo hicho.

Kushindwa kwa Kapinga kutimiza wajibu wake kama mwanamume kulisambaratisha ndoa yake. Mwandishi anachora taswira hii anaposema kuwa *usiku huo ngoma hazikuchezwa*. Ngoma ni ala ya muziki. Muziki huchezwa kunapokuwa na furaha na sherehe maalum katika jamii. Kauli kuwa *ngoma hazikuchezwa* inaashiria kwamba kulikuwa na huzuni na hakukuwa na jambo la kusherehekea licha ya kuwa Kapinga alikuwa amefunga ndoa. Kwa kawaida arusi inapofanywa wanajamii hufurahia na kusherehekea lakini kushindwa kwa Kapinga kushiriki ngono na mke wake kulitia doa arusi yao na hivyo basi hakukuwa na sababu yoyote ya wanajamii kusherehekea.

Ulemavu wa Kapinga unatumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui kuhusu mtazamo wa jamii kuhusu watu wenye ulemavu wa viungo vya uzazi. Inabainika kuwa wanajamii wana mtazamo hasi kuhusu watu wenye ulemavu huu. Kwa mujibu wa Oje (2006), suala la ngono na uwezo wa mtu wa kushiriki ngono huwa na athari kubwa kwa wanaume na wanawake katika tamaduni nyingi za Kiafrika kwa kuwa ngono inahusiana na hali ya ubinadamu. Kwa hivyo, mwanajamii anayekisiwa kuwa hatimizi matarajio ya jamii kuhusu ngono hutengwa na wanajamii wengine.

Aidha, mwandishi anawasilisha maudhui kuhusu mila na desturi za jamii nyingi za Kiafrika ambapo mwanamume huhitajika kulipa mahari kwa wazazi wa mke wake ili aruhusiwe kumuoa rasmi. Katika bara la Afrika mahari ni kigezo muhimu katika

kuunganisha mwanamume na mwanamke katika ndoa. Kadhalika, inaaminika kuwa mtoto anapozaliwa inaashiria kuwa ndoa imekamilika na uhusiano kati ya wanandoa umeimarika. Jamii nyingi za Kiafrika huchukulia watoto kuwa sababu kuu ya watu kuoana kwa kuwa asasi ya ndoa huhalalisha tendo la ndoa na uzazi. Kwa hivyo, mwanamume anaposhindwa kushiriki kitendo cha ngono na mke wake hawezi kutimiza matarajio ya jamii kwamba kizazi kipya kitapatikana. Moore anaendelea kusema kuwa jambo hili linaweza kuwa msingi wa talaka ambapo mke hulazimika kurudi kwao kwa mujibu wa mila na desturi za jamii.

Umuhimu wa mwanamume kukamilisha ndoa na mke wake kupitia kitendo cha ngono unasisitizwa kupitia kwa jinsi ambavyo wanajamii wanawalaumu wazazi wa Kapinga kutokana na ulemavu wa mtoto wao. Jambo hili linamwathiri mama yake Kapinga kiasi kwamba anajaribu kujiua kutokana na aibu alioletewa na mwanawe kwa kushindwa kushiriki tendo la ndoa na mke wake. Mke wa Kapinga aliathirika pia na ulemavu wa mume wake kiasi kwamba alijaribu kumsaidia lakini hakufua dafu. Mwandishi anaeleza:

> Kapinga alijaribu tena siku ya pili-kazi bure! Siku ambayo kwa desturi ilikuwa ya mwisho, bibi aliona kwamba hapakuwa na usalama. Alikata shauri kuvunja sheria. Alijitahidi kumsaidia bwana wake. Akiwa amevaa shanga nyingi sana kiunoni, alimchoma choma Kapinga kwa matiti kifuani; alimtekenya tumboni, mgongoni na kisogoni lakini Kapinga alikuwa baridi, alikuwa akiguna tu. Bibi arusi alitokwa na machozi: “Kapinga! Kapinga kweli nirudi kwetu!” alilia. Kapinga, ingawa jasho lilikuwa limemtoka, alishindwa. Alinyang’anywa mwanamke. Kesho yake bibi arusi alirudi kwao. (Kezilahabi, 1975, uk. 10).

Baada ya Kapinga kushindwa kukamilisha ndoa yake kwa kitendo cha ngono mara ya kwanza alipewa nafasi nyingine ya mwisho ili ajaribu kutekeleza wajibu huo. Hata hivyo, inabainika kuwa bado Kapinga alishindwa hata baada ya kusaidiwa na mke wake. Mwandishi anachora taswira ya namna mke wake Kapinga alikuwa amejiandaa ili kumvutia mumewe kwa kuvaa shanga nyingi kiunoni na kutumia mbinu

mbalimbali ili kumsisimua kimapenzi. Hata hivyo, Kapinga alishindwa. Mwandishi anatumia msemo '*alikuwa baridi*.' Kitendo cha ngono ni suala la kimwili na kihisia ambapo mtu hupata hamu ya kushiriki ngono na mtu mwingine. Hamu hii ni ya kimaumbile na inajikita kwenye hali ya mtu kibayolojia na kisaikolojia. Kwa hivyo, msemo kuwa Kapinga '*alikuwa baridi'* ni mtindo unaotumiwa na mwandishi kusisitiza kuwa Kapinga hakuweza kupata msisimko wa kushiriki ngono na mke wake hata baada ya juhudi za mke wake za kumsisimua. Wanaume hupata msisimko wa ngono wanapoona vitu vinavyohusu ngono. Kwa mfano, wanaweza kupata msisimko wanapoona uchi wa mwanamke. Maelezo kuhusu juhudi za mke wake Kapinga za kujaribu kumsisimua kwa kumwonyesha uchi wake na kutumia mbinu mbalimbali bila mafanikio yoyote yanalenga kusisitiza kiwango cha ulemavu wa Kapinga. Aidha, mwandishi anaeleza kuwa Kapinga '*alitokwa na jasho'* kuashiria kuwa alikuwa na woga na wasiwasi.

Kushindwa kwa mwanamume kushiriki kitendo cha ngono humwathiri kwa njia nyingi. Mwanamume huyu anaweza kupatwa na hisia za kutojiamini, mfadhaiko, wasiwasi, mawazo mengi na ukosefu wa maelewano katika uhusiano wake na watu wengine. Kwa hivyo, inaelekea kuwa Kapinga aliathirika sana kutokana na ulemavu wa kushindwa kushiriki ngono kwa kuwa alikisia kuwa hali hii ingeathiri uhusiano wake na mke wake. Maneno ya mke wake Kapinga yanachora taswira ya mwanamke aliyekuwa na hofu ya kurudi kwao. Alijaribu kumsuta mumewe kwa kusema: '*Kapinga! Kapinga kweli nirudi kwetu!'* Kauli hii inadhihirisha masikitiko aliyokuwa nayo kwamba ulemavu wa mume wake ungemlazimu arudi kwao kwa kuwa ndoa huhalalisha tendo la ngono ambalo ni muhimu katika kuendeleza kizazi cha jamii. Aidha, suala la kutokuwa na uwezo wa kuzaa miongoni wa jamii nyingi lilionekana kama njia mojawapo ambayo ingesababisha kusambaratika kwa ndoa.

Kulingana na Wischmann (2013), katika jamii nyingi ulemavu wa mwanamume kushindwa kumtunga mwanamke mimba unafedhehesha zaidi kuliko wa mwanamke kushindwa kupata mimba. Hata hivyo, kuna mikakati inayowekwa na jamii na familia ili kukabiliana na tatizo hili. Ulemavu wa viungo vya uzazi ni suala nyeti katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa hivyo, mwanamume anaposhindwa kukamilisha ndoa yake kwa kitendo cha ngono jambo hili linamfedhehesha yeye binafsi na jamii kwa jumla. Kwa mfano, inabainika kuwa ulemavu wa Kapinga katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni jambo lililoaibisha kijiji kizima. Mwandishi anasema:

> Kapinga aliaibisha kijiji kizima. Wapiga zeze walikuwa wamekwishaanza kuimba:
> Wanaume wa Bugolola
> Mchana hawajambo
> Usiku hawana tendo
> Vifaranga vya kuku
> Baridi kujikunyata
> (Kezilahabi, 1975, uk. 10).

Mwandishi anatumia wimbo kama mtindo wa kuwasilisha mtazamo wa jamii kuhusu ulemavu wa Kapinga na namna ambavyo aliaibisha kijiji cha Bugolola. Inadhihirika kuwa wapiga zeze kupitia wimbo wao wanamfanyia stihizai Kapinga na kumkejeli pamoja na wanaume wote wa kijiji cha Bugolola. Wanatumia sitiari ya kifaranga kuwarejelea wanaume wa kijiji cha Bugolola na kusema kuwa wanaume hawa hawawezi kufanya kitendo cha ngono na hawasisimuki ila wanajikunyata tu kwa baridi kama vifaranga vya kuku. Wimbo wa wapiga zeze unawasilisha ujumbe kwa kutumia sitiari ya vifaranga kama tasfida kwa kuwa ilikuwa mwiko kuzungumza kuhusu ngono kwa uwazi katika jamii nyingi za Kiafrika.

Kama wanavyodai Tabong na Adongo (2013), katika jamii nyingi za Afrika, inaaminika kuwa ugumba unaweza kusababishwa na ushirikina. Kwa kuzingatia

msingi huu, inaaminika kuwa suluhisho la ugumba linaweza kupatikana iwapo mwathiriwa atatafuta usaidizi kutoka kwa mganga. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* madai ya Tabong na Adongo yanadhihirika mwandishi anapoeleza kuwa:

> Kapinga alitafutiwa waganga wa kienyeji. Baada ya majuma mawili alikuwa mwanamume. Baada ya kulipa baba mkwe wake ng'ombe mmoja, Kapinga alipewa tena bibi ili ajaribu. Alipita. Ingawa alipita, watu walikuwa wamekwishamdharau. Walisema kwamba kaka yake alimsaidia. Sherehe ilifanywa tena lakini ilikuwa ya hivi hivi tu. (Kezilahabi, 1975, uk. 10).

Kwa mujibu wa imani ya jamii husika, baada ya majuma mawili Kapinga alipelekwa kwa mganga ili kupata suluhu ya ulemavu wa kiungo cha uzazi. Ingawa Kapinga alipata usaidizi kutoka kwa mganga wa kienyeji aligharamika kwa kuwa kulingana na mila na desturi za jamii alihitajika kulipa ng'ombe kwa baba mkwe. Ng'ombe huyu alikuwa faini kwa kushindwa kukamilisha ndoa yake kwa kitendo cha ngono mara ya kwanza jambo lililomlazimu mke wake kurudi kwa wazazi wake. Kadhalika, athari za ulemavu wa Kapinga inadhihirika kwa kuwa hata baada ya kutibiwa na mganga wa kienyeji jamii iliendelea kumdharau na hata kuushuku uwezo wake na kudai kuwa alisaidiwa na kaka yake kuikamilisha ndoa yake kingono.

Kwa kusawiri ulemavu wa Kapinga, Kezilahabi anawasilisha ujumbe kuhusu namna jamii inavyowasukuma watu wanaokumbwa na ulemavu wa kutoweza kushiriki ngono kiasi kwamba wanakiuka maadili na hata kupoteza rasilimali zao katika juhudi za kujaribu kujiondolea fedheha. Wanajamii wanaonekana kutofahamu kuwa ugumba ni ulemavu unaoweza kumwathiri mtu yeyote na kuwa unaweza kusuluhishwa kwa njia ya tiba za kisasa badala ya kufuata mila zilizopitwa na wakati zinazoweza kuhatarisha afya ya mtu binafsi. Kama anavyodai Mbiti (1969), utamaduni wa Kiafrika uliruhusu mwanamume gumba kusaidiwa na kaka yake kutekeleza majukumu ya ngono na kumtia mke wake mimba ili kuokoa ndoa yao. Hata hivyo

mila hii huenda ikawa chanzo cha madhara ya kiafya wakati huu ambapo magonjwa ya zinaa yamekithiri katika jamii.

Leke (2016) anasema kuwa katika muktadha wa Kiafrika, watoto wanathaminiwa sana katika ndoa. Kwa hivyo, ugumba huchukuliwa kama laana na ni tukio la kuhuzunisha sana kwa wanandoa, familia na jamii kwa jumla. Kutokana na mtazamo huu inadhihirika kuwa Kapinga hakutambulika kama mwanamume kamilifu aliposhindwa kushiriki katika kitendo cha ngono na mke wake na ni baada ya kutibiwa ambapo mwandishi anatueleza kwamba '*alikuwa mwanamume.'* Kauli hii inaashiria kuwa awali Kapinga hakutambulika kama mwanamume kamili kutokana na ulemavu aliokuwa nao. Athari za ulemavu wa Kapinga hata baada ya kutibiwa zinaendelea kujitokeza kwa kuwa inabainika kuwa alikuwa anamlinda mkewe sana kiasi kwamba alimchunga kila alikoenda. Mwandishi anaeleza:

> Kweli maskini akiokota, almasi ataimeza na ili kuhakikisha kwamba haitapotea, hatakwenda kujisaidia chooni. Ndivyo kapinga alivyokuwa. Baada ya kumwoa bibi yake alimchunga sana. Mke wake akienda kuoga, yeye hunyata nyuma. Alizifahamu sana nyayo za mke wake. Akiziona tu, basi ataanza kuzifuata kuona mahali zinapokomea. (Kezilahabi, 1975, uk. 10).

Maelezo ya mwandishi yanaashiria wasiwasi aliokuwa nao Kapinga wa kumpoteza mke wake. Alikuwa akimfuata mke wake kila pahali kwa kuhofia kuwa angempoteza. Mwandishi anatumia msemo '*kweli maskini akiokota almasi ataimeza*' kueleza tabia ya Kapinga. Almasi ni aina ya madini yenye thamani kubwa na hivyo inaweza kuwa na manufaa makubwa. Mwandishi anatumia jazanda ya almasi kuashiria thamani ya mke wake Kapinga. Kapinga alimchukulia mkewe kama kifaa chenye thamani kubwa hasa ikizingatiwa kuwa alikuwa amerudi kwa wazazi wake hapo awali kutokana na Kapinga kushindwa kutekeleza wajibu wake kama mwanamume katika ndoa. Tabia ya Kapinga ya kumchunga mke wake inaashiria hali ya kutojiamini kama

mwanamume. Aidha, tabia hii inamsawiri Kapinga kama mtu asiye na akili timamu kwa kuwa ni tabia ambayo haitarajiwi kutoka kwa mtu mwenye akili razini.

Ugumba wa Kapinga unatumiwa na mwandishi kuwahamasisha wasomaji kuhusu utamaduni na imani potofu kuhusu swala la uwezo wa kupata mtoto katika muktadha wa ndoa. Miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika wanandoa wanapokosa kupata mtoto, anayelaumiwa sana ni mwanamke. Kama anavyosema Mbiti (1969), katika jamii nyingi za Kiafrika talaka husababishwa na ugumba au utasa. Hii ni kwa sababu inaaminika kuwa ulemavu huu huziba mkondo wa kuendeleza maisha ya jamii kupitia kwa kuzaliwa kwa vizazi vipya. Kwa kumchora mwanamume mwenye ulemavu wa kuzaa, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa wanaume pia wanaweza kuathiriwa na ulemavu huu na jamii haipaswi kuwalaumu wanawake pekee mtoto anapokosekana katika ndoa. Mwanamume aliyeathiriwa na ugumba hudharauliwa na jamii na kuonekana kama kwamba si mwanamume kamilifu. Mwandishi anatumia ulemavu wa Kapinga kuihamasisha jamii kuhusu hali hii na kuonyesha kuwa mwanamume mwenye ulemavu huu akidhalilishwa na jamii anaweza kuathirika akili na kufanya vitendo visivyo vya kawaida.

Utasa unajitokeza pia katika riwaya ya *Rosa Mistika*. Katika riwaya hii, inabainika kuwa Bigeyo na mumewe Ndalo hawakuwa na mtoto. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Ndalo na mkewe walikuwa wakisumbuliwa na jambo moja uzazi. Walikuwa wamekwishapoteza pesa nyingi sana kutafuta dawa ya uzazi. Mwaka mmoja walikwenda nchi za mbali kuitafuta. Walirudi na nusu debe la mizizi ya miti. Mizizi ilikwisha, na wala hapakuwa na alama yoyote ya Bigeyo kupata mimba. Mwaka uliofuata walikwenda pengine. (Kezilahabi, 1976, uk. 17).

Bigeyo na mumewe Ndalo wanajitokeza kama wahusika waliopitia masaibu mengi kwa kukosa mtoto. Walitumia pesa nyingi na wakati mwingi kuwatembelea waganga wengi katika harakati za kutafuta tiba. Kuhangaika kwao kunadhihirisha namna jamii

inavyothamini watoto na kwamba, kama anavyosema Mbiti (1969), katika jamii nyingi za Kiafrika, ndoa haitambuliki kuwa kamilifu ikiwa mtoto hajazaliwa.

Katika harakati za kutafuta tiba, Bigeyo na mumewe waliwatembelea waganga wengi ambao waliwahadaa na kuwatapeli. Inabainika kuwa licha ya kupewa matibabu mbalimbali Bigeyo hakushika mimba. Mwishowe waliamua kwenda hospitalini kutafuta usaidizi. Huko hospitalini, daktari aliwachunguza na kuwaarifu kuwa hawakuwa na uwezo wa kupata mtoto. Hata hivyo, hawakuridhika na waliamua kwenda kwa mganga mwingine aliyewashauri wale nyama ya kuku mweupe huku wakikimbia kuzunguka nyumba ili wautakase mji wao.

Ni kinaya kuwa Bigeyo na mumewe waliamua kutafuta ushauri kutoka kwa mganga mwingine licha ya kuwa walikuwa wamewatembelea waganga wengi hapo awali bila mafanikio yoyote. Maamuzi ya Bigeyo na mumewe ya kutafuta tiba kutoka kwa waganga yanaibua maudhui ya suala la imani za kitamaduni zinazojitokeza kuhusu ugumba na utasa. Kwa mfano, kama wanavyoeleza Tabong na Adongo (2013), katika jamii za Kiafrika, kuna imani kuwa mtu huathiriwa na ugumba kwa kukiuka miiko ya jamii. Maneno ya Bigeyo yanaashiria kwamba aliamini kuwa ulemavu wake ulitokana na laana. Anasema:

> "Yuuu! Yuuu! Sisi wengine tulilaaniwa umhuuu!'' (Kezilahabi, 1976, uk. 18).

Bigeyo aliyasema maneno haya kutokana na kushangazwa kwake na habari aliyokuwa anaelezwa na Regina jirani yake, kuhusu namna ambavyo wasichana wengi walikuwa wanatoa mimba. Ni kinaya kuwa katika jamii kuna wanawake wanaoavya mimba ilhali wengine wanataabika kwa kukosa kupata mimba. Kwa mujibu wa Kilangwa (2016), jamii nyingi za Kiafrika hulichukulia suala la uavyaji wa mimba kwa uzito sana kwa kuwa uhai huwa na thamani kubwa. Kadhalika, uavyaji

mimba ni ukiukaji wa maadili ya jamii. Katika kuwasilisha hali hizi mbili ambapo wanawake wanakosa kupata watoto kutokana na sababu za kibayolojia na wengine wanaoavya mimba, Kezilahabi anausawiri mkinzano wa mitazamo baina ya kizazi kimoja na kingine kuhusu suala husika. Bigeyo ana umri mkubwa na anathamini watoto ilhali wasichana wa kisasa hawako tayari kupata watoto.

Kauli ya Bigeyo inadhihirisha kuwa aliamini kwamba ulemavu wao ulitokana na laana. Aidha, kauli hii inaonyesha masikitiko makubwa aliyokuwa nayo Bigeyo kutokana na ulemavu aliokuwa nao. Imani kuwa Bigeyo na mumewe walikuwa wamelaaniwa inaendelezwa kupitia kwa mganga wa kaskazini waliyemtembelea. Mganga huyu alidai kuwa ulemavu wa Bigeyo ulitokana na kukataa kwa Bigeyo kuwabeba wadogo zake mgongoni alipokuwa msichana. Kwa hivyo walishauriwa kuwa nyumba yao ilihitaji kutakaswa ili waweze kupata mtoto. Mwandishi anaeleza:

> Huko walimkuta mganga mmoja wa kienyeji aliyewaambia kwamba Bigeyo alikuwa hazai kwa sababu alipokuwa bado msichana alikataa kuwabeba wadogo zake mgongoni. Dawa ya uzazi sasa ilikuwa lazima kupata mkojo wa wadogo zake ajimwagilie mgongoni. Lakini jambo hili halikuwa rahisi: wadogo zake sasa walikuwa watu wazima. (Kezilahabi, 1975, uk. 17).

Mwandishi anatumia ulemavu wa Bigeyo ili kuwasilisha ujumbe kuhusu namna watu wanavyotapeliwa na waganga wa kienyeji wanapoenda kutafuta usaidizi kutoka kwao. Kuhangaika kwa Bigeyo na mume wake katika juhudi za kutafuta tiba kunaashiria kuwa lengo la waganga waliowatembelea lilikuwa ni kujinufaisha. Aidha, mkinzano kati ya tiba ya kale na matibabu ya kisasa unadhihirika kwa kuwa licha ya daktari waliyempata kule hospitalini kuwaambia Ndalu na Bigeyo kuwa hawakuwa na uwezo wa kupata mtoto, waliamua kutafuta usaidizi kutoka kwa mganga wa kienyeji. Mwandishi anadhamiria kuwahamasisha wanajamii kuhusu imani na desturi

zilizopitwa na wakati. Kadhalika, anawaonya wanajamii dhidi ya waganga wa kienyeji ambao wanawapotosha na kuwatapeli.

Katika sehemu inayofuata ulemavu wa miguu utaangaziwa kwa kuzingatia matumizi yake kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe.

### 4.3 Matumizi ya Ulemavu wa Miguu kama Mtindo

Kulingana na Shirika la Watu Wenye Ulemavu (2015), ulemavu wa miguu ni mojawapo ya aina za ulemavu unaotatiza uwezo wa mtu kutembea. Ulemavu huu unaweza kuathiri sehemu yoyote ya mguu. Kadhalika, ulemavu wa miguu unaweza kudhihirishwa na upungufu wa uwezo wa mtu wa kutumia miguu yake kwa namna ya kawaida. Upungufu huu unatatiza kutembea kwake kwa kiwango fulani. Ulemavu wa mguu unaweza kusababishwa na ajali, ugonjwa au uzee. Mtu mwenye ulemavu wa mguu anahitaji kutumia vifaa maalum vinavyomsaidia kutembea. Vifaa hivi ni kama: bakora, gongo, miguu bandia au kiti cha magurudumu.

Katika riwaya ya *Utengano*, mwandishi anachora taswira ya mhusika mkuu kwa jina Maksuudi baada ya kutoka jela. Maksuudi alikuwa amefungwa jela baada ya kupatikana na hatia ya ufisadi na wizi wa fedha za umma. Taswira inayojitokeza baada ya Maksuudi kutoka jela ni ya mtu aliyekuwa  na upweke. Maksuudi anaonekana akiwaza kuhusu mke wake na watoto wake ambao hakujua walikokuwa. Mwandishi anaeleza hali yake:

> Maksuudi alisita ghafla, akautazama mkono wake wa kushoto uliokuwa ukitetemeka, akajaribu kuuvuta mguu wake, ukamfuata kwa shida. Sivyo alivyotaka umfuate. Sivyo mguu na mkono wake ulivyokuwa. Alielewa kuwa kile sasa kimeshakuwa kilema. Aliumia moyoni kuona watoto wake hawapo karibu yake. (Mohamed, 1980, uk. 103).

Kutokana na maelezo haya inabainika kuwa Maksuudi alikuwa na ulemavu wa mguu na mkono wa kushoto. Maksuudi alifahamu kuwa ashakuwa kilema. Jambo

lililomsikitisha zaidi ni kufahamu kwamba hakuwa na jamaa yake karibu na hakujua walikokuwa.

Kwa mujibu wa Harknett (1996) imani za kale kuhusu chanzo cha ulemavu zinadhihirika katika jamii nyingi za Afrika Mashariki. Harkett anadai kuwa katika Afrika Mashariki inaaminika kuwa ulemavu ni ishara ya matokeo ya vitendo viovu alivyotenda mtu au ushirikina anaotendewa mtu na mwingine. Watu wenye imani ya kidini wanaamini kuwa ulemavu unatokana na mapenzi ya Mungu. Mallory na wengine (1993) na Mbah-Ndam (1998) wanadai kuwa kuna jamii zinazoamini kuwa ulemavu ni adhabu inayotokana na miungu na ni dalili ya bahati mbaya na kwa hivyo watu wenye ulemavu wanatengwa na kutelekezwa na jamii.

Mohamed (1980) katika riwaya ya *Utengano* anaashiria kuwa ulemavu wa Maaksudi ulitokana na tabia yake ya hapo awali na kwamba hali hii ililenga kuwa funzo kwake ili aweze kubadilika. Mawazo haya yanadhihirika katika maelezo haya:

> Hasira hasara, na kweli jiwe la tumbawe lilengwapo lina hatari. Ndiyo kwanza leo Maksuudi ajuwe- baada ya kuhasirika. Amejifunza hivyo toka kuondokewa na wale ambao kumbe ndio waliodhibiti furaha yake; wale aliowamwaia mapenzi ya ndani kwa ndani, akawanyima kuridhika. Mbali na yale mengine ya ulimwengu yaliyomkuta, na maradhi juu! Anajuta. Huu ulikuwa wakati uliomjulisha Maksuudi kuwa pesa si kitu. Pesa zilitumwa na watumishi walitenda waliyoyatenda, lakini kuna mengi yasiyofanyika kwa pesa. Na sasa Mungu kamuafu. Kamuafu si haba angalau anaweza kuokota mguu. Na sasa anajiona jinsi alivyodhoofika na zile fedha alizozirundika benki hazikufaa kitu sasa. (Mohamed, 1980, uk. 103-104).

Maksuudi anajuta kwa sababu ya maovu aliyokuwa amewafanyia jamaa zake. Alikuwa amewanyima mapenzi na aliwakosesha amani kwa kuwahangaisha wakati alipokuwa mwenye nguvu na mamlaka. Anaona kuwa kufungwa kwake jela na kupatwa na maradhi yaliyomlemaza ilikuwa ni adhabu kwa matendo yake maovu.

Mwandishi anaeleza kuwa Mungu alikuwa amemsamehe Maksuudi kwa makosa aliyokuwa ametenda, vinginevyo hangeweza hata kuokota mguu.

Ulemavu wa Maaksudi unatumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya mabadiliko. Kabla ya kufungwa jela, Maksuudi alikuwa katili, alimnyanyasa mke wake Tamima na binti yake Maimuna. Kadhalika, alitumia cheo na mamlaka aliyokuwa nayo kuwadhulumu wanajamii wengine. Hata hivyo ulemavu ulikuwa umembadilisha na akaanza kuwathamini watu wengine.

Kupitia kwa mhusika Maksuudi, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa pesa sio kila kitu kwa kuwa licha ya pesa nyingi alizokuwa nazo Maksuudi hakuwa na furaha. Aidha, mwandishi anadhamiria kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa familia. Maksuudi anajuta kutokana na makosa yake ya awali ambayo yalisababisha kusambaratika kwa familia yake. Mwandishi anaeleza:

> Maksuudi aliwaza aliowatendea vibaya. Aliwavuta akilini wote alioweza kuwakumbuka lakini alipofika kwa Mwanasururu aliyekuwa mkewe alikataa kuwaza zaidi. Aliyomtendea Mwanasururu ulikuwa unyama. Kutoka hapo alipokuwa Maksuudi amejinyoosha, huku akiteswa na matendo yake mwenyewe, alimshtukia Bwana Haji kamsimamia… Sasa hapana mipaka kati ya Maksuudi na Bwana Haji, ila mtu na mwenzake au mtu na jirani yake. (Mohamed, 1980, uk. 104).

Haya ni mawazo ya Maksuudi kuhusu maisha yake ya awali kabla ya kufungwa jela. Alikuwa anawaza kuhusu watu mbalimbali aliokuwa ametendea maovu. Alimkumbuka zaidi Mwanasururu aliyekuwa mkewe na kujuta kutokana na unyama aliomfanyia.

Mwandishi anatumia tashihisi anapoeleza kuwa Maksuudi ‘*aliteswa na matendo yake mwenyewe*’ kuashiria namna ambavyo Maksuudi alikuwa akijuta kwa matendo aliyokuwa amefanya hapo awali. Hatima ya matendo haya ilikuwa ni kufungwa jela na kulemaa kutokana na ndwele. Tofauti na hapo awali alipokuwa mzima, mwandishi

anamsawiri Maksuudi kama mtegemezi. Alikuwa anatumia bakora yake kama mkongojo ili aweze kusimama. Aidha, alimtegemea Mzee Mabruki kumfanyia kazi ndogondogo. Mwandishi anadhihirisha haya anaposema:

> Maksuudi alitaka kuinuka kwa ghafka, lakini alitanabahi kuwa alikuwa na ndwele. Basi, taratibu, huku kamtumbulia macho Bwana Haji, alisimamia ile bakora yake ambayo sasa ilikuwa ina huduma ya mkongojo badala ya pozi. (Mohamed, 1980, uk 104).

Inabainika kuwa Maksuudi alikuwa anatumia bakora yake hapo awali kama kifaa cha kuashiria hadhi na mamlaka, aliyokuwa nayo lakini matumizi ya bakora hiyo yalikuwa yamebadilika baada ya kulemaa na akalazimika kuitumia kama mkongojo.

Katika kuwasilisha maudhui ya mabadiliko, mwandishi anatumia Mzee Mabruki aliyekuwa msaidizi wa Maksuudi. Mzee Mabruki alikuwa mkuza katika ujana wake lakini athari za uzee zilikuwa zimemlemaza. Mwandishi anaeleza hali ya Mzee Mabruki:

> Labda Mzee Mabruki aliwahi kuwa mkuza katika ujana wake. Na leo kwa sababu amelemewa na shehena ya miaka, ilimmudu na kumtoa kibyongo. Miguu yake miembamba mirefu, iliyokuwa imechoka kuzuia uzito wa mwili miaka mingi imefanya kupinda magotini, kwa kile kibyongo chake, mwendo wake ulikuwa wa kuchupiachupia. Kifua chake kilionyesha kilikuwa kipandikizi hapo kale, lakini kimekaliwa na sulubu za kupanda minazi ya toka zama za Bwana Lembani hata zikaja zama za Bwana Maksuudi. (Mohamed, 1980, uk. 105).

Taswira ya mabadiliko ya Mzee Mabruki inajitokeza katika maelezo haya. Maumbile yake yalikuwa yamebadilika na kudhoofika kutokana na umri na kazi ngumu aliyokuwa anafanya katika ujana wake. Inabainika kuwa mbali na umri, ulemavu wa Mzee Mabruki ulikuwa umesababishwa na kazi gumu ya kupanda minazi aliyokuwa akifanya shambani kwa Maksuudi na Bwana Lembani. Wakati huo Maksuudi alikuwa mwenye nguvu na mamlaka na Mzee Mabruki alikuwa mtumishi wake lakini hali

ilikuwa imebadilika kutokana na kulemaa kwa Maksuudi na hakuwa na budi kumheshimu Mabruki. Mwandishi anaeleza:

> Baina ya Maksuudi na Mabruki kumebakia kufaana. Maksuudi si bwana tena mbele ya Mabruki. Hata hivyo Mabruki hakuwa na mtu mwingine wa kutegemea. (Mohamed, 1980, uk. 105).

Maelezo haya yanaashiria uhusiano uliokuwapo kati ya Maksuudi na Mzee Mabruki. Uhusiano wao ulikuwa wa kufaana tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo Maksuudi alikuwa bwana mkubwa  na Mabruki mtumishi wake.

Kulingana na Kamusi ya Karne ya 21, neno bwana ni jina la heshima linalotumiwa kwa mwanamume ambaye amemwajiri mtu. Kwa hivyo, mabwana ni watu wenye nguvu kifedha na kimamlaka. Mwandishi anaposema kuwa Maksuudi hakuwa bwana tena anasisitiza kuhusu mabadiliko yaliyokuwa yametokea katika maisha yake kiasi kwamba alimuona Mzee Mabruki aliyekuwa mtumishi wake, kama mtu aliyekuwa na hadhi sawa na yeye. Mabadiliko ya Maksuudi yanasisitizwa na mwandishi anaposema:

> Sasa ameacha mengi ati, na mwenyewe anayaita laana. Sasa ati anajua huruma, utu, imani na hisia kwa wengine. Sasa haendi tena nje. (Mohamed, 1980, uk. 106).

Maksuudi anaonekana kukubali kuwa ulemavu uliompata ulitokana na laana kwa sababu ya maovu aliyokuwa amefanya hapo awali. Kuteseka kwake kunambadilisha na kumfanya mtu mwenye hisia za ubinadamu, aliyewajali wengine na mwaminifu. Mwandishi anadhihirisha mabadiliko haya anaposema:

> Siku hizi sala ndiyo jambo la pekee linalomtakasa moyo Maksuudi. 'Mshibe Mungu, staghafiru, naye mwepesi wa kusamehe waja wake.' Ndiyo busara aliyokuwa nayo sasa. Ingawa miaka mitatu nyuma hakujua kuwa kumshiba Mungu si kudhulumu au kwenda nje au kufanya magube chungu nzima. Kati yake na ucha Mungu kulikuwa na unafiki. Alivaa nguo ya udanganyifu. Alilolijua ni mradi wake tu. (Mohamed, 1980, uk. 106).

Maelezo haya yanaashiria mabadiliko ya Maksuudi hasa kuhusu imani yake ya dini. Mwandishi anaeleza kuwa Maksuudi alikuwa akimuomba Mungu amsamehe. Alikuwa akisali kila wakati, jambo ambalo alikuwa amejitenga nalo miaka mitatu iliyopita. Kufungwa jela na kulemaa mguu kulikuwa kumembadilisha na akaanza kuithamini dini tofauti na hapo awali ambapo alithamini zaidi miradi ya kujitajirisha. Ulemavu wa miguu wa Maksuudi umetumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwahamasisha jamii ili waishi maisha yenye maadili, wasiwe na tamaa ya mali kiasi kwamba wanasahau Mungu na hata familia zao katika jitihada za kujitajirisha.

Mhusika mwingine katika riwaya ya *Utengano* mwenye ulemavu wa mguu ni Kabi. Kabi alikuwa amekatwa mguu wake wa kushoto na alitembea kwa kutumia gongo. Maisha ya Kabi yanawasilishwa na mwandishi kupitia kwa uhusiano wake na Maimuna binti yake Maksuudi. Maimuna alikuwa ametoroka nyumbani kutokana na dhuluma ya baba yake. Siku moja akiwa katika harakati za kutafuta samaki wa kuuza alikutana na Kabi aliyekuwa mvuvi. Maimuna alipogundua kuwa Kabi alikuwa na ulemavu wa mguu alishangaa. Mwandishi anaeleza:

> Maimuna alikuwa na mshangao wa mambo mawili. Kwanza ule mguu wa Kabi. Kafanya nini kijana huyu maskini? Moyo ulimpiga wala hakuweza kujua kwa nini. Alizidi kumchanganyishia macho Kabi, akamwona jinsi alivyonawiri na kushiba nguvu; kijana mwenye sura ya kiume ya kuvutia- mwenye siha, weusi uliokoza, macho makali, kifua kikubwa, lakini maskini kapoteza mguu. Maimuna kwa wakati huu alishindwa kuuliza umbeya. Adabu haikumpa nafasi afanye hivyo. (Mohamed, 1980, uk. 155).

Mwandishi kupitia kwa Maimuna anachora taswira ya maumbile ya Kabi. Maimuna anadhihirisha hisia za huruma na mshangao. Inabainika kuwa licha ya ulemavu wa mguu uliomwathiri Kabi, bado alikuwa mwanamume mwenye afya, nguvu na sura ya kuvutia lakini Maimuna anaonekana kuzingatia zaidi ulemavu wake na chanzo chake.

Beuchamp na Chung (2010) wanatambua kuwa kwa kiasi kikubwa fasihi ya kisasa imewachora wahusika walemavu wa kike na kiume kama wanaoogofya, wanaotengwa, wasioeleweka na wanaohitaji huruma. Kimsingi, wahusika hawa wametumiwa kuzua hali ya kusikitisha, woga au chuki. Mitazamo inayoshikiliwa na watu wasio na ulemavu kuhusu watu wenye ulemavu mara nyingi huwa ni ya huruma, woga au maudhi. Mitazamo hii inasababisha kutengwa kwa watu hawa. Watu wenye ulemavu wanaposawiriwa kwa njia chanya, wanapewa sifa zisizo za binadamu wa kawaida. Kwa mfano, wanachorwa kama wenye wema na uzuri wa kupindukia au kama majitu wabaya. Kama wanavyosema Beuchamp na Chung usawiri wa wahusika wenye ulemavu kwa namna hii katika fasihi ni mtindo unaotumiwa na waandishi kuendeleza na kukuza maudhui ya ubaguzi. Kadhalika, sifa za wema, uzuri na ubaya zilizopewa wahusika hawa zinatumiwa kuendeleza maudhui ya kimaadili katika jamii. Madai ya Beuchamp na Chung yanadhihirika kupitia kwa mhusika Kabi na maingiliano yake na Maimuna katika riwaya ya *Utengano*. Kabi anasawiriwa kama mtu mwenye utu na huruma:

> Kwa kweli Kabi alikuwa mja wa huruma kwa wenzake, lakini leo huruma zake zimeingia kitu kingine. Hakukijua kitu gani. Aliuhisi moyo wake ukienda mbiombio. Alipojaribu kufumbua mdomo wake kusema, midomo ilimtetemeka. Aliishia kumkabidhi Maimuna ile shazi ya samaki. 'Hutaki…hutaki pesa?' Aliuliza Maimuna kwa wasiwasi. 'Pesa? Nini pesa mbele ya utu?' (Mohamed, 1980, uk. 156).

Maelezo ya mwandishi yanatoa taswira ya mkutano kati ya Kabi na Maimuna kwenye ufuo wa bahari. Inabainika kuwa ingawa Kabi alikuwa mkarimu kuna hisia za pekee alizohisi wakati alipomwona Maimuna. Utu na ukarimu wake unajitokeza alipompa Maimuna samaki na kukataa kupokea malipo yoyote. Kadhalika, Kabi alimuuliza Maimuna ni jambo lipi lilikuwa likimsumbua kwa kuwa alionekana mnyonge na mwenye huzuni.

Tamko la Kabi kuwa utu ni bora kuliko pesa lilimshangaza sana Maimuna na akaanza kuyatathmini maisha yake:

> Maimuna alisita hivyo hivyo kwa muda, akiwaza maana ya maneno hayo aliyoambiwa na Kabi. Maneno yenyewe yalimpanda kichwani kama chemchem. Alihisi, toka lini yeyé kuwa bora kuliko fedha na kama ni utu, utu gani alionao yeye? Labda aliwahi kuwa mtu, lakini sio leo. Leo ni nguo mbovu iliyovaliwa na mwanadamu, ikafuliwa, ikakwachuliwa, ikavaliwa na kuvaliwa tena na sasa imekuwa nyamunyamu, tambara bovu. Bado kijana huyu leo anamzumbulia yeye utu. Ama kweli jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza. Machozi Maimuna yalianza kumlengalenga , lakini hakungoja kufedheheka. (Mohamed, 1980, uk. 156).

Kitendo cha Kabi cha kutothamini pesa kilimfanya Maimuna awaze kuhusu maisha yake. Alijiona kama mtu aliyekuwa ametenda maovu na asiyekuwa na utu. Aliyarejelea maisha yake ya hapo awali ambapo alikuwa mlevi na kahaba. Aliingizwa katika biashara ya ukahaba baada ya kutoroka kwao nyumbani alikokuwa amedhibitiwa na baba yake mzazi.

Mwandishi wa riwaya ya *Utengano* anachora taswira ya mawazo ya Maimuna kuhusu maisha yake. Maimuna alijilinganisha na nguo mbovu ambayo ilikuwa imechakaa kwa sababu ya kuvaliwa na kuvuliwa mara nyingi kiasi kwamba ilikuwa imegeuka na kuwa tambara bovu. Nguo iliyochakaa inaashiria maisha ya ukahaba aliyokuwa akiishi Maimuna. Alikuwa ameshiriki ngono na wanaume wengi kiasi kwamba alijiona kama tambara bovu ambalo halikuwa na thamani. Katika mazungumzo yake na Kabi, Maimuna anabaini kuwa Kabi alikuwa anazungumza kuhusu utu kwa kuwa hakuwa anafahamu ukweli kuhusu maisha yake. Ni dhahiri kuwa Maimuna alikuwa anajuta na kufedheheshwa na maisha hayo na ndiyo maana machozi yalimtoka alipoyawaza.

Matumizi ya ulemavu wa mguu wa Kabi kama mtindo wa kukuza maudhui ya maadili yanajitokeza katika uhusiano wa mapenzi unaoishia katika ndoa kati ya Kabi na

Maimuna. Uhusiano wao wa kimapenzi unatumiwa na mwandishi kuashiria kuwa mtu yeyote anaweza kubadilika na kuwa mwenye maadili ikiwa jamii itamwelewa na kumkubali. Maisha ya ukahaba aliyokuwa akiishi Maimuna yanamfanya ajifananishe na mnyama. Kwa kawaida tabia ya uhusiano wa kingono miongoni mwa wanyama hautawaliwi na kaida zozote, wanyama wanaweza kushiriki ngono na mnyama mwingine bila kufungwa na masuala ya uadilifu, uaminifu au uhusiano wa kinasaba. Maimuna alihisi kwamba hakuwa na ubinadamu wowote kutokana na tabia zake za awali ambapo alikuwa akishiriki ngono na wanaume wengi bila kujali kaida na maadili ya jamii na ndio maana hakutaka kuolewa. Kabi alijitahidi kubadilisha mawazo haya ya Maimuna alipomwambia:

> 'Usiseme hivyo Maimuna, sote sisi binadamu, tu sawa. Sote sisi tumewahi kukosa katika maisha yetu… Usiwe hivyo Maimuna, binadamu anaweza kuwa mnyama, lakini anaweza kurejea ubinadamu wake, na unapokuwa huna budi, ukatenda mambo wasiyoyapenda watu, watu huwa hawatazami sababu za wewe kutenda hivyo, basi tu watakupagaza unyama.' (Mohamed, 1980, uk. 162).

Sifa ya utu ya Kabi inadhihirika katika mawaidha aliyompa Maimuna. Kutokana na wasia huu inafahamika kuwa Kabi alielewa kuwa binadamu husukumwa na sababu fulani zinazomfanya kupotoka kimaadili na kwamba mtu yeyote anaweza kupotoka. Kwa mfano, Maimuna alikuwa amesukumwa kwenye ukahaba na baba yake mzazi ambaye alikuwa amemtawisha pamoja na mama yake nyumbani kwao. Alipopata nafasi ya kutoroka kutoka nyumbani aliingizwa katika biashara ya ukahaba na Farashuu. Farashuu alimwingiza Maimuna katika biashara hii kimaksudi kama njia yake ya kulipiza kisasi kwa hila aliyokuwa amefanyiwa na Maksuudi, baba yake Maimuna. Licha ya kupotoka kimaadili, kama anavyoashiria Kabi, jambo lililo muhimu ni kuweza kubadilika na kujitenga na tabia zinazokinzana na maadili yaliyokubalika katika jamii.

Kupitia kwa uhusiano wake na Maimuna, Kabi anajitokeza kama mwanamume mwenye utu kwa kuwa hakumtolea hukumu Maimuna kutokana na maisha yake ya zamani. Anamwambia Maimuna:

> 'Uanaume wangu hautotiwa doa na uliyofanya zamani, ndiyo umeshayafanya. Mimi sihusiki na ya zamani, nahusika na ya sasa. Hoja masikilizano.' (Mohamed, 1980, uk. 162).

Kabi alimwambia Maimuna maneno haya kutokana na wasiwasi aliokuwa nao Maimuna kwamba angemwaibisha Kabi iwapo angekubali kuolewa naye. Ingawa Maimuna alifikiri kuwa ndoa kati yake na Kabi ingemletea Kabi fedheha na aibu, Kabi hakuyajali maisha aliyokuwa akiishi Maimuna hapo awali, kilichokuwa muhimu kwake ni maisha mapya ambayo wangeanza.

Kupitia kwa taswira ya ulemavu wa mhusika Kabi, mwandishi anawasilisha maudhui kuhusu mahusiano ya watu na umuhimu wa wanajamii kutowahukumu au kutowalaumu wengine bila kuwapatia nafasi ya kujieleza au kuwaelewa. Uhusiano wa Kabi na Maimuna unatumiwa na mwandishi kuwahamasisha watu dhidi ya ubaguzi kwa misingi ya tabia zao au mwonekano wao kimaumbile kwa kuwa licha ya ulemavu aliokuwa nao, Kabi anajitokeza kama mwanamume kamilifu mwenye utu na ubinadamu. Aidha, Maimuna hakumuona Kabi kama mtu mwenye upungufu kwa kuwa na ulemavu ila alimpenda jinsi alivyokuwa na kukubali kuolewa naye.

Ujumbe mwingine unaowasilishwa kupitia kwa mhusika Kabi ni uwezo wa watu wenye ulemavu wa kutekeleza majukumu yao na kujitafutia riziki. Licha ya ulemavu wa mguu, Kabi anajihusisha na kazi ya uvuvi. Ustadi wa Kabi alipokuwa akivua ulimshangaza Maimuna hasa alipompata juu ya jabalí. Mwandishi anasema:

> Maimuna alipotupa jicho upande ilikotokea sauti alimwona Kabi juu ya jabali kakaa anampungia mkono. Maimuna alistaajabu vipi Kabi kaweza kupanda jabali lile kwa mguu mmoja na gongo lake. Lakini hiyo isiwe ajabu, Kabi

> kajifunza mambo mengi magumu ambayo kwa mwenye kilema wa kawaida, yangalikuwa katika jumla ya yasoyumkinika. (Mohamed, 1980, uk. 158).

Inabainika kuwa Kabi alikuwa mwenye bidii na ulemavu wa mguu aliokuwa nao haukuwa kikwazo kwa kuwa matatizo aliyokuwa amepitia maishani yalimlazimu kujifunza mambo mengi.

Zaidi ya hayo, ulemavu wa Kabi umetumiwa na mwandishi kama mtindo wa kuwasilisha maudhui kuhusu mikinzano katika ndoa na athari zake. Inabainika kuwa Kabi alikatwa mguu kutokana na ajali aliyopata katika harakati za kwenda kumtafutia mama yake usaidizi. Mama yake alikuwa na ulemavu wa akili uliosababishwa na ulevi wa kupindukia. Kabi anamweleza Maimuna chanzo cha ulemavu wa mguu wake:

> 'Mimi nilizaliwa na miguu yangu miwili lakini nimepoteza mguu wangu wa pili kwa kumuokoa mamaangu. Mamaangu katika siku za mwisho za umri wake alikuwa mwendawazimu. Na wazimu huo aliupata kwa ulevi mwingi alioushiriki siku zake za mwisho. Siku moja aliniita chumbani kwake, na mimi mdogo siku hizo, mtoto wa miaka kumi na tatu. Nilipofika chumbani, niliyojionea na lile ambalo alitaka nifanye lilinipa hapo hapo nitoke mbio. Nyumba yetu iko kando kando na barabara. Niliufungua mlango wa nje kwa pupa. Kuchupa kizingiti tu, nataka kukata barabara, gari hili limefika, pua na mdomo nami. Mtume! Mtume!' Mtume! aaa, wapi! Gari lilinipiga dafurao moja na kunirusha huko! Sikujijua tena.' (Mohamed, 1980, uk. 163).

Athari ya ulevi miongoni mwa jamii inadhihirika kupitia kwa mama yake Kabi. Inaelekea kuwa mama yale Kabi aliathiriwa na ulevi kiasi kwamba alipata ulemavu wa akili. Mwandishi anaashiria kwamba tabia ya ulevi ya mama yake Kabi ilianza walipoachana na mumewe. Kupitia kisa hiki mwandishi anaonyesha uhusiano uliopo kati ya ulemavu wa tabia, ulemavu wa akili na ulemavu wa viungo na namna ambavyo kuwepo kwa ulemavu mmoja kunaweza kusababisha ulemavu mwingine. Hii ni kwa sababu ulemavu wa tabia wa kushiriki ulevi kupindukia ndio uliosababisha

ulemavu wa akili wa mama yake Kabi na hatimaye ukachangia kwenye ajali iliyomlemaza Kabi mguu.

Mbali na matatizo katika asasi ya ndoa, taswira ya ulemavu wa Kabi inatumiwa na mwandishi kuwasilisha maudhui kuhusu dhuluma dhidi ya mwanamke. Inabainika kuwa mama yake Kabi alikuwa ameolewa na mwanamume ambaye alikuwa kiongozi. Mwanamume huyo alipopata mamlaka alianza kumtesa mama yake Kabi kwa kumpiga na kumtawisha. Kadhalika, alimnyang'anya kijishamba chake, vyombo vya dhahabu na pesa kisha akamtaliki na kumuoa mwanamke mwingine. Tukio hili lilimwathiri sana mama yake Kabi na kumfanya ajiingize katika tabia ya ulevi kama njia ya kujiliwaza. Ulevi wa kupindukia hatimaye ulimtia wazimu. Aidha, alijiingiza katika mahusiano na wanaume wengi kiasi kwamba alipomzaa Kabi hakujua baba yake halisi ni nani.

Kupitia kwa mhusika Kabi, mwandishi analenga kuonyesha kuwa katika jamii bado kuna wanaume wazuri wanaowathamini wanawake. Aidha, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa katika ulimwengu wa sasa ambapo mapenzi yanafungamanishwa na mambo mengi kama vile dini, kabila, tabaka, mali, cheo na vigezo vingine vingi; pendo la dhati lisilojikita kwenye vigezo vyovyote ila maelewano na mapenzi linaweza kupatikana. Kabi ni kielelezo cha mwanamume ambaye anamheshimu mwanamke. Alipoamua kumuoa Maimuna hakuzingatia maisha ya ukahaba aliyokuwa akiishi hapo awali. Aidha, alimpatia Maimuna muda wa kutosha kufanya maamuzi kuhusu pendekezo lake la kumuoa. Kadhalika, Kabi alifuata utaratibu ufaao kabla ya kumuoa Maimuna kwa kuwashirikisha wazazi wao. Inabainika kuwa Kabi alikuwa na mchango mkubwa katika kubadilisha maisha na mtazamo wa Maimuna hasa kuhusu kukubalika kwake katika jamii kama mwanamke mwenye maadili. Mwandishi anaeleza:

> Sasa (Maimuna) alikuwa tayari kuishi maisha mapya. Alikuwa tayari kufungua ukurasa mpya. Yeye na Kabi na Kabi na yeye. Yeye si mhuni tena, si mlevi tena, ni mwanamke maridhia atakayeingia katika mikono ya mwanamme aliyempenda na kumhurumia. Atakuwa mke wa watu. (Mohamed, 1980, uk. 166).

Maimuna anadhihirisha azma yake ya kubadilika na kuishi kama mwanamke mwenye maadili. Kupitia kwa ndoa yake na Kabi, mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa mui huwa mwema. Mtu yeyote katika jamii anaweza kubadilika na kuwa mwema iwapo atapewa nafasi ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, jamii ina jukumu kubwa katika kukuza maadili kwa kuwa ina uwezo wa kuleta mabadiliko kimaadili na kuondoa uozo uliokithiri miongoni mwa wanajamii.

Mwandishi anawasilisha maudhui kuhusu umuhimu wa kuelimisha wanajamii kuhusu haki na nafasi ya wanawake kama kiungo muhimu cha kuleta maendeleo nchini. Kupitia kwa taarifa iliyokuwa kwenye gazeti waliokuwa wanasoma Kabi na Maimuna inadhihirika kuwa serikali ilikuwa imetambua umuhimu wa kuwahamasisha watu kuhusu suala la nafasi ya mwanamke katika jamii. Ndoa kati ya Maimuna na Kabi ambaye alikuwa na ulemavu wa mguu ni kielelezo kuwa ndoa inaweza kufanikiwa hata pale ambapo mhusika mmoja ana ulemavu. Kadhalika, kupitia kwa mhusika Kabi, Said Ahmed Mohamed anawasilisha ujumbe kwa wanajamii kuwa watu wenye ulemavu hawapaswi kudharauliwa au kudunishwa kwa sababu ya kuwa na ulemavu. Inabainika kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kuishi kama watu wengine wasio na ulemavu na kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kama wasemavyo Cieza na wengine (2018) ulemavu haupaswi kutumiwa kama kigezo cha kupima uwezo au ukamilifu wa mtu. Watu wenye ulemavu wana thamani sawa na binadamu mwingine yeyote na wanapaswa kuwezeshwa na kupewa nafasi ya kuishi maisha yao kama watu wengine katika jamii.

Katika sehemu inayofuata ulemavu wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kinyume na maumbile ya kawaida utashughulikiwa

### 4.4 Matumizi ya Ulemavu wa Ubongomaji kama Mtindo

Ulemavu wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa umeshughulikiwa katika sura hii kama mojawapo ya taswira za ulemavu wa viungo kwa kuwa kichwa ni kiungo mojawapo cha binadamu. Aidha, kama ilivyo katika ulemavu wa viungo vingine vya mwili ulemavu wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida unadhihirika kwa kuzingatia mwonekano wa mwathiriwa kimaumbile. Taswira ya ulemavu huu imejitokeza katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Anwani ya riwaya ya *Kichwamaji* inaashiria ulemavu wa kichwa. Ulemavu huu unaweza kuhusishwa na ulemavu wa kichwa wa watoto wa wahusika Manase na Kazimoto katika riwaya husika. Si kawaida kwa mwandishi kuzungumzia suala la ulemavu wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kwa kuwa ni suala linaloegemea zaidi kwenye mambo yanayohusu sayansi ya tiba. Hata hivyo, mwandishi ametumia ulemavu huu ambao si wa kawaida kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe mahsusi.

Kwa mujibu wa Johorey (2016), ugonjwa wa kuwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida unaitwa ubongomaji. Dalili za ugonjwa huu ni kuongezeka kwa maji ndani ya kichwa. Maji haya husababisha uvimbe katika ubongo na kumfanya mwathiriwa kuwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida. Kama anavyosema Johorey, ingawa ugonjwa huu unaweza kuwaathiri watu wote, unapatikana zaidi miongoni mwa watoto wadogo. Mtoto anaweza kuzaliwa akiwa na ugonjwa huu au akaupata baada ya kuzaliwa. Kulingana na Delgado na Higuera (2017), ubongomaji ni hali ambapo kichwa huwa kikubwa kutokana na kuzibwa kwa njia za kusafirisha maji katika

ubongo. Delgado na Higuera wanaendelea kusema kuwa neno ubongomaji kimsingi lina maana ya '*maji ubongoni.'* Watoto wa Manase na Kazimoto katika riwaya ya *Kichwamaji* wanadhihirisha dalili za kuathiriwa na ubongomaji. Ingawa kwa misingi ya tiba hali hii inaainishwa kama ugonjwa, utafiti huu umeiainisha kama ulemavu kwa kuwa inadhihirika katika kiungo cha binadamu, na pia kifasihi umechorwa kwa namna hiyo. Aidha, kama anavyodai McAllister (2012), asilimia sabini na nane ya watu walio na hali hii huathirika na upungufu wa neva jambo ambalo linaweza kusababisha ulemavu.

Katika riwaya ya *Kichwamaji,* mtoto wa Manase anasawiriwa kama mwenye ulemavu wa kichwa kwa kuwa alizaliwa akiwa na kichwa kikubwa kuliko mtoto wa kawaida. Kutokana na maumbile haya, watu walimchukulia kuwa mtoto wa ajabu ambaye hakuwa wa kawaida. Msimulizi (Kazimoto) anaeleza mambo aliyokuwa akiyasikia kuhusu mtoto wa Manase:

> Habari nilizosikia kuhusu yeye (Manase) ni kwamba mke wake alikuwa amekwishajifungua mtoto wa ajabu. Wale walioniambia habari hizi walikataa kunieleza sura ya mtoto huyo kwa kuogopa kwamba wakisemasema huenda wao pia wakazaa mtoto kama huyo. Jambo waliloniambia ni kwamba alikuwa akiishi kama watoto wengine. Alionekana mtu wa kawaida lakini sura yake ilikuwa ya kutisha sana. (Kezilahabi, 1974, uk. 137).

Katika sehemu hii, Kazimoto anaeleza kuhusu mabadiliko yaliyokuwa yametokea miongoni mwa jamaa na marafiki zake ambao hawakuwa wameonana kwa muda mrefu. Manase alikuwa mmoja wa marafiki hawa. Kazimoto anaeleza kuhusu habari alizokuwa amesikia kuhusu kujifungua kwa mke wa Manase. na maumbile ya ajabu ya mtoto huyo. Kauli kuwa mtoto wa Manase alikuwa wa ajabu na mwenye sura ya kutisha inaashiria kuwa maumbile yake hayakuwa ya kawaida na hivyo basi alikuwa na ulemavu ingawa waliokuwa wamemuona hawakutaka kutoa maelezo zaidi kuhusu sura yake kwa kuhofia kuwa wangezaa watoto wenye ulemavu kama huo.

Kwa mujibu wa Ogechi na Ruto (2002), katika jamii nyingi za Kiafrika, iliaminika kuwa kumcheka mtu mwenye ulemavu kungemfanya mtu kuzaa mtoto mwenye ulemavu au kuleta laana katika vizazi vya baadaye. Imani hii inadhihirika katika kisa hiki ambapo watu hawakutaka kusema mengi kuhusu ulemavu wa mtoto wa Manase kwa kuhofia kuwa wangezaa mtoto mwenye ulemavu. Kwa hivyo, Kazimoto hakupata maelezo kamili kumhusu mtoto huyo. Hata hivyo, Kazimoto alipata kukutana na mtoto wa Manase alipoenda kuwatembelea Manase na mke wake Salima nyumbani kwao. Mwandishi anachora taswira ya mtoto huyu ambaye kimaumbile hakuwa wa kawaida. Anaeleza:

> Tulinyamaza tena kwa muda. Wakati wote huu Salima alikuwa amenyamaza. Mara tulisikia kelele za watoto wadogo nje. Nilifikiri kwamba walikuwa wengi lakini watoto walioingia ndani ya nyumba walikuwa wawili tu. Mmoja nafikiri alikuwa mtoto wa jirani. Mara nilishangaa kumwona mtoto ambaye nilikuwa sijapata kumwona maisha yangu. Sikuweza kujizuia kuuliza kwa mshangao, " mtoto huyu mwenye kichwa kikubwa namna hii ni wa nani?" (Kezilahabi, 1974, uk. 191).

Baada ya kumuona mtoto wa Manase, msimulizi (Kazimoto) anasema kuwa hakuwahi kuona mtoto kama huyo maishani mwake. Anaonyesha mshangao mkuu kutokana na maumbile ya mtoto huyo. Swali alilowauliza Manase na Salima linadhihirisha mshangao wake Kazimoto: '*mtoto huyu mwenye kichwa kikubwa namna hii ni wa nani?'* Swali hili lilimuumiza roho Salima, mke wake Manase na mama wa mtoto husika. Jambo hili linajitokeza kwa kuwa pindi tu Kazimoto alipouliza swali hili, Salima alimsukumia mume wake chakula na kwenda zake katika chumba cha kulala ambako alisikika akilia, ishara kuwa alikuwa na uchungu mwingi moyoni.

Kupitia ulemavu wa ubongomaji mwandishi anawasilisha maudhui kuhusu ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu. Konzela (2013), alichunguza athari za ubaguzi wa

watu wenye ulemavu katika Bara la Afrika na kubaini kuwa ubaguzi wa watu wenye ulemavu unadhihirika kwa kiasi kikubwa katika bara hili. Aidha, anatambua kuwa ubaguzi wa watu wenye ulemavu na familia zao ni jambo lililokithiri Barani Afrika. Ubaguzi huu huwakwaza na kuwaumiza sana kihisia walioathiriwa pamoja na jamaa zao. Kwa mfano, kuondoka mezani kwa Salima na kujifungia chumbani baada ya Kazimoto kutaka kujua mtoto aliyekuwa na kichwa kikubwa alikuwa wa nani ni ishara kuwa Salima, ambaye alikuwa mama wa mtoto huyu alikwazwa na swali hili. Kadhalika, kilio chake kinaashiria uchungu aliokuwa nao kuhusu ulemavu uliomwathiri mtoto wake.

Ingawa uchungu wa Salima ulitokana na aibu ya kuwa na mtoto mwenye ulemavu, inabainika kuwa uchungu wake pia ulizidi zaidi kwa kufahamu chanzo cha ulemavu wa mwanawe. Kutokana na maelezo ya Manase, inabainika kuwa ulemavu wa mtoto huyu ulisababishwa na tabia ya Manase; mume wake Salima, na baba mzazi wa mtoto huyu. Manase anamwambia Kazimoto:

> Kazimoto umetonesha kidonda kikubwa cha mji huu. Hili ni janga ambalo mimi mwenyewe nilileta. Kazimoto, unamkumbuka yule msichana aitwaye Pili? Basi siku moja nilitembea naye. Wakati huo alikuwa amekwishapatwa na ugonjwa mbaya. Mimi bila kufahamu, usiku huo huo nilimwambukiza mke wangu. Kwa bahati mbaya mtoto aliumbika nyakati hizo za ugonjwa wangu. Wakati wa kuzaa ulipofika, tulimzaa mtoto huyu mwenye kichwa kikubwa ambaye ametushangaza. (Kezilahabi, 1974, uk. 191).

Manase anakiri kuwa ulemavu wa mtoto wake ulitokana na kutokuwa mwaminifu katika ndoa. Anamwambia Kazimoto kuwa alishiriki mapenzi na Pili ambaye tayari alikuwa na ugonjwa wa zinaa na kuambukizwa ugonjwa huo. Hatimaye alimwambukiza Salima mke wake, ugonjwa huo. Salima alishika mimba wakati huo na matokeo yake ni mtoto aliyekuwa na ulemavu wa kichwa.

Kwa mujibu wa Ogechi na Ruto (2002), katika jamii nyingi za Kiafrika inaaminika kuwa ukiukaji wa maadili miongoni mwa wanafamilia unaweza kusababisha ulemavu. Ulemavu unachukuliwa kama adhabu ya utovu wa nidhamu. Kadhalika, kama anavyodai Kisanji (1995), watu wengi katika nchi ya Tanzania wanaamini kuwa ulemavu wa kichwa unaweza kusababishwa na magonjwa ya zinaa. Kwa upande wa utafiti wa kimatibabu, kama anavyoeleza Nordqvist (2017), ugonjwa wa 'kichwamaji' unatokana na mambo mbalimbali kama vile uvimbe, maumivu ya kichwa, ugonjwa wa surua, matumbwitumbwi na kaswende. Kwa kuzingatia maoni haya, inabainika kuwa ulemavu wa mtoto wa Manase kama anavyodai yeye ulitokana na mambo mawili. Kwanza, Manase alikuwa amekiuka maadili ya jamii kwa kutokuwa mwaminifu katika ndoa. Pili, uzinifu wake ulimletea ugonjwa wa zinaa aliomwambukiza Salima mkewe na kumdhuru mtoto wao.

Mwandishi anatumia ulemavu wa mtoto wa Manase kama mtindo wa kuangazia kuhusu athari ya uzinzi miongoni mwa jamii, kwamba tabia hii inaweza kuleta maafa katika jamii na kuathiri hata vizazi vyao. Athari za ulemavu huu wa tabia katika jamii zinadhihirika zaidi inapobainika kuwa Kazimoto, licha ya kuwa na mke, yeye pia alikuwa ameshiriki ngono na Pili nje ya ndoa. Inabainika kuwa ugonjwa uliompata Manase ulikuwa umemwathiri Kazimoto pia. Kadhalika, Kazimoto alikuwa amemwambukiza mke wake Sabina. Inabainika kuwa Sabina alijifungua mtoto ambaye aliaga dunia punde tu baada ya kuzaliwa. Tukio hili linajitokeza katika maneno ya mhudumu wa hospitali:

> Kazimoto, mtoto wako amerudi. Hakuweza kuishi. Wakati wa kujifungua ulipofika daktari alikuwa akifanya upasuaji kwa mtu mwingine. Mke wako alipata shida ya kuweza kupitisha kichwa cha mtoto ambacho kilikuwa kikubwa kupita kiasi. Daktari alichelewa kufika. Alipokuja mtoto alizaliwa muda wa saa moja tu. Tulifanya tulivyoweza ili kuokoa maisha yake, lakini kwa kuwa hakuzaliwa ili apate kuishi, alirudi. (Kezilahabi, 1974, uk. 179).

Kazimoto alikuwa ameenda hospitalini kumjulia hali mke wake ambaye alikuwa ameenda kujifungua. Mhudumu anamweleza Kazimoto yaliyojiri wakati mke wake alikuwa akijifungua. Anamfahamisha kuwa mtoto wake aliaga dunia kwa kuwa mke wake alipata shida wakati wa kujifungua. Inabainika kuwa kichwa cha mtoto kilikuwa kikubwa kupita kiasi na hivyo basi hangeweza kupitia kwenye njia ya uzazi. Kauli ya mhudumu kuwa; *'mtoto alikuwa na kichwa kikubwa kupita kiasi;'* inachora taswira ya mtoto aliyekuwa na ulemavu.

Sabina, mke wake Kazimoto alifahamu kuwa Kazimoto alikuwa ameshiriki ngono na Pili. Kwa hivyo, aliposikia kuwa Manase aliambukizwa ugonjwa uliosababisha ulemavu wa mtoto wake na Pili, alizimia. Sabina alihusisha kifo cha mtoto wake na ugonjwa huu kwa kuwa alimpoteza kwa sababu ya kuwa na kichwa kikubwa kupita kiasi. Ulemavu huu ndiyo uliokuwa umemwathiri pia mtoto wa Manase na Salima, ishara kuwa asili yake ilikuwa ni maambukizi ya ugonjwa wa zinaa ambao Manase na Kazimoto walipata kutokana na uhusiano wao wa kimapenzi na Pili.

Kupitia taswira ya ulemavu wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida, uliowaathiri watoto hawa wa Kazimoto na Manase, mwandishi anaendeleza maudhui ya uzinzi na kutoaminiana katika ndoa. Matukio katika riwaya ya *Kichwamaji* yanaashiria kuwa tabia hii imekithiri katika jamii. Mwandishi analenga kuwahamasisha wanajamii kuhusu athari za magonjwa ya zinaa ambayo hayana tiba. Inaelekea kuwa ugonjwa walioambukizwa Manase na Kazimoto haungeweza kutibiwa kwa kuwa daktari aliyekuwa na ujuzi wa kuutibu alikuwa ameaga dunia. Aidha, vidonge vyote alivyokuwa navyo viliharibiwa kimakosa na watu waliosafisha nyumba ya daktari huyo. Inabainika kuwa Kazimoto alipotambua kuwa hangepata tiba, alikata tamaa na kujiua kwa kuhofia kuzaa kizazi kibaya.

Katika utafiti uliofanywa na Devlieger (1998) nchini Uganda kuhusu mwelekeo wa jamii kwa watoto walioathiriwa na ulemavu wa ubongomaji, ilibainika kuwa jamii nyingi Barani Afrika zinaamini kuwa ulemavu huu unatokana na ushirikina, laana, bahati mbaya, matumizi ya dawa za kupanga uzazi, adhabu kutoka kwa Mungu, imani za dini au hitilafu za kinasaba. Inaaminika kuwa ugonjwa huu hauna tiba na suluhu inapatikana tu iwapo laana itaondolewa ama iwapo Mungu atafanya miujiza. Mwandishi wa riwaya ya *Kichwamaji* anaashiria imani hii katika mazungumzo baina ya Manase na Kazimoto ambapo inabainika kuwa ugonjwa huu haukuwa na tiba kwa kuwa daktari mwenye ujuzi wa kutibu ugonjwa wa zinaa uliosababisha ugonjwa husika aliaga dunia.

> Bahati mbaya sana, Kazimoto, huyo daktari alikufa juma lililopita, na watu waliopelekwa kusafisha nyumba yake ili mwingine aingie walichoma vidonge vyote hivyo bila kufahamu. Sasa hapatikani tena daktari yeyote. (Kezilahabi, 1974, uk. 192).

Mazungumzo haya yalitokea wakati Kazimoto alipotaka kujuzwa zaidi kuhusu uwezekano wa kupata tiba ya maradhi aliyokuwa nayo.

Mwandishi analenga kuwasilisha mkinzano baina ya imani za kitamaduni na tiba ya kisasa kuhusu asili ya magonjwa mbalimbali yanayopatikana miongoni mwa jamii. Kama wanavyosema Mac-Donald na Butera (2010), ufahamu wa mielekeo na miktadha ya kijamii na kitamaduni ni muhimu katika kuelewa jinsi ulemavu unavyosawiriwa katika jamii. Ingawa wengi wanaamini kwamba ulemavu unaweza kusababishwa na hitilafu za kinasaba, ushirikina, ukiukaji wa miiko, adhabu kutoka kwa Mungu au mapenzi ya Mungu, mwandishi wa riwaya ya *Kichwamaji* anadhamiria kuwasilisha ujumbe kuwa magonjwa ya zinaa yanayosababishwa na ukosefu wa maadili yanaweza kuwa chanzo cha ulemavu. Kwa hivyo wanajamii wanapaswa kujiepusha na uzinzi na tabia zinazokiuka maadili.

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii taswira ya ulemavu wa viungo imezingatiwa. Kadhalika, nafasi ya taswira ya ulemavu wa viungo kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule imeshughulikiwa. Kati ya riwaya teule sita zinazojumlishwa katika utafiti huu ni riwaya nne ambazo zimedhihirisha matumizi ya ulemavu wa viungo kama mtindo. Riwaya hizi ni: *Utengano*, *Kichwamaji*, *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo*.

Ulemavu wa viungo ambao umejitokeza katika riwaya hizi ni ulemavu wa viungo vya uzazi, ulemavu wa mguu na ulemavu wa kichwa. Katika sura hii, imebainika kuwa waandishi wametumia ulemavu huu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali. Maudhui haya ni kama vile: nafasi ya mwanamke katika jamii, dhuluma dhidi ya mwanamke, mila na desturi za jamii, mabadiliko na mwelekeo wa jamii kuhusu watu wenye ulemavu. Kadhalika, uozo wa kimaadili uliokithiri katika jamii na athari zake ni ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa taswira ya ulemavu wa viungo. Katika sura ifuatayo tutashughulikia muhtasari, matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya taswira za ulemavu kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Riwaya za Said Ahmed Mohamed zilizochunguzwa ni: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980) na *Tata za Asumini* (1990). Riwaya za Kezilahabi zilizochanganuliwa katika utafiti huu ni *Rosa Mistika* (1976), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Kichwamaji* (1974). Taswira za ulemavu zilizochunguzwa ni ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo. Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

i. Kubainisha namna taswira za ulemavu wa akili zilivyotumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase. Kezilahabi.
ii. Kupambanua namna ambavyo taswira za ulemavu wa tabia zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.
iii. Kuchunguza jinsi ambavyo taswira za ulemavu wa viungo zimetumiwa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi.

Ili kutimiza malengo haya, utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya mtindo na nadharia ya semiotiki. Mihimili ya nadharia ya mtindo ilimwezesha mtafiti kutambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika riwaya teule. Kwa kuwa nadharia ya mtindo haingeweza kumwongoza mtafiti katika kutambua ishara za ulemavu zinazowakilisha maana, nadharia ya semiotiki ilitumiwa ili kumwongoza mtafiti katika kutambua maana iliyowakilishwa na taswira za ulemavu na hivyo basi

kumwezesha kutambua maudhui yaliyowasilishwa na taswira hizi. Mihimili ya nadharia ya semiotiki ilimwongoza mtafiti kutambua maana mbalimbali zinazoashiriwa na waandishi kupitia kwa taswira za ulemavu, na hivyo basi kubaini ujumbe uliowasilishwa katika riwaya teule. Kadhalika, nadharia ya semiotiki ilimwongoza mtafiti kubaini mazingira ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyochangia katika uteuzi wa mtindo husika. Katika sehemu inayofuata muhtasari wa matokeo ya utafiti huu utatolewa kwa kuzingatia sura za tasnifu.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ndiyo msingi wa tasnifu yote. Katika sura hii utangulizi wa mada na usuli wake umeshughulikiwa. Dhana ya ulemavu imeelezwa kulingana na namna inavyofasiriwa katika jamii, tamaduni na miktadha mbalimbali. Kwa kuwa dhana ya ulemavu ni pana mno, sehemu ya utangulizi inaweka wazi mtazamo wa ulemavu ulioshirikishwa katika utafiti huu. Katika sehemu ya utangulizi inabainika kuwa utafiti huu umeshughulikia ulemavu jinsi tatu; ya ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo.

Katika sura ya kwanza suala la utafiti limeshughulikiwa. Utafiti huu ulichunguza namna ambavyo taswira za ulemavu zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Umuhimu wa utafiti huu umeshughulikiwa pia katika sura ya kwanza. Aidha, mbinu za utafiti zikiwemo zile za ukusanyaji data na uchanganuzi wa data zimeshughulikiwa. Nadharia zinazoongoza utafiti huu na mihimili yake zimechanganuliwa katika sura ya kwanza. Kadhalika, tafiti zingine zinazohusiana na mada ya utafiti huu, matokeo yake na yale yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti yameshughulikiwa katika sura ya kwanza.

Katika sura ya pili matumizi ya taswira za ulemavu wa akili kama mtindo wa mwandishi yamechanganuliwa kwa kuzingatia riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizi ni *Dunia Mti Mkavu*, *Tata za Asumini*, na *Rosa Mistika*. Kati ya riwaya sita zilizochunguzwa katika utafiti huu, riwaya hizi tatu ndizo zinazodhihirisha matumizi ya taswira ya ulemavu wa akili kama mtindo. Katika riwaya hizi wahusika ambao wanadhihirisha sifa za ulemavu wa akili wamechanganuliwa kwa kuzingatia namna ambavyo wametumiwa na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kuwasilisha jumbe zao. Katika sura hii imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametumia taswira ya ulemavu wa akili kama mtindo wa kuwasilisha jumbe mahsusi. Katika sura hii imebainika kuwa taswira za ulemavu wa akili zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui ya dhuluma na unyanyasaji, malezi na maadili.

Sura ya tatu imeshughulikia taswira ya ulemavu wa tabia na namna ambavyo taswira hizi zimetumiwa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali katika riwaya teule. Wahusika wanaodhihirisha ulemavu wa tabia wamechanganuliwa kwa kuzingatia tabia, mienendo, maneno na matendo yao yanayokiuka maadili kwa mujibu wa matarajio ya jamii zao. Katika sura hii imebainika kuwa ulemavu wa tabia umetumika na Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi kama mtindo wa kukuza maudhui. Maudhui yaliyowasilishwa kupitia kwa ulemavu wa tabia yamejadiliwa. Ulemavu wa tabia ambapo mtu hujidhuru mwenyewe, ulemavu wa tabia unaoiathiri jamii kwa jumla na ulemavu wa tabia unaohusu suala la mahusiano ya ngono umedhihirika katika riwaya teule. Ulemavu wa tabia unaashiria uozo uliokithiri katika jamii na kusambaratika kwa misingi ya kijamii inayoongoza uadilifu miongoni mwa wanajamii kwa jumla. Inabainika kuwa kuzorota kwa maadili kwa

kiasi fulani kumetokana na athari za utamaduni, mila na desturi za kigeni ambazo zinawaathiri Waafrika.

Katika sura ya nne, taswira za ulemavu wa viungo na matumizi yake kama mtindo katika riwaya teule zimechanganuliwa. Wahusika wenye ulemavu wa viungo mbalimbali wamejitokeza katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Wahusika hawa wamezingatiwa kwa mujibu wa matumizi ya ulemavu wao kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali. Kadhalika, maudhui mbalimbali yaliyowasilishwa kupitia kwa taswira ya ulemavu wa viungo yamejadiliwa kwa kuzingatia mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yanayozunguka jamii husika. Riwaya ambazo zinadhihirisha matumizi ya ulemavu wa viungo kama mtindo kati ya riwaya sita zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ni: *Utengano*, *Kichwamaji*, *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Ulemavu wa viungo ambao umejitokeza katika riwaya hizi teule ni ulemavu wa viungo vya uzazi, ulemavu wa miguu na ulemavu wa kuwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida. Maudhui yanayowasilishwa kupitia kwa taswira za ulemavu wa viungo ni kama vile: nafasi ya mwanamke katika jamii, dhuluma dhidi ya mwanamke, mila na desturi za jamii, mabadiliko na mwelekeo wa jamii kuhusu watu wenye ulemavu. Kadhalika, uozo wa kimaadili uliokithiri katika jamii na athari zake ni ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa taswira ya ulemavu wa viungo.

Sura hii ya tano imeshughulikia muhtasari, matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti huu. Katika sura hii masuala yanayoshughulikiwa na kila sura yamefafanuliwa kwa muhtasari. Aidha matokeo na mapendekezo ya utafiti yameelezwa. Kadhalika, ni katika sura hii ambapo utafiti unahitimishwa.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wameshirikisha aina tatu za taswira za ulemavu katika riwaya teule zilizoshughulikiwa katika uchunguzi huu. Taswira hizi ni za ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo. Utafiti huu umethibitisha kuwa taswira za ulemavu zimetumiwa na waandishi hawa kama mtindo wa kuwasilisha maudhui. Katika riwaya hizi taswira za ulemavu wa akili, ulemavu wa tabia na ulemavu wa viungo zimedhihirika kupitia kwa wahusika mbalimbali. Kadhalika, imebainika kuwa maudhui yaliyowasilishwa kupitia kwa taswira hizi yanafungamana na mazingira ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Katika utafiti huu imebainika kuwa taswira za ulemavu wa akili zinajitokeza katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika*. Katika uchanganuzi wa riwaya hizi, imebainika kuwa taswira za ulemavu wa akili zimetumiwa na waandishi kwa lengo la kuwasilisha ujumbe mahsusi katika kazi zao. Wahusika wanaoibua taswira za kulemaa akili ni: Mzee Gae, Asumini na Rosa. Wahusika hawa wanadhihirisha ulemavu huu kupitia kwa matendo, maneno na tabia zinazoonekana na wanajamii kuwa si za kawaida kwa mujibu wa matarajio ya wanajamii. Katika sura hii imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametumia taswira za ulemavu wa akili kama mtindo kwa sababu za hali za kisiasa na kijamii zilizowazunguka. Kwa mfano, imebainika kuwa mfumo wa ubepari na unyanyasaji uliokuwapo Kisiwani Zanzibar kabla ya mapinduzi ya mwaka wa 1964 uliathiri kwa kiasi kikubwa matumizi ya taswira ya ulemavu wa akili kama mtindo katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Mwandishi ulemavu wa akili kama mtindo wa kuwahamasisha wanajamii na kuwazindua ili wapiganie haki na usawa.

Katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, ulemavu wa akili wa Mzee Gae umetumiwa na mwandishi kama mbinu ya kuwasilisha maudhui ya dhuluma na unyanyasaji. Mzee Gae ametumiwa kama mhusika anayewazindua wanajamii kuhusu hali ya dhuluma na unyanyasaji inayowazunguka. Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* imejikita katika matukio yaliyotokea katika kisiwa cha Zanzibar ambapo Waarabu walikuwa wanawadhulumu wenyeji. Imebainika kuwa tabia na maneno ya kiwazimu ya Mzee Gae yanalenga kuwafikirisha wanajamii ili watambue uhalisi uliowazunguka. Licha ya kuwa wanajamii walimchukulia kama mtu mwenye ulemavu wa akili asiyekijua alichosema au kufanya, katika utafiti huu inabainika kuwa mwishowe Mzee Gae alifanikiwa katika azimio lake la kubadili mtazamo wa wanajamii kwa kuwa walichukua hatua ya kuleta mabadiliko kwa kupigania haki yao. Said Ahmed Mohamed ametumia taswira ya ulemavu wa akili wa Mzee Gae kama jazanda ya kuwasilisha ujumbe kwa nia ya kuwaathiri wanajamii kwa namna ya kipekee. Watu waliokuwa na nguvu za kiuchumi, kijamii na kisiasa waliwadhulumu wengine na kuwatesa kila walipojaribu kutetea haki yao, hivyo basi mwandishi ametumia taswira ya ulemavu wa akili wa Mzee Gae kwa lengo la kuyaweka wazi masuala haya bila kuhatarisha maisha yake. Hii ni kwa sababu kama alivyodai Mzee Gae, mtu yeyote aliyethubutu kusema ukweli kuhusu hali ya dhuluma iliyokithiri katika jamii alikamatwa na kufungwa jela.

Kadhalika, katika utafiti huu imebainika kuwa katika riwaya za *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika*, maudhui ya malezi yamewasilishwa kupitia kwa ulemavu wa akili wa wahusika Asumini na Rosa. Kupitia kwa wahusika hawa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametathmini nafasi ya asasi mbalimbali katika malezi ya mtu binafsi na namna ambavyo malezi yanawaathiri watoto hasa wa jinsia ya kike. Katika utafiti huu imebainika kuwa wazazi wa Asumini na baba yake Rosa walikuwa wanatumia mbinu ya malezi ya kimabavu na hawakuwapa binti zao uhuru wowote wa

kujiamulia mambo kuhusu mienendo na tabia zao. Kutokana na malezi haya inabainika kuwa Asumini alivurugika akili kutokana na mkinzano wa mawaidha aliyopewa na wazazi wake alipokuwa mtoto na maisha halisi aliyopatana nayo baada ya kujiunga na chuo kikuu. Kadhalika, Asumini alipatwa na mfadhaiko kutokana na hamu yake kuu ya kupata uhuru hasa kuhusu maamuzi ya mahusiano kati yake na wanaume.

Aidha, maudhui ya malezi na uhusiano wake na uozo uliokithiri katika jamii yamejitokeza kupitia kwa taswira ya ulemavu wa akili katika riwaya teule za *Rosa Mistika* na *Tata za Asumini*. Kwa mfano, mhusika Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* anaonekana na wenzake kama mtu mwenye ulemavu wa akili kutokana na tabia yake ya kushiriki ngono kiholela, tabia ambayo ilitokana na malezi aliyopewa na wazazi wake, hasa baba yake. Matatizo yaliyotokana na mahusiano yake na wanaume ndiyo yaliyomfanya Rosa kuamua kujitia kitanzi. Uamuzi huu unaashiria hali ya mtu aliyekuwa na tatizo la akili. Kwa upande mwingine, tabia ya Asumini inaashiria hali ambapo anajaribu kuitakasa jamii kutokana na uozo wa kimaaadili uliokithiri katika jamii. Imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed ametumia ulemavu wa akili wa Asumini kuweka wazi suala la uozo wa kimaadili hasa uzinzi na unafiki unaotawala miongoni mwa wanajamii. Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wanatumia ulemavu wa akili wa Asumini na Rosa kwa lengo la kuwafikirisha wanajamii kuhusu umuhimu wa malezi bora katika kukuza vijana walio na maadili na mienendo mizuri. Aidha, wanatoa onyo kwa wazazi wawe makini wanapowalea watoto wao kwa kuwa baadhi ya mbinu na mitindo ya malezi, hasa ya kimabavu, inaweza kuwa chanzo cha ulemavu wa akili miongoni mwa vijana na huenda ikasababisha upotovu wa kimaadili.

Utafiti huu umebainisha kuwa taswira za ulemavu wa tabia zimetumika kama mtindo katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizi ni *Dunia Mti Mkavu*, *Tata za Asumini*, *Utengano*, *Kichwamaji*, *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Kupitia uchambuzi wa data imebainika kuwa Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametumia ulemavu wa tabia kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mahsusi katika kazi zao. Kadhalika, imebainika kuwa ulemavu huu unachukua mikondo mitatu. Kuna ulemavu wa tabia ambapo mtu hujidhuru mwenyewe, kuna ulemavu wa tabia unaoiathiri jamii kwa jumla na kuna ulemavu wa tabia unaohusu swala la mahusiano ya ngono. Ulemavu wa tabia umedhihirika katika wahusika mbalimbali kupitia kwa tabia na mienendo yao, maneno, mawazo na matendo yao. Aidha, mambo yanayosemwa na wahusika wengine na maelezo ya mwandishi kuwahusu yamezingatiwa kama kigezo cha kuainisha ulemavu wa tabia wa wahusika mbalimbali. Imebainika kuwa ulemavu wa tabia wa kujidhuru unajitokeza kupitia wahusika ambao wana taathira ya pombe. Imethibitishwa kuwa wahusika mbalimbali wameathiriwa na ulemavu wa unywaji pombe kupindukia kwa namna mbalimbali. Athari hizi ni kama vile kutowajibika kazini, kuachishwa kazi, kuzorota kwa afya, mikinzano ya ndoa, madeni, wizi na vifo. Kadhalika, imebainika kuwa kuna sababu mbalimbali zinazowasukuma wahusika kujiingiza katika tabia ya unywaji pombe kupindukia. Ingawa kuna watu wanaojiingiza katika tabia hii ili kujistarehesha, imedhihirika kuwa kuna wanajamii wanaotumia pombe kama kiliwazo kutokana na huzuni, umaskini, majuto na dhuluma inayowakumba maishani. Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi wametumia ulemavu wa tabia wa unywaji pombe kupindukia ili kuwasilisha maudhui ya dhuluma, utamaushi, maisha ya ndoa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, umaskini na malezi. Matumizi ya pombe kiasi cha kumwathiri mtu ni ishara ambayo imetumiwa na waandishi husika kuashiria

matatizo mbalimbali yanayowakumba wanajamii na kwa hivyo tabia hii inapaswa kukabiliwa kwa kushirikisha mbinu mwafaka zaidi zinazohusisha utaalamu wa kimatibabu na kijamii.

Katika utafiti huu imebainika kuwa matumizi ya mihadarati ni ulemavu wa tabia unaotumika kama mtindo katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*. Katika riwaya hii, Said Ahmed Mohamed ametumia taswira ya  ulemavu wa tabia wa matumizi ya mihadarati kama mtindo wa kuwasilisha maudhui kuhusu athari mbalimbali za matumizi ya mihadarati. Matumizi ya mihadarati kama vile marijuana na hashishi yamejitokeza katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* kupitia kwa mhusika Haji. Athari za matumizi ya mihadarati ni: kukosa heshima, kudhoofika kiafya, uchafu na ghasia. Aidha, imebainika kuwa mwandishi Said Ahmed Mohamed ametumia ulemavu wa tabia wa matumizi ya mihadarati kama mtindo wa kuwasilisha maudhui kuhusu malezi, athari za watu kuhama kutoka vijijini hadi mijini, uhaba wa mahitaji ya kimsingi miongoni mwa watu wanaoishi mijini, ukosefu wa ajira na dhuluma. Mwandishi anawahamasisha wasomaji wake kuhusu umuhimu wa kutambua kiini cha tabia ya matumizi ya dawa za kulevya. Utambuzi huu utawawezesha kutafuta suluhisho mwafaka badala ya kuwalaumu na kuwatenga watu walioathirika.

Tabia ya mtu kufanya uamuzi wa kujiua ni ulemavu wa tabia wa kujidhuru unaodhihirika katika riwaya teule zilizochambuliwa katika utafiti huu. Utafiti huu, umebainisha kuwa tabia ya kujiua inasababishwa na kufadhaika kwa wahusika kutokana na malezi waliyoyapata, majuto na kukata tamaa. Wahusika hawa wanaathiriwa na ulemavu wa akili na hatimaye wanaamua kujitoa uhai. Waandishi wa riwaya teule zilizochanganuliwa katika utafiti huu wametumia ulemavu wa tabia ya kujiua kuwasilisha maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii ambapo mwanamke

anachukuliwa na mwanamume kama chombo cha starehe na hivyo basi kuvunjiwa heshima hasa katika uhusiano wa kimapenzi. Ubikira unasisitizwa sana miongoni mwa wanawake kiasi kwamba unatumiwa kama kigezo cha kupima thamani yake. Kwa mfano, Rosa katika riwaya ya *Rosa Mistika* anajiua baada ya kuachwa na mpenzi wake kwa madai kuwa hakuwa bikira. Hata hivyo, jamii haizingatii sifa ya ubikira kwa upande wa mwanamume na thamani yake haipungui machoni mwa jamii hata akishiriki ngono na wanawake wengi.

Katika utafiti huu taswira za ulemavu wa tabia unaojikita kwenye suala la ngono zimedhihirika. Imebainika kuwa kuna wahusika ambao wamezorota kimaadili kwa kuwa wanashiriki katika vitendo vya ngono vinavyokiuka kanuni zilizokubalika miongoni mwa jamii kuhusu mahusiano ya ngono. Ubakaji, umalaya, uzinzi kutoaminiana katika ndoa ni tabia ambazo zimejitokeza katika riwaya teule. Waandishi wametumia ulemavu wa tabia unaohusu ngono kudhihirisha namna ambavyo jamii imezorota kimaadili. Kuzorota kwa maadili katika jamii kwa kiasi fulani kumefungamanishwa na athari za utamaduni wa kigeni. Mbali na hayo, ulemavu wa tabia unaohusu ngono umetumiwa kama mtindo wa kuangazia nafasi ya mwanamke katika jamii ambapo mwanamke anasawiriwa kama kiumbe anayedhalilishwa, kudhulumiwa na kuchukuliwa na mwanamume kama kifaa cha starehe. Matatizo yanayomkumba mwanamke katika jamii inayotawaliwa na jinsia ya kiume yamedhihirishwa katika sura hii. Kadhalika, imebainika kuwa ulemavu unaohusiana na ngono unajikita kwenye mazingira, tamaduni na malezi ya mtu binafsi. Hivyo basi ulemavu huu umetumiwa na waandishi ili kuihamasisha jamii kuhusu haja ya kuwa waangalifu wanapowalea watoto kwa kuwa kuna mbinu za malezi zinazochangia katika kumlemaza mtoto kitabia.

Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa taswira za ulemavu wa viungo zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi. Kati ya riwaya teule sita zinazojumlishwa katika utafiti huu ni riwaya nne ambazo zimedhihirisha matumizi ya ulemavu wa viungo kama mtindo. Riwaya hizi ni: *Utengano, Kichwamaji*, *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo*.

Ulemavu wa viungo ambao umejitokeza katika riwaya hizi teule ni ulemavu wa viungo vya uzazi, ulemavu wa miguu na ulemavu wa kuwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida. Katika utafiti huu imebainika kuwa waandishi wametumia ulemavu wa viungo mbalimbali kama mtindo wa kuwasilisha maudhui tofauti. Maudhui haya ni kama vile: nafasi ya mwanamke katika jamii, dhuluma dhidi ya mwanamke, mila na desturi za jamii, mabadiliko na mwelekeo wa jamii kuhusu watu wenye ulemavu. Kadhalika, uozo wa kimaadili uliokithiri katika jamii na athari zake ni ujumbe muhimu unaowasilishwa kupitia kwa taswira ya ulemavu wa viungo.

Kwa kuzingatia taswira ya ulemavu wa viungo vya uzazi unaosawiriwa kupitia kwa mhusika Kapinga katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na mhusika Bigeyo katika riwaya ya *Rosa Mistika*, inabainika kuwa imani za kitamaduni zinatawala mielekeo ya jamii kuhusu ulemavu huu. Jambo hili linadhihirika kwa kuwa wahusika hawa wanaamini kuwa ulemavu huu unasababishwa na laana. Kwa hivyo, wanatafuta usaidizi kutoka kwa waganga wa kienyeji ambao inaaminika wana uwezo wa kutibu ulemavu husika. Hata hivyo, inabainika kuwa waganga hawa wanawatapeli tu kwa kuwa suluhisho halipatikani. Ingawa Kapinga alisemekana kuwa alipata tiba kutoka kwa mganga wa kienyeji inabainika kuwa watu bado walimshuku na kudai kuwa alisaidiwa na ndugu yake kumtia mimba mke wake. Bigeyo na mume wake Ndalu licha ya kuwatembelea waganga wengi na kutumia hela nyingi hawakufanikiwa kupata mtoto. Aidha, inadhihirika kuwa jitihada za kutafuta tiba ya ugumba na utasa

zinatokana kwa kiasi kikubwa na mwelekeo wa watu kuhusu watu wenye ulemavu huu. Jamii inawadharau na kuwabeza watu ambao hawana uwezo wa kupata mtoto. Kwa kumchora mwanamume mwenye ulemavu wa viungo vya uzazi, Kezilahabi anawasilisha ujumbe kuhusu mwelekeo wa jamii kuwa mara nyingi mtoto anapokosekana katika ndoa, anayelaumiwa ni mwanamke. Mwandishi anawasilisha ujumbe kuwa imani hii haifai kwa kuwa wanaume wanaweza kuathirika na ulemavu huu na si haki kwa mwanamke kulaumiwa kila wakati.

Taswira ya ulemavu wa mguu imejitokeza kupitia kwa wahusika Maksuudi, Mabruki na Kabi katika riwaya ya *Utengano*. Katika utafiti huu, imebainika kuwa ulemavu wa viungo wa Maksuudi na Mabruki ulitokana na mabadiliko katika umri wao. Ulemavu wa Maksuudi umetumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe kuhusu namna ambavyo Maksuudi alivyokuwa amebadilika baada ya kufungwa jela kwa tuhuma za ufisadi. Inabainika kuwa Maksuudi alibadilisha mtazamo wake kuhusu maisha na kujuta kwa dhuluma aliyokuwa ameitendea familia na nchi yake. Ulemavu wa Maksuudi ulimfanya kuwa mtegemezi kwa kuwa alishindwa kujifanyia hata mambo madogo. Ulemavu wa mguu uliomwathiri Kabi umetumiwa na mwandishi kuashiria mabadiliko yaliyotokea kwa Maimuna. Maimuna alikuwa kahaba na mlevi lakini alipokutana na Kabi aliyekuwa na huruma na utu alibadilisha mtazamo wake kuhusu maisha. Ulemavu wa Kabi unatumiwa na mwandishi kudhihirisha kuwa watu wenye ulemavu si wategemezi; wana uwezo wa kujitafutia riziki na hata kuwa na familia zao kama wanajamii wengine. Kadhalika, kupitia kwa ulemavu wa Kabi mwandishi ameangazia kuhusu dhuluma na unyanyasaji wa wanawake. Inabainika kuwa ulemavu wa Kabi ulitokana na ajali ya barabarani iliyotokea alipokuwa akimhangaikia mama yake aliyekuwa mlevi na mwenye ulemavu wa akili. Ulevi wa mama yake Kabi

ulitokana na dhuluma aliyopata kutoka kwa mumewe aliyemnyang'anya mali na hatimaye kumtaliki.

Katika utafiti huu ulemavu mwingine ambao umejitokeza ni wa mtoto kuzaliwa akiwa na kichwa kikubwa kuliko kawaida. Inabainika kuwa watoto wa Manase na Kazimoto walizaliwa na ulemavu wa kuwa na kichwa kikubwa kuliko watoto wa kawaida. Mwandishi anaashiria kuwa ulemavu wa watoto hawa ulisababishwa na uzinzi. Manase na Kazimoto walikuwa wameshiriki ngono na Pili, msichana ambaye alikuwa na ugonjwa wa zinaa. Kwa kuwa walikuwa wameoa, waliwaambukiza wake zao na ndiyo maana walizaa watoto waliokuwa na vichwa vikubwa kuliko kawaida. Mwandishi anatumia ulemavu huu kutoa tahadhari kwa wanajamii dhidi ya tabia ya uzinzi. Kadhalika, anazungumzia kuhusu suala la magonjwa ya zinaa ambayo hayana tiba na umuhimu wa wanajamii kujiepusha na tabia ya uzinzi ili wasiambukizwe magonjwa haya.

## 5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umeshughulikia riwaya za waandishi teule walioshirikishwa katika uchunguzi huu pekee. Hata hivyo waandishi hawa wameandika kazi zingine za fasihi kama: tamthilia, mashairi na hadithi fupi ambapo wameshirikisha matumizi ya taswira mbalimbali kama mtindo. Kwa hivyo kuna haja ya uchunguzi zaidi kufanywa ili kubainisha namna taswira mbalimbali zimetumika kama mtindo wa kuwasilisha maudhui mbalimbali katika tanzu hizi. Kadhalika, inapendekezwa kuwa utafiti utakaohusisha waandishi wengine bali na wale waliochunguzwa katika utafiti huu ufanywe ili kubainisha iwapo kuna matumizi ya ulemavu kama mtindo wa kuwasilisha maudhui katika kazi zao.

Utafiti huu umeongozwa na mihimili ya nadharia ya mtindo na nadharia ya semiotiki katika uchanganuzi wa riwaya teule. Kwa hivyo, kuna haja ya kuchunguza riwaya na tanzu zingine za fasihi kwa kutumia nadharia tofauti ili kuibua mitazamo mipya ya kuhakiki kazi zingine za fasihi.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, imebainika kuwa fasihi hufungamana na mazingira yanayoizunguka jamii. Riwaya zilizoshughulikiwa katika utafiti huu zilichapishwa katika miaka ya sabini, themanini na tisini. Kwa hivyo kuna haja ya kuchunguza kazi zingine za fasihi zilizochapishwa katika miaka ya baadaye ili kubainisha iwapo taswira za ulemavu zimetumika kama mtindo katika kazi hizo kwa kuwa mazingira yake ni tofauti na ya kazi zilizochunguzwa hapa.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kuzingatia vipengele vingine vya fasihi kama vile wahusika na maudhui. Kwa kuwa utafiti huu ulishirikisha aina tatu tu za ulemavu na matumizi yake kimtindo, tafiti zingine zinaweza kufanywa kwa kuzingatia taswira za ulemavu wa aina tofauti. Kadhalika, inapendekezwa kuwa utafiti zaidi ufanywe ili kubainisha iwapo kuna vipengele vingine vya kimtindo zaidi ya matumizi ya ulemavu ambavyo vinajitokeza katika riwaya teule zilizochambuliwa .

Kama anavyosema Bakhtin (1981), kabla ya karne ya ishirini, matatizo yanayohusiana na mtindo wa riwaya hayakuwa yamebainishwa. Ubainishaji ungewezekana iwapo kungekuwa na utambuzi mwafaka wa upekee wa mbinu za kimtindo za riwaya. Utafiti huu umedhihirisha kuwa kuna mbinu zaidi na za kipekee mbali na zile zinazohusiana moja kwa moja na tamathali za lugha, ambazo watunzi wa riwaya wanatumia katika uwasilishaji wa ujumbe wao. Hivyo basi inapendekezwa kuwa wahakiki wa kazi ya fasihi wazingatie zaidi vipengele ambavyo havijitokezi moja kwa moja na ambavyo vimezoeleka zaidi wanapohakiki kazi ya fasihi.

### 5.4 Mchango wa Utafiti

Kitaaluma, utafiti huu umetoa mchango wa mawazo mapya kuhusu matumizi ya ulemavu katika kazi ya fasihi kwa lengo la kuihamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali. Aidha ni msingi muhimu wa kuangazia mwelekeo tofauti wa uhakiki wa suala la ulemavu tofauti na tafiti nyingi ambazo zimezingatia upungufu na haki za watu wenye ulemavu. Utafiti huu umedhihirisha kuwa kuna mbinu zaidi na za kipekee zinazotumika kama mtindo katika kazi za fasihi bali na zile zinazohusiana moja kwa moja na tamathali za lugha; na hivyo basi kuchochea uchunguzi zaidi.

Utafiti huu utawafaa watu wengi katika kutambua matatizo mbalimbali yanayoathiri jamii na kiini cha matatizo haya. Kwa mfano, kupitia utafiti huu walezi watatambua kuwa kuna uhusiano kati ya mbinu za malezi na ulemavu wa akili na wa tabia. Maarifa haya yatawapa mwongozo ufaao katika malezi ya watoto wao hasa vijana. Kwa kuwa utafiti huu umejadili suala la uozo kwa kuzingatia chanzo na athari zake, utawafaa wanajamii katika kukabiliana na kuzorota kwa maadili. Kadhalika, utafiti huu ni hatua muhimu katika kuwazindua wanajamii kuhusu nafasi ya watu wenye ulemavu. Uchunguzi huu utawawezesha wanajamii kutambua kuwa licha ya ulemavu, waathiriwa wanaweza kushiriki katika shughuli mbalimbali ili kujikimu wao wenyewe na kuendeleza jamii kwa jumla.

## MAREJELEO


Acquaviva, G. (2004). Jazanda ya Njozi katika Baadhi ya Mashairi ya Euphrase Kezilahabi, katika *Swahili Forum, 11, 69-73*

Alayi, Z. (2013). Relationship Between Parentng Styles and Mental Disorder of Teenage Girls, in Tehran, in *European Psychiatry*, *28*.Tehran: Elzevier.

Allen, E. S., et al (2008). Premarital Precursors of Marital Infidelity, in *Family Process,47 (2),* 243-259. Wiley Online Library

Allerton, D. J. (1987). The Linguistic and Sociolinguistic Status of Proper Names, in *Journalof Pragmatics, 11*, 61-92.

Bakhtin, M. M. (1981). "Epic and Novel," in Holoquist, M. (Ed), *Dialogic Imagination*, 3-40. UTP: Austin.

Baloyi, E. (2010). An African View of Women as Sexual Objects as a Concern for Gender Equality: A Critical Study, in *Verbum et Ecclesia*, *31(1).*

Barber, B. K. et al (2005). Patterns of Parenting Across Adolescence, in *Changing Boundaries of Parental Authority During Adolescence, 2005 (108),* 5-16. John Wiley and Sons, Inc.

Barnes, C. (1992). *Disability Imagery and the Media: An Exploration of the Principles for Media Representations of Disabled People.* Halifax: Ryburn Publishing.

Barrett, L. (1997). *The Rastafarians*. Boston: Beacon Press.

Barthes, R. (1977). *Elements of Semiology*. New York:Hill & Wang

Barton, E.L. (2001). Textual Practices of Erasure: Representation of Disability and the Founding of the United Way, in Wilson, C. J and Lewieck, C. (Eds.), *Embodied Rhetorics*: *Disability in Language and Culture*. Edwardsville: Southern Illinois University Press.

Baumrind, D. (1975). The Contributions of the Family to the Development of Competence in Children, in *Schizophrenia Bulletin*, *1 (14)*, 12-37.

Bennet, A. & Royale, N. (1999). *Introduction to Literature, Criticism and Theory*. (2nd ed) England: Prentice Hall.

Benston, M. (1989). Feminism and the Critique of Scientific Method, in Miles, A. na Finn, G. (Eds.); *Feminism from Pressure to Politics;* 57-76. Montreal: Black Rose Books.

Beachamp, M. & Chung, N. (2010). Disabled Individuals in American Literature: Reflecting Culture(s). *Review of Disability Studies*: *An International Journal, 6 (10).*

Beresford, P.et al (2007). *Palliative Care, Socal Work and Service Users: Making Possible.* London: Jessica Kingsley.

Berger, A. (2004). *Semiotic Analysis*. Stuart Hall: SAGE Publications Limited.

Berube, M. (2005). " Disability and Narrative," in *PMLA, 120 (2),*567-576. Purdue University. Retrieved from: https://ow/purdue-edu.

Bertocini-Zubkhova, E. (1989). *Outline of SwahiliLiterature*. Berlin: Leiden.

Biklen, D. & Bogdan, R. (1977). Media Portrayals of Disabled People: A study in Stereotypes, in *Interracial Books for Children Bulletin*, *8 (6-7),* 4-9.

Blackstone, M. A. (2003). Gender Roles and Society, in Julia, R.M. et al (Eds.) *Human Ecology:An Encyclopedia of Children, Families, Communities and Environments*; 335-338. Santa Barbara: California.

Bogdan, R. et al (2012). *Picturing Disability. Beggar, Freak, Citizen, and other Photographic Rhetoric*. Syracuse:Syracuse University Press.

Brand, R . J. & Markey, C. M. & Hodges, S. D. (2007). Sex Differences in Self-reported Infidelity and its Correlates Sex Roles, in Pinto, R. et al (Eds) *Athens Journal of Social Sciences:The Relationship Between Sexual and Emotional Promiscuity and Infidelity, 57*,101- 109.

Bryant, C. (Ed.) (2011). *The Routledge Handbook of Deviant Behaviour*. London: Routledge.

Buckham, J. (1971). *Psychology of Drug Abuse*. Charlottesville: Virginia School of Medicine.

Burton, D. & Carter, R. (1982). *Literary Text and Language Study*. London:Edward Arnold. Publishers.

Centre for Disease Control (CDC). (2015). New York.

Cieza , A. et al (2018). Rethinking Disability, in *BMC Medicine, 16(1)*. Retrieved from https//doi.org/101186/s/2916-117-1002-6.

Clinard, M. B. (1968) *Sociology of Deviant Behaviour*. New York: Holt Rinehart and Winston.

Coleridge, P. (2000). Disability and Culture. *Selected Readings in Community Based Rehabilitation Series*, 22-41. Bangalore: National Printing Press.

Crossman, A. (2018). An Overview of Qualitative Research Methods. Retrieved from https://www.thoughtco.com/qualitative-research-methods-3026555 on 30th August, 2018.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. New York: Longman.

Damrosch, D. (2008). *The Longman Anthology of World Literature: Nineteenth Century*. London: Longman.

Danesh, M. (2002). *Understanding Media Semiotics*. Newyork: Oxford University Press.

Darling, N. & Steinberg, L. (1993). Parenting Style as Context: An Integrative Model, in *Psychological Bulletin*, *113 ( 2)*, 487-496.

Davies, K. (937).The Sociology of Prostitutes in American Sociological Review, 5 (2),744-755.America Sociological Assocition, https://www.jstor.org/stable/08387. Retrieved on 9th January 0.

Delgado, A. & Higuera, V. (2017). Hydrocephalus (Water on the Brain). Retrieved from https://www/healthline.com/health/hydrocephalus on 2nd September, 2018

Devlieger, P. J. (1999). 'Frames of Reference in African Proverbs on Disability', in *International Disability and Education*, *46*, 439-451.

Devlieger, P.J. (1998). Physical 'Disability' in Bantu Languages: Understanding the Relativity of Classification and Meaning, in *International Journal of Rehabilitation Research*, *21 (1)*, 51-62.

Drigotas, S.M. et al (1999). An Investment Model Prediction of Dating, Infidelity, in *Journal of Personality and Social Psychology*, *77 (3)*, 15.

Ebeisten, W. (2006). Towards an Archetypal Psychology of Disability Based on the Hephaestus Myth, in *Disability Studies Quarterly*, Fall, *(26)* 4.

Eco, U. (1976). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indian University Press.

Elran, R. (2011). *Metaphors of Madness in Narratives of Schizophrenia*. Jerusalem: Hebrew University Press.

Erikson, H. E. (1959). *Identity and the Life Cycle*. New York: Norton.

Exner, J. E. et al (1977). Some Psychological Characteristics of Prostitutes, in *Journal of Personality Assessment*, *41 (5),* 474-485.

Familusi O. (2011). Human Sexuality in African Thought and the HIV/AIDs Scourge, in *Lumina*, *22*, 2.

Felman, S. (2003). *Writing and Madness*.California: Stanford University Press.

Ferguson, P.M. et al (1992). *Interpreting Disability*. New York: Teachers College Press.

Foucault, M. (1977). *Madness and Civilization: A History of Insanity in the Age of Reason*.New York: Vintage Books.

Franks, B. (2001).Gutting the Golden Goose: Disability in Grimms Fairy Tales, in Wilson, J. C. and Lewiecki, C (Eds), *Embodied rhetorics: Disability in Language and Culture*, 242-258. Edwardsville : Southern Illinois University Press.

Freud, S. (1920). *A General Introduction to Psychoanalysis*. New York: Bono and Liveright.Galbicsek, C. (2016). *Alcoholism: Causes and Risk Factors*. New York: Alcohol Rehab Guide.

Garry, J. & Hasan, E. (Eds.) (2005). *Archetypes and Motifs in Folklore and Literature: A Handboo*k. New York: M. E. Sharpe Inc.

Geertz, C. (1973). *The Interpretation of Culture*: *Selected Essays*. New York: Basic.

Gerberth, V. J. (1996). The Psychology of Suicide: An Investigative Assessment, in *Practical Homicide Investigation, Law and Order, 44 (9).*

Ghafoor, A. (2014). An Islamic Perspective on Sexual Deviation, in *Faith and society*. New Jersey: Piscataway.

Glasgow, R. (2015). Madness, Marks and Laughter: An Essay on Comedy (Introduction). Retrieved from https://www.academia.edu on 12th, March 2019.

Halpenny, A. M. et al (2010). Parents' Perspectives on Parenting Styles and Disciplining Children, in *The National Children's Strategy Research Series*. Dublin: The Stationery Office.

Harknett, S. G. (1996). Cultural Factors in the Definition of Disability: A Community Study in Nyankunde, Zaire, in *African Journal of Special Needs, 1*, 18-24.

Hickey, L. (1993). Pragmatics, Stylistics and Pragmastylistics, in *Revue belge de Philologie et d'Histoire, 71(30)*, 573-886.

Hinz, E. J. & Teunissen, J. J. (1985). *War, Love and Industrialism*: *The Ares /Aphrodite/ Hephaestus Complex in Lady Chatterley's Lover*. Athens: University of Georgia Press.

Hsieh, H. F. & Shannon, S. F. (2005). Three Approaches to Qualitative Content Analysis, in SAGE Journals Retrieved from https://journals.sagepub.com>doi>pdf on 11th May 2019.

Ingstad, B. & Whyte S. R., (1995). *Disability and Culture*.California: University of California Press.

Irwin, M. & Moeller, R. (2010). 'Seeing Different: Portrayals of Disability in Young Adult Graphic Novels,' in *School Library Research: American Library Association*. *13*, 1-13.

Jensen, G. (2011). Deviance and Social Control. In Bryant, C. (Ed.), *The Routledge Handbook of deviant behaviour*; 39-45. London: Routledge.

Jirapramukpitak, T. et al (2008). Rural-Urban Migration, Illicit Drug Use and Harzadous/ Harmful Drinking in the Young Thai Population, in *Journal Compilations Society of the Study of Addiction.*

Johorey, J. (2016). Hydrocephalus Symptoms, Picture, Causes and Treatment . Retrieved from https://www.healthresource4u.com>Brain and Nervous System on 2nd September,2018.

Joiner, T. (2006). *Why people die by suicide*. Harvard: Harvard University Press.

Jones, H. & Learning, B. (2010). *An Overview of Deviant Behaviour*. London: Jones & Barlett Learning Publishers.

Jordan, S. (2017). It's Time to rethink the Social Construction of 'Virginity'. Retrieved from www.statepress.com>article>2017/02 on 25th July 2018.

Jung, C. G. (1990). *The Archetype and the Collective Unconscious*. New York: Princetown University Press.

Kairu, W. M. (2005). Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kahle, K.T. et al (2016). Hydrocephalus in Children, in *The Lancet*, *387 (10020),* 788-799.

Kaye, N. S. (1990). Sexual Deviancy, in *Current Opinion in Psychiatry*, *3 (6),* 749-753 Wilmington: Delaware.

Kayode, J.O. (1989): “African Ethics on Sex,” in Abogunnin (Ed), *Religion and Ethics in Nigeria*. Ibadan: Daystar Press.

Kenyatta, J. (1965). *Facing Mount Kenya: The Tribal Life of the Gikuyu*. London: Mercury Books.

Kerenyi, C. (1974). *The Gods of the Greeks*. London: Thames and Hudson.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji.* Dar es Salaam: East African Publishers.

Kezilahabi, E. (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi:East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1976). *Rosa Mistika.* Nairobi : Kenya Literature Bureau.

Kilanga, B. S. (2014). Ishara Katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo Mtazamo wa Kisemiotiki. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kilangwa, J. (2016). Abortion and Christian Moral Decisions: An African Ecofeminist Perspective, in *SAGE Journals*, *129 (2)*, 62-72.

Kilpatrick, D. G. (1992). Rape and Sexual Assault, in *National Violence Against WomenPrevention Research Center*. Carolina: University of South Carolina.

Kimble, G. A. et al (1980). *Principles of General Psychology.*California: Wiley Publishers.

Kings James Version Bible. Retrieved from https://www.bible.com/ on 7th July 2017.

Kisanji, J. (1998). Culture and Disability: An Analysis of Inclusive Education Based on African Folklore, in *International Journal of Disability and Development and Education*. 1-18.

Kisanji, J. (1995), Attitudes and Beliefs about Disability in Tanzania, in O’Toole, B. & McConkey, R. (Eds). *Innovations in Developing Countries for People with Disabilities*,51- 74.

Klonsky, E. D, et al (2012). Hopelessness as a Predictor of Attempted Suicide Among First Admission Patients with Psychosis: A 10-year Cohort Study, in *Suicide and Life Threatening Behaviour, 42 (1),* 1-10. University of British Columbia: Columbia.

Kontula, O. & Mannila, E. (2009). *Sexual Activity and Sexual Desire*. Routledge:Routledge

Konzela, K. (2013). *The Stigmatization of Disabilities.*Austin: University of Texas.

Kroger, J. (1996). Adolescence as Identity Synthesis: Erikson's Psychosocial Approach, in *Identity in Adolescence-The Balance Between Self and Other*, 13-47. New York: Routledge.

Lang, J.S. (1999). *The Biblical view of sexuality*. New York: CBN.

Leech, G & Short (1981). *Style in Fiction: A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.

Leke, J. I. (2016). *Infertility in Africa South of the Sahara*. Yaounde: Geneva Foundation for Medical Education and Research.

Lewis, J. R. (2001). Who Serves Satan? A Demographic and Ideological Profile, in *Marburg Journal of Religion, 6 (2).* Stevens Point: University of Wisconsin.

Llewellyn, A. & Hogan K. (2000). The Use and Abuse of Models of Disability, i*n Disability and Society*, 15 (1), 157-165. Taylor and Francis Online.

Lutz, J. B. & Bowers, J. B. (2003). Understanding how Disability is Defined and

Conceptualized in Literature, in *Rehabilitation Nursing*, 28 (3), 74-78. Wiley Online Library.

Mac-Donald .S. & Butera, G. (2010). Cultural Beliefs and Attitudes about Disability in East Africa. (Unpublished Manuscript).

Mackenzie, P. (2014*). Psychopathy, Antisocial Personality and Sociopathy: The basics, Historical Review*. Illinois: The Forensic Examiners. *53/1*, 198-207. Dar es Salaam: TUKI.

Martin, N. G. et al., (1999). Genetic Differences in Alcohol Sensitivity and the Inheritance of Alcoholism Risk, in *Psychological Medicine 29 (5),* 1069-1081. Cambridge: Cambridge: University Press.

Martinez et al (2011). Alcohol Abstinence and Drinking Among African Women: Data From the World Health Surveys, in *Journal of Medical Case Reports*. Biomed Central Limited.

Mathooko, P. et al (2012). Literature Review on Media Portrayal of People with Disabilities in Kenya. In *International Journal of Humanities and SocialSciences, 2 (8),* 223-228.

Mahamuth, N. M. et al. (1993). Predicting Men's antisocial Behavior Against Women: The Interaction Model of Sexual Aggression, in G. C. N. Hall, R. Hirschman, J. R. Graham, & M. S. Zaragoza (Eds.), *Sexual aggression: Issues in etiology, assessment and treatment* 63–97. Washington, D C: Taylor & Francis.

Mallory, B. L. et al (1993). *Traditional and Changing Views of Disability in Developing Societies: Causes, Consequences, Cautions*. New York: World Rehabilitation Fund.

Masinde, E. (1992). Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Kenyatta University: (Haijachapishwa).

Mastin, L. (2008). The Basics of Philosophy. Retrieved from *www. Philosophybasics.com/branch-Existentialism. htm/*on 5th October 2017.

Mazrui, A. M. (1984). Dunia Mti Mkavu: A Swahili Literary Treatise on Marxism, in *Kiswahili, 53(1)*, 198-207. Dar es Salaam: TUKI.

Mazrui, A. (1978). *Political Values and the Educated Class in Africa*. Berkeley: University of Carlifornia Press.

Mbah-Ndah, J.N. (1998). Caring for the Disabled: The African Experience, in *The Parliamentarian: Journal of the Parliaments of the Commonwealth,79*, 251-252

Mbiti, S. J. (1969). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: East African Educationa Publishers

Mbiti, S. J. (2012). *Concepts of God in Africa*. Nairobi: Action Press.

McAllister, J.P.(2012). Pathophysiology of Congenital and Neonatal Hydrocephalus, in *Semin Fetal Neonatal Med, 17(5)*, 286-294.

McKelle, E, (2013). Five Reasons Why We Need to Ditch the Concept of Virginity for Good, in *Everyday Feminism's School for Social Justice*.

Mckibbin W. F. et al (2008). Review of General Psychology, in *American Psychological Association, 10*.

Mdee, J.S. et al (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*.Nairobi: Longhorn Publishers.

Mezger, S. (2002). Roman Catholic Faith Represented in Kezilahabi's Mzingile, in *Swahili Forum*, 10, 75-85.

Mkota, A. & Sakara, F. (2011). *Kamusi ya Semi*. Nairobi:Vide-Muwa Publishers.

Mlacha, S.A. (1987). Aggression as a Social and Mental Disorder: A Study of Swahili Novels, in *Kiswahili,54 (3)*, 146-166. Dar es Salaam: TUKI.

Moges, B.& Weber (2014). Parental Influence on the Emotional Development of Children.Retrieved from https://my.vanderbilt.edu>2014/047pp on 10th July 2018

Mori, (2007): *Anti-Social Behaviour: People, Place and Perceptions*. Retrieved from https://www. ipsos-Mori.com on 5th October 2017.

Mohamed, S. A. (1980). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longman.

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mohamed, S.A. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longman.

Moir, A. & Jessel. D. (1989). *Brain Sex: The Real Difference Between Men and Women*. Michael Joseph: London.

Moore, H. (1994) '*Is There a Crisis in the Famil?*' Geneva: UN Research Institute for Social Development.

Mrikaria, S. E. ( 2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili-Tanzania, katika *Swahili Forum*, *17*, 104-125.

Mungai, M. (2009). For I Name Thee…Disability Onosmatics in Kenyan Folklore and Popular Music, in*Disability Studies Quarterly*,*29 (4).*

Mulokozi, M.M. (1989). Tanzu za Fasihi, katika *Mulika*, *21*, 1-24.

Mulready, S. (2003). Oedipus the King – Imagery and Humanism, in *Iris: Journal of the Classical Association of Victoria*, *16 (17*), 40-45.

Murithi, J. J. (2017). Itikadi katika Riwaya za S. A. Mohamed, katika *Kioo cha Lugha*, *157 (14)*, 9-15. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Murugami, M.W. (2009). Disability and Identity, in *Disability Studies Quarterly*. *29(4).*

National Council for Persons with Disabilities (2015). Nairobi: Kenya.

National Institute of Health (NIH). (2013). "*Hydrocephalus Fact Sheet*". Bethesda: National Institute of Health.

National Institute of Drug Abuse (NIDA) (2011). *Causes of Drug Abuse*. New York: United States National Institute of Health and Human Services.

Ngubane, J. S. (2010). *Gender Roles in the African Culture*. Stellenbosch: Stellenbosch University Press.

Nixon, J. et al (2003). *Developing Good Practice in Tackling Anti-social Behaviour in Mixed Tenure Areas*. Sheffield: Sheffield Hallam University.

Njogu, K. (2001). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nordqvist, C. (2016). *Infertility: Causes, Diagnosis, Risks, Treatments*. Brighton: Healthline Media Limited.

Obono, A. (2007). *When Reproduction is not a Choice: Infertility in Sub-Saharan Africa* Princeton: University of Ibadan.

Ogechi, N. O. & Ruto, S. J. (2002). Potrayal of Disability Through Personal Naming and Proverbs in Kenya: Evidence from Ekegusii and Nandi, in *Vienna Journal of African Studies, 3(2),* 63-82.

Ohly, R. (1981). *Aggressive prose: A Study of Kiswahili Prose of the Seventies*.

Dar es Salaam: TUKI.

Oiko, F.G. (2017). Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Masai Mara (Haijachapishwa).

Oje, R. (2006). Against Desire and Pleasure: Tradition, Morality and the Woman in African Culture, in *Magazine and Monographs*, *6 (1),* 16-20.

Oliver, M. (1990). *The politics of Disablement*. Basingstoke: Macmillan.

Onchangu, R. (2016). Mtindo katika Hadithi Fupi za Clara Momanyi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Petersen, R. C. (1980). The Epidemiology of PCP Use in the Late 1970s, in *Journal of*

*Psychedelic Drugs, 12 (3-4),* 205- 209. Ashbury: Stach.

Polashek, D.et al (1997). Rape and Rapists: Theory and Treatment in *Clinical Psychology Review*, *17,* 117–144.

Prahlad, A. (1996). *African-American Proverbs in Context.* Mississippi: University Press of Mississippi.

Prakash, H. (2013). Prostitution and its Impact on Society- A Criminological Perspective, in *International Research Journal of Social Science,2 (3*); 31-39. Dharwad: Karnataka Science College.

Prendergast, C. (2001). On the Rhetorics of Mental Disabiility, in Wilson, C. J. and

Lewieck, C. (Eds.), *Embodied Rhetorics*: *Disability in Language and Culture*; 45-60. Edwardsville: Southern Illinois University Press.

Prun et al (2010). Attitudes Towards Alcoholism and Drug Taking: A Survey of Rural and Slum Areas of Chandigarh, India, in *International Journal of Culture and Mental Health,* 3 (2), 126-136. New Delhi: Routledge.

Rexed, B. et al (1984). *Guidelines for the Control of Narcotic and Psychotropic Substances in the Context of International Treaties*. Geneva: World Health Organization.

Roberts, D. C. (1980). *Madness and Culture: A Study of Madness in the Works of Wolf Chekhov and Fitzgerald.* B.A: Simon Fraser University.

Roberts, P. (1988). The *Swahili Novel as a Disseminator of Bourgeois Individualism*.

Oregon: University of Oregon.

Robin, R. (1983). Sociology and the Disease Concept of Alcoholism, in *Research Advances in Alcohol and Drug Problems,7,* 47- 91. New York: Plenum Press.

Rono, P. (2016). Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili . Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Rossler, W. et al (2010). The Mental Health of Female Sex Workers, in *Acta Psychiatr Scand* 1-10. Zurich: University of Zurich.

Sanchez, J. (Ed.) (2010). *Media Guidelines for Portrayal of Disability*. Geneva: Internation Labour Organization.

Saussure, F. (1983). *A Course in General Linguistics*. London: Duckworth.

Senkoro, F.E.M. (1984). *The Prostitute in African Literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Schifano, F. (2011). *Is Urbanization a Risk Factor for Substance Abuse?* University of Hertfordshire: Hartfield.

Sherry, M. (2007). (Post) Colonising Disability: Intersecting Gender and Disability

Perspectives in Rethinking Postcolonial identities, in *Wagadu, 4,* (summer 2007).

Senkoro, F. K. (1982). *Fasihi*. Dar es salaam. Press and Publicity Centre.

Singh, (2012). Humour, Irony and Satire in Literature, in *International Journal of English and Literature* (IJEL), *3 (4),* 65-72. TJPRC Pvt. Ltd.

Singh, J.V. et al (1999). A Study of Hopelessness, Suicidal Intentent and Depression in Cases of Attempted Suicide, in *Indian Journal of Psychiatry*, *41 (2)*,122-130. KG Medical College: New Delhi.

Spera, C. (2005). A Review of the Relationship Among Parenting Practices, Parenting Styles And Adolescent School Achievement in *Educational Psychology Review*, *17 (2)* 125-146.

Spooner, C. (1999) Causes and Correlates of Adolescent Drug Abuse and Implications for Treatment, in *Drug and Alcohol Review,18,* 453-475. Wales: University of New South Wales.

Stromwall, L.A. et al (2012). Rape Victim and Perpetrator Blame and the Just World Hypothesis:The Influence of Victim and Age, in *Journal of Sexual Aggression,* 1-11. iFirst Article, Routledge: Taylor & Francis Groups.

Strunk, W. & White E. B. (2009).*The Elements of Style*. NewYork: New Campbell & Co.

Sukamolson, S. (2007). *Fundamentals of Qualitative Research*. Language Institute: Chulalongkom University.

Swegan W. E. & Chestnut, G.F. (2011). The Effects of Alcohol on Our Emotional Development, in *ThePsychology of Alcoholism*. Bloomington: iUniverse, Inc.

Tabong, N. P. & Adongo, P. B. (2013). *Understanding the Social Meaning of Infertiliy and Childbearing: A Qualitative Study of the Perception of Childbearing and Childlessness in Northern Ghana*. Carlifornia: PLOs One.

Thomas, R. M. (1990). The Aids Risks, Alcohol, Drugs and the Sex industry: A Scottish Study, in *Aids, Drugs and Prostitution*, 88-108. London:Travistock/Routledge.

Thomas, J. (2006). *Why People Die by Suicide*. Cambridge: Harvard University Press.

Thompson, H. (2017). *Reviewing Blindness in French Fiction, 1789-2013*. Palgrave: Macmillan.

Torr J. D. (2000). *Alcoholism: Current Controversies*. Greenhaven Presss, San Diego.

Traore, F. A. (2008). Family and Society in Said Ahmed Mohamed's Novels, in *Swahili Forum 15*, 63-72.

Tsuma , M. S. (2014). Uhakiki wa Mtindo katika Vipanya vya Maabara. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: (Haijachapishwa).

TUKI, (2004*). Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

United Nations Development Programme (UNDP). (1990). *Drugs and Development: Human Development Report*. New York: Oxford University Press.

United Nations Economic and Social Council (1963). Urban Problems: The Role of Women in Urban Development, in *Economic Commission for Africa E/CN,14/URB/13*. Addis Ababa: UN/ECA.

Vitelli, R. (2017). How Dangerous is a Broken Heart?, in *Psychology Today.com*. Retrieved From https://www.psychologytoday.com>blog. on 1st June, 2018.

Wafula, R. (1989). The Use of Allegory in Shabaan Roberts's Prose Works. M. A Thesis, University of Nairobi. (Unpublished).

Wainright, W. (2012). Concepts of God, in *Stanford of Encyclopedia of Philosophy*. Stanford: Stanford university.

Waliaula, W.K. (2009). Negotiating Local Knowledge 11: Kiswahili and Attitude Towards Disability, in *Disability Studies Quarterly,4 (29).*

Wasserstrom, R. (1997). On Racism and Sexism, in Gould, C. (ed), *Gender*, 337-338. Humanities Press: New Jersey.

Wellek, R. & Warren, A. (1982). *Theory of Literature*. London: Jonathan Cape.

Wales, K. (2001). *A Dictonary of Stylistics*. New York: Longman.

Wilson, A. (2013). *The Threat of Liberation: Imperialism and Revolution in Zanzibar.* Chicago: Pluto Press.

Wischmann, T. & Thorn, P. (2013). *(Male) Infertility: What Does it Mean to Men? New Evidence from Quantative and Qualitative Studies.* Moerfelden: Elsevier Limited.

Woods, T. (2012). From Female Sexuality and Hysteria to Feminine Psychology: The Gender of Insanity in Literature. M.A. Thesis. University of Jerusalem: (Unpublished).

World Health Organisation, (WHO). (2019). *Health report*. Geneva: WHO.

World Health Organisation, (WHO). (2018). *Management of Substance Abuse: Global Status Report on Alcohol and Health*. Geneva: WHO.

World Health Organization (WHO), (2017). Violence Against Women. Retrieved from www.who.int>News>fact Sheets>Detail on 20th June, 2018.

World Health Organization (WHO) (2011). World Report on Disability. Retrieved from www.who Int>disabilities >report on 4th June, 2018.

World Health Organisation (WHO), (1990). *Health Report*. Geneva:WHO.

World Facts and Statistics on Disability and Disability Issues 2013. Retrieved from : *http://www.disabled–world.com*on8th November, 2014.

Wright, P. (2006). *A Language of the body: Images of disability in the works of D.H. Lawrence.*Washington: Washington State University.

Zare, B. (2011). Review of Studies on Infidelity. In *3rd International Conference on Advanced Management Science IPEDR*, 19. LAC SIT Press. Singapore.

# VIAMBATISHO

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013

The Grant of Research Licenses is guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014.

**CONDITIONS**

1. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
2. The License and any rights thereunder are non-transferable.
3. The Licensee shall inform the County Governor before commencement of the research.
4. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
5. The License does not give authority to transfer research materials.
6. NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project.
7. The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report within one year of completion of the research.
8. NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.

National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O. Box 30623 - 00100, Nairobi, Kenya
TEL: 020 400 7000, 0713 788787, 0735 404245
Email: dg@nacosti.go.ke, registry@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI

National Commission for Science, Technology and Innovation

RESEARCH LICENSE

Serial No.A 24074

CONDITIONS: see back page

THIS IS TO CERTIFY THAT:
*MS. BETH NJERI MUTUGU*
of KENYATTA UNIVERSITY, 0-100
Nairobi,has been permitted to conduct research in *Nairobi County*

on the topic: *MATUMIZI YA TASWIRA ZA ULEMAVU KAMA MTINDO KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID AHMED MOHAMED NA EUPHRASE KEZILAHABI*

for the period ending:
*12th April,2020*

Permit No : NACOSTI/P/19/93302/28713
Date Of Issue : 12th April,2019
Fee Recieved :Ksh 2000



..............................
Applicant's Signature

..............................
Director General
National Commission for Science, Technology & Innovation